# MAPITIO YA AGANO JIPYA

shepherds
GLOBAL CLASSROOM

Shepherds Global Classroom ipo kwa ajili ya kuujenga mwili wa Kristo kwa kutoa mtaala kwa ajili ya kuwaendeleza viongozi wa Kikristo duniani kote. Tunalenga kuongeza programu za mafunzo ya asili kwa kuweka chombo cha mtaala wa kozi 20 mikononi mwa viongozi wa kiroho wanaotoa mafunzo katika kila nchi duniani.

Kitabu hiki kinapatikana bure kwa njia ya kupakua kutoka katika https://www.shepherdsglobal.org/courses

Mwandishi Mkuu: Dr. Randall D. McElwain.

Hakimiliki © 2025 Shepherds Global Classroom.

Ilitafsiriwa kutoka Toleo la Tatu la Kiingereza.

Haki zote zimehifadhiwa.

Nyenzo za wahusika wengine zilizotumika ni hakimiliki ya wamiliki husika ambazo zimeshirikishwa na kutumika humu chini ya leseni mbalimbali.

Tafsiri ya Maandiko "yaliyonukuliwa" kutoka chapisho la Kiingereza kwa ajili ya chapisho hili la Kiswahili yanatoka katika Biblia Takatifu ya Kiswahili, "Swahili Union Version Bible" (SUVB®)." Yametumika kwa kibali. Haki zote zimehifadhiwa.

**Taarifa kuhusu vibali:**

Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa na kutawanywa bure kikiwa kimechapishwa na katika mifumo ya kidigitali chini ya miongozo ifuatayo: (1) Maudhui yaliyoko kwenye kitabu hiki hayawezi kubadilishwa kwa namna yeyote ile; (2) Nakala zinazopatikana haziwezi zikauzwa kwa ajili ya kupata faida; (3) Taasisi za elimu zina uhuru wa kutumia na kukinakili kitabu hiki, hata kama wanalipisha ada za masomo ya ziada; na (4) Kitabu hiki hakiwezi kufanyiwa tafsiri pasipokuwepo na kibali na usimamizi wa Shepherds Global Classroom.

# Yaliyomo


Muhtasari wa Kozi ........ 5
Ramani ya Ulimwengu wa Agano Jipya ........ 6
Ramani ya Israeli ........ 7
(1) Utangulizi wa Agano Jipya ........ 9
(2) Mathayo, Marko, na Luka ........ 23
(3) Yohana ........ 37
(4) Matendo ya Mitume ........ 45
(5) Warumi ........ 59
(6) Wakorintho na Wagalatia ........ 69
(7) Waefeso, Wafilipi, Wakolosai, na Filemoni ........ 83
(8) Wathesalonike ........ 99
(9) Timotheo na Tito ........ 109
(10) Waebrania na Yakobo ........ 119
(11) Petro, Yohana, na Yuda ........ 131
(12) Ufunuo ........ 141
Vyanzo Vinavyopendekezwa ........ 149
Fomu kwa ajili ya Kumbukumbu ya Kazi za Kufanya ........ 157

# Muhtasari wa Kozi

Kabla ya kukutana kwa ajili ya kila kipindi cha darasa, wanafunzi wasome au wasikilize kitabu (vitabu) vya Biblia ambavyo watajifunza. Mwishoni mwa kila kipindi cha darasa, tafadhali wakumbushe wanafunzi kuhusu **zoezi la kusoma** kwa ajili ya somo linalofuata. Usomaji huu utahakikisha kwamba wanafumzi wanakuwa na uelewa wa yaliyomo ambayo ni ya msingi kwa kitabu (vitabu) kabla ya darasa kuanza.

Mnapojifunza kama darasa, mnaweza kupokezana kusoma makala. Mara kwa mara mnatakiwa kutulia kidogo kwa ajili ya majadiliano. Kama kiongozi wa darasa, unawajibika kwa ajili ya kuhakikisha majadiliano yanalenga makala zinazosomwa. Itasaidia sana kuwa na kipimo cha muda kwa kila kipindi cha majadiliano.

**Maswali ya majadiliano** na **shughuli za ndani ya darasa** yameoneshwa kwa alama ►. Unapaswa kuuliza swali na kuwapa wanafunzi muda wa kujadili majibu yao. Jaribu kuwahusisha wanafunzi wote katika majadiliano. Kama itahitajika, unaweza kuwataja wanafunzi kwa majina yao.

Rejea nyingi za **Maandiko** zimetolewa katika maandishi. Wanafunzi wanapaswa kutumia Biblia zao wakati wa darasa, ili kuangalia vifungu vinavyojadiliwa.

Kila somo litahusisha **jaribio** na angalau **mradi** au **zoezi la kuandika** ambalo linahusiana na kitabu (vitabu) na dhana kuu zinazojadiliwa katika somo.

Mwishoni mwa kila kipindi, unaweza ukapitia tena maswali ya jaribio pamoja na wanafunzi. Kipindi cha darasa kinachofuata kinapaswa kuanza na jaribio. Jaribio linaweza kufanyika kwa mdomo au kwa maandishi. Kila mwanafunzi anapaswa ajibu maswali kwa kujitegemea (peke yake), pasipo msaada kutoka kwa wengine au pasipo kutumia nyenzo zilizoandikwa. Angalau majibu ya majaribio yanapatikana kwa kuyapakua kutoka katika shepherdsglobal.org.

Kila somo litaanza na **zoezi** fupi **la kukariri andiko,** ambalo litahusisha mstari mkuu kutoka katika vitabu vinavyosomwa. Wanafunzi wanategemewa kuandika au kunukuu kifungu cha maandiko kutoka katika kumbukumbu yao wakati wa majaribio.


Endapo mwanafunzi anataka kupata cheti kutoka **Shepherds Global Classroom**, anapaswa ahudhurie vipindi vya darasa na kukamilisha mazoezi yote. Fomu itatolewa mwishoni mwa kozi kwa ajili ya kunakili mazoezi yote yaliyokamilika.

Kama unaipata kozi hii kupitia SGC mobile app, tafadhali weka umakini katika vyanzo vifuatavyo ambavyo vinapatikana katika kiambatanisho:

- Ramani ya Ulimwengu wa Agano Jipya
- Ramani ya Israeli

# Ramani ya Ulimwengu wa Agano Jipya

Tafadhali rejea katika ramani hii wakati wote wa kipindi cha kozi.[1]




**Paulo aliandika kwa**

(1) Rumi (mji)

(2) Korintho (mji)

(3) Galatia (jimbo)

(4) Efeso (mji)

(5) Filipi (mji)

(6) Kolosai (mji)

(7) Thesalonike (mji)

**Maeneo muhimu katika AJ**

(8) Italia (jimbo)

(9) Asia (jimbo)

(10) Antiokia of Shamu (mji)

(11) Uyahudi (jimbo)

(12) Yerusalemu (mji)

(13) Krete (kisiwa)

(14) Bahari ya Mediterranea

(15) Akaya (jimbo)

(16) Makedonia (jimbo)

**(17) Makanisa katika Ufunuo**

- Efeso (mji)
- Smirna (mji)
- Pergamo (mji)
- Thiatira (mji)
- Sardi (mji)
- Filadelfia (mji)
- Laodikia (mji)

[1] "Map of the NT World" ilitengenezwa na SGC kwa kutumia taarifa kutoka NED na mfumo wa Kibiblia wa kubadilisha anwani au jina la mahali kuwa kuratibu za kijiografia (CC BY 4.0), inapatikana kutoka https://www.flickr.com/photos/sgc-library/52344115203, umiliki wa umma (CC0).

# Ramani ya Israeli

(1) Tiro (mji)[2]

(2) Kaisaria-Filipi (mji)

(3) Galilaya (mkoa)

(4) Kana (mji)

(5) Kapernaumu (mji)

(6) Nazareti (mji)

(7) Dekapoli (mkoa)

(8) Samaria (mkoa)

(9) Mto Yordani (maji)

(10) Emau (mji)

(11) Yerusalemu (mji)

(12) Bethlehemu (mji)

(13) Uwanda wa Pwani (mkoa wa kijiografia)

(14) Nyanda za juu za kati (mkoa wa kijiografia)

(15) Jagwa la Yudea (mkoa wa kijiografia)


(16) Bahari Mfu (maji)

(17) Bahari ya Galilaya (maji)

(18) Bahari ya Mediterranea (maji)

(19) Kaisaria (mji)

(20) Uyahudi (mkoa)




[2] "Ramani ya Israeli" ilitengenezwa na SGC kwa kutumia taarifa kutoka NED, SRTM, NASA, na mfumo wa Kibiblia wa kubadilisha anwani au jina la mahali kuwa kuratibu za kijiografia (CC BY 4.0), inapatikana kutoka https://www.flickr.com/photos/sgc-library/52344178339, umiliki wa umma (CC0).

# Somo la 1
# Utangulizi wa Agano Jipya

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kufahamu jiografia ya Palestina na umuhimu wake kwa Agano Jipya.

(2) Kuelewa mazingira ya Kihistoria ya Agano Jipya.

(3) Kutambua ushawishi wa Kirumi, Kiyunani/Kigiriki, na Kiyahudi kwa Agano Jipya.

(4) Kuelewa baadhi ya desturi za kale za Agano Jipya.

(5) Kuwa na uwezo wa kuelezea sababu za kuamini mamlaka ya Agano Jipya.

(6) Kutambua namna Mungu alivyouandaa ulimwengu kwa ajili ya ujio wa Kristo na kusambaa kwa Injili.

## Maandalizi kwa ajili ya Somo hili

► Soma Mathayo 1:1-7, Luka 1:1-5, Luka 2:1-5.

► Kariri Wagalatia 4:4-5.

## Umuhimu wa Historia na Jiografia kwa Agano Jipya

► Je, usahihi wa historia ya Kibiblia ni muhimu kwa imani ya Kikristo? Kwa nini?

Imani ya Kikristo imejengwa juu ya matendo makuu ya Mungu katika historia ya mwanadamu na katika maisha ya Yesu ambaye alikuja katika mwili na kuishi kati kati yetu (Yohana 1:14). Kwa hiyo, kufahamu muktadha wa kihistoria wa Ukristo unatusaidia sisi kulielewa Agano Jipya. Sehemu za maandiko kutoka Mathayo na Luka mwanzoni mwa somo hili wanaonesha masisitizo wa waandishi wa Injili juu ya mazingira ya kihistoria ya maisha ya Yesu.

Ukristo uko tofauti sana na dini nyingi sana za ulimwengu. Wanafunzi wa Dini za Mashariki wameonesha kwamba Ubudha kimsingi unaweza kuwa sawa sawa (hauna shida yeyote) pasipo Budha; Uhindu kwa sehemu kubwa unaweza kuwa sawa pasipo miungu yake mingi. Hata hivyo, Ukristo utakuwa tupu pasipo maisha, kifo, na ufufuo wa Yesu wa Nazareti. "tena kama Kristo hakufufuka, basi, kuhubiri kwetu ni bure na imani yenu ni bure" (1 Wakorintho 15:14).

Ukristo ni ukweli wa kihistoria; Biblia ni kitabu cha kihistoria. Hainakili hadithi za kufikirika au simulizi tupu; ni rekodi ya matukio ya kihistoria. Baadhi ya wasomi wanadai kwamba Biblia ni mkusanyiko wa mafundisho makuu ya kimaadili yanayoelezewa na hadithi za kufikirika za kabla ya sayansi. Hata hivyo, Biblia haitupi sisi chaguo hili; maandiko yanathibitisha wazi kuwa ni kweli ya kihistoria.

Agano Jipya lina msingi katika matukio ambayo yalitokea katika muda, mahali, na utamaduni halisi. Muda ni karne ya kwanza B.K; mahali ni Palestina na ulimwengu wa dola ya Rumi; utamaduni ni wa Kiyahudi, Kiyunani, na Kirumi. Kwa sababu ya umuhimu wa mazingira haya ya kihistoria na kijiografia, tutaanza kujifunza kwetu na maelezo ya ulimwengu wa Yesu na wa kanisa la kwanza.

## Mazingira ya Kijiografia ya Agano Jipya

► Rejea katika ramani ya Israeli ili kuelewa vema sehemu hii ya somo. (Kama unatumia SGC mobile app, kujifunza kozi hii, ramani inapatikana katika kiambatanisho.).

Ardhi ya Palestina ni kiini cha historia ya Israeli na huduma ya Yesu ya duniani. Hata jina "Yesu wa Nazareti" linaonesha umuhimu wa sehemu halisi katika maisha yake.

Palestina inakadiriwa kuwa na upana wa kilometa 75 na urefu wa kilometa 235.[3] Ingawaje ni dogo, eneo hili lilikuwa limewekwa kimkakati kwa ajili ya matukio ya historia ya kale. Mahali lilipo kati kati ya Misri kusini magharibi, Shamu kaskazini, Ashuru kaskazini mashariki, na Babeli upande wa mashariki ulilifanya liwe njia panda kwa ajili ya biashara na sehemu muhimu ya kimkakati kijeshi.

### Sifa za uso wa ardhi za Magharibi-Mashariki

Kutembea kutoka magharibi kwenda mashariki (kutoka Bahari ya Mediterranea hadi Mto Yordan), mtu anayesafiri kupitia Palestina atakutana na maeneo manne ya mikoa ya kijiografia. Kutoka Uwanda wa Pwani pembezoni mwa Bahari ya Mediterranea, ardhi inainuka kupitia Nyanda za juu za kati kwenda kilele cha juu kama mita 800[4] juu ya usawa wa bahari. Yerusalemu ilikuwa ni sehemu ya juu zaidi ya Israeli, katika vyote viwili kiroho na kijiografia.

Mashariki zaidi ni Jangwa la Yudea. Sehemu yenye ukiwa ya milima na ardhi yenye miamba, eneo hili lilikuwa hatari na gumu kwa watu kuishi.

Mashariki mwa eneo hili la milima, Bonde la Yordani linashuka hadi mita 415[5] chini ya usawa wa bahari, sehemu ya chini sana ya ardhi duniani. Mto Yordani hupuliza kilomita 100[6] kutoka milimani kaskazini mwa bahari ya Galilaya kwenda Bahari Mfu upande wa kusini.

Kwa huduma yake kubwa, Mto Yordani ulikuwa ndio mpaka mkuu wa mashariki wa safari za Yesu. Hata hivyo, mara chache alivuka bahari ya Galilaya ili kusafiri katika maeneo mashariki mwa Mto Yordani. Eneo hili lilijumuisha Dekapoli ("Miji kumi" ilitengenezwa wakati wa utawala wa Wagiriki/Wayunani) na Perea. Kwa mshangao wa wafuasi wake, Yesu alikuwa tayari kuwahudumia Mataifa katika eneo hili. Huduma hii ilisaidia kuandaa

[3] Maili 45 upana kwa Maili 145 urefu
[4] futi 2, 600
[5] futi 1,370
[6] Maili 65

wanafunzi kwa ajili ya agizo kuu la baadae la kuhubiri "…katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi" (Matendo ya Mitume 1:8).

### Sifa za uso wa Ardhi za Kaskazini-Kusini

Kutembea kutoka kaskazini kwenda kusini, msafiri angeweza kusafiri kutoka Galilaya kupitia Samaria kwenda Uyahudi, kitovu cha kidini na kisiasa cha Palestina. Galilaya ulikuwa ni mkoa wa kibiashara uliozunguka bahari ya Galilaya, ziwa lenye maji baridi yasiyo na chumvi. Nazareti ilikuwa ni mojawapo kati ya vijiji vidogo vidogo katika eneo hili zuri. Galilaya ilifurahia samaki tele kutoka katika bahari ya Galilaya, na pia matunda na mboga mboga ambazo zilizalishwa wakati wote wa mwaka katika uwanda wa Genesareti, eneo lenye hali ya hewa ya wastani kaskazini-magharibi pembezoni mwa bahari ya Galilaya.

Mkoa wa Samaria uliwatenga Wayahudi kutoka Kaskazini na hekalu la Yerusalemu. Wasamaria walikuwa wazao wa wageni na Wayahudi ambao walioleana baada ya Waashuru kuvamia mwaka 722 B.C. Wasamaria walifuata sheria za Agano la Kale, walitahiri, walisheherekea sherehe mbalimbali za kidini, na walitegemea ujio wa Masihi. Hata hivyo, Wasamaria walikuwa na sehemu yao ya kuabudu juu ya mlima wa Gerizimu na Wayahudi waliwachukulia kuwa watu wasio safi. Wayahudi wengi waliokuwa wanasafiri kutoka Galilaya kwenda Uyahudi kwa makusudi kabisa waliepuka Samaria. Walivuka Mto Yordani na kusafiri kupitia fukwe zake za mashariki kabla ya kuvuka tena kwenda Uyahudi. Yesu, hata hivyo, alisafiri kupitia Samaria ili kumuhudumia mwanamke pale kisimani. Mwanamke huyu Msamaria alimsikia Yesu akikiri moja kwa moja kwamba Yeye ndiye Masihi (Yohana 4:25-26).

Uyahudi na mji wake mkuu, Yerusalemu, ulikuwa kusini. Ukionekana kutoka mbali, mlima wa Sayuni (jina lingine kwa ajili ya Yerusalemu) ulikuwa ni kitovu cha kidini cha imani ya Kiyahudi. Kila mwaka katika Pasaka, familia za Kiyahudi zilitembelea Hekaluni. Familia ya Yesu walifanya safari hii wakati alipokuwa mtoto, na ilikuwa ni kule, katika nyumba ya Baba yake, kwamba Yesu alipatikana akiwa ameketi kati kati ya waalimu (Luka 2:41-49).

## Mazingira ya Kihistoria ya Agano Jipya

Kuanzia kuanguka kwa Yerusalemu kwenda Babeli mwaka 586 K.K., historia ya Palestina ni historia ya majanga. Yuda haikuwahi kupata utukufu wake wa kwanza.

Dola ya Babeli ilidhibiti Palestina hadi Babeli ilipoanguka kwa mtawala wa Kiajemi, Koreshi, mwaka 539 K.K. Koreshi kisha akawaruhusu Wayahudi kurudi Yerusalemu. Wakati wa karne iliyofuata, mji ulijengwa upya chini ya uongozi wa Ezra, Zerubabeli, na Nehemia. Hata hivyo, Yerusalemu ulikuwa chini ya udhibiti wa Uajemi. Karne nyingi baade, Wayahudi wa wakati wa Yesu bado walikuwa wanazungumza Kiaramaiki, lugha ya Dola ya Uajemi.

Katika mwaka 334 K.K., Alexander mkuu aliishinda Uajemi. Palestina ikawa sehemu ya Dola ya Uyunani. Baada ya kufa kwamka 323 K.K., dola yake ikagawanywa kwa majenerali wake wanne. Palestinea ikawa uwanja wa vita kati ya majenerali hawa na waliofuata: Waptolemi na Waseleucidi. Hiki kilikuwa ni mojawapo ya vipindi vya giza katika historia ya Kiyahudi.

Katika wakati huu, Antiochus Epiphanes (mtawala wa Kiyunani wa Kiseleucidi) alilinajisi Hekalu alipojenga madhabahu ya mungu wa Kiyunani Zeu Hekaluni.

Ukatili wa Antiochus Epiphanes ulichochea mapinduzi yalioongozwa na Wamakabayo, familia ya Kiyahudi. Familia ya Wamakabayo walichukua udhibiti wa Uyahudi na kuanzisha ukoo wa Wahasmonia. Tangu mwaka 166-63 K.K., Palestina ilitawaliwa na familia ya Wamakabayo. Kwa bahati mbaya, hiki kilikuwa kipindi cha msukosuko wa kitaifa kutokana na ushindani katika familia na ungengeufu wa kidini. Mwaka 67 K.K., familia ikaingia katika vita ya wenyewe kwa wenyewe.

Rumi haraka wakachukua fursa ya mgawanyiko kati ya viongozi wa Kiyahudi na kuanzisha udhibiti juu ya Palestina. Mwaka 63 K.K., Jenerali wa Kirumi Pompey akaushinda Yerusalemu. Pompey akamchagua mzao wa Wakabayo, Hyrcanus II, kama kuhani mkuu na kumfanya mtawala *de facto* wa Uyahudi. (Mtawala wa *de facto* ni mtu ambaye ana nguvu katika nchi, hata kama mtu mwingine anaweza kuwa na cheo cha mtawala. Pompey alikuwa na cheo cha mtawala, lakini Hyrcanus II alikuwa na nguvu za kisiasa.) Wakati wa Kristo, Palestina ilikuwa inatawaliwa na Rumi.

Mwaka 37 K.K., Herod mkuu akachaguliwa na Seneta wa Kirumi kuwa mfalme wa Uyahudi. Herode alikuwa Muidumea, uzao wa Waedomi. Wamakabayo waliongeza kwa nguvu Edomu katika ufalme wao, lakini Wayahudi wengi walimchukulia Herode kwamba si mtawala halali. Waedomi ni wazao wa Esau, wakati Wayahudi ni uzao wa Yakobo. Kwa karne nyingi, Edomu amekuwa adui wa Israeli: Edomu alikataa Israeli wasipite katika ardi yao walipokuwa wanakwenda Kanaani wakati wa Kutoka (Hesabu 20:14-21). Edomu pia alimsaidia Babeli wakati wa kuharibu Yerusalemu (Obadia 1). Kama Muedomi, Wayahudi hawakumuamini Herod mkuu.

Hadi mwaka 30 K.K., Herode alikuwa amewashinda wapinzani wake na akawa kiongozi mkuu wa Uyahudi chini ya mamlaka ya Rumi. Herode alikuwa mtu mgumu sana. Tabia yake ilionesha vyote viwili sifa nzuri na sifa mbaya. Upande chanya/mzuri, Herode alionesha heshima kubwa kwa Wayahudi. Alijenga Hekalu na alifuata taratibu za vyakula za Kiyahudi. Hata hivyo, upande wake hasi/mbaya, Herode alikuwa na uchu wa madaraka na wivu sana kwa chohote ambacho kingetishia mamlaka yake. Aliwaua watoto wake kadhaa ambao walikua na kuwa wakubwa kwa sababu aliogopa kwamba wanaweza wakajaribu kuwa wafalme mahala pale. Baadae, alijaribu kumuua Yesu mamajusi walipouliza, "Yuko wapi yeye aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi?" (Mathayo 2:2).

Baada ya kifo cha Herode Mkuu mwaka 4 K.K., Rumi iligawanya ufalme wake kwa watoto wake watatu. Watawala hawa walikuwa na mchango kwa historia ya Agano Jipya na huduma ya Yesu.

**Herode Arkelao** alipewa udhibiti wa Uyahudi. Kwa sababu Alkaleo alikuwa na sifa ya ukatili, Yusufu na Mariamu walirudi Nazareti badala ya Bethlehemu (Mathayo 2:19-23).[7]

[7] Bethlehemu katika Uyahudi ilikuwa chini ya Alkaleo; Nazareti katika Galilaya ilikuwa chini ya udhibiti wa Herode Antipa.

Ukatili wa Alkaleo ulisababisha wawakilishi wa Wayayhudi kukata rufaa Rumi ili kupata msaada. Alkaleo aliondolewa, na Uyahudi ikawekwa chini ya utawala wa *procurator* (au gavana) aliyetumwa na Rumi.

Wakati wa kesi ya Yesu, Pontio Pilato alikuwa procurator wa Kirumi, aliyekuwa anakaa Kaisaria[8] na alisafiri kwenda Yerusalemu wakati wa sherehe muhimu.[9] Pilato alipaswa kulazimisha matakwa ya Rumi pasipo kusababisha Wayahudi Kuasi. Ili kukamilisha hili, aliruhusu baraza lote kuwa namna fulani ya uhuru. Baraza hili, ambalo lilijumuisha Marabi wa Kiyahudi walioheshimika, lilikutana kwa ajili ya maamuzi ya kitaifa ya kidini, kitamaduni, na kimahakama. Kayafa, kuhani mkuu, aliogopa kwamba uhuru huu unaweza kuondolewa endapo matendo ya Yesu yangewafanya Rumi kukasirika (Yohana 11:49-50).

**Herode Filipo** alikuwa mvumilivu sana kati ya watoto wa Herode. Alitawala eneo la kaskazini mashariki mwa Galilaya. Yesu litumia muda katika mkoa huu ili kuepuka hatari za kukamatwa na viongozi wa Kiyahudi huko Yerusalemu. Herode Filipo alijenga mji wa Panias na akaupa jina Kaisaria-Filipi. Hapa ndio mahali ambapo Petro alitoa ukiri mkuu: "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai" (Mathayo 16:16).

**Herode Antipa** alikuwa mtawala wa Galilaya na Perea tangu 4 K.K. hadi 39B.K. Antipas alimfunga na kumuua Yohana Mbatizaji (Marko 6:17-29). Kwa sababu Herode Antipa alikuwa juu ya Galilaya, Pilato alijaribu kuepuka wajibu kwa ajili ya hatma ya Yesu na akampeleka kwa Antipas kwa ajili ya kesi (Luka 23:6-12). Hata hivyo, Herode alikataa kufanya hukumu na kumrudisha Yesu kwa Pilato kwa ajili ya kutoa hukumu.

## Mazingira ya Kitamaduni ya Agano Jipya

Mazingira ya kiutamaduni ya Agano Jipya ni muhimu sana. Mungu alimtuma Yesu katika ulimwengu ambao ulikuwa umepata ushawishi wa tamaduni tatu tofauti. Kila mojawapo ya tamaduni hizi zina mchango muhimu juu ya ulimwengu wa Agano Jipya.

### Mazingira ya Kiyunani ya Agano Jipya

Ushawishi wa Alexander mkuu uliendelea hata baada ya kifo chake mwaka 323 K.K. Alitaka kila mmoja katika dola aongee lugha moja. Kwa sababu hii, Kiyunani kikawa lugha ya Agano Jipya. Wayahudi wengi waliongea Kiaramaiki na Kiyunani

Kuna namna tatu ambazo lugha ya Kiyunani ilichangia katika kanisa la kwanza:

1. **Lugha moja ambayo ilileta urahisi wa kushirikisha Injili**. Agano Jipya liliandikwa kwa *Koine Greek*, Kiyunani cha kawaida kilikuwa kinazungumzwa katika ulimwengu wote wa Mediterranea katika karne ya kwanza. Wakati Kiaramaiki (lugha iliyo zungumzwa katika Palestina) na Kiebrania (lugha ya Agano la Kale) ilikuwa ni

[8] Huu si mji sawasawa na Kaisaria-Filipi. Badala yake, huu ni Kaisaria Maritima, Mji wa bandari kuu ya Kirumi katika bahari ya Mediterranea kwenye pwani ya Uyahudi.
[9] Pilato alitawala kutoka mwaka 26-36 B.K.x

kwa ajili ya Wayahudi, Kiyunani kilizungumzwa katika Dola yote ya Rumi. Ujumbe wa mitume ulieleweka na wote Wayahudi na Mataifa popote walipohubiri.

2. **Ilikuwa ni lugha iliyoeleweka, kamilifu kwa ajili ya kuwasilisha dhana za Kitheolojia.** Ilimruhusu Paulo kuandika kuhusu fundisho la kuhesabiwa haki na kutakaswa.

3. **Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale (*Septuagint*) ilikuwa ndio Maandiko ya kanisa la kwanza.** Tafsiri hii, kutoka karne ya tatu K.K, iliwaruhusu Wayahudi waliokuwa wanazungumza Kiyunani kusoma Agano la Kale na ikaleta urahisi wa upatikanaji kwa waamini wapya wa Mataifa.

### Mazingira ya Kirumi ya Agano Jipya

#### *Injili*

Ushawishi wa Kirumi katika maisha ya Yesu ulionekana wakati wa kuzaliwa kwake. Mungu alitumia sensa iliyofanywa na mtawala wa kipagani ili kutimiliza unabii wa Mika kwamba Masihi atazaliwa Bethlehemu (Mika 5:2, Luka 2:1-5). Kama ambavyo mtawala wa Kiajemi Koreshi alivyokuwa chombo cha Mungu ili kuwarudisha watu wake kutoka utumwani, Kaisari Augusto alikuwa chombo cha Mungu kumleta Yusufu na Mariamu toka Nazareti hadi Bethlehemu.

Kulikuwa na njia mbili zilizokuwepo za kufanya sensa. Warumi walipendelea kumuorodhesha kila mtu katika mji aliokuwa anaishi. Hata hivyo, Wayahudi walipendelea kuendeleza rekodi za kikabila katika kila vijiji vya koo zao, kwa hiyo Rumi iliruhusu Uyahudi kufanya sensa katika utaratibu wao wa kiutamaduni. Hii iliwataka Yusufu na Mariamu kusafiri kilometa 100[10] toka mji wao Nazareti.

Ingawaje Yesu alisema kidogo kuhusiana na Rumi na siasa zake, maafisa wa Kirumi kama Herode Antipa na Pontio Pilato walitafsiri ujumbe wake kuhusiana na ufalme wa Mungu kama tishio kwa nguvu zao. Ujumbe wa ufalme wa Mungu ulikuwa ni changamoto kwa ufalme wa ulimwengu huu.

#### *Kitabu cha Matendo ya Mitume*

Matendo ya Mitume inaonesha namna Mungu alivyotumia Dola ya Rumi kusaidia kueneza Injili. Neno la Kilatini *pax Romana* ("Amani ya Rumi") linarejea karne mbili za kushurutisha kwa ukatili amani katika Dola ya Rumi. Wakati nguvu za Rumi mara nyingi zilitumika pasipo haki (kama wakati wa kusulubishwa kwa Yesu), nguvu ya Rumi pia iliwasaidia wasafiri kutoka Wabarbari/makabila katili ya kigeni, waliunganisha Dola, na na walifanya safari za mitume kuwezekana. Rumi ilijenga kilometa 85,000[11] za barabara, iliyonyooka kutoka mto. Frati mashariki kwenda Scotland huko magharibi, na iliimarisha njia za bahari kupitia bahari

[10] Maili 65
[11] Maili 53,000

ya Mediterranea. Safari za kimishenari za Paulo kwa sehemu kubwa ziliwezekana kwa sababu ya barabara na njia za baharini ambazo zilijengwa na Rumi.

Tofauti na utamaduni wa kale wa Kiyahudi, ambao ulikua kuzunguka miji midogo na maeneo ya vijiji, Rumi ilikuwa ni Dola ya miji mikubwa. Miji hii mikubwa ilikuwa ni yenye umuhimu mkubwa kwa ajili ya kusambaa kwa Injili. Katika kila mkoa, Paulo alihubiri ili kufikia watu wengi zaidi. Paulo alihubiri Injili katika miji ya msingi ya Dola ya Rumi na kupanga kuhubiri Rumi yenyewe, kitovu cha ulimwengu wa karne ya kwanza (Warumi 1:11-15).

Paulo alitumia kikamilifu haki yake kama raia wa Rumi ili kusaidia kusambaza Injili. Mifano ya hii inajumuisha madai yake ya ulinzi wa kisheria kule Filipi (Matendo ya Mitume 16:35-39) na yeye kukata rufaa ili kusikilizwa mbele ya Kaisari (Matendo ya Mitume 25:11).

### *Nyaraka za Paulo*

Kitabu cha Wafilipi kinatumia dhana ya uraia kuwakumbusha wasomaji kwamba wao ni raia wa kweli wa mbinguni (Wafilipi 3:20). Paulo aliandika barua yake ya maombi kwa Filemoni akijua kwamba sheria ya Kirumi ilikuwa imetolewa kwa ajili ya kutekeleza hukumu ya Onesimo, mtumwa aliyetoroka na mwongofu mpya wa Paulo. Katika Warumi, Wagalatia, na Waefeso, Paulo anatumia lugha ya kisheria ya Kirumi ili kuelezea dhana za kitheolojia kama vile kuhesabiwa haki na kusamehewa.

Hata picha ya Paulo ya kuasiliwa (kufanywa mwana) ilikuwa inafahamika sana katika jamii ya Kirumi kuliko ya Kiyahudi (Wagalatia 4:5, Waefeso 1:5). Kuasili kulikuwa ni jambo la kawaida katika jamii ya Kirumi. Paulo alielewa kwamba kuasili kulihusisha kufutiwa deni la zamani, na kutoa haki ya urithi kwa kijana mpya, na kuanza kwa maisha mapya. Paulo alitumia dhana hizi za kisheria za Kirumi ili kuelezea mabadiliko ambayo yanatokea wakati mwamini anapokuwa ameasiliwa katika familia ya Mungu.

### *Kitabu cha Ufunuo*

Rumi ilijivunia uvumilivu wake wa imani mbalimbali; hata hivyo, watu wote walitakiwa kutambua uungu wa empara (mtawala). Rumi iliruhusu Wayahudi au mafundisho ya Kikristo endapo tu waabudu wangelitamka kwamba “Kaisari ni bwana.” Hata hivyo, ujumbe wa Wakristo kwamba “Yesu Kristo ni Bwana” haukukubaliwa na serikali ya Rumi (Wafilipi 2:11).

Kitabu cha Ufunuo kiliandikwa katika mazingira ya mateso ya Kirumi. Maono ya Yohana yaliwahakikishia waamini waliokuwa wanateseka kwamba Rumi (au nguvu yeyote ambayo inampinga Mungu) lazima itashindwa. Mungu, na si Kaisari, anadhibiti historia ya mwanadamu.

## Mazingira ya Kiyahudi ya Agano Jipya

### *Matarajio ya Kimasihi*

*Kristo* Kiyunani cha neno la Kiebrania kwa ajili ya neno *Masihi*. Makutano waliomfuata Yesu walikuwa wanamtafuta Masihi. Paulo alitangaza, “Yesu huyu ninayewapasha ninyi habari

zake ndiye Kristo" (Matendo ya Mitume 17:3). Matarajio ya kuja kwa Masihi yalifungua masikio ya watu kwa ajili ya ujio wa mahubiri ya Yesu.

### *Masinagogi*

Baada ya kuharibiwa kwa Hekalu mwaka 586 K.K., masinagogi yalikuwa sehemu ya kuabudu kwa ajili ya Wayahudi. Kila mkutaniko wa watu angalau wanaume 10, walikuwa na sinagogi. Sinagogi lilitumika kama sehemu ya ibada, shule, mahakama ya kidini na kisiasa, na kituo cha shughuli za kijamii. Yesu alihubiri ujumbe wake wa kwanza ulionakiliwa katika sinagogi (Luka 4:16-30), aliponya katika siangogi (Marko 3:1-5), na alifundisha katika sinagogi (Yohana 18:20).

Hata baada ya Koreshi kuruhusu Wayahudi kurudi nyumbani kwao, wengi walibaki Babeli; Iskanderia, Misri; na miji mingine ambayo walikuwa wamekimbilia baada ya kuanguka kwa Yerusalemu. Mtawanyiko huu ulikuwa muhimu kwa ajili ya kusambaa kwa Injili. Karibu kila mji ambao mitume walihubiri, walikuta sinagogi kwa ajili ya wakazi wa Kiyahudi.

Paulo alipotembelea mji mpya, alianza kwa kuhubiri katika sinagogi kwa waabudu wa Kiyahudi na waliojikita katika kumuhofu Mungu (Mataifa ambao walikuwa wanatafuta kweli).[12] Hawa Mataifa walikuwa wazi kwa ajili ya ujumbe wa Injili.

### *Makundi ya Kiyahudi ya Kidini*

Mafarisayo ("waliotengwa") walikuwa ni watu wa kidini waliokuwa maarufu sana wakati wa Yesu. Ingawaje walikuwa wachahe kwa idadi (takribani watu 6,000), walikuwa maarufu miongozi mwa watu. Waliheshimikwa kwa kuwa makini katika kufuata sheria za Musa. Kama Wakristo, Mafarisayo waliamini juu ya ufufuo na malaika na waliheshimu Agano la Kale. Hata hivyo, waliongeza simulizi-tamaduni nyingi katika sheria za Musa. Hata kama alitarajia ujio wa Masihi, Mafarisayo wengi walikataa madai ya Yesu kuwa Masihi.

Masadukayo walikuwa na nguvu ya kisiasa wakati wa Yesu. Kwa kushirikiana na Rumi, Masadukayo walipata udhibiti wa Ukuhani na wa baraza lote. Masadukayo walikubali *Tora Pekee* kama mamlaka ya mwisho (*Tora*, inamaanisha "sheria," ni neno la Kiebrania linalorejelea vitabu vitano vya Musa). Walikataa vitabu vya manabii na simulizi-tamaduni. Na matokeo yake, walikataa imani juu ya malaika, roho, na ufufuo (Matendo ya Mitume 23:8). Kwa sababu nguvu zao zilitokana na nafasi yao Hekaluni, Masadukayo walipotea baada ya uharibifu wa Hekalu mwaka 70 B.K.

## Desturi za Ulimwengu wa Agano Jipya

Kuelewa mila na desturi za ulimwengu wa Agamo Jipya unaweza kutusaidia sisi kuelewa vizuri ujumbe wa Agano Jipya. Mifano miwili inaelezea thamani ya kujifunza mila na desturi za Agano Jipya.

[12] Kwa mfano, ona Matendo ya Mitume 13:5.

**Mfano wa 1**

Familia nyingi za Kiyahudi waliishi katika nyumba yenye chumba kimoja. Wanyama waliwekwa katika chumba cha nje ya nyumba ambapo palikuwa na mtu aliyewalisha. Wakati Mariamu na Yusufu walipokuja Bethlehemu, pengine waliruhusiwa kukaa katika chumba cha nje, kwa sababu vyumba vya wageni vilikuwa vimejaa wakati wa sensa. Walioneshwa ukarimu wa hali ya juu uliostahili kwa wakati huu uliokuwa na shughuli nyingi.

**Mfano wa 2**

Wachungaji wa Kiyahudi mara nyingi waliruhusu makundi kadhaa ya kondoo kuchunga pamoja. Wakati wa kutenganisha kondoo ulipofika, kila mchungaji angewaita kondoo wake. Kondoo walifahamu sauti ya mchungaji wao. Yesu anasema kwamba "…kondoo humfuata, kwa maana waijua sauti yake. Mgeni hawatamfuata kabisa, bali watamkimbia; kwa maana hawazijui sauti za wageni" (Yohana 10:4-5).

Ili kupata taarifa nyingi za mila na desturi za ulimwengu wa Agano Jipya, unaweza kusoma *Manners and Customs of the Bible*, inapatikana mtandaoni.[13]

## Kuangalia kwa Ukaribu Mamlaka ya Agano Jipya

Je, tunaweza kuiamini mamlaka ya Agano Jipya? Mafundisho mengi potofu yanatokana na wale ambao wanakataa uadilifu wa Biblia au wale ambao wanadai kuwa wamepata chanzo kipya nje na Biblia. Mambo mawili ambayo ni muhimu kwa ajili ya uelewa wa mamlaka ya Agano Jipya:

1. **Kanoni**: Vitabu gani ni Neno la Mungu lililovuviwa?
2. **Uadilifu wa Kimaandishi**: Ni kwa kiasi gani maandiko yetu ni maaminifu kwa maandiko ya mwanzo ya asili?

### Kanoni: Vitabu Gani vya Biblia ni Neno la Mungu Lililovuviwa?

Kanoni ya maandiko ni suala muhimu kwa waamini. Linajibu swali, "Vitabu gani ni Neno la Mungu kwa watu wa Mungu?" Ni kwa namna gani tunafahamu kwamba vitabu vya Agano Jipya ni neno la Mungu kweli?

Neno *kanoni* linatokana na neno la Kiyunani linalomaanisha "kanuni" au "viwango." Kanoni ya Agano Jipya inajumuisha vile vitabu ambavyo vinafikia viwango vilivyotumiwa na kanisa la kwanza ili kutambua ni maandiko yapi ni neno la Mungu kweli. Utengenezaji wa Kanoni ulisababishwa na masuala mawili:

1. **Mafundisho Potofu**. Katika kanisa la kwanza, kama ilivyo leo, waalimu wa uongo wanakana sehemu za ufunuo wa kibiblia. Kwa mfano, katika karne ya pili, Marcion alifundisha kwamba Mungu wa Agano la Kale alikuwa mwovu. Ili kuunga mkono mafundisho yake, Marcion alikataa vitabu vyote vya Biblia ispokuwa maandiko ya

[13] Fred H. Wight. *Manners and Customs of the Bible,* (Chicago: Moody Press, 1953). Inapatikana mtandaoni katika https://archive.org/details/B-001-014-057/

Paulo na sehemu za Luka. Kukubaliwa kwa Kanoni ya pamoja lilikuwa ni jambo la muhimu ili kutoa msingi imara kwa ajili ya mafundisho. Waalimu wangekuwa na uhakika kwamba mafundisho wanayohubiri yalikuwa na msingi katika Neno la Mungu.

2. **Mateso**. Wakati wa mateso, wafusai wa Kristo wangeuawa kwa kuwa na maandiko ya kikristo. Walitakiwa kufahamu, "Ni vitabu gani ambavyo mimi nitakuwa tayari kufa kwa ajili yake?"

Hadi kufikia karne ya nne, kanisa la Kikristo lilikuwa limekubaliana juu ya orodha ya maandiko yaliyovuviwa ya kimungu. Waliweka viwango vitatu ili kujua ni vitabu gani ni maandiko. Ili kukubaliwa kuwa sehemu ya Kanoni ya Agano Jipya, kitabu kilitakiwa kufikia viwango vitatu:

1. **Mwandishi**. Mwandishi alikuwa mtume au mtu aliyekuwa karibu na mtume. Kwa habari ya uandishi wa Injili, Mathayo na Yohana walikuwa mitume; Marko alisafiri na Petro; Luka alisafiri na Paulo.
2. **Ujumbe**. Ujumbe wa kitabu lazima uwe:
   - Usiopingana na Agano la Kale.
   - Mwaminifu kwa ujumbe wa Yesu.
   - Wa kujenga kiroho.
3. **Kukubalika***.* Kitabu ni lazima kikubalike kama maandiko na kanisa lote. Vitabu vya Agano Jipya vilinukuliwa kwa wingi na mababa wa mwanzo wa kanisa.

Wapingaji wa nyakati za leo wamedai kwamba Kanon ilitengenezwa na mamlaka ya kanisa kama njia ya kupata nguvu. Upingaji wa namna hii unashindwa kutambua kwamba Kanoni ilikuwa ni kiwango kilichokubaliwa na wote; haikuwa matokeo ya matakwa ya maaskofu wachache. Kanoni ya Agano Jipya ilikubalika rasmi mwaka 397 B.K. Katika baraza la Carthage. Hata hivyo, vitabu vya Agano Jipya vilikuwa vimeorodheshwa na wanatheolojia miaka 200 kabla ya baraza.

Mwanatheolojia J. I. Packer aliandika, "kanisa halikutupa Kanoni ya Agano Jipya kama ambavyo Sir Isaac Newton kutupa sisi nguvu ya uvutano."[14] Newton hakugundua nguvu ya uvutano; aligundua kile ambacho tayari Mungu alikuwa amekiumba. Vivyo hivyo, kanisa halikugundua Kanon; kanisa liligundua vitabu ambavyo tayari Mungu alikuwa amevivuvia.

Baraza la Carthage lilihakiki kanoni kwamba ilikuwa tayari imekubaliwa katika nyumba yote ya Imani. Kanon ilijumuisha vitabu ambavyo waamini wa nyakati zote walikuwa wamekubaliana kwamba ni Neno la Mungu lililovuviwa.

**Vitabu vya Apokrifa** ni vitabu ambavyo vimekuwa vikidaiwa na kanisa la kwanza kuwa ni maandiko matakatifu ya Kikristo, lakini hayakutambuliwa na kanisa la kwanza kuwa ni maandiko. Katika karne ya pili, waandishi kama Tertullian na Irenaeus waliandika kinyume

[14] J. I. Packer, *God Speaks to Man.* (Westminster Press, 1965), 81

(dhidi) na mafundisho potofu ambayo yalikuwa yanafundishwa katika vitabu vya uongo. *Kanoni ya Muratorian*, orodha ya karne ya pili ya vitabu halisi vya Agano Jipya, ilivionesha vitabu vingine kuwa kwa uzushi au uongo ambavyo vilionekana kuwa ni vya mitume. Waraka wa Yuda unaonesha kwamba hata katika karne ya kwanza, ilikuwa ni muhimu kuishindania imani ambayo walikuwa wamekabidhiwa watakatifu (Yuda 1:3). Waalimu wa uongo tayari walikuwa "…wamejiingiza kwa siri…" (Yuda 1:4).

Baadhi ya vitabu vya Apokrifa ni maandiko mazuri ambayo yana thamani kwa ajili ya kuonesha matendo ya kanisa la kwanza. Vitabu vya Apokrifa vinavyoheshimika ni pamoja na *I Clement, Epistle of Barnabas, Didache,* na *Shepherd of Hermas.* Maandiko haya ni ya kiorthodox katika mafundisho yake, lakini hayakufikia viwango vilivyowekwa na kanisa la kwanza ili kujumuishwa katika Kanoni.

Vitabu vya Apokrifa ambavyo ni vya uzushi vinajumuisha *Gospel of Thomas*, maandishi ya Kinostiki ya karne ya pili ambayo kwa uongo yalihusianishwa na mtume Tomaso, *Epistle to the Laodiceans*, na *Apocalypse of Peter*. Maandiko haya hayakukubaliwa kwa sababu yalikuwa yanapinga kweli ya msingi ya Kikristo. Badala ya kukataliwa na baraza la Carthage, ni sahihi sana kusema kwamba kanisa kwa ujumla halijawahi kuvichulia vitabu hivi kama maandiko.

Maandiko ya kiapokrifa sio vyanzo halisi kwa ajili ya Waamini wa Kikristo. Imani yetu imejengwa juu ya "…imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu" (Yuda 1:3). Imani hiyo haijawahi kubadilika na haitabadilika. Imani yetu iko juu ya msingi imara wa neno la Mungu.

**Uadilifu wa Kimaandiko: Je, maandiko yetu ni maaminifu kwa maandiko ya asili/kwanza?**

Wapingaji mara nyingi wamesema kwamba Agano Jipya si la kuaminiwa. Wanadai kwamba makosa yaliingizwa wakati wa kunakili. Wapingaji hawa wanasisitiza kwamba hata kama maandiko ya kwanza yalivuviwa, hatuna njia ya kufahamu kama Biblia tuliyo nayo leo ni sahihi.

Je, tunaweza kuamini uadilifu wa kimaandiko wa Biblia yetu? Jibu kwa swali hili ni "Ndio!" ni kweli kwamba vitabu vya Agano Jipya vilisambazwa kwa kuandikwa kwa mfumo wa kuandikwa kwa mkono, na ni kweli kwamba makosa yanaweza kufanyika wakati wa kunakili maandiko kwa mkono. Hata hivyo, kwa sababu hili ni neno la Mungu lililovuviwa, waandishi walifanya kazi kwa umakini mkubwa. Wasomi waliyatoa maisha yao kwa ajili ya kunakili Agano Jipya kwa usahihi kwa kadiri ilivyowezekana.

Usahihi na mfanano ulionekana katika manuscripts (maandishi ya awali ambayo yalitumika ili kunakili maandiko kwenda sehemu nyingine) 5,000 ambazo zilikuwa na sehemu zote au sehemu kadhaa za Agano Jipya ni ushahidi tosha kwamba maandiko yetu walinakiliwa kwa umakini. Hakuna andiko lolote la kale lenye manuscript nyingi ili kuliunga mkono kama Agano Jipya.

| Ulinganifu wa Maandiko Mawili ya Kale | |
|---|---|
| **Agano Jipya** | ***Iliad* ya Homer** |
| Zaidi ya manuscripts 5,000 | Takriban manuscripts 1,800 |
| manuscripts za mwanzo ambazo bado zipo ni za chini ya miaka 100 baada ya kuandikwa | Manuscript za mwanzo ambazo bado zipo ni kutoka miaka 400 baada ya kutengenezwa kwa mara ya kwanza |
| Chini ya 0.5% ya maneno yana maswali ya aina yeyote* | 5% ya maneno hayana uhakika |
| **Unaamini Andiko lipi?** | |
| * Hakuna neno hata moja kati ya haya ambalo linaathiri masuala ya kimafundisho au kweli za kihistoria. Utofauti kati ya manuscripts unaonekana katika mistari kama Luka 10:1; baadhi ya manuscripts zinaonesha watendakazi 70 wakati nyingine zinaonesha watendakazi 72. Hakuna maswali kuhusiana na usahihi ambayo yanahusiana na ujumbe wa injili au mafundisho ya Kikristo. | |

## Hitimisho

Paulo aliandika katika Wagalatia 4:4, "Hata ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe ambaye amezaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria." Kifungu cha maneno "ulipowadia utimilifu wa wakati" kinamfanya msomaji afikirie kuhusiana na mama mjamzito ambaye yuko tayari kujifungua mtoto. Kwa wakati sahihi, Mungu alimtuma mwana wake katika ulimwengu ambao ulikuwa umetayarishwa na Mungu. Ulimwengu ulikuwa tayari:

- **Kijiografia**. Palestina ilikuwa sehemu ndogo ya ardhi katika njia panda ya utamaduni wa kale. Hili lilitengeneza jukwaa la kuanzia kwa ajili ya kusambaa kwa Injili ulimwenguni.
- **Kihistoria***.* Dola ya Rumi iliandaa mazingira tayari kwa ajili ya kusambaa kwa Injili.
- **Kitamaduni**. Mchanganyo wa lugha ya Kiyunani, mfumo wa kisiasa wa Kirumi, na tamaduni za kidini za Kiyahudi zilisaidia kutengeza mazingira kwa ajili ya kuzaliwa kanisa la Kikristo.

Mungu aliuandaa ulimwengu barabara ili kupokea Injili katika karne ya kwanza. Leo, anatenda kazi vile vile ili kuandaa watu kwa ajili ya Injili.

Unapomaliza somo hili, omba, "Mungu, ni nini unafanya ili kuuandaa ulimwengu wangu kwa ajili ya huduma ambayo umenipatia?"

**Somo la 1 Zoezi**

Mwanzoni mwa somo linalofuata, utafanya jaribio kulingana na somo hili. Soma maswali ya jaribio kwa umakini katika maandalizi.

**Somo la 1 Jaribio**

(1) Kutembea kutoka magharibi kwenda mashariki, orodhesha mikoa minne ya kijiografia ya Palestina.

(2) Kwa nini ni muhimu kwamba Yesu alisafiri kupitia Samaria ili kumuhudumia mwanamke pale kisimani?

(3) Orodhesha namna tatu ambazo lugha ya Kiyunani ilichangia katika kanisa la kwanza.

(4) Neno *pax Romana* linarejelea nini?

(5) Ni kwa njia gani Masinagogi ya Kiyahudi yalitumika?

(6) Ni imani gani ambayo Mafarisayo na Wakristo wanashiriki (inayofanana)?

(7) Ni sehemu gani ya Agano la Kale ambayo Masadukayo walikubali kama yenye mamlaka?

(8) Ni imani gani ambayo Masadukayo waliikataa?

(9) Ni masuala gani mawili yalipelekea kutengenezwa kwa kanoni?

(10) Orodhesha viwango vitatu vilivyotumika katikankutengeneza kanoni ya Agano Jipya.

(11) Ni swali gani tunalouliza tunapozingatia masuala ya Uadilifu wa kimaandishi?

(12) Andika Wagalatia 4:4-5 kutoka katika kumbukumbu.

# Somo la 2
# Mathayo, Marko, na Luka
# Maisha ya Kristo

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kuelewa sababu za kuwepo Injili nne.

(2) Kumfahamu mwandishi, makisio ya tarehe, na mazingira ya kihistoria ya Injili za kuona pamoja.

(3) Kutambua mada kuu katika kila Injili za kuona pamoja.

(4) kuhusianisha ujumbe wa Injili za kuona pamoja na mahitaji ya ulimwengu wa leo.

## Maandalizi kwa ajili ya Somo hili

► Soma Mathayo, Marko, na Luka.

► Kariri Mathayo 5:48, Marko 10:45, Luka 19:10.

## Injili za Kuona Pamoja

► Kwa nini tuna simulizi zaidi ya moja ya maisha ya Yesu?

Baada ya kupaa kupaa mbinguni, mitume waliandika simulizi za maisha ya Yesu ili kufundisha waamini wapya na kulinda dhidi ya simulizi potofu za maisha ya Yesu. Kwa kadiri kanisa lilivyokuwa linasambaa katika Dola ya Rumi, wachungaji na waalimu walihitaji simulizi yenye malmaka ya maisha na huduma ya Yesu. Hizi zilikuwa sababu muhimu za kuandikwa kwa Injili.

Injili tatu za kwanza zinaitwa Injili za kuona pamoja kwa sababu zinatoa nyanja na mtazamo tofauti tofauti juu ya matukio mengi yanayofanana. (Neno *Injili za kuona pamoja* linamaanisha "kuona pamoja" Injili.) wakati Injili ya Yohana inajumuisha nyenzo nyingi tofauti ambazo hazipatikani katika Injili zingine, Mathayo, Marko, na Luka zinashiriki nyenzo nyingi ambazo zinazofanana.

Waandishi wa Injili, mara nyingi huitwa "wainjilisti," hawakuwa makatibu wakinakili tu imla. Badala yake, Roho Mtakatifu kwa muujiza alifanya kazi kupitia utu na sifa za kila mwinjilisti ili kuwasilisha, pasipo makosa, ujumbe wa Mungu.

Mfano mmoja unaoonesha utofauti kati ya Injili. Mathayo anatoa simulizi ya kina kuhusiana na ushuhuda wa Petro kuhusu Uungu wa Yesu, baraka ya Yesu kwa Petro, na Petro

kumkemea Yesu (Mathayo 16:13-23). Marko na Luka wanatoa toleo fupi la habari (Marko 8:27-33, Luka 9:18-22). Marko anaondoa baraka ya Yesu kwa Petro, wakati Luka anaondoa vyote viwili baraka na habari ya Petro kumkemea Yesu. Hakuna utata au kukinzana katika habari; ni tukio moja ambalo linawasilishwa katika mitazamo mitatu tofauti.

| Mathayo 16:13-23 | Marko 8:27-33 | Luka 9:18-22 |
|---|---|---|
| "Simoni Petro akajibu akasema, Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai" | "Petro akamjibu, akamwambia, Wewe ndiwe Kristo." | "Petro akamjibu akasema, Ndiwe Kristo." |
| "Yesu akajibu, akamwambia, Heri wewe Simoni Bar-yona" | Haijajumuishwa | Haijajumuishwa |
| "Petro akamchukua, akaanza kumkemea, akisema, Hasha, Bwana, hayo hayatakupata" | "Petro akamchukua, akaanza kumkemea." | Haijajumuishwa |

Hakuna Injili moja inayoelezea habari yote ya maisha ya Yesu kikamilifu. Kimsingi, Yohana alisema, "Kuna na mambo mengi aliyoyafanya Yesu; ambayo yakiandikwa moja moja, nadhani hata ulimwengu usingetosha kwa vile vitabu vitakavyoandikwa" (Yohana 21:25). Injili si wasifu uliokamilika kikamilifu. Ispokuwa, Roho Mtakatifu alimvuvuia kila mwandishi kusisitiza nyanja tofauti za huduma ya Yesu. Kwa kusoma usuli wa kila Injili, tutaelewa kwa ufasaha uchaguzi wa nyenzo katika kila Injili. Kila mwandishi aliwaandikia wapokeaji tofauti na aliandika kwa makusudi tofauti.

## Mathayo

### Usuli (historia ya nyuma ya mambo) wa Mathayo

Injili ya Mathayo pengine iliandikwa kati ya mwaka 50 na 70 B.K. Dhamira kuu katika Mathayo ni utimilifu wa unabii. Kwa sababu Mathayo hataji utimilifu wa unabii wa Yesu kuhusiana na kuharibiwa kwa hekalu (Mathayo 24:2), inawezekana kwamba Injili ya Mathayo imeandikwa kabla ya 70 B.K.[15]

Sifa mbalimbali zinaonesha kwamba Injili ya Mathayo kwa asili ilikelekezwa kwa wapokeaji wa Kiyahudi:

- Mathayo haelezei mila za Kiyahudi.

[15] Unabii ulitimizwa mwaka 70 B.K. wakati ambapo jenerali wa Kirumi Tito alipoushinda Yerusalemu. "Sanamu ya Tito," alisheherekea ushindi juu ya Yerusalemu, bado unasimama huko Rumi.

- Mathayo ananukuu Agano la Kale mara nyingi kuliko waandishi wengine wa Injili wanavyo nukuu.
- Mathayo anaweka umakini wa kipekee kwa Yesu kutimiliza unabii wa Agano la Kale.
- Mathayo anatumia sana kifungu cha maneno "ufalme wa mbinguni." Tofauti na Mathayo, Marko na Luka wanatumia kifungu cha maneno "ufalme wa Mungu." Maneno ya Mathayo yanaakisi ugumu wa Wayahudi kutumia jina la Mungu.

**Mada kuu za Mathayo**

► Ni kwa namna gani Mathayo anaonesha kwamba Yesu ni mfalme?

***Yesu ni Mfalme***

Mathayo mara nyingi huitwa "Injili ya Mfalme." Katika Mathayo yote, Yesu ameoneshwa kama Mfalme wa Wayahudi na, juu ya yote, wa mataifa. Mamajusi walisafiri kutoka Mashariki wakitambua kuzaliwa kwa mfalme mpya. Herode alitaka kumharibu mfalme huyu pinzani. Katika Mathayo, Yesu anaonekana kama mfalme.

Mathayo anatumia kifungu cha maneno "Mwana wa Daudi" mara nyingi kuliko Injili nyingine. Hili ni jina la Kifamle, likionesha kwamba Yesu yuko katika ukoo wa Daudi. Jina hili lilitumika wakati Yesu alipopanda punda kuingia Yerusalemu, kuingia kifalme ambako kunatimiliza Zekaria 9:9 (Mathayo 21:4-5, 9).

Yesu anafundisha sheria mpya ya ufalme katika Mahubiri yake juu ya mlima (Mathayo 5-7). Anafundisha kuhusiana na ufalme wa mbinguni kupitia mlolongo wa mifano (Mathayo 13). Juu ya yote maandishi katika msalaba wake, "HUYU NI YESU, MFALME WA WAYAHUDI" (Mathayo 27:37). Mathayo ni Injili ya Mfalme.

***Yesu kama Utimilifu wa Agano la Kale***

Mathayo anarejelea utimilifu wa unabii katika maisha ya Yesu mara 11. Nabii zilizo orodheshwa katika Mathayo zinajumuisha:

- Yesu kuzaliwa na bikira (Mathayo 1:22-23).
- Safari kwenda Misri (Mathayo 2:15).
- Herode kuuwa watoto (Mathayo 2:17-18).
- Huduma ya Yesu ya uponyaji (Mathayo 8:17).
- Yesu kuingia Yerusalemu kwa ushindi (Mathayo 21:4-5).
- Vipande 30 vya fedha kwa ajili ya kusalitiwa kwake (Mathayo 27:9-10).

***Mahubiri ya Yesu***

Mathayo alitunza mafundisho mengi ya Yesu kuliko waandishi wa Injili zingine. Wakati Marko anaweka umakini juu ya matendo ya Yesu, Mathayo anaweka umakini katika maneno ya Yesu. Kuna mfundisho makuu matano katika Mathayo, ambayo yanatoa muundo mzima wa Injili. Wafafanuzi wa mwanzo waligundua kwamba kama ambavyo vitabu vitano vya

Musa vilivyoweka msingi kwa ajili ya Israeli, mahubiri haya matano yameweka msingi kwa ajili ya kanisa. Mahubiri makuu matano katika Mathayo ni:

- Mahubiri ya mlimani (Mathayo 5-7).
- Kuwatuma mitume kumi na mbili (Mathayo 10).
- Mifano ya ufalme (Mathayo 13).
- Mafundisho juu ya mahusiano katika ufalme (Mathayo 18).
- Mafundisho juu ya Mlima wa Mizeituni kuhusiana na mwisho wa wakati (Mathayo 24-25).

**Mathayo katika Kanisa Leo**

Mahubiri katika Injili ya Mathayo huzungumza kwa kanisa leo kwa nguvu ile ile kama wakati Yesu alipoyahubiri alipokuwa Galilaya na Uyahudi.

> "'Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.' Alijua fika namna kutoamini kwetu kutakuwa na kulia kwa sauti , 'Hili haliwezekani!' Na kwa hiyo, akaweka juu yake nguvu zote, kweli, na uaminifu wake kwa yeye ambaye yote yanawezekana."
>
> - Imechukuliwa kutoka John Wesley *Notisi juu ya Agano Jipya*

Mahubiri ya mlimani yanatoa muhtasari kamilifu wa maisha katika ufalme wa Mungu. Kwa kuonesha utofauti kati ya tamaduni za Mafarisayo na sheria ya upendo, Yesu alifundisha namna ya kuishi kama raia wa ufalme wa mbinguni. Mada kuu ya mahubiri ya mlimani ni "Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu" (Mathayo 5:48). Agizo hili linakuja katika muktadha likionesha kwamba Baba yetu ni Mungu wa Upendo. "…yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki" (Mathayo 5:45). Kuwa mkamilifu katika ufalme wa Mungu inamaanisha kuwa na moyo wa Baba yetu wa mbinguni, moyo wenye upendo usio wa kibinfasi. Ingawaje moyo wenye upendo usio wa kibinafsi hauwezekani kwa nguvu zetu za kibinadamu, Baba yetu wa mbinguni ambaye anatuagiza sisi kuwa na moyo mkamilifu ni Mungu ambaye atafanya hili liwezekane kupitia neema yake.

Mafundisho ya Yesu juu ya mahusiano katika ufalme wa Mungu yanatoa mfano wa mahusiano katika kanisa leo (Mathayo 18). Mathayo 18:15-20 ni mwongozo kwa ajili ya nidhamu ya kanisa kibiblia ambapo dhambi inashughulikiwa kupitia kanisa, na si kupitia kusengenya na tetesi. Adabu hii inatekelezwa katika muktadha unaotoa msamaha na urejesho, kanuni ambayo inaonekana katika jibu la Yesu kwa swali la Petro kuhusiana na msamaha (Mathayo 18:21-35).

Agizo kuu linatuita sisi kufanya mataifa yote kuwa wanafunzi (Mathayo 28:18-20). Kama agizo la Yesu la kuwa wakamilifu, tutautimiza wito huu si kwa nguvu zetu, bali kwa nguvu za yeye aliyetupa agizo. Yeye aliyetoa wito ndiye aliyeahidi, "…mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari" (Mathayo 28:20).

## Marko

### Usuli wa Marko

> “Kama Petro alihubiri Neno kwa wazi kule Rumi, wengi wanaona kwamba Marko, ambaye alimfuata kwa muda mrefu na akakumbuka misemo yake, lazima ataiandika."
>
> - Clement wa Iskanderia
> nukuu katika Eusebius,
> *Historia ya Kanisa* 6.14.5-7

Yohana Marko alikuwa binamu wa Barnaba, ambaye alisafiri pamoja na Paulo na Barnaba katika safari yao ya kwanza ya kimisheni (Wakolosai 4:10, Matendo ya Mitume 12:25). Ingawaje kushindwa kwake kulisababisha mgogoro kati ya Paulo na Barnaba, Yohana Marko baadae aliaminiwa na Paulo na akawa mtumishi mzuri kwa huduma yake (Matendo ya Mitume 15:36-40, 2 Timotheo 4:11).

Mababa wa mwanzo wa kanisa wanamtambulisha Simoni Petro kama chanzo cha kitume cha Marko. Wanasema kwamba Marko aliandika kumbukumbu ya Petro mara baada ya Petro kuuawa kama mfia imani. Kama ni hivyo, hii inamaanisha kwamba Injili ya Marko iliandikwa kati kati au mwishoni mwa mwaka 60. Wakati Injili haitaji kwa uwazi kwamba Petro alikuwa chanzo, tunafahamu kwamba Yohana Marko alifanya kazi kwa ukaribu sana na Petro kiasi kwamba Petro alimrejelea kama “mwanangu” (1 Petro 5:13). Injili ya Marko inarekodi kumbukumbu za Petro kuhusiana na huduma ya Yesu.

Matukio katika Marko mara nyingi hayafuati mititiko wa matukio katika Mathayo na Luka. Itasaidia kufahamu kwamba Askofu Papias, kama baba wa mwanzo wa kanisa, alimnukuu Mtume Yohana akisema kwamba Marko kwa usahihi alirekodi kwamba Petro alikumbuka kile ambacho Bwana alisema na alifanya lakini si katika mfululizo wa matukio.[16] Habari za Marko ni sahihi, lakini hakujaribu kuyaweka matukio katika mfululizo wa kina wa matukio.

Injili ya Marko pengine iliandikwa kutoka Rumi na kimsingi ilielekezwa kwa wasikilizaji wa Kimataifa. Marko mara nyingi anaelezea maneno ya Kiaramaiki yaliyotumiwa na Yesu.[17] Kwa nyongeza, Marko anaelezea maneno ya Kiyahudi kwa wasomaji wake wa Kirumi. Kwa mfano katika Marko 12:42, anaelezea kwamba sarafu mbili ndogo za shaba (sarafu za Kiyahudi) zinatengeneza peni moja (sarafu ya Kirumi).

Marko ndio Injili fupi, ikiwa na taarifa chache zaidi ukilinganisha na Injili zingine. Marko ni Injili ya matendo, sifa ambayo inaakisi ushawishi wa Petro. Ni rekodi iliyonyooka ya maisha na huduma ya “…Yesu Kristo, Mwana wa Mungu” (Marko 1:1).

### Mada Kuu za Marko

► Kwa namna gani Injili ya Marko ni tofauti na ya Mathayo?

---

[16] Eusebius, Historia ya Kanisa, *(Ecclesiastical History*, 3.39.14-17.)

[17] Kiaramaiki kilikuwa ni lugha ya kawaida iliyotumiwa katika Palestina wakati wa karne ya kwanza, ikiwa ni mbadala wa Kiebrania. Mifano ya melezo ya Marko akielezea maneno ya kiaramaiki ni pamoja na Marko 5:41, Marko 7:11, na Marko 14:36.

### *Yesu ni Mtumishi*

Marko mara nyingi huitwa "Injili ya Mtumishi." Marko anaweka umakini katika matendo ya Yesu kuliko maneno yake. Ikitofautiana na Mahubiri matano makuu ya Mathayo, Marko anajumuisha mahubiri moja tu (Marko 13). Injili ya Marko hutoa umakini mkubwa katika miujiza; Marko ananakili miujiza 19 katika kitabu kifupi cha sura 16.

Mstari mkuu katika Injili ya Marko unaonesha nyanja mbili za huduma ya Yesu ya ulimwenguni: "Kwa maana Mwana wa Adamu naye hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi" (Marko 10:45). Yesu alikuja kutumika na kuyatoa maisha yake kama sadaka.

### *Yesu Mwana wa Mungu*

Marko anaanza na tamko la uungu wa Yesu, "Mwanzo wa Injili ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu" (Marko 1:1). Msalabani, akida wa Kirumi alikiri, "Hakika mtu huyu alikuwa Mwana wa Mungu" (Marko 15:39).

Marko anaonesha kwamba Yesu alikuwa mtumishi, lakini pia alionesha mamlaka ya Yesu kama Mwana wa Mungu. Msomaji wa Kirumi angetegemea kiongozi wa kiroho aoneshe nguvu juu ya ulimwengu huu. Marko anaonesha hilo katika namna mbalimbali. Katika Injili yote, Marko amejumuisha ushuhuda wa uungu wa Yesu:

- Wakati wa kubatizwa, Baba alishuhudia, "Wewe ndiwe Mwanangu, mpendwa wangu; nimependezwa nawe" (Marko 1:11).
- Wakati wa Kugeuka sura, Baba alitangaza, "Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, msikieni yeye" (Marko 9:7).
- Mapepo yalimtambua Yesu kama "…Mtakatifu wa Mungu" (Marko 1:25) na "…Mwana wa Mungu" (Marko 3:11, Marko 5:7).
- Yesu alionesha mamlaka ambayo ni ya Mungu aliposamehe dhambi (Marko 2:5) na alipodai kuwa na mamlaka juu ya Sabato (Marko 2:28).
- Miujiza ya Yesu ilionesha mamlaka yake juu ya asili (Marko 4:39, Marko 6:47-48), magonjwa (Marko 5:27-30, Marko 7:32-37), na hata kifo (Marko 5:38-42).

### *Siri ya Kimasihi*

Marko anarekodi mahali mbalimbali ambapo Yesu anawaagiza watu au roho chafu kunyamaza na kutokusema kile ambacho wanafahamu kuhusiana na Yesu alikuwa nani au kile alichokifanya. Hii imekuja kufahamika kama siri ya kimasihi.

1. **Roho chafu**, ambao walifahamu kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu, hawakuruhusiwa kuzungumza (Marko 1:34, Marko 3:11-12). Yesu hakutaka mahusiano yeyote na mapepo.

2. Yesu aliwaambia **baadhi ya wale aliowaponya** wasiozungumze kuhusiana na kile ambacho amewafanyia (Marko 1:44, Marko 5:43, Marko 7:36). Uponyaji wa Uponyaji wa kimwili hauukuwa kipaumbele cha huduma ya Yesu ya hapa duniani. Badala yake, Yesu aliweka umakini katika kuwafundisha wanafunzi kusambaza Injili na kujenga kanisa. Mwenye ukoma alipokiuka agizo la Yesu na kutangaza kuhusiana na nguvu yake ya uponyaji, watu wengi walikusanyika hata "Yesu asiweze tena kuingia mjini kwa wazi; bali alikuwako nje mahali pasipokuwa na watu" (Marko 1:45).

3. Ingawaje **Wanafunzi** walifahamu Yesu ni nani, hakuwaruhusu wao kuwaambia wengine (Marko 8:29-30). Hata baada ya Petro kushuhudia kwamba Yesu alikuwa Masihi, wanafunzi hawakuelewa kikamilifu kwa nini Yesu alikuja (Marko 9:31-32). Wakati baadhi ya wanafunzi walipoona utukufu wa Yesu, aliwaambia wasiwaambie wengine kuhusiana na uzoefu walioupata hadi wakati wa baada ya ufufuo (Marko 9:9-10).

### Marko katika kanisa leo

Kipaumbele cha huduma katika huduma ya Yesu kinatukumbusha sisi kwamba tunapokutana na mahitaji ya kimwili na kihisia ya ulimwengu wetu, tunapata fursa ya kuwahudumia watu kiroho. Wafuasi wa Kristo katika Dola ya Rumi walihatarisha maisha yao kwa ajili ya wale waliokuwa wanakufa katika miji iliyokumbwa na majanga. Waamini katika nyakati wa kati walianzisha hospitali ili kusaidia wenye ukoma na masikini. Taasisi za kikristo leo zinavalisha yatima, zinatembelea magerezani, zinalisha wenye njaa, na kujali wagonjwa. Huduma kwa eneo lenye uhitaji zaidi katika jamii zetu inatakiwa mara zote kuwa sehemu ya umisheni wa kanisa. "Kwa maana Mwana wa Adamu naye hakuja kutumikiwa, bali kutumika..." (Marko 10:45).

## Luka

### Usuli wa Luka

Mamlaka ya Luka kama mwandishi wa Agano Jipya yanatoka kwa ushirika wake na Mtume Paulo. Luka alikuwa ni msomi mmataifa aliyejulikana sana, tabibu ambaye alisafiri na Paulo na alikuwa na Paulo karibu na mwisho wa maisha yake. Baadhi ya sehemu za Matendo ya Mitume zinaonesha uwepo wake; Luka alibadili kutoka kwa "wa-" kwenda kwa "tu-" alipokuwa anaandika kuhusiana na matukio ambayo yalitokea wakati alipokuwa na Paulo.[18]

Tarehe ya kuandikwa Injili ya Luka ina msingi mkubwa katika mahusiano yake na kitabu cha Matendo ya Mitume. Injili ya Luka ni mwanzo wa simulizi ambayo inaendelea katika kitabu cha Matendo ya Mitume. Kwa msingi wa hitimisho kutoka katika kitabu cha Matendo ya Mitume, inaweza kukisiwa kwamba Matendo ya Mitume kiliandikwa wakati fulani kabla

[18] Sehemu ya Matendo ya Mitume ambayo yanaonesha uwepo wa Luka katika kundi ni Matendo ya Mitume 16:10-17, Matendo ya Mitume 20:5-21:18, Matendo ya Mitume 27:1-28:16.

ya mateso ya Nero kuanza mwaka 64 B.K.[19] Hii inamaanisha kwamba Luka pengine kiliandikwa mwishoni mwa miaka ya 50 au mwanzoni mwa miaka ya 60.

Wapokeaji wa Luka na kusudi la kuandikwa linatambulishwa katika utangulizi (Luka 1:1-4). Luka anamwandikia Theofilo, pengine Afisa wa Kirumi. Luka 1:4 inaonesha kwamba Theofilo alikuwa mwamini mpya ambaye amefundishwa kuhusiana na maisha ya Yesu. Waamini wapya, hasa hasa Wamataifa, walipewa miezi kadhaa ya mafundisho kuhusiana na maisha ya Yesu, maisha mapya ya mwamini, na mafundisho ya Kanisa la Kikristo. Luka iliandikwa kuonesha msingi wa kihitoria wa kile ambacho Theofilo alikuwa amefundishwa.

**Mada Kuu za Luka**

► Taarifa gani za Luka zinasisitiza ili kuonesha uanadamu wa Yesu?

***Yesu Mwana wa Adamu***

Kanuni ya Imani ya Kalkedoni iliandikwa mwaka 451 B.K ili kuweka wazi mafundisho ya kanisa kuhusiana na asili ya Kristo: Yesu ni Mungu halisi na mwanadamu halisi. Kristo alikuwa na asili mbili (uungu na uanadamu), zikiwa ndani ya mtu mmoja. Yeye ni "kamili katika uungu na pia kamili katika uanadamu; Mungu halisi na Mwanadamu halisi."[20] Luka anatupa mifano ya picha halisi ya uanadamu wa Yesu, "kamili katika uanadamu."

Luka anaonesha kwamba Yesu alikuwa mwanadamu kamili. Anatoa taarifa ya kuzaliwa kwa Yesu (Luka 2:1-39). Wakati kuchukuliwa mimba kulikuwa kwa muujiza, Yesu alizaliwa kawaida kama mtoto mchanga. alikuwa mwanadamu kamili.

Kitabu cha ukoo kama kilivyoandikwa na Mathayo, kimsingi kiliwalenga Wayahudi, kikiufuatilia ukoo wa Yesu nyuma hadi kwa Ibrahimu. Kitabu cha ukoo wa Yesu kama kilivyoandikwa na Luka, kikielekezwa kwa wapokeaji wa Kiyunani na kikimuonesha Yesu kama Mwana wa Mwanadamu, kikifuatilia ukoo wa Yesu nyuma hadi kwa Adamu (Luka 3:23-38).

Mfuatano wa sura za kwanza za Luka zinaonesha kusudi lake la kumuonesha Yesu kama Adamu wa pili. Badala ya kuanza na kitabu cha ukoo wa Yesu kama Mathayo alivyofanya, Luka anaweka ukoo wa Yesu baada ya maelelezo ya ubatizo. Ukoo unaishia na "…mwana wa Adamu, Adamu alikuwa mwana wa Mungu" (Luka 3:38 NENO). Hii inafuatiwa mara moja na maelelezo ya majaribu ya Yesu. Adamu wa kwanza (aliishi katika bustani nzuri) alianguka katika jaribu; Adamu wa pili (akidhoofishwa na siku 40 pasipo chakula na akiwa peke yake jangwani) alishinda majaribu. Kama mwanadamu, Yesu alikuwa mfano wa kuigwa kwa kila mwamini anayepitia majaribu. Yesu alionesha kwamba tunapaswa kukabiliana na

Katika Matendo ya Mitume 28:30, Paulo alikuwa chini ya nyumba ya kifungo lakini hakuwa katika hataru kwa ajili ya maisha yake.

[20] "Kanuni ya Imani ya Kalkedoni (451 B.K.)," Utetezi wa Kikristo wa Imani na Huduma ya Utafiti Ministry, ilipatikana Januari 23, 2025, https://carm.org/creeds-and-confessions/chalcedonian-creed-a-d-451/

mashambulizi ya Shetani kwa nguvu za Roho Mtakatifu (aliyepatikana kupitia maombi) na Maandiko (Luka 4:1-13).

Katika Injili yote, Luka anaonesha nyanja za kimwili za maisha ya Yesu duniani: njaa (Luka 4:2), kulala (Luka 8:23), na uchungu wake Gethsemane (Luka 22:44). Yesu alikuwa mwanadamu kamili.

### *Yesu Mwokozi wa Ulimwengu*

Injili ya Luka inaonesha kwamba Yesu alikuja kama mwokozi wa wanadamu wote. Simeoni aliongea kuhusu Yesu kama "Nuru ya kuwa mwangaza wa Mataifa…" (Luka 2:32).

Shahuku ya Luka ya kumuonesha Yesu kama mwokozi wa ulimwengu wote inaonekana katika umakini wake kwa wale ambao walikuwa hawana nafasi/daraja lolote katika jamii. Mathayo anawaonesha mamajusi, wasomi walioheshimika kutoka mashariki, wakiheshimu kuzaliwa kwa Yesu; Luka anawaonesha wachungaji (Luka 2:15-20). Wachungaji walikuwa hawana mamlaka na wasingetegemewa kama mashahidi; ushuhuda wao usingekubaliwa katika mahakama ya Kiyahudi. Luka analenga tangazo la malaika kwa wachungaji kama ushuhuda kwamba Yesu alikuja kwa watu wote.

Wanawake, kundi lingine ambalo lilikuwa na nafasi/daraja la chini sana wakati wa Yesu, walifanya kazi kubwa katika Injili ya Luka. Ana, nabii mke, alisimama pembeni ya Simeoni katika kumuweka wakfu Yesu kule Hekaluni (Luka 2:36-38). Yesu alimruhusu Mariamu kukaa katika miguu yake pamoja na wanafunzi wanaume (Luka 10:39). Kwa mshangao, wanawake walikuwa wafadhili rasmi wa kifedha wa huduma ya Yesu (Luka 8:1-3).

Makundi mengine mengi ya nafasi ya chini katika jamii waliwasilishwa katika Luka. Yesu alitembelea nyumba ya Zakayo, mtoza ushuru (Luka 19:1-10). Watoza ushuru walikuwa mojawapo ya makundi yaliyotiliwa shaka katika Palestina ya Karne ya kwanza. Yesu alitoa mfano ambapo shujaaa alikuwa Msamaria (Luka 10:25-37). Na baadae alimponya Msamaria mwenye ukoma (Luka 17:11-16). Msalabani, Yesu alionesha huruma kwa mwizi asiyestahili chochote bali hukumu (Luka 23:39-43).

### *Umuhimu wa Maombi*

Luka anaonesha kwamba maombi yalikuwa muhimu katika maisha ya Yesu. Katika rejea 15 mahususi za maombi ya Yesu katika Injili, 11 zinapatikana katika Luka. Alipokuwa anafanya maamuzi makubwa, Yesu aliutoa usiku mzima kwa ajili ya maombi (Luka 6:12). Mifano miwili muhimu ya Yesu kuhusiana na maombi imenakiliwa katika Luka 18. Mifano hii inafundisha kuhusiana na kutokukata tamaa na unyenyekevu katika maombi (Luka 18:1-8, Luka 18:9-14). Maombi ni mada muhimu katika Luka.

### *Kazi za Roho Mtakatifu*

Injili ya Luka inatoa umakini mkubwa kuhusiana na kazi ya Roho Mtakatifu katika maisha ya Yesu na wengine. Mada hii inaendelea katika kitabu cha Matendo ya Mitume, ambapo Luka anaonesha jukumu la Roho Mtakatifu katika kanisa la kwanza.

Luka mahususi kabisa anataja kuhusika kwa Roho Mtakatifu katika maisha ya Yesu katika nyakati hizi:

- Yesu alichukuliwa mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu (Luka 1:35).
- Roho Mtakatifu alikuja juu ya Yesu katika ubatizo wake (Luka 3:21-22).
- Roho Mtakatifu alimuongoza Yesu hadi jangwani ili kujaribiwa (Luka 4:1-2).[21]
- Roho Mtakatifu alimtia nguvu Yesu alipokuwa anarudi Galilaya (Luka 4:14).
- Yesu alifurahia katika Roho Mtakatifu (Luka 10:21).

Luka pia anazungumza kuhusu Roho Mtakatifu katika mazingira haya:

- Yohana Mbatizaji, Elizabeti, na Zekaria kila mmoja alijazwa na Roho Mtakatifu (Luka 1:15, 41, 67).
- Roho Mtakatifu alikuwa juu ya Simeoni ambaye alingojea kumwona Bwana Kristo (Luka 2:25-27).
- Yohana Mbatizaji aliahidi kwamba Yesu angebatiza kwa Roho Mtakatifu (Luka 3:16).
- Yesu alisema kwamba Baba wa Mbinguni atawapatia Roho Mtakatifu wao wamwombao (Luka 11:13).

**Luka Katika Kanisa Leo**

Kwa ulimwengu wa leo wenye mashaka, umakini wa Luka katika taarifa za kina unatoa ushuhuda wenye nguvu kwa kweli ya Maandiko. Luka anaweka mwanzo wa kuanza kwa huduma ya nje ya Yesu katika muktadha ambao unaonesha umakini katika taarifa zake za kina:

> Mwaka wa kumi na tano wa kutawala kwake Kaisari Tiberio, Pontio Pilato alipokuwa liwali wa Uyahudi, na Herode mfalme wa Galilaya, na Filipo, ndugu yake, mfalme wa Iturea na nchi ya Trakoniti, na Lisania mfalme wa Abilene, wakati wa ukuhani mkuu wa Anasi na Kayafa… (Luka 3:1-2).

Tunapomuwasilisha Kristo katika ulimwengu huu wenye mashaka, tunaweza kuhubiri tukiwa na ujasiri. Imani yetu sio imani mfu katika mtu wa kidini wa kufikirika. Imani yetu ina misingi katika mtu wa kihistoria, Mwana wa Mungu aliyefanyika mwili ambaye aliishi katikati yetu, akafa kwa ajili ya dhambi zetu, na akafufuka siku ya tatu, na akapaa mbinguni na ameketi mkono wa kuume wa Mungu Baba.

Kazi ya maombi katika maisha ya Yesu ulikuwa mfano wa kuigwa kwa kila mfuasi wake. Kama Yesu, ambaye hakujua dhambi yeyote na ambaye alikuwa na mahusiano ya karibu na Baba yake, aliona umuhimu wa maombi, ni kwa kiasi gani sisi tunaona maombi kama

[21] Mathayo 4:1 inataja moja kwa moja kusudi hili.

kipaumbele katika maisha yetu? Mwinjilisti Leonard Ravenhill aliandika, "Hakuna mtu ambaye ni mkuu kuliko maisha yake ya maombi. Mchungaji asiyeomba anacheza…."[22]

Mwisho, kama ambavyo Roho Mtakatifu alikuwa muhimu katika huduma ya Yesu, Roho Mtakatifu anapaswa kuwa kitovu cha maisha ya kanisa leo. Historia ya kanisa inaonesha hatari mbili kuhusiana na Roho Mtakatifu. Hatari moja ni kusisitiza wajibu wa Roho Mtakatifu kwa kuziacha nafsi nyingine za Utatu.

Hatari inayokinzana na hiyo ni kuufanya wajibu wa Roho Mtakatifu kuwa mdogo sana katika kanisa. A. W. Tozer anaonya kwamba kanisa linauwezo wa kuruhusu " nguvu bandia ya bei rahisi kuwa mbadala wa nguvu ya Roho Mtakatifu."[23] Hivi karibuni, Francis Chan alionya: "Kanisa halitakuwa na maana endapo litakuwa limetengenezwa kibinadamu. Hatutakuwa kama tulivyokusudiwa kuwa endapo kila kitu katika maisha na makanisa yetu yataweza kuelezewa nje na kazi na uwepo wa Roho wa Mungu."[24]

Kitabu cha Matendo ya Mitume kinaonesha umuhimu wa Roho Mtakatifu ndani ya kanisa; kitabu cha Luka kinaonesha umuhimu wa Roho Mtakatifu katika maisha ya mtu binafsi. Yesu alitegemea uongozi na nguvu za Roho Mtakatifu katika huduma yake ya hapa duniani; hatupaswi kuruhusu nguvu bandia na ya bei rahisi kuwa mbadala wa nguvu ya Roho Mtakatifu katika kanisa leo.

## Hitimisho

Thomas Linacre alikuwa profesa wa chuo kikuu cha Oxford na tabibu wa kibinafsi wa mfalme Henry wa VIII. Baada ya kusoma Injili kwa mara ya kwanza, aliandika katika shajara yake, "Ama hii sio Injili, au sisi sio Wakristo." Linacre alitambua kwamba maisha ya mwamini wa kweli yanabadilishwa na Yesu Kristo. Alipolinganisha maisha yake na maisha ya wale wanaodai kuwa wanamfuata Kristo kwa picha ya Yesu inayotolewa katika Injili, Linacre alitambua, "Tunadai kuwa Wakristo, lakini hatuoneshi sura ya Yesu Kristo."

Kutoka mahubiri ya Mathayo juu ya ufalme, kwenda kwa picha ya Marko ya utumishi wa Yesu kwa wahitaji, kwenda kwa msisitizo wa Luka juu ya Roho Mtakatifu, Injili zinatoa taswira ya huduma ya Yesu Kristo. Kupitia hii, Injili zinaonesha ina maana gani kuwa Mkristo. Tunaposoma Injili, tunapaswa kujiuliza sisi wenyewe, "Je, ninaishi maisha ambayo yanaakisi neema ya Yesu Kristo inayobadilisha maisha?"

---

[22] Leonard Ravenhill, *Why Revival Tarries,* (Minneapolis: Bethany House Publishers, 2004), 25. Inapatikana mtandaoni katika: https://archive.org/details/whyrevivaltarrie0000rave/page/25

[23] A. W. Tozer. *Of God and Men* (Chicago, IL: Moody Publishers, toleo lililotumiwa tena, 2015)

[24] Francis Chan. *Forgotten God: Reversing Our Neglect of the Holy Spirit* (Colorado Springs, CO: David C Cook, 2009)

## Somo la 2 Mazoezi

(1) Chagua mawili kati ya mazoezi yafuatayo:

- Andaa ujumbe au somo la Biblia juu ya mfano mmojawapo wa Yesu. Unaweza kuwasilisha hii ama katika maandishi (kurasa 5-6) au wasilisha rekodi ukiwa unahubiri au kufundisha.
- Andaa ujumbe au somo la Biblia juu ya umuhimu wa ama kusulubiwa au ufufuo katika maisha ya Mkristo. Unaweza kuwasilisha hii ama katika maandishi (kurasa 5-6) au wasilisha rekodi ukiwa unahubiri au kufundisha.
- Andaa mstari wa muda wa matukio makuu katika wiki ya mwisho ya maisha ya Yesu hapa duniani. Wiki hii imenakiliwa katika Mathayo 21-28, Marko 11-16, Luka 19-24, na Yohana 12-21. Unaweza kuwasilisha mstari wako wa muda wa matukio katika karatasi au katika mfumo wa kidigitali.
- Chora ramani ya Palestina ukionesha kila mkoa na mji ufuatao: Uyahudi, Galilaya, Samaria, Dekapoli, Yerusalemu, Nazareti, na Kaisaria-Filipi.

(2) Mwanzoni mwa somo linalofuata, utafanya jaribio kulingana na somo hili. Soma maswali ya jaribio kwa umakini katika maandalizi.

## Somo la 2 Jaribio

(1) Kwa nini Injili tatu za kwanza zinaitwa Injili za kuona pamoja?

(2) Gani zinaonesha kwamba Injili ya Mathayo kwa asili ilikelekezwa kwa wapokeaji wa Kiyahudi?

(3) Orodhesha mada kuu tatu katika Mathayo.

(4) Orodhesha mada kuu tatu katika Marko.

(5) Ni makundi gani matatu waliohusika katika Siri ya Kimasihi? Kwa nini Yesu aliwaagiza kila mmoja kuwa kimya?

(6) Luka alikuwa nani?

(7) Luka 1:4 inaonesha nini kuhusiana na Theofilo?

(8) Orodhesha mada kuu nne katika Luka.

(9) Kanuni ya Imani ya Kalkedoni inafundisha nini kuhusiana na asili ya Yesu?

(10) Luka anajumuisha habari nyingi kuhusiana na watu ambao hawakuwa au walikuwa na nafasi ndogo/ya chini ya kijamii. Taja makundi matatu yeyote au watu watatu waliotajwa katika somo hili.

(11) Kutoka Luka, taja mifano mitatu ya kuhusika kwa Roho Mtakatifu katika maisha ya Yesu.

(12) Andika Mathayo 5:48, Marko 10:45, na Luka 19:10 kutoka katika kumbukumbu.

# Somo la 3
# Yohana
# Injili ya Kuamini

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kufahamu mwandishi, tarehe, na mazingira ya kihistoria ya injili ya Yohana.

(2) Kutofautisha Injili ya Yohana na Injili za Kuona Pamoja.

(3) Kutambua dhamira na kusudi la Injili ya Yohana.

(4) Kuthamini umuhimu wa vyote viwili uanadamu na uungu wa Yesu.

(5) Kuhusianisha ujumbe wa Injili ya Yohana kwa mahitaji ya dunia ya leo.

(6) Kutumia yaliyomo ya hili somo katika mazingira ya huduma ya kidini.

## Maandalizi kwa ajili ya Somo hili

► Soma Injili ya Yohana. Unavyosoma, kuwa na shajara ambayo unaitumia kuitikia namna Yesu anavyowasilishwa katika kila sura. (huu ni msisitizo wa kwanza kwa somo hili.) Kwa mfano, katika sura ya kwanza, unaweza kuitikia uwasilishwaji wa Yesu kama "Neno" la Mungu la milele. Hii inamaanisha nini kwako kama mwamini? Ni namna gani asili ya uungu ya Yesu inaathiri imani na ujasiri wako kama mtoto wake?

► Kariri Yohana 20:30-31.

## Utangulizi

► Wakristo wanaitwa "walioamini." Hiyo inamaanisha nini kuamini? Kivipi imani ya kweli inaathiri maisha yetu?

> Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye. Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu (Yohana 3:16-18).

Haya ni baadhi ya maneno yanayojulikana zaidi katika Maandiko. Yanaahidi kuwa yoyote anayeamini katika Yesu atakuwa na uzima wa milele. Haya ni baadhi ya maneno yanayokiukwa au kutumiwa vibaya mara nyingi zaidi katika Maandiko. Dhana ya imani mara nyingi hufasiriwa vibaya kumaanisha kutambua kiakili (bila ya mabadiliko ya maisha). Injili ya Yohana inaonesha kuwa ni zaidi sana kuliko kukubali kiakili. Maneno "Ninaamini," yakiongewa toka moyoni, yatabadili maisha yako. Imani ya kweli inabadili mapenzi na tabia ya mtu.

## Usuli wa Yohana

### Mwandishi, tarehe, na mahali

Yohana, mwana wa Zebedayo, alikuwa mwandishi wa Injili ya nne. Ignatius wa Antiokia, Justin Martyr, Polycarp, na Irenaeus wote walishuhudia kwamba Yohana ni mwandishi. Ushuhuda wa Polycarp ni wa muhimu sana kwa sababu alikuwa mwanafunzi wa Yohana.

Yohana, pamoja na ndugu zake Yakobo, na Simoni Petro, walikuwa wanafunzi wa karibu zaidi wa Yesu. Hawa walikuwa wanafunzi pekee katika chumba wakati Yesu alipomfufua msichana aliyekufa (Marko 5:37-43). Walikuwa pekee katika mlima wa kugeuka sura kule Gethsemane (Mathayo 17:1-9, Marko 14:32-36).

Yohana alikuwa kiongozi mwenye ushawishi katika kanisa. Paulo pekee aliandika vitabu vingi vya Agano jipya kuliko Yohana. Yohana aliandika Injili ya Yohana, nyaraka tatu, na Ufunuo.

Kulingana na utamaduni, Yohana aliishi Efeso. Wakati wa utawala Domitian, Yohana alihamishwa na kupelekwa Patmo, ambapo aliandika kitabu cha Ufunuo. Baadaye alirudi Efeso na alifia hapo akiwa na takribani miaka 100. Kuna uwezekano kwamba Injili ya Yohana iliandikwa kutokea Efeso. Mara nyingi inaoneshwa kwamba iliandikwa takribani mwaka 85-95 B.K., na hivyo kuifanya kuwa injili ya mwisho.

### Kusudi

Injili ya Yohana inatofautiana sana na Injili za Kuona Pamoja. Yohana haina habari zozote za Yesu kutoa mapepo; haina mifano; na, tofauti na Marko, hakuna siri ya Kimasihi.

Wakati waandishi wengi wameorodhesha tofauti kati ya Yohana na Injili za Kuona Pamoja, ni muhimu kuona pia ufanano uliopo. Yohana anawasilisha mtazamo tofauti wa maisha ya Yesu, lakini ujumbe wake ni sawa na Wainjilisti wengine. Yohana anaonesha kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu aliyeishi kati yetu, aliteswa kwa ajili ya dhambi zetu, na alifufuka siku ya tatu kutoka kwa wafu.

Kulikuwa imani potofu mbili za awali zinazohusiana na Yesu. Moja ilikana utu wake kamili, ikidai kwamba Yesu alionekana tu kama mtu. Luka alilizungumzia upotofu huu kwa maelezo ya Yesu kama mwanadamu kamili. Imani nyingine potofu ilikana uungu wa Yesu ikidai kwamba Yeye alikuwa mwalimu mkuu sana lakini si Mwana wa Mungu. Yohana anaweka umakini katika uungu wa Yesu kupitia mfululizo wa miujiza ambayo inamfunua Yeye kama Mwana wa Mungu na kupitia matamko yanayomuonesha Yeye kuwa ni Neno aliyefanyika mwili. Yohana anasema aliandikwa kwa sababu hizi: "…ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake" (Yohana 20:31).

## Yaliyomo katika Yohana

### Utangulizi (Yohana 1:1-18)

Kumuwasilisha **Yesu mfalme** kwa wapokeaji wa Kiyahudi, Mathayo alifuatilia ukoo wa Yesu kupitia Daudi na kurudi nyuma hadi kwa Ibrahimu. Kumuwasilisha **Mtumishi Yesu** kwa wapokeaji wa Kirumi, Marko hakujumuisha kitabu chochote cha ukoo. Kumuwasilisha **mwanadamu Yesu** kwa wapokeaji wa Kiyunani, Luka alifuatilia ukoo wa Yesu na kurudi nyuma hadi kwa Adamu, mwanadamu wa kwanza. Kumuwasilisha **Yesu mwana wa Mungu**, Yohana anaanza na kitu ambacho tungekiita "ukoo wa kiuungu":

> Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika (Yohana 1:1-3).

Injili ya Yohana inaanza na madai yenye uhankika kwamba Yesu alikuwa Neno la milele la Mungu. Yohana anaandika, "Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli" (Yohana 1:14). Sehemi iliyobaki ya Injili inawasilisha ushahidi ili kuthibitisha madai yake.

### Kitabu cha Ishara (Yohana 1-12)

#### *Miujiza Saba ya Yesu*

Katika nusu ya kwanza ya Injili, Yohana ananakili ishara—saba za Miujiza ya Yesu ambayo inaonesha nguvu zake za kiuungu:

> Muujiza ni zaidi ya tukio ambalo haliwezi kuelezeka. Muujiza huusisha "kuingilia kusiko kwa kawaida kwa uungu katika asili au mwenendo wa matukio. Katika historia ya kanisa, miujiza imeonekana sio tu kama onesho la kipekee la neema ya Mungu, bali kama ushuhuda wa kiuungu wa utu na mafundisho ya yule anayetenda muujiza." Hii ndiyo sababu kwanini Yohana anatumia neno *ishara* ili kuelezea miujiza ya Yesu.
>
> - Sinclair B. Ferguson na J. I. Packer, *New Dictionary of Theology*, 1988.

- Kubadilisha maji kuwa divai huko Kana (Yohana 2:1-11).
- Kumponya mtoto wa diwani huko Kapernaumu (Yohana 4:46-54).
- Kumponya mtu aliyekuwa hawezi huko Bethzatha (Yohana 5:1-18).
- Kulisha watu 5,000 (Yohana 6:5-14).[25]
- Kutembea juu ya maji (Yohana 6:16-21).
- Kumponya mtu aliyekuwa kipofu tangu kuzaliwa (Yohana 9:1-7).
- Kumfufua Lazaro kutoka kwa wafu (Yohana 11:1-45).

[25] Huu ni muujiza pekee ambao unaandikwa katika Injili zote nne (Mathayo 14:13-21, Marko 6:30-44, Luka 9:10-17). Mathayo anaandika kwamba walikuwepo takribani wanaume 5,000, pamoja na wanawake na watoto.

Kila muujiza unamuonesha Yesu kama Mwana wa Mungu. Yohana anatumia neno *ishara* ili kuelezea Miujiza ya Yesu kwa sababu zilikuwa ni ushahidi wa uungu wake.

Yesu aligeuza maji na kuwa divai katika harusi, alijifunua kwa wanafunzi wake: "Mwanzo huo wa ishara Yesu aliufanya huko Kana ya Galilaya, akaudhihirisha utukufu wake, nao wanafunzi wake wakamwamini" (Yohana 2:11).

Muujiza wa mwisho wa Yesu, kumfufua Lazaro, umeandikwa katika Yohana pekee na ni kilele cha nusu ya kwanza ya Injili. Muujiza huu moja kwa moja ulipelekea mapambano ya moja kwa moja kati ya Yesu na viongozi wa kidini. Kwa sababu Wayahudi wengi walikuwa nwanamgeukia Yesu kama matokeo ya muujiza huu usioweza kuukana, viongozi walitaka kumuua Yesu na Lazaro (Yohana 11:45-53, Yohana 12:9-11).

***Matamko Saba Yanayoshuhudia Uungu wake***

Kwa nyongeza katika miujiza saba, Yohana ana nakili mfululizo wa matamko saba yaliyotolewa na Yesu ambayo yanathibitisha uungu wake. Wakati Marko anataja nyakati ambazo Yesu aliwazuia wanafunzi wake kushuhudia kwamba alikuwa Masihi, Yohana anaandika nyakati ambazo Yesu alifunua asili yake kwa wengine. Shuhuda zilizoandikwa katika Yohana zinajumuisha:

- Ushuhuda wa Yesu kwa Nikodemo (Yohana 3:1-21).
- Ushuhuda wa Yesu kwa mwanamke Msamaria (Yohana 4:1-42).[26]
- Ushuhuda wa Yesu baada ya kumponya mtu katika Bethzatha (Yohana 5:17-18).
- Ushuhuda wa Yesu baada ya kulisha watu 5,000 (Yohana 6:24-59).
- Ushuhuda wa Yesu katika sikukuu ya vibanda (Yohana 7:14-44).
- Ushuhuda wa Yesu kwamba "…Yeye Ibrahimu asijakuwako, mimi niko" (Yohana 8:52-59).
- Ushuhuda wa Yesu katika Sikukuu ya Kutabaruku (Yohana 10:22-38).

> "...watu mara nyingi husema: Niko tayari kumkubali Yesu kama mwalimu mkuu wa maadili, lakini sikubaliani na madai yake kwamba Yeye ni Mungu.' Hilo ni jambo moja ambalo hatupaswi kulisema. Mtu aliyesema mambo ambayo Yesu aliyasema asingeweza kuwa mwalimu mkuu wa maadili. Ni ama angekuwa mwehu au vinginevyo angekuwa pepo wa jehanamu. Lazima ufanye uchaguzi.... Unaweza kumnyamazisha kama mpumbavu; unaweza kumuua kama pepo; au uanguke miguuni pake na kumwita Bwana na Mungu. Lakini tusije na upuuzi unaomfanya kuwa mdogo kuhusiana na yeye kuwa mwanadamu aliye mwalimu mkuu. Hajaliacha hilo wazi kwa ajili yetu."
>
> \- C. S. Lewis
> *Mere Christianity.*

Wapingaji wamekuwa wakidai kwamba Yesu hakudai kuwa yeye ni Mungu. Yohana anaonesha kwamba kwa kurudia rudia Yesu ameshuhudia kuhusu uungu wake. Hadhira ya Yesu ilifahamu fika alicho kimaanisha

[26] Hasa hasa ona Yohana 4:25-26.

aliposema, "…Yeye Ibrahimu asijakuwako, mimi niko" (Yohana 8:58). Haya ni maneno ambayo Mungu aliyatumia kujifunua kwa Musa: "MIMI NIKO AMBAYE NIKO" (Kutoka 3:14). Wale waliomsikia Yesu walifahamu alimaanisha nini; walijaribu kumpiga kwa mawe, adhabu kwa ajili ya kukufuru (Yohana 8:59). Viongozi wa Kiyahudi hawakutaka kumuua Yesu kwa sababu alikuwa mwalimu mkuu na mponyaji; walitaka kumuua kwa sababu alidai kuwa Mungu. Watu wanaweza kutataa madai ya Yesu ya uungu, lakini ni upuuzi kukataa kwamba yeye alitoa madai hayo.

**Kitabu cha Utukufu (Yohana 13-20)**

Katika Yesu, tunaona "…utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli" (Yohana 1:14). Wakati wa wiki ya mwisho ya huduma ya Yesu duniani, utukufu wake ulifunuliwa katika namna ya tofauti na vile ambavyo wanafunzi walitegemea. Wanafunzi walitegemea utukufu wa Yesu katika namna ya ushindi wa kijeshi, kisiasa, na umashuhuri na umaarufu katika huduma ya nje. Badala yake, Yesu anaonesha kwamba utukufu wake unahusisha msalaba na kujitoa.

Katika chakula chake cha mwisho, Yesu alitoa kielelezo cha unyenyekevu ambapo wanafunzi wake wanatakiwa kuhudumiana (Yohana 13:1-17). Katika mafundisho yake ya mwisho, Yesu alifundisha kuhusiana na Msaidizi ambaye atakuwa pamoja nao siku zote (Yohana 14:16). Kwa kutumia kielelezo cha mzabibu na matawi, alifundisha kuhusiana na umuhimu wa kuendelea kukaa ndani yake: "Mtu asipokaa ndani yangu, hutupwa nje kama tawi na kunyauka …" (Yohana 15:6). Mifano hii ilikuwa kinyume cha ngvu ya kisiasa na kijeshi; njia ya Yesu ni ile ya kujitoa mwenyewe na unyenyekevu.

Katika maombi yake ya kuhani mkuu, aliyaombea mambo yale yaliyokuwa ndani kabisa ya moyo wake. Akiukabili msalaba, Yesu aliomba:

- Kwa ajili yake mwenyewe: kwamba atukuzwe kupitia Baba (Yohana 17:1-5).
- Kwa ajili ya wanafunzi wake: kwamba walindwe na kutakaswa (Yohana 17:6-19).
- Kwa ajili ya waamini wote: kwamba umoja wao uwe ushuhuda kwa ulimwengu (Yohana 17:20-26).

Yohana anaandika kukamatwa, mashitaka, kusulubiwa, na kufufuka kwa Yesu. Mwanzoni kwa Injili ya Yohana, Yesu anamwambia Nikodemo, "…vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa; ili kila mtu aaminiye awe na uzima wa milele katika yeye" (Yohana 3:14-15). Baadae, anazungumza namna ya kifo chake: "Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu" (Yohana 12:32). Juu ya msalaba, Mwana wa Adamu aliinuliwa ili kuwaleta watu kwake, ili kwamba wasipotee bali wawe na uzima wa milele. Hili lilikuwa lengo ambalo kwa hilo maisha yote ya Yesu yalielekezwa. Hata kusulubiwa kwake kunaitwa saa ya kutukuzwa kwake (Yohana 12:23). Huu ulikuwa utukufu ambao kwa ajili ya huo alikuja ulimwenguni.

Yohana anahitimisha sehemu hii kwa ushuhuda wa Tomaso baada ya ufufuo: "Bwana wangu na Mungu wangu!" (Yohana 20:28). Nguvu ya Yesu ya kubadilisha inaonekana katika maisha ya baadae ya Tomaso, aliuawa kama mfia imani wakati akihubiri huko India.

### Hitimisho (Yohana 21)

Sura ya mwisho ya Yohana inaripoti Yesu kuonekana baada ya ufufuo kwa kundi la wanafunzi katika bahari ya Galilaya (Yohana 21:1).[27] Yohana anahitimisha Injili yake kwa kuthibitisha ukweli wa maelezo yake: "Huyu ndiye yule mwanafunzi ayashuhudiaye haya, na aliyeyaandika haya: nasi twajua ya kuwa ushuhuda wake ni kweli" (Yohana 21:24).

## Yohana katika Kanisa Leo

Kwa waamini wapya, Yohana anafunua asili ya Yesu ya Uungu. Kwa sababu ya uwasilishaji wake rahisi na unaoeleweka kuhusiana na Yesu, mara nyingi wachungaji huwatia moyo waamini wapya kusoma Injili ya Yohana. Katika Yohana, tunamuona Yesu kama mkate wa uzima (Yohana 6:35); nuru ya ulimwengu (Yohana 8:12); mchungaji mwema (Yohana 10:11); ufufuo na uzima (Yohana 11:25); na njia, kweli, na uzima (Yohana 14:6).

Kwa ulimwengu wenye mashaka, Yohana anatoa picha ya Yesu kama mwana wa Mungu. Miujiza katika Yohana inazungumza na wale wanaotafuta ishara yenye nguvu ili kuthibitisha madai ya Yesu ya uungu. Kupitia miujiza, Yesu anaonesha kwamba madai yake ya kuwa MIMI NIKO yaliungwa mkono na nguvu zake za kiuungu (Yohana 8:58).

Kwa kanisa la leo linalohubiri neema ya bei rahisi pasipo wito wowote wa uanafunzi,[28] Injili ya Yohana inaonesha maana halisi ya imani. Imani ya kweli inabadilisha maisha ya mwamini. Baada ya kusikia Yesu alifafanua Mkate wa uzima, "…wengi miongoni mwa wanafunzi wake wakarejea nyuma, wasiandamane naye tena" (Yohana 6:66). Wafuasi hawa walidai kumwamini Yesu. Walimfuata, walifurahia mikate na samaki, lakini kiukweli hakauamini. Hawakuiishi imani waliyoikiri kwa utii endelevu kwa matakwa ya Yesu. Injili ya Yohana inafundisha maana ya imani ya kweli.

## Hitimisho

Injili ya Yohana inaonesha kwamba imani ya kweli hubadilisha maisha ya mwamini; hata kugharimu maisha yake. Dietrich Bonhoeffer alitofautisha kile alichokiita "neema ya beo rahisi" na "neema yenye gharama." Aliandika, "Yesu anapomuita mtu, anammtaka kuja na kufa."[29] Aina hii ya imani inaonekana katika maisha ya mfia imani wa karne ya pili, Polycarp.

Polycarp, mwanafunzi wa Yohana, alimsikiliza Yohana akifundisha na alisikia mkusanyiko wa habari za maisha ya Yesu aliokusanya Yohana. Katika umri wa miaka 86, Polycarp

[27] Yohana anaita bahari ya Galilaya kwa kutumia jina mbadala, Bahari ya...Tiberia. Tiberia ulikuwa mji mkuu wa Galilaya.
[28] Neno *cheap grace* (neema ya bei rahisi) linatoka katika Dietrich Bonhoeffer, *The Cost of Discipleship*, imetafsiriwa na R.H. Fuller. (New York: Touchstone, 1995), 89
[29] Dietrich Bonhoeffer, *The Cost of Discipleship*, kimetafsiriwa kwenda kiingereza na R.H. Fuller. (New York: Touchstone, 1995), 89

alikamatwa. Maafisa hawakutaka kumuua mzee aliyeheshimiwa na wakatoa nafasi ya kuokoa maisha yake kwa kutangaza na kwa kuapa kwamba "Kaisari ni bwana." Hakimu alisema, "Apa kiapo, na nitakuachia huru." Mwitikio wa Polycarp ulisikika katika karne nyingi kama shahidi kwa maana halisi ya imani ya kweli: "miaka 86 nimekuwa mtumishi wake, na hajawahi kunitendea ubaya wowote. Inakuwaje basi mimi nimkane mfalme wangu aliyeniokoa?"[30] Polycarp alijifunza masomo yaliyofundishwa na mwalimu wake, Yohana. Alifahamu kwamba imani ya kweli inambadilidha mwamini, hata katika kifo.

## Somo la 3 Mazoezi

(1) (Yatakamilishwa katika maandalizi kwa ajili ya Somo la 3.) unaposoma Injili ya Yohana, kuwa na shajara ambayo unaitumia kuitikia namna Yesu anavyowasilishwa katika kila sura. Kwa mfano, katika sura ya 1, unaweza kuitikia kwa Yesu kuwasilishwa kama Neno la Milele. Hilo lina maana gani kwako wewe kama mfuasi wa Kristo? Ni kwa namna gani asili ya Yesu ya uungu inaathiri maisha yako na ujasiri wako kama mtoto wake?

(2) Mwanzoni mwa somo linalofuata, utafanya jaribio kulingana na somo hili. Soma maswali ya jaribio kwa umakini katika maandalizi.

## Somo la 3 Jaribio

(1) Kwa nini Ushuhuda wa Polycarp kuhusiana na uandisho wa Yohana ni wa umuhimu mkubwa sana?

(2) Injili ya Yohana inaanza na madai yenye uhankika kwamba Yesu alikuwa Neno la milele la Mungu.

(3) Katika Yohana 1-12, ni mambo gani na ni aina gani ya ushahidi ambayo inatolewa ili kuunga mkono madai yake?

(4) Orodhesha ishara zinazoelezewa katika Yohana 1-12.

(5) Toa mifano mitatu ya ushuhuda wa Yesu kwa uungu wake.

(6) Nini ulikuwa mwitikio wa viongozi wa Kiyahudi kuhusiana na Ushuhuda wa Yesu wa uungu?

(7) Katika maombi ya kuhani mkuu ya Yesu, aliombea mambo gani matatu?

(8) Andika Yohana 20:30-31 kutoka katika kumbukumbu.

---

[30] "The Martyrdom of Saint Polycarp," katika *Early Christian Fathers*, kilichotafsiriwa na Cyril C. Richardson (Philadelphia: Westminster Press, 1953). https://www.ccel.org/ccel/richardson/fathers.vii.i.iii.html

# Somo la 4
# Matendo ya Mitume
# Kanisa la Kwanza

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kufahamu usuli (nyuma ya mambo) wa kihistoria na kijiografia wa kanisa la kwanza.

(2) kumfahamu mwandishi na tarehe ya Matendo ya Mitume.

(3) Kutambua kusudi na umuhimu wa mada kuu za Matendo ya Mitume.

(4) Kufuatilia kusambaa kwa Injili kutokea Yerusalemu na katika ulimwengu wote wa Rumi.

(5) kufahamu tofauti kati ya mafundisho ambayo ni maelekezo na maelezo katika Matendo ya Mitume.

(6) Kupata ufahamu wa muhtasari wa huduma ya Paulo.

(7) Kuhusianisha ujumbe wa Matendo ya Mitume na mahitaji ya ulimwengu wa leo.

## Maandalizi kwa ajili ya somo hili

► Soma Matendo ya Mitume.

► Kariri Matendo ya Mitume 1:7-8.

## Utangulizi

Katika Agano la Kale, kitabu cha Yoshua kinaonesha mpito wa Israeli kutoka maisha ya jangwani kwenda maisha ndani ya Kanaani, na kutoka uongozi wa Musa kwenda uongozi wa Yoshua. Kitabu cha Yoshua kinaonesha mpito muhimu katika historia ya watu wa Mungu, Israeli.

Katika Agano Jipya, kitabu cha Matendo ya Mitume kinaonesha mpito kutoka huduma ya Yesu ya duniani kwenda huduma ya Roho Mtakatifu kupitia kanisa. Kinatembea kutoka mkazo wa kazi ya Yesu kwenda kwenye mkazo katika kazi ya Mitume. Matendo ya Mitume kinaonesha umuhimu katika historia ya watu wa Mungu, kanisa.

Kitabu cha Yoshua kinaonesha mpito uliofanikiwa kwa kiasi. Mwishoni mwa kitabu, watu wa Israeli wanatoa ahadi ya uaminifu kwa Mungu (Yoshua 24:16-27, 31). Hata hivyo, Wakanaani walikuwa hawajashindwa kikamilifu (Waamuzi 1:27-33). Kwa Kizazi kingine, Israeli wanaabudu miungu ya Wakanaani (Waamuzi 2:8-13).

Matendo ya Mitume kinaonesha mpito uliokamilika zaidi. Agizo lililofungua kitabu linakamilika katika kitabu chote (Matendo ya Mitume 1:7-8). Matendo ya Mitume kinaanza na kanisa la Kiyahudi likiwa na kituo Yerusalemu; kinaishia na kanisa lenye watu wa tamaduni tofau tofauti lenye kituo huko Antiokia. Matendo ya Mitume kinaanzia Yerusalemu; kinaishia Rumi. Matendo ya Mitume kinaanza na Petro—mmojawapo wa wanafunzi watatu wa Yesu wa karibu zaidi—katika mstari wa mbele; kinamalizikia na Paulo—awali alikuwa mtesaji wa kanisa—katika mstari wa mbele.

## Ulimwengu wa Kanisa la Kwanza

Somo la 1 liliwasilisha muhtasari wa ulimwengu wa Agano Jipya. Marejeo ya somo hilo yatakupa kumbukumbu nzuri kwa ajili ya kujifunza Matendo ya Mitume. Maadhi ya taarifa za nyongeza ni muhimu kwa ajili ya uelewa wa kusambaa kwa kanisa la kwanza katika Dola yote ya Rumi.

### Jiografia

Umakini wa Matendo ya Mitume unatembea kutoka Palestina kuelekea ulimwengu mpana wa Dola ya Rumi. Tafadhali chukua muda kuangalia ramani ya ulimwengu wa Agano Jipya iliyotolewa katika kozi hii. (Endapo unatumia app ya kwenye simu, ramani hii inapatikana katika nyongeza.) kuwa makini na miji ifuatayo ambayo ni muhimu sana katika Matendo ya Mitume:

- **Antiokia** ulikuwa ni mji mkuu wa jimbo la Shamu.[31] Kilikuwa ni kituo cha Wakristo kufikia wasio wakristo zaidi ya Uyahudi.
- **Filipi** ulikuwa mji wa koloni la Rumi katika jimbo la Makedonia. Kanisa la Filipi lilikuwa ni kanisa la kwanza lililopandwa Ulaya.
- **Efeso** ulikuwa mji mkuu wa jimbo la Asia.[32] Mkakati wa Paulo ulikuwa ni kupanda makanisa katika miji mikubwa katika Dola ya Rumi. Kutoka kanisa hilo la mwanzo katika eneo la kati, Injili ingesambaa kwenda sehemu zote za jimbo.
- **Korintho** ulikuwa mji mkuu wa jimbo la Akaya. Eneo la Korintho kama bandari katika bandari ya Mediterranea ulikuwa ni mji muhimu kwa injili, kwa sababu watu kutoka mataifa mbalimbali walitembelea hapa.
- **Rumi** ulikuwa mji mkuu wa Dola yote ya Rumi. Lengo la Paulo lilikuwa ni kutembelea Rumi ili kusaidia kufanya uinjilisti katika dola. Alipanga kutoka Rumi kwenda Spania baadae katika huduma yake.

[31] Kulikuwa na miji miwili iliyoitwa Antiokia iliyotajwa katika Matendo ya Mitume. Antiokia ya Shamu imetajwa sana na ni muhimu katika historia ya kanisa. Antiokia ya Pisidia ni moja ya miji ambapo Paulo alihubiri injili katika sinagogi la Kiyahudi wakati wa safari yake ya kwanza ya kimisheni (Matendo ya Mitume 13:14).
[32] Wakati waandishi wa Agano Jipya wanzungumza kuhusu "Asia," wanarejelea Asia ndogo (Anatolia ya Leo). Hawazungumzii bara ambalo leo katika karne ya 21 tunaliita "Asia".

### Historia

Maempara wawili wa Kirumi ambao walilitesa kanisa la kwanza:

- **Nero** alikuwa mtawala mwaka 54-68 B.K. Nero aliwalaumu Wakristo kwa ajili ya moto mkubwa ulioharibu sehemu kubwa ya Rumi. Kushitakiwa huku kwa uongo kulipelekea mateso yaliyosambaa sehemu kubwa kwa wafuasi wa Kristo. Petro na Paulo walikuwa miongozi mwa wengi waliouawa na Nero.

- **Domitian** alikuwa mtawala mwaka 81-96 B.K. alidai cheo cha "Bwana na Mungu" na aliwatesa wafuasi wa Kristo ambao walikataa kuapa kuwa waaminifu kwake. Inawezekana kitabu cha Ufunuo kiliandikwa katika wakati.

## Usuli wa Matendo ya Mitume

### Mwandishi na Tarehe

Katika Matendo ya Mitume, Luka anaendeleza simulizi aliyoianza katika Injili yake. "Kitabu kile cha kwanza nalikiandika, Theofilo, katika habari ya mambo yote aliyoanza Yesu kufanya na kufundisha" (Matendo ya Mitume 1:1).

Mwishoni mwa Matendo ya Mitume, Paulo yuko chini ya nyumba ya kifungo huko Rumi (Matendo ya Mitume 28:16, 30). Aliuawa mnamo 66 au 67 B.K. Hii inaonesha kwamba Matendo ya Mitume pengine iliandikwa mwishoni mwa miaka ya 50 au mwanzoni mwa miaka ya 60.

### Kusudi

Injili ya Luka inaonesha Yesu akiwafundisha wanafunzi kuongoza kanisa. Matendo ya Mitume inaonesha wanafunzi wanachukua injili na kuipeleka ulimwenguni. Inaonesha kusambaa kwa injili kutokea Yerusalemu na Uyahudi hadi Samaria na mwisho wa nchi.

## Mada kuu za Matendo ya Mitume

### Taarifa za Kihistoria

Kama injili ya Luka, Matendo ya Mitume inaweka umakini mkubwa katika taarifa za kihistoria. Matendo ya Mitume inataja zaidi ya nchi 30, zaidi ya miji 50, na karibu watu 100.[33]

### Uinjilisti na Umisheni

Mwanzoni mwa Matendo ya Mitume, Yesu anawaagiza wanafunzi wake kuichukua Injili kutoka Yerusalemu, Uyahudi, Samaria, na hata mwisho wa nchi. Mwishoni mwa Matendo ya Mitume, injili imehubiriwa katika Dola yote ya Rumi.

---

[33] Walter A. Elwell na Robert W. Yarbrough, *Encountering the New Testament* (Ada: Baker Academic, 2005), 211.

## Kazi ya Roho Mtakatifu

Injili ya Luka inaweka umakini katika wajibu au kazi za Roho Mtakatifu katika huduma ya Yesu ya hapa duniani. Katika Matendo ya Mitume, Luka anaonesha wajibu au kazi ya Roho Mtakatifu katika kanisa la kwanza. Roho Mtakatifu ni kiini kikuu katika Matendo ya Mitume. Ni kupitia Roho Mtakatifu kwamba wanafunzi wanapewa nguvu kwa ajili ya huduma.

## Ujumbe wa Injili

Injili ya Luka imeandikwa ili kuthibitisha ukweli wa mambo ambayo Theofilo amekuwa akifundishwa kama mwamini mpya. Kitabu cha Matendo ya Mitume pia kinafundisha mwaamini wapya Injili. Karibu moja ya nne ya kitabu inajumuisha mahubiri. Mahubiri muhimu katika Matendo ya Mitume yanajumuisha:

- Mahubiri ya Petro siku ya Pentekoste (Matendo ya Mitume 2).
- Utetezi wa Stephano mbele ya baraza lote (Matendo ya Mitume 7).
- Mahubiri ya Petro katika nyumba ya Kornelio (Matendo ya Mitume 10).
- Mahubiri ya Paulo juu ya mlima Mars huko Athene (Matendo ya Mitume 17).

Mahubiri haya yanaonesha kiini cha ujumbe mkuu uliohubiriwa na mitume:[34]

- Ubwana wa Yesu Kristo
- Ukweli wa kihistoria wa Injili
- Wokovu kwa neema kupitia imani.

## Yaliyomo katika Matendo ya Mitume

Matendo ya Mitume inaanza na mitume wakiwa katika hali ya kuchanganyikiwa. Kufuatiwa kuingia kwake Yerusalemu kwa shangwe siku ya jumapili ya mitende, wanafunzi walitegemea Yesu kuanzisha ufalme wake wa hapa duniani. Badala yake, alikamatawa, akawekwa katika kesi, na kusulubiwa. Kwa ufufuo wake, tena walifurahishwa na matarajio au matumaini ya ufalme wake wa kimasihi.

Mwanzoni mwa Matendo ya Mitume, Yesu anawaambia wanafunzi wake kubakia Yerusalemu ili kungojea ahadi ya Baba. Waliuliza, "Je! Bwana, wakati huu ndipo unapowarudishia Israeli ufalme?" (Matendo ya Mitume 1:6). Wasingeweza kuelewa mwitikio wake hadi hapo baadae:

> Si kazi yenu kujua nyakati wala majira, Baba aliyoyaweka katika mamlaka yake mwenyewe. Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi (Matendo ya Mitume 1:7-8).

---

[34] Wanatheolojia wanaita ujumbe huu mkuu kerygma, injili iliyohubiriwa.

Agizo hili linatoa njia moja ya kuelewa muundo wa Matendo ya Mitume: Injili katika Yerusalemu (Matendo ya Mitume 1-7), Injili katika Uyahudi na Samaria (Matendo ya Mitume 8-12), na Injili kwenda mwisho wa nchi (Matendo ya Mitume 13-28).

### Injili katika Yerusalemu (Matendo ya Mitume 1-7)

Kituo cha shughuli katika Matendo ya Mitume 1-7 ni Yerusalemu. Simulizi inajumuisha habari ya Pentekoste, picha ya maisha ya kanisa la kwanza, na kuuawa kwa Stefano.

#### *Pentekoste: Siku ya kuzaliwa kwa Kanisa*

Kufuatia kupaa kwa Kristo, wanafunzi walirudi Yerusalemu na kwa nia moja wakajikita katika maombi (Matendo ya Mitume 1:14). Walikuwa pale katika sikukuu ya Pentekoste, sikukuu ya majuma wakizingatia majuma saba baada ya Pasaka (Kumbukumbu la Torati 16:16). Pentekoste ilisheherekea zawadi ya Sheria. Kwa waamini leo, Pentekoste inasheherekea zawadi ya Roho Mtakatifu. Katika mahubiri yake ya Pentekoste akielezea ishara ya kimuujiza ya siku hiyo, Petro aliwakumbusha waikilizaji wake kwamba Yoeli alitabiri siku ambayo Mungu atamwaga Roho Wake juu ya wote wenye mwili. Ahadi hii ilitimizwa siku ya Pentekoste (Yoeli 2:28-32, Matendo ya Mitume 2:16-21).

#### *Maisha katika kanisa la Kwanza*

► Ni kwa namna gani kanisa la kwanza ni mfano kwa kanisa la leo? Ni maeneo gani ya Pentekoste tunatakiwa tuyaone na kuyapata leo?

Picha ya maisha katika kanisa la kwanza inaibua maswali muhimu kwa ajili ya kutafsiri kitabu cha Matendo ya Mitume. Matendo ya Mitume ni kitabu cha historia, sio kitabu cha kitheolojia kama Warumi. Kitabu cha historia kinajumuisha vyote viwili **maelezo** ("hiki ni kile walichokifanya") na **maelekezo** ("hiki ni kile unachotakiwa kukifanya"). Tunaposoma kuhusiana na maisha katika kanisa la kwanza, msomaji anapaswa kuuliza, "Je, Matendo ya Mitume kinatuambia sisi kwamba sifa hizi zinatakiwa kuwa sehemu ya kanisa la leo? Au je, Matendo ya Mitume kinaelezea tu kipindi katika historia ya kanisa? Njia moja ya kupata jibu ni kuuliza, "Ni kwa namna gani hili linakaa vizuri katika mafundisho mengine ya Biblia? Je, hili limeagizwa tena sehemu nyingine katika maandiko?"

Mifano miwili ili kuonesha utofauti kati ya maelekezo na maelezo katika Matendo ya Mitume:

- Kulingana na Matendo ya Mitume 2:42, wafuasi wa Kristo wa karne ya kwanza walijikita katika mafundisho ya mitume, ushirika pamoja na waamini, na maombi. Kujifunza Biblia, kukusanyika kwa ajili ya kuabudu, na maombi yameagizwa katika nyaraka zote za Paulo. Tunaweza kugundua kutokana na hili kwamba shughuli hizi zimeagizwa kwa ajili yetu leo; sio tu maelezo ya kipindi cha historia.

- Kulingana na Matendo ya Mitume 2:45, wafuasi wa kwanza waliuza mali zao na wakawa na vitu vyote shirika. Kwa sababu agizo hili halijaagizwa sehemu nyingine

katika maandiko, tunaweza kukubaliana kwamba hili lilikuwa ni maelezo ya maisha ya wakati huo, na sio maelekezo kwa ajili ya leo.[35]

► Kabla ya kwenda mbali katika somo hili, zingatia baadhi ya shughuli katika kanisa la kwanza. Katika kila moja, zingatia, "Je, shughuli hii imeagizwa kwa ajili yetu leo au ni maelezo ya maisha ya kanisa la kwanza tu?" jibu lako linatakiwa kutokana na kuangalia maandiko yote, na si tu kwa kujiuliza, "Ni nini ninapenda?"

- Kujifunza mafundisho ya mitume
- Kuabudu Hekaluni kila siku
- Kuuza mali zao
- Uinjilisti endelevu/unaoendelea
- Ushirika na waamini wengine
- Ishara na miujiza ili kuhakikisha kazi ya Roho
- Kumsifu Mungu
- Kuzungumza kwa lugha nyingine

### *Stefano: Mkristo wa kwanza Mfia Imani*

Baada ya Pentekoste, kanisa liliendelea kukua kwa kasi. Watu wengi waliokoka, wakiwemo makuhani wengi (Matendo ya Mitume 6:7). Pamoja na juhudi za viongozi wa Kiyahudi kuficha ukweli wa ufufuo, makuhani hawa walifahamu ukweli: kupasuka kwa pazia la Hekalu (Mathayo 27:51), mwili haukuwepo kaburini (Mathayo 28:6), njama ili kuficha ukweli (Mathayo 28:11-15). Ishara na miujiza iliendelea katika kipindi chote cha mwanzo cha kanisa, kama hakikisho la huduma ya mitume ikiwa ni muendelezo wa huduma ya Yesu.

Katika mazingira ya kanisa, upinzani lilikuwa jambo lisiloepukika. Baada ya mashahidi wa uongo kumshitaki Stefano kwamba amekufuru, alipigwa kwa mawe hadi kufa. Katika kesi yake, Stefano alihubiri ujumbe wenye nguvu ambao ulifuatilia kazi ya Mungu tangu Ibrahimu kupitia Yesu. Matendo ya Mitume inamtambulisha Sauli kwa sentensi hii, "Na Sauli alikuwa akiona vema kwa kuuawa kwake [Stefano]…" (Matendo ya Mitume 7:60). Paulo, ambaye atakuja kuwa mmishenari mkubwa wa kanisa, alionekana kwanza kama Sauli, adui wa kanisa, ambaye anawakamata waamini (Matendo ya Mitume 8:3).

### Injili katika Uyahudi na Samaria (Matendo ya Mitume 8-12)

Katika Matendo ya Mitume 8-12, injili inasambaa. Mateso yanawasukuma waamini kutoka Yerusalemu hadi kwenda sehemu nyingine za Uyahudi na pia kwenda Samaria. Walipokuwa wanakimbia, walibeba injili pamoja nao. Mungu alitumia mateso ili kutimiza agizo la Matendo ya Mitume 1:8. Katika Matendo ya Mitume 8-12:

[35] Wengi wanaamini kwamba kitendo hiki kilihusiana na scholars believe that this practice was related to (1) hitaji la kuwasaidia waamini waliopoteza kazi na nyumba zao kwa sababu ya imani yao na (2) imani ya kanisa la kwanza katika ujio wa haraka wa Yesu.

- Filipo, Myahudi anayeongea Kiyunani, anahubiri huko Samaria akiwa na matokeo makubwa (Matendo ya Mitume 8:4-25).
- Filipo anamuhubiria towashi wa Ethiopia aliyekuwa anasafiri akitokea kuabudu (Matendo ya Mitume 8:26-40).
- Sauli, alisafiri ili kwenda kuwakamata waamini huko Dameski, anabadilishwa/anaokoka (Matendo ya Mitume 9:1-22).
- Petro anahubiri kwa Kornelio, mkuu katika jeshi la Rumi (Matendo ya Mitume 10:1-11:18).
- Barnaba anahudumu huko Antiokia, mji mkuu wa jimbo la Kirumi la Shamu (Matendo ya Mitume 11:22-30). Huduma hii ni muhimu kwa sababu mbili:
    - Barnaba anamtambulisha Sauli katika kanisa huko Antiokia. Huduma ya Sauli huko inafanya kazi muhimu sana katika maendeleo yake.
    - Kanisa huko Antiokia kimsingi likawa kanisa la karne ya kwanza linalotuma wamishenari. Kila safai ya Paulo ya kimishenari ilianzia Antiokia.

### Injili hadi Mwisho wa Dunia (Matendo ya Mitume 13-28)

#### *Safari ya kwanza ya Kimisheni (Matendo ya Mitume 13-14)*

Nusu ya mwisho ya Matendo ya Mitume inanakiri huduma ya mtume Paulo. Kufuatia kuokoka kwake, Paulo alitumia muda Arabuni, Dameski, na Kilikia. Na kisha aliletwa na Barnaba ili kufundisha katika kanisa huko Antiokia, kanisa lililoanzishwa na waamini waliofukuzwa kutoka Yerusalemu kutokana na mateso ya Sauli.

Tangu mwaka 47-49 B.K., Paulo na Barnaba, pamoja na binamu wa Barnaba Yohana Marko, walisafiri toka Kipro (Nyumbani kwa Barnaba) na Asia ndogo.[36] Sehemu kubwa ya safari hii ilielekezwa katika kupanda makanisa katika Galatia, jimbo la Kirumi katika Asia Ndogo. Kutoka katika safari hii kwenda mbele, Sauli alijulikana kama Paulo. Sauli lilikuwa jina la Kiebrania; Paulo lilikuwa jina la Kirumi. Mabadiliko haya ya matumizi ya majina yanaonesha wito maalumu wa Paulo wa kuwafikia mataifa.

Wakati wakiwa Perge katika Pamfilia, Yohana Marko aliwaacha na kurudi nyumbani (Matendo ya Mitume 13:13). Baada ya kusafiri umbali wa hadi Derbe, Paulo na Barnaba walirudisha hatua zao nyuma, kutembelea tena makanisa ambayo walikuwa wameyapanda kabla ya kurudi katika kanisa huko Antiokia.

#### *Baraza la Yerusalemu (Matendo ya Mitume 15:1-35)*

Wamataifa waliookoka kupitia huduma ya Paulo waliinua suala gumu katika kanisa. Kulikuwa na mgawanyiko katika ya Wayahudi waliokuwa wafuasi wa Yesu. Baadhi yao

[36] Anatolia ya Leo

walisisitiza kwamba Wamataifa ni lazima wafuate nyanja zote za Sheria ya Musa.[37] Wengine walikuwa na uhakika kwamba Sheria ya Musa haikuwabana Waamini wa Wamataifa.

Katika mwaka 49 B.K., viongozi wa kanisa walikutanika huko Yerusalemu ili kutatua tatizo. Wale ambao walitaka tohara kwa Wamataifa waliongea kwanza. Kisha Petro akazungumza kuhusiana na uzoefu wake katika nyumba ya Kornelio: "…[Mungu] hakufanya tofauti kati yetu sisi na wao, akiwasafisha mioyo yao kwa imani" (Matendo ya Mitume 15:9). Paulo na Barnaba walionesha ushahidi wa kazi ya Mungu kati kati ya Mataifa.

Yakobo, kiongozi wa kanisa la Yerusalemu, alihitimisha na maamuzi ya baraza kwamba waamini wa Mataifa watatakiwa kuepuka mambo manne:

- Kula nyama zilizotolewa kwa sanamu.
- Kula nyama zilizosongolewa.
- Kula nyama pamoja na damu ndani yake.
- Uzinzi na Uasherati.

Hii haikuwa orodha ya sheria ambazo Wamataifa walipata wokovu. Badala yake, ilikuwa ni mfano wa umoja kati kati ya waamini ambao wanatokea historia mbalimbali. Masharti yaliyohusiana na vyakula yaliwasaidia Wayahudi na Wamataifa kuweza kula pamoja, alama kuu ya umoja katika kanisa la kwanza. Msisitizo juu ya uasherati na uzinzi ulikuwa muhimu kwa sababu ya historia ya uasherati kwa wengi wa waamini wa Kimataifa.

Baraza la Yerusalemu lilitaka kuweka uwiano katika kanuni mbili. kanuni ya uhuru iliwazuia waamini wa Kiyahudi kuwaweka wanafunzi chini ya mzigo na matakwa yasiyo ya lazima ya Uyudaizimu (Matendo ya Mitume 15:10). Kanuni ya Ushirika iliwataka Wamataifa kuepuka mambo ambayo yatazuia ushirika pamoja na ndugu zao wa Kiyahudi.

► Ni kwa namna gani tunaweza kuzitendea kazi kanuni hizi leo? Ni kwa namna gani tunaweza kuruhusu uhuru wa dhamiri katika maeneo ambayo maandiko hayajatoa maagizo yeyote? Ni kwa namna gani tunaweza kuepuka kuwakosea wengine ambao wana msimamo ambao ni tofauti na wa kwetu?

### *Safari ya Pili ya Kimisheni (Matendo ya Mitume 15:36-18:22)*

Si kila mgogoro katika kanisa la kwanza ulihusisha kanuni za kitheolojia. Paulo na Barnaba waligawana njia kwa sababu ya kutokukubaliana kibinafsi kuhusiana na Yohana Marko (Matendo ya Mitume 15:36-41). Kutokukubaliana huku kunaonesha Mungu akiwa kazini hata katika mazingira binafsi. Sila akawa mtenda kazi wa thamani sana katika kanisa, na juhudi za Paulo na Barnaba zilizidishwa mara mbili kwa kazi zao baada ya kugawanyika. Paulo baadae alipatana na Yohana Marko (2 Timotheo 4:11).

Paulo na Sila walianza safari yake ya pili ya kimisheni kwa kutembelea tena makanisa yaliyopandwa na Paulo na Barnaba katika safari yake ya kwanza. Paulo na Sila pia

[37] Wakristo hawa walitoka katoka kundi la Mafarisayo (Matendo ya Mitume 15:5). Suala hili uya halikuwa mabishano ya kiulimwengu "Wayahudi dhidi ya Mataifa". Yakobo, Myahudi, aliongoza katika kutafuta suluhisho la tatizo.

walihudumu katika Filipi, Thesalonike, Beroya, Athene, na Korintho. Katika safari hii, Injili ilihubiriwa Ulaya baada ya Paulo kuona maonoo ya mtu kutoka Makedonia akiomba msaada (Matendo ya Mitume 16:9-10). Kijana Timotheo alijiunga na timu ya Paulo huko Listra, na Luka alijiunga na Paulo huko Troa.[38] Paulo alitumia takribani mizezi 18 kupanda kanisa huko Korintho. Timu ilirudi Antiokia baada ya zaidi ya miaka mitatu ya kusafiri (50-53 B.K.).

Safari ya pili ya kimisheni inaonesha upinzania ambao Paulo aliupata katika kuhubiri. Paulo na Sila waliwekwa gerezani huko Filipi (Matendo ya Mitume 16:23-39); nyumba waliyokuwa wanakaa huko Thesalonike ilivamiwa na kundi wa watu (Matendo ya Mitume 17:5-7); maadui toka Thesalonike walifuata hadi Beroya (Matendo ya Mitume 17:13); na Paulo alipandishwa mahakamani huko Korintho (Matendo ya Mitume 18:12-17).

Kukua kwa kanisa kulikuja na gharama kubwa. Shetani haachii himaya yake pasipo vita. Hata hivyo, Matendo ya Mitume inaonesha nguvu za Roho Mtakatifu na ushindi wa injili makanisa yalipopandwa katika Aisa yote, Makedonia, na Akaya.

### *Safari ya Tatu ya Kimisheni (Matendo ya Mitume 18:23-21:15)*

Paulo alitumia muda mfupi huko Antiokia kabla ya kuondoka ili kutembelea tena makanisa katika majimnbo ya Galatia na Frigia. Sehemu ya kwanza ya safari hii ilielekezwa katika kuimarisha waamini katika makanisa yaliyopandwa katika safari za mwanzoni (Matendo ya Mitume 18:23). Safari ya tatu ya kimisheni ilidumu tangu 53-57 B.K. muda mrefu sana (miaka mitatu) ulitumiwa huko Efeso. Wakati akiwa Efeso, Paulo aliandika nyaraka zote mbili za Wakorintho, akitatua matatizo katika kanisa hili gumu.

Baada ya kuondoka Efeso kutokana na upinzani kutoka kwa maadui, Paulo alisafiri kwenda Makedonia na Akaya. Alikusanya michango kutoka katika makanisa yaliyokuwa na Wamataifa wengi katika majimbo haya ili kuwasaidia wafuasi wa Yesu wa Kiyahudi huko Yerusalemu. Uthibitisho huu wa umoja wa kanisa unaonesha kwamba Wayahudi na Wamataifa walikuwa ndugu katika kanisa la Kristo.

### *Kukamatwa na Kufungwa (Matendo ya Mitume 21:15-28:31)*

Akirudi toka safari ya tatu ya kimisheni, Paulo alizuiwa huko Kaisaria[39] mahali ambapo nabii Agabo alimuonya kwamba atakamatwa huko Yerusalemu (Matendo ya Mitume 21:10-11). Sehemu ya mwisho ya Matendo ya Mitume inaeleza kuhusiana na kukamatwa kwa Paulo, kufungwa kwake huko Kaisaria, kukata rufaa kwenda Rumi (haki ya raia wa Kirumi), safari hatari kwenda Rumi (ikijumuisha kuvunjika kwa meli katika kisiwa cha Melita), na miaka miwili ya huduma huko Rumi akiwa chini ya nyumba ya kifungo.

Mwisho wa Matendo ya Mitume unaonesha kwamba agizo la Yesu toka Yerusalemu, Uyahudi, Samaria, na hata mwisho wa dunia lilitimilizwa. Akiwa katika nyumba ya kifungo,

[38] Katika Matendo ya Mitume 16:10, Luka anaanza na kutumia kiwakilishi "tu" badala ya "wa."
[39] Huu sio mji sawasawa na Kaisaria-Filipi. Badala yake, hii ni Kaisaria Maritima, mji mkubwa wenye bandari katika bahari ya Mediterranea katika pwani Uyahudi.

Paulo alikuwa huru kuhudumia, “akihubiri habari za ufalme wa Mungu, na kuyafundisha mambo ya Bwana Yesu Kristo, kwa ujasiri mwingi, asikatazwe na mtu” (Matendo ya Mitume 28:31). Pamoja na upinzani kutoka kwa viongozi wa Kiyahudi au serikali ya Rumi, Roho Mtakatifu alilitia nguvu kanisa ili kutimiliza Agizo la Kristo.

| **Ratiba ya Matukuio ya Huduma ya Paulo.** (Makadirio ya Tarehe.) | |
|---|---|
| **Tarehe** | **Tukio** |
| 33 B.K. | Uongofu wa Paulo |
| 35-46 B.K. | Paulo katika Arabuni, Dameski, na Kilikia |
| 47-49 B.K. | Safari ya kwanza (pamoja na Barnaba) |
| | Wagalatia iliandikwa |
| 49 B.K. | Baraza la Yerusalemu |
| 50-53 B.K. | Safari ya Pili (pamoja na Sila) |
| | 1 na 2 Wathesalonike ziliandikwa |
| 53-57 B.K. | Safari ya tatu (pamoja na Sila) |
| | Warumi, 1 na 2 Wakorintho ziliandikwa |
| 57-59 B.K. | Paulo alifungwa huko Kaisaria |
| | Paulo alipelekwa Rumi |
| 60-62 B.K. | Paulo chini ya nyumba ya kifungo huko Rumi |
| | Nyaraka za Kifungoni ziliandikwa |
| 64-65 B.K. | Paulo alifunguliwa toka gerezani |
| | Safari ya nne |
| | 1 Timotheo, Tito ziliandikwa |
| 66-67 B.K. | Kufungwa kwa mwisho kwa Paulo |
| | 2 Timotheo iliandikwa |
| | Paulo akauawa na Nero |

## Matendo ya Mitume katika Kanisa Leo

Injili ya Luka inaonesha umuhimu wa Roho Mtakatifu katika huduma ya Yesu ya duniani; kitabu cha Matendo ya Mitume kinaonesha umuhimu wa Roho Mtakatifu katika huduma ya kanisa. Baadhi ya nyanja za uzoefu wa kanisa la kwanza zinaweza kuzidishwa pasipo uwepo wa Roho Mtakatifu. Tunaweza kusoma Biblia kwa nguvu zetu, tunaweza kudumisha baadhi

ya viwango vya ushirika wa kanisa kwa nguvu zetu; hata pia tunaweza kufanya ishara na maajabu bandia kwa nguvu zetu. Lakini kusipokuwa na uwepo wa Roho Mtakatifu kati kati yetu, hatutaweza kuwa na uhalisia wa picha katika Matendo ya Mitume.

Kukua kwa kanisa kwenda tamaduni zingine katika Matendo ya Mitume kunatoa mfano kwa ajili ya kanisa la leo. Pentekoste ilileta waamini wapya kutoka Ulaya (Rumi), Asia (Parthia na Media), na Africa (Misri na Libia) katika kanisa changa. Lengo la uinjilisti leo linatakiwa kuwa lile lile: kusambaza injili ya Yesu Kristo zaidi ya mipaka ya kitamaduni. Matendo ya Mitume inatoa mfano kwa ajili ya kanisa ambalo linafungamanisha waamini wote katika mwili wa Kristo.

Matendo ya Mitume inaonesha kanisa ambalo linajumuisha tamaduni tofauti tofauti zikifanya kazi kwa umoja. Mgogoro unapoinuka, kanisa linajifunza kutafuta suluhisho kupitia uongozi wa Roho mtakatifu . Kanuni za uhuru na ushirika zinazooneshwa katika Baraza la Yerusalemu zinatoa mfano kwa ajili ya kushughulika na masuala ya dhamira katika kanisa la leo. Kama Paulo anavyoelezea katika Warumi 14 na 1 Wakorintho 8, wafuasi wa Kristo wanapaswa kuepuka makosa mawili:

- Kanuni ya Uhuru ilihitaji kwamba tuepuke kuweka imani zetu binafsi kwa waamini.
- Kanuni ya Ushirika inahitaji kwamba tuepuke kutendea kazi uhuru wetu kwa gharama ya ndugu dhaifu.

Kunyenyekeana huko kulienda mbali zaidi katika kuondoa vikwazo kati kati ya ndugu wakristo.

Kwa makanisa yanayopitia mateso, ukuaji wa kanisa la kwanza katika mateso ni hamasa ya kubakia waaminifu. Zaidi ya kulisaidia kanisa kuendelea kuwepo, Mungu aliyatumia mateso kuwasambaza wanafuanzi kwenda nje ya Yerusalemu na kutimiza utume wake kwa kanisa. Tunapomruhusu Mungu kutenda kazi upitia sisi, atalijenga kanisa lake, hata katika nyakati za upinzani kutoka katika ulimwengu wetu.

## Hitimisho

Katika Matendo ya Mitume, tunaona badiliko la wanafunzi waliosita wakiwa wamekusanyika huko Yerusalemu ambao walikuja kuwa wainjilisti wenye ujasiri wakibubiri huko Rumi na maeneo zaidi ya Rumi. Matendo ya Mitume inaonesha nguvu ya Roho Mtakatifu ikifanya kazi katika kanisa.

Mojawapo ya ushuhuda wa nguvu ya kubadilisha ya Roho Mtakatifu ni katika maisha ya mitume. Kutoka kuwa watu waliokimbia wakati Yesu anakamatwa, wanafunzi hawa walikuja kuwa ni watu waliokubali kufa kwa ajili ya Bwana wao aliyefufuka. Ufupisho mfupi wa tamaduni kuhusiana na vifo vya mitume vinashuhudia nguvu ya kubadilisha katika siku ya Pentekoste. Wanafunzi walitia muhuri ushuhuda wao kwa damu zao:

- **Yakobo** aliuawa na Herode Agripa miaka 12 tu baada ya Pentekoste.

- **Simoni Petro** alisulubiwa. Kwa kuwa aliona hastahili kufa kifo kama cha Bwana wake, aliomba kusulubiwa kichwa chini miguu juu.
- **Andrea**, ndugu yake na Petro, alisulubiwa huko Akaya, karibu na Korintho.
- **Tomaso** alibadilishwa kutoka kuwa "Tomaso Aliyesita" hadi kuwa mtu mwenye kujitoa kiasi hicho kwamba aliende India kama mmishenari mahali ambapo alikufa kama mfia imani, pengine kwa kuchomwa mkuki.
- **Filipo** aliteswa na kusulubiwa huko Frigia.
- **Mathayo** alikatwa kichwa huko Nad-Davar karibu na Ethiopia.
- **Nathanaeli (Bartholomayo)** alipigwa viboko na kuteswa na kisha kusulubiwa.
- **Yakobo mdogo** alichukuliwa hadi kilele cha Hekalu ili amkane Yesu. Alipokataa, alirushwa kutoka Hekaluni.
- **Simoni Mkananayo** alisulubiwa huko Shamu baada ya kuhubiri huko Misri na Uajemi.
- **Yuda Thadayo** alipigwa hadi kufa alipokuwa anamuhubiria kuhani wa kipagani huko Mesopotamia.
- **Mathiya** alichaguliwa ili kuziba pengo la Yuda Iskariote. Alihubiri Ethiopia na kisha kupigwa kwa mawe akiwa amesulubiwa msalabani.
- **Yohana** ni mtume pekee aliyekufa kifo cha kawaida. Hata hivyo, alitumia miaka kadhaa akiwa uhamishoni katika kisiwa cha Patmo.

Kwa kuhitimisha, tafadhali zingatia, "Ni nini Mungu anataka kufanya kupitia kanisa leo?" Kulikuwa na wanafunzi 120 katika Pentekoste; kwa wakati huo, takribani watu milioni 45 waliishi katika Dola ya Rumi. Kutokana na mtazamo wa kibinadamu, kazi ya kuuhubiri ulimwengu huu ingekuwa haiwezekani. Cha kushangaza, mwishoni mwa karne ya kwanza, injili ilikuwa imesambaa kutoka waamini 120 waliojazwa na Roho Mtakatifu kwenda kila kona ya Dola ya Rumi. Ni nini Mungu anataka kufanya kupitia kanisa leo?

## Somo la 4 Mazoezi

(1) Chagua moja katika ya mazoezi yafuatayo:

- Mwanzoni katika somo hili uliombwa kuzingatia orodha ya shughuli za kanisa la kwanza. Ulitakiwa kuamua endapo kila shughuli ilikuwa maelezo tu ya kanisa la kwanza au yalikuwa pia ni maelekezo kwa ajili ya nyakati za leo. Kwa kila mojawapo zingatia maelekezo, tafuta angalau rejea ya andiko moja ambalo linaagiza kwa uwazi na ufasaha shughuli hiyo.

- Kwa kutumia mahubiri ya Petro katika Matendo ya Mitume 2 au ujumbe wa Paulo katika Matendo ya Mitume 17, andika insha ya ukurasa mmoja ukifupisha mada kuu za mahubiri ya mitume.

(2) Mwanzoni mwa somo linalofuata, utafanya jaribio kulingana na somo hili. Soma maswali ya jaribio kwa umakini katika maandalizi.

## Somo la 4 Jaribio

(1) Kwa nini Efeso ni eneo la kimkakati kwa Paulo kupanda kanisa?

(2) Kwa nini Rumi ni eneo la kimkakati kwa Paulo Paulo kuhubiri?

(3) Ni watawala gani wa Rumi walilitesa kanisa la kwanza?

(4) Kwa nini inaonekana kwamba Matendo ya Mitume iliandikwa mwishoni mwa miaka ya 50 au mwanzoni mwa miaka ya 60?

(5) Ni nini kilikuwa kiini cha ujumbe mkuu uliohubiriwa na mitume?

(6) Nani alikuwa mfia imani wa Kwanza?

(7) Ni kwa namna gani Injili ilisambaa zaidi ya Yerusalemu?

(8) Ni kanisa gani lenye utamaduni tofauti tofauti ambalo lilikuwa kimsingi lilikuwa ni kanisa linalotuma wamishenari wakati wa kati kati ya marne ya kwanza?

(9) Ni mambo gani manne ambayo Baraza la Yerusalemu liliwahitaji Waamini wa Mataifa kuepuka?

(10) Ni nini matokeo chanya ya kutokukubaliana kati ya Paulo na Barnabas katika Matendo ya Mitume 15?

(11) Andika Matendo ya Mitume 1:7-8 kutoka katika kumbukumbu.

# Somo la 5
# Warumi
# Haki ya Mungu

## Malengo ya somo

Mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kufahamu tarehe na kusudi la Warumi.

(2) Kufupisha mafundisho ya msingi ya Warumi.

(3) Kufahamu uhusiano kati ya hukumu na injili.

(4) Kuyaishoi mafundisho ya Paulo kuhusu uhuru wa mwamini kutoka dhambi ya kukusudia.

(5) Kuhusianisha ujumbe wa Warumi na mahitaji ya ulimwengu wa leo.

## Maandalizi kwa ajili ya Somo hili

► Soma Warumi.

► Kariri Warumi 1:16-17.

## Utangulizi

Hakuna kitabu kingine cha Biblia kilicho na mchango kubwa zaidi kwa kanisa kuliko barua ya Paulo kwa Warumi. Uamsho katika vipindi vitatu vikubwa ulianza na kujifunza Warumi.

> "[Warumi] ni injili safi. Inastahili kwa Mkristo si tu kukariri neno kwa neno lakini pia kujijaza mwenyewe na hiyo kila siku, kana kwamba ni mkate wa kila siku wa nafsi. Haiwezekani kuisoma au kuitafakari kwa kiasi kikubwa au kikamilifu. Kwa kadiri mtu anavyoshughulika nayo, ndivyo inavyokuwa ya thamani na tamu zaidi."
>
> \- Martin Luther
> "Preface to Romans".

Katika siku za giza zinazozunguka kuanguka kwa Dola ya Rumi, uamsho katika kanisa la kikristo uliongozwa na Augustine. Augustine alihusisha ukombozi wake kutoka utumwa wa dhambi na yeye kusoma kitabu Warumi. Kitabu cha Warumi kilimfundisha Augustine kuhusiana na uwezo wa Mungu wa kukomboa kutoka kwenye dhambi.

Katika wakati ambao Romani kathoriki walipolipeleka kanisa katika utumwa ibaada za Mila na mafundisho potofu, Martin Luther alijifunza kutoka Warumi 1:17 kwamba "haki ya Mungu ni haki ambayo, ipatikanayo kwa neema na rehema thabiti Mungu hutuhesabia haki kwa njia ya imani…."[40] Warumi ilimfundisha Martin Luther kuhusu nguvu ya Mungu kuhesabia haki kwa njia ya imani.

[40] Imenakiliwa kwa Roland H. Bainton, *Here I Stand: A Life of Martin Luther* (Nashville: Abingdon Press, 1950), 49-50

Katika karne ya 18 Uingereza , ilikuwa haikuwa ya kawaida kwa kudai wakristo kuamini huo uhakika binafsi wa wokovu kuwa unawezekana. John Wesley aliongeza uhakika wa Imani kupitia somo lake la Warumi na kuanzisha uamsho ambao bado unaathiri ulimwengu hivi leo. Warumi ilimfundisha John Wesley kuhusu nguvu ya Mungu ya kutoka.

## Usuli wa Warumi

### Tarehe

Warumi iliandikwa wakati wa safari ya tatu ya Paulo ya kimisheni, takribani mwaka 57 B.K. Paulo akiwa Korintho. Ingawa Paulo hakuwa ametembelea Rumi, hitimisho la barua huonyesha kwamba Paulo aliwafahamu washirika wengi wa kanisa la Rumi. Alitumaini kutembelea Rumi, lakini alipaswa kwanza kwenda Yerusalemu kutoa misaada ya sadaka zilizotolewa na makanisa ya Asia ndogo (Warumi 15:23-28). Alipokuwa Yerusalemu, Paulo alikamatwa na kupelekwa Rumi kama mfungwa.

### Kusudi

Paulo alikuwa na makusudi matatu ya kuandika Warumi:

1. Kusudi la haraka: kuhutubia kuhusiana na kanisa la Rumi.
2. Kusudi binafsi: kueleza malengo yake yajayo kwa ajili ya Uinjilisti.
3. Kusudi la mwisho: kuwafundisha namna gani watu wanafanywa kuwa wenye haki kwa Mungu.

Kusudi la haraka la Paulo lilikuwa ni kuhutubia kuhusiana na wasiwasi wa kanisa ambalo lilijumuisha Wayahudi na Wamataifa. Kanisa la Rumi lilianzishwa na Wayahudi, pengine waongofu walirudi kutoka Yerusalemu baada ya Pentekoste. Katika mwaka 49B.K., mtawala Klaudio aliwafukuza Wayahudi kutoka Rumi (Matendo ya Mitume 18:2).[41] Wayahudi waliporudi Rumi miaka michache baadae kanisa likawa na makumdi mawili: Wayahudi waliogundua sheria ya Musa na Mataifa ambao waliokuwa wamezoea kuishi kwa uhuru bila vikwazo vya sheria. Paulo alihutubia maswali ambayo yalilihusu kanisa hilo lililoundwa na wote Wayahudi na Mataifa:

- Je! Wokovu hupatikana kwa njia ya kutii sheria?
- Ni nini malengo ya Israeli kama watu wa Mungu?
- Namna gani wafuasi wa Kristo wanapaswa kushughulikia mitazamo tofauti katika maswala kama vile sheria ya chakula?

Mwishoni Warumi inaonyesha maukumo binafsi wa Paulo wa kuandika. Paulo alikuwa na shauku kuhusu mkakati wa kufikia vituo vya ulimwengu wa Rumi na injili. Tangu Spania ilipoongezeka kuwa sehemu muhimu ya himaya ya Rumi, Paulo alitaka kuhubiri pale. Barua

[41] Mwana historia Suetonius aliandika kwamba tangazo hili lilitolewa kwa sababu ya machafuko ambayo yalitokea miongoni mwa Wayahudi juu ya *Christos*. Kwa sababu *Christos* ni matamshi ya Kilatini ya Kristo, inaonekana pengine mgogoro huu ulikuwa kati ya Wayahudi na Wakristo.

hii iliwasilisha mipango yake kuitumia Rumi kama msingi wa kazi yake ya kampeni za kiinjilisti Spania (Warumi 15:24).

Kusudi na mwisho la Paulo lilikuwa ni kuwafundisha namna gani tunafanywa wenye haki mbele za Mungu. Wayahudi wafuasi wa Kristo walijifunza kwamba kuhesabiwa haki hakukuja kwa njia ya utii wa sheria; bali kwa neema kwa njia ya imani tu. Waumini wa mataifa walikumbushwa kwamba Mungu alichagua kufanya kazi kupitia Wayahudi; walipaswa kuheshimu ndugu zao wa kike na wa kiume. Waumini wote Wayahudi, au Wamataifa, ni wenye haki kwa Mungu kwa sababu ya neema tu.

## Yaliyomo katika Warumi

### Utangulizi: Nguvu ya injili kwa ajili ya wokovu (Warumi 1:1-17)

Wasomaji wakati mwingine huruka utangulizi ilikupata sehemu kuu ya kitabu. Hata hivyo katika Biblia hata utangulizi ni wa muhimu. Ni Neno la Mungu lililovuviwa na "…lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki" (2 Timotheo 3:16). Utangulizi wa Paulo mara nyingi hutoa taarifa ambayo ni kiini cha kusudi lake. Katika utangulizi wa Warumi, tunajifunza kweli nne ili kujua injili:

- Injili ilitabiriwa katika Agano la kale.
- Injili ilimtangaza YESU kama masihi. Alikuwa:
    - Mwana wa Daudi.
    - Mwana wa Mungu.
    - Alifufuliwa kutoka wafu.
- Injili ni nguvu ya Mungu iletayo wokovu kwa yoyote aaminiye, Myahudi na Mmataifa.
- Injili hufunua haki ya Mungu.

### Haki ya Mungu inafunuliwa katika hukumu (Warumi 1:17-3:20)

► Kwa nini ukweli wa hukumu ni wa lazima kwenye habari njema ya injili?

Paulo anaanza na habari mbaya ya hukumu; wanadamu wote watasimama mbele ya Mungu mwenye haki, mataifa, waadilifu na wayahudi.

> "Hawawezi kuikubali neema hadi watakapotetemeka mbele za sheria ya haki na takatifu."
>
> - Charles Spurgeon.

Katika Warumi 1:18-32, Paulo anaandika kuhusu dhambi ya mataifa, hasa wapagani ambao "…wakaubadili utukufu wa Mungu asiye na uharibifu kwa mfano wa sura ya binadamu aliye na uharibifu…" (Warumi 1:23). Katika kipindi hiki, Paulo anahutubia dhambi ambayo wasomaji wake wa kiyahudi wangeizingatia kuwa ni Dhambi ya mataifa kama vile: ibaada ya sanamu, uzinzi, uuwaji, na ukatili. Paulo anawaonya wote ambao wanafanya dhambi hizo wanastahili kifo.

Katika Warumi 2:1-16, Paulo anajadili kuhusu **waadilifu**. Hawa ni watu ambao hudhania kuwa ni wema. Huwalaani wapagani wa mataifa wanaozungumziwa katika Warumi 1, lakini ni wao wenyewe pia wenye hatia ya dhambi.

> "Hatuwezi kuja kwa Kristo ili kuhesabiwa haki kabla ya kuwa kwa Musa kwanza ili kuhukumiwe."
>
> - John Stott.

Katika Warumi 2:17-3:8, Paulo anazungumza kwa wasikilizaji wake wakiyahudi. Kupitia mfululizo wa maswali ya kejeli, Paulo analinda haki ya Mungu katika kuwahukumu **Wayahudi** ambao wametenda dhambi chini ya sheria.

Katika Warumi 3:9-20, Paulo anahitimisha, "…Hakuna mwenye haki hata mmoja" (Warumi 3:10). Wanadamu wote watahukumiwa mbele ya Mungu Mtakatifu.

**Haki ya Mungu inafunuliwa katika wokovu (Warumi 3:21-8:39)**

Kufuatia taarifa mbaya ya kuhukumiwa, Paulo anahamia katika habari njema (injili) ambayo tunafanywa wenye haki mbele za Mungu si kwa matendo, lakini kupitia "haki ya Mungu iliyo kwa njia ya imani katika Yesu Kristo…" (Warumi 3:22). Paulo anaonyesha namna haki ya Mungu inavyofunuliwa katika wokovu na mabadiliko ya waamini.

***Kuhesabiwa haki kupitia Imani tu (Warumi 3:21-5:21)***

Kama Ibrahimu alihesabiwa haki kwa njia ya imani tu, tunahesabiwa haki kwa njia ya imani, na si kwa mtendo. Tuna amani na Mungu kupitia upatanisho uliotokana na kifo cha YESU Kristo. Kupitia yeye, tuna furaha katika tumaini la utukufu. Kupitia yeye tunao uzima. Paulo anaonyesha kwamba Myahudi wala Myunani hana sababu ya kujisifu, isipokuwa katika neema na huruma iliyotolewa na Mungu kupitia YESU Kristo. Haki ya Mungu inafunuliwa katika neema ya bure waliyopewa wanadamu wote.

***Haki na dhambi (Warumi 6)***

Sikia furaha ya ushuhuda wa Paulo katika nguvu ya neema, masomaji ni lazima aulize, "Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi?" (Warumi 6:1). Mojawapo anaweza kushambulia mafundisho ya Paulo ya neema kwa kulalamika kwamba itapelekea mtu kuendelea kuishi katika mapenzi ya dhambi. Paulo anajibu kwa maisitizo, "Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi?" (Warumi 6:2). Tulipokuwa tukibatizwa katika Kristo, tuliifia dhambi. Kwa sababu ya neema, hatuishi tena chini ya nguvu ya dhambi. Miili yetu si vyombo vya kutokuwa na haki; kupitia nguvu wokovu, miili yetu imetolewa kwa Mungu kama vyombo vya haki (Warumi 6:18). Haki ya Mungu inafunuliwa katika nguvu zake kutuweka huru kutoka dhambini.

***Dhambi na sheria (Warumi 7)***

► Soma Warumi 7. Ni nani anaelezwa katika sura hii?

Kwa sababu tulihesabiwa haki bure kupitia neema ya Mungu, sasa tuna "…tumika katika njia mpya ya Roho na si katika njia ya zamani ya andiko" (Warumi 7:6). Msomaji wa

kiyahudi anaweza kumuuliza Paulo, "Je! Ni nini Unasema? Je! Sheria ni dhambi?" Katika swali hili, Paulo anajibu, "Hasha!" (Warumi 7:7). Sheria inafafanua dhambi. Katika kufanya hivyo, inatuamsha sisi katika uhalisia wa dhambi na kuamsha mioyo yetu ya uasi kwa shauku ya dhambi. Sheria ambayo Mungu alitupa kwa faida yetu, imegeuka na kuwa chombo cha maovu.

Paulo anaonyeaha kanuni hii katika kifungu ambacho kimekuwa moja ya kipindi cha majadiliano ya Warumi. Kuna tafsiri tatu tofauti za Warumi 7:7-25:

1. **Paulo anafafanua maisha ya kawaida ya kikristo**. Baadhi wa watoa maoni wanasema kwamba Paulo anaonyesha maadili ya maisha ya waamini ambao wana shauku ya kutunza sheria ya Mungu lakini haiwezekani kufanya hivyo. Ni vigumu, hata hivyo kupatanisha picha ya utukufu ya maisha ya haki yaliyoelezewa katika Warumi 4-6 (Warumi 5:1, Warumi 6:18) na utumwa ulioelezewa katika Warumi 7 (Warumi 7:24).
2. **Paulo anafafanua maisha ya waamini ambao hawajajisalimisha kwa Roho Mtakatifu.** Tena, Kuna magumu katika kupatanishaa mtazamo huu na picha ya Paulo ya waumini washindi wanaoishi kwa amani na Mungu.
3. **Paulo anafafanua maisha ya wanaotenda dhambi wanaomtafuta Mungu**. Mababa wa kanisa la Kwanza waliona hii sura kama picha ya hali ya kabla kuokoka kwa Paulo, wakati alipojaribu kutunza sheria katika nguvu zake mwenyewe. Ni picha ya mtenda dhambi ambaye anatambua matendo yake, lakini ambao hawajahesabiwa haki bado kwa neema kwa njia ya imani. Huyu mtu anatafuta haki katika baadhi ya njia lakini Bado hajapata uzoefu wa furaha ya Warumi 8:1: "Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu."

### *Utakaso: Misha katika Roho (Warumi 8:1-17)*

Jibu katika mapambano ya Warumi 7 ni nguvu ya Roho. "Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti" (Warumi 8:2). Badala ya kutamani kujaribu kutunza sheria kwa nguvu zetu, tunawezeshwa na Roho kuyafisha matendo ya mwili (Warumi 8:13). Sauti ya ushindi wa Warumi 8 ni alama tofauti ya mapambano ya Warumi 7. Kwa nini? "Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu" (Warumi 8:16). Maisha haya ya ushindi yasiyo katika Warumi 7, ni mfano wa Paulo kwa uzoefu wa wakristo.

Maisha ya ushindi hayaishwi kwa nguvu zetu wenyewe, lakini katika nguvu za Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu anatukomboa sisi kutoka katika utumwa wa dhambi (Warumi 8:2), hutupa uhakika wa wokovu (Warumi 8:15-16), na huongoza maombi yetu (Warumi 8:26). Maisha ya waamini yanaongozwa katika nguvu za Roho Mtakatifu.

### *Uhakika wa Tumaini (Warumi 8:18-39)*

Kilele cha mafundisho ya Paulo juu ya wokovu ni sherehe yake ya utukufu ambao unawasubiri waumini wote. Paulo anaandika "…mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu" (Warumi 8:18). Anawatia moyo wasomaji wake na ahadi kwamba, "…katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake" (Warumi 8:28). Na anatukumbusha kwamba tumaini letu linatoka kwa Mungu aliyefanya wokovu wetu kuwezekana: "…Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu?" (Warumi 8:31).

Ni Mungu ambaye anatuhesabia haki; ni Mungu ambaye anatutunza. Paulo anasherekea ujasiri wetu kama watoto wa Mungu:

> Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu (Warumi 8:38-39).

### Haki ya Mungu inafunuliwa katika Uchaguzi (Warumi 9-11)

Swali lingine ambalo lilitokea baada ya mtu kumsikiliza Paulo akifundisha ni, "vipi kuhusu Israeli? Je! Mungu ameshindwa katika ahadi zake kwa watu wake wateule?" katika Warumi 9-11, Paulo anaeleza kwamba asili kutoka kwa Ibrahimu inatokana na imani, si kwa kabila la asili (Warumi 9:6-8). Mungu hajawaacha Israeli; badala yake, Mungu anafanya kazi kupitia Israeli kubariki mataifa yote. Baraka za mataifa zilitabiriwa kwa Ibrahimu (Mwanzo 12:3) na zikatangazwa na manabii wa Israeli;[42] Na sasa zinatimizwa miongoni mwa mataifa (Warumi 11:11). Baraka za Mungu kwa mataifa si kukataliwa kwa mwisho kwa Israeli. Kusudi lake kwa Israeli litatimizwa.

Warumi 9-11 inashighulikia tatizo la kutokuamini la Israeli kwa kutumia kweli tatu:[43]

1. **Ahadi za Mungu mara zote zilikuwa ni kwa ajili ya waamini**. Ahadi kwa Israeli hapo zamani zilikuwa ni kwa ajili ya wale wote walioamini (Warumi 9:6-29).
2. **Israeli imekuwa ikikataliwa kutokana na kutokuamini kwake**. Katika wakati uliopo, Wamataifa wamepokea haki ambayo ni kwa njia ya Imani, wakati Israeli hawajapata haki kwa sababu wameitafuta kupitia matendo ya sheria (Warumi 9:30-10:21).

[42] Isaya 56 ni mojawapo ya mifano mingi.
[43] Ilichukuliwa kutoka William M. Greathouse na George Lyons, *Romans: A Commentary in the Wesleyan Tradition* (Kansas City: Beacon Hill Press, 2008).

3. **Kukataliwa kwa Israeli ni kwa mudu tu, si mwisho**. Mungu hajazisahau ahadi zake. Mbeleni Israeli wataokolewa watakaporudisha Imani yao kwa Mungu (Warumi 11).

Paulo anamalizia sehemu hii ya Warumi na Sifa na kuabudu ambapo anamsifu Mungu kwa Hekima yake isiyochunguzwa, ufahamu, hukumu na njia zake (Warumi 11:33-36). Wakati ambapo hatuelewi kabisa njia za Mungu, tunamsifu Yeye kwa sababu tunaamini wema wake na haki yake. Njia zake zinastahili sifa zetu. "Kwa kuwa vitu vyote vyatoka kwake, viko kwa uweza wake, tena vinarejea kwake. Utukufu una yeye milele. Amina" (Warumi 11:36).

**Haki ya Mungu inaonekana katika maisha ya mwamini (Warumi 12:1-15:13)**

Theolojia ya Paulo wakati wote ni ya matendo. Baadhi ya barua za Paulo zimegawanyika katika sehemu kuu mbili. Katika sehemu ya kwanza, Paulo anafundisha kile tunachokiamini; katika sehemu ya pili, anafundisha namna gani tunaweza kuishi. Mfano huu unaweza kuonekana katika Warumi:

1. **Mafundisho**. Paulo anafundisha namna gani mtu anafanya kuwa mwenye haki mbele za Mungu (Warumi 1-11).
2. **Kuyaishi**. Paulo anafundisha namna gani mtu mwenye haki ataishi (Warumi 12-16).

Warumi 12-15 inatuonyesha namna ambavyo tunaweza kuziishi kanuni za Warumi 1-11 katika maisha ya kila siku. Katika Warumi 12, Paulo anawatia wasomaji wake wajitoe wao wenyewe kama dhabihu hai takatifu kwa Mungu. Haki ya Mungu inaonekana katika kuhesabiwa haki na kutakaswa na kubadilishwa katika maeneo yote ya maisha. Anayetembea katika Roho kuliko mwili ataonyesha haki ya Mungu katika maisha ya kila siku. Paulo anatambua baadhi ya vipengele vya matendo ya njia hii mpya ya kuishi:

- Tunatumia vipawa vyetu vya kiroho kuhudumia wengine (Warumi 12:3-8).
- Tunaingiliana na wengine tukiwa tunafanana na Kristo (Warumi 12:9-21).
- Tunatii mamlaka inayoongoza (Warumi 13:1-7).
- Tunatimiza sheria kwa njia ya upendo (Warumi 13:8-14).
- Hatuwahukumu ndugu zetu (Warumi 14:1-12).
- Hatutumii uhuru wetu katika njia ambayo itasababisha ndugu zetu wadhaifu kuanguka (Warumi 14:13-23).
- Tunafuata mfano wa Kristo (Warumi 15:1-13).

**Hitimisho (Warumi 15:14-16:27)**

Katika hitimisho lake, Paulo anashirikisha mipango yake kutembelea Rumi njiani kuelekea Spania. Alitumaini kwamba Rumi itakuwa ndio msingi wa misheni yake kwenda Spania. Alituma salamu kwa watendakazi wenzake, na kama ilivyo desturi katika barua za Paulo

alihitimisha na Sifa na kuabudu (Warumi 16:25-27). Anamsifu Mungu kwa ajabu ambazo alijifunua: Injili ni kwa ajili ya watu wote. Haki ya Mungu imekwisha kufunuliwa, na wote wanao amini wanaokolewa (Warumi 1:16-17).

## Warumi katika kanisa la leo

Warumi inafundisha kanisa la leo kuhusu umuhimu wa mafundisho sahihi. Kumbuka kwamba Paulo aliandika waraka huu kwa wafuasi wa kwanza wa YESU Kristo. Katika nyakati ambazo waamini wanahudumiwa kama watoto wachanga kiroho ambao hawawezi kula nyama ya kweli ya Biblia, Warumi inaonyesha washirika hao wanaweza kupatiwa mafundisho kwa undani.

Warumi pia inafundisha kanisa la leo kuhusu kuyaishi mafundisho katika maisha ya kila siku. Paulo anaonyesha hakuna mvuto katika kujadili mafundisho kwa kutafuta midahalo ya kiakili tu. Anafundisha mafundisho ili kubadilisha maisha ya waamini.

Baada ya kweli kuu za Warumi 1-11, Paulo anaendelea, "Basi...nawasihi…" (Warumi 12:1). Neno *basi* linaunganisha kile alicho kiandaa kusema na kile alichokwisha kusema. Tungeliweza Kufupisha: "kwa sababu ya kweli hizi (haki, utakaso na uchaguzi), ninakutaka wewe ujitoe kama dhabihu hai kwa Mungu ambaye amekupa baraka hizi. Hivi ndivyo mabadiliko haya yatakavyo onekana katika maisha yako ya kila siku." Paulo anaendelea na kuyaishi kwa vitendo mabadiliko haya katika Warumi 12-15. Haitoshi tu kuwa na mafundisho sahihi; tunapaswa kuyaishi mafundisho hayo katika maisha yetu ya kila siku.

## Hitimisho

Jumatano ya, mei 24, 1738, John Wesley alihudhuria mkutano wa wamoroviani katika mtaa wa Aldersgate huko uingereza. Wesley alisumbuka kwa miaka, kutafuta uhakika wa wokovu. Kama wengi wakati huo, wakiamini kwamba haki ililenga uwezo wa mtu kuishi maisha ya haki. Alipokuwa akimsikiliza William Holland alisoma kutokea kwenye "utangulizi kwa Warumi," kutoka kwa Martin Luther Wesley Alibadilishwa. Wesley baadae akaandika:

> Wakati wa jioni, nilikwenda kwenye kusanyiko pasipo kutaka ambapo mmoja alikuwa akisoma utangulizi wa Luther wa waraka wa Warumi. kuhusu [8:45 pm], wakati wasomaji walipokuwa wakielezea mabadiliko ambayo Mungu alikuwa akiyafanyia kazi ndani ya mioyo kupitia Imani katika Kristo, nilihisi joto moyoni mwangu. Nilihisi natakiwa kuamini katika Kristo tu kupata wokovu; na **uhakika nilioupata ni kwamba ameondoa dhambi zote, hata zangu, na ameniokoa kutoka katika sheria ya dhambi na mauti**.[44]

Usiku huo, John Wesley alielewa ukweli wa Warumi 1:17, "Mwenye haki ataishi kwa imani." Ukweli huu mkubwa ulileta uamsho ambao ulisambaa kupitia Uingereza na ulimwengu kote.

[44] John Wesley, *The Journal of John Wesley*, May 24, 1738.

## Somo la 5 Mazoezi

(1) Chagua moja katika ya mazoezi yafuatayo:

- Andaa ujumbe au somo la Biblia juu wa kuhesabiwa haki kwa imani kutoka katika kitabu cha Warumi. Unaweza kuwasilisha hii ama katika maandishi (kurasa 5-6) au wasilisha rekodi ukiwa unahubiri au kufundisha.
- Andika muhtasari wa ukurasa mmoja wa kitabu cha Warumi ambacho kinaonesha vyote viwili mafundisho ya Warumi 1-11 na matumizi ya Warumi 12-16. Huu unatakiwa kuwa muhtasari wako binafsi, sio ule uliochukuliwa kutoka kitabu cha mafafanuzi au kujifunza Biblia.

(2) Mwanzoni mwa somo linalofuata, utafanya jaribio kulingana na somo hili. Soma maswali ya jaribio kwa umakini katika maandalizi.

## Somo la 5 Jaribio

(1) Orodhesha makusudi matatu ya Paulo kuandika Warumi.

(2) Orodhesha kweli nne kuhusiana na Injili zinazopatikana katika utangulizi wa Warumi.

(3) Orodhesha makundi matatu ambayo yanahukumiwa katika Warumi 1-3.

(4) Katika Warumi 6, mwitikio wa Paulo ni nini kwa mtu ambaye atauliza kama tutaendelea kutenda dhambi ili neema izidi kuwa nyingi?

(5) Katika sentensi moja, orodhesha tafsiri tatu za Warumi 7:7-25.

(6) Paulo anaitikia tatizo la kutokuamini la Israeli kwa kutumia kweli tatu. Orodhesha kweli hizo.

(7) Kutoka Warumi 12-15, orodhesha vipengere vya kivitendo vya kuiishi haki ya Mungu.

(8) Andika Warumi 1:16-17 kutoka katika kumbukumbu

# Somo la 6
# Wakorintho na Wagalatia
# Barua kwa Makanisa Yenye Shida

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kujua tarehe na makusudi ya Wakorintho wa 1 na 2 na Wagalatia.

(2) Kutoa muhtasari wa dhamira kuu ya Wakorintho wa 1 na 2 na Wagalatia.

(3) Kuelewa masuala muhimu ya kutafsiri Wakorintho wa 1.

(4) Kujadili mahusiano kati ya mwamini na sheria.

(5) Kutambua maana ya kibiblia ya imani kwamba watu wanaokolewa kwa kushika sheria.

(6) Kutambua maeneo ya migogoro na mkanganyiko katika kanisa la mwanzo.

(7) Kuhusianisha ujumbe wa vitabu hivi na mahitaji ya dunia ya leo.

## Maandalizi kwa ajili ya Somo hili

► Soma Wakorintho wa 1 na 2 na Wagalatia.

► Kariri 1 Wakorintho 1:20-21 and Wagalatia 5:22-23.

## Utangulizi

Wasomaji wa kisasa mara kadhaa hudhani kuwa kanisa la kwanza lilikuwa huru mbali na matatizo makubwa. Tunadhani, "Ingekuwa nzuri sana na ajabu kuishi katika kanisa la kwanza ambapo kila kitu kilitendeka katika umoja na kujawa na uamsho" Lakini barua za Paulo kwa Korintho na Galatia zinaonesha picha ya tofauti sana. Makanisa ya karne ya kwanza yalipambana na fundisho la uongo, dhambi kati ya washirika, mkanganyiko kuhusu mafundisho ya muhimu ya Biblia, na maswali kuhusu mamlaka na nidhamu ya kanisa. Kwa maneno mengine, vitabu hivi vinaonesha ulimwengu unaofanana sana na ulimwengu wa leo. Kwa sababu ya hili, barua hizi kwa makanisa yenye shida ya karne ya kwanza zina mengi ya kufundisha makanisa yenye shida ya karne ya 21.

## 1 Wakorintho

### Usuli wa 1 Wakorintho

#### *Mwandishi na Tarehe*

Korintho ilikuwa ni bandari iliyoko kwenye sehemu ya ardhi kati ya bahari ya Aegea na Ionia. Shehena ilipakuliwa, kusafirishwa kuvuka ukanda mwembamba wa ardhi, na kupakiwa katika meli zilizokuwa upande mwingine. Eneo la kimkakati la Korintho lilitoa fursa

kubwa kwa kusambaa wa injili. Mahali ulipo uliwavuta mabaharia wengi ktuoka dola yote ya Rumi. Hii ilitoa fursa ya kuwahubiria Injili watu kutoka ulimwenguni kote.

Paulo alipanda kanisa Korintho wakati wa safari yake ya pili ya umisheni, mnamo mwaka wa 50 B.K. (Matendo ya Mitume 18:1-18). Pmoja na Akila na Prisila, waamini wawili toka Rumi, Paulo alitumia miezi 18 akihubiri Korintho. Alianza kwa kuhubiri katika sinagogi, Alipotolewa nje ya sinagogi, alihamia kwenye nyumba binafsi iliyokuwa karibu. Wakorintho wengi ikiwepo mtawala wa sinagogi, waliitikia mahubiri ya injili.

Paulo aliandika 1 Wakorintho kuhusu miaka mitano mbele. Barua iliandikwa wakati Paulo akikaa Efeso katika safari yake ya tatu ya umisheni (1 Wakorintho 16:8). Paulo aliandika kwa kujibu matatizo yaliyoibuka katika kanisa la Korintho. Kwa vile asingeweza kusafiri kwa haraka kwenda Korinhto, alituma barua kupitia Timotheo. Timotheo aliteuliwa pia kutoa maelekezo ya ziada wakati wa ziara yake (1 Wakorintho 4:17).

### *Muundo*

1 Wakorintho ni rahisi na vilevile ngumu kutafsiri. Ni rahisi kutafasiri kwa sababu iliandikwa kujibu hali fulani. Katika Warumi, Paulo alielezea masuala magumu ya kimafundisho kwa undani, lakini katika 1 Wakorintho, anashughulikia matatizo moja kwa moja.

Hata hivyo, barua ya aina hii pia yaweza kuwa ngumu kutafasiri kwa sababu hatuna barua kutoka katika kanisa la kikorintho. Lazima tujaribu kutambua matatizo ambayo kwayo Paulo anayajibu kwa kuangalia barua zake. Wakati mwingine, lazima tutofautishe kati ya ushauri wake na nukuu zake kutoka kwa Wakorintho.

Mifano miwili inaonesha jinsi gani Paulo anajibu maswali kutoka Korintho:

- 1 Wakorintho 7:1 inaanza, "Basi kwa habari ya mambo yale mliyoandika…" Paulo kisha anaandika kifungu ambacho huenda ni nukuu kutoka kwenye barua yao: "ni heri mwanamume asimguse mwanamke." Paulo kisha anajibu wazo hili (kuwa ni vizuri zaidi kwa wanaume na wanawake kuepuka mahusiano yoyote ya zinaa). Anasema, "Lakini kwa sababu ya zinaa kila mwanamume na awe na mke wake mwenyewe, na kila mwanamke na awe na mume wake mwenyewe" (1 Wakorintho 7:2).
- Vile vile, 1 Wakorintho 8:1 huanza, "Na kwa habari ya vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu…" Anachokisema Paulo baadae ni kama nukuu toka katika barua zao "sisi sote tuna ujuzi." Paulo anajibu, "…Ujuzi huleta majivuno, bali upendo hujenga" (1 Wakorintho 8:1).

### *Kusudi*

Barua ya kwanza ya Paulo kwa kanisa la Korintho ilichochewa na ripoti alizopokea kuhusu matatizo haya katika kanisa:

- Kulikuwa na matengano.

- Uasherati wa waziwazi ulikuwa ukivumiliwa.
- Mamlaka ya kitume ya Paulo yalikuwa yakipingwa.

Paulo aliandika 1 Wakorintho kujibu matatizo haya na kujibu maswali ya waamini.

**Yaliyomo katika 1 Wakorintho**

Katika utangulizi, Paulo anaeleza mamlaka yake kama mtume wa Yesu Kristo na kuwakumbusha waamini wa Korintho kuwa wametakaswa katika Kristo Yesu, na kuitwa kuwa watakatifu (1 Wakorintho 1:1-2). Pia anashughulikia muendelezo wa matatizo yanayoonesha kushindwa kwa wakorintho kuishi kulingana na wito wa Mungu kwa watu wake.

***Mgawanyiko (1 Wakorintho 1-4)***

Paulo alipanda kanisa Korintho. Mzungumzaji mwenye kipawa Apolo alihubiri baadae baada ya kuelekezwa na Akila na Prisila (Matendo ya Mitume 18:24-28). Yawezekana pia kuwa Petro alitembelea Korintho (1 Wakorintho 9:5). Kanisa lililoko Korintho liligawanyika katika makundi, na kila kundi likidai mmoja wa waalimu hawa kama kiongozi wao. Baadhi walidai kuwa juu ya mgawanyiko, "Mimi ni wa Kristo" (1 Wakorintho 1:12). Hata hivyo, hata kundi hili lilichochewa na roho ya kiburi, na si unyenyekevu. (1 Wakorintho 1:10-12).

Mambo yaliyojadiliwa baadae katika 1 Wakorintho yanaonesha kuwa mgawanyiko huu uliathiri ibada ya wiki na mashangilio ya chakula cha Bwana katika Korintho. Kwa kuongezea, mgawanyiko huu waweza kuwa sababu ya kanisa kutokuwa tayari kushughulikia dhambi kati ya waumini wake.

Paulo anaanza kwa kulinda huduma yake. Wale waliodai kumfuata Apolo walikataa mamlaka ya kitume ya Paulo na kudhihaki muonekano usiopendeza wa Paulo na usemi wake. Paulo anatetea mamlaka yake ya kitume ili kuweka jukwaa la kuhutubia matatizo katika kanisa. Kama baba wa kiroho, Paulo anapenda sana watoto wake (1 Wakorintho 4:14-15) kiasi cha kutowaacha wapotee katika njia zao. Kwa hiyo, Paulo anaanza na ulinzi mkali wa huduma yake: "Paulo, aliyeitwa kuwa mtume wa Yesu Kristo kwa mapenzi ya Mungu…" (1 Wakorintho 1:1).

Tangu baadhi ya waumini watofautishe hotuba rahisi ya Paulo na hotuba ya kuvutia ya Apolo, Paulo anaelezea, "…neno langu na kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali kwa dalili za Roho na za nguvu" (1 Wakorintho 2:4). Paulo hamvamii Apolo[45] lakini anaonesha kuwa huduma yake mwenyewe katika Korintho ilijikita katika nguvu za Roho Mtakatifu akifanyia kazi ujumbe wake. Wakorintho walikuwa wakijisifu kwa hekima ya kibidanamu; Paulo anawaita kurejea katika injili.

[45] 1 Wakorintho 16:12 inaonesha kuwa Paulo na Apolo waliungana katika kufanya kazi kwa ajili ya ufalme wa Mungu

### *Uasherati na Ukosefu wa Maadili (1 Wakorintho 5-6)*

► Ni kwa jinsi gani viongozi wa kanisa wangeshuhulikia dhambi waziwazi kati ya waumini?

Kama mji bandari wa Kirumi na mji uliojaa mahekalu ya kipagani yaliyohusisha ukahaba kama sehemu ya ibada zao za sanamu, Korintho ilijulikana kwa upotovu wake wa kizinaa. Neno *Corinthianize* ("kuwa mkorintho") lilimaanisha kuharibu maadili ya mtu.

Kanisa la Korintho lilikataa kunidhamisha moja kati ya waumini ambaye alikuwa akiishi katika uhusiano wa kiasherati na mama yake wa kambo, tabia ambayo hukataliwa hata na wapagani (1 Wakorintho 5:1). Kanisa la Korintho lilikuwa na kiburi kiasi cha kukataa kushughulikia tatizo hili.

Maelekezo ya Paulo ni muhimu katika kuelewa nidhamu sahihi ya kanisa. Paulo anataka kuwa wamtenge mkosaji kwa matumaini kuwa atatubu.[46] Kanisa linatakiwa kuhukumu dhambi kati ya waumini wake kwa sababu mbili: kumleta mtenda dhambi katika toba na kuepusha lawama na aibu dhidi ya injili. Paulo hashughulikii matendo ya wasioamini au hata aliyerudi nyuma na kutubu. Anahutubia kwa makusudi dhambi inayoendelea kwa muumini hai wa kanisa.

Kuhusiana na hili, Paulo pia anahutubia kesi za kisheria kati ya waamiini. Wakati Wakorintho wanakataa kuhukumu dhambi wazi katika kanisa, ni wepesi kuchukua malalamiko binafsi kwenda katika mahakama za umma. Paulo anauliza ni kwa jinsi gani wanaweza kuhukumu ulimwengu kama hawana hekima kutosha kuweza kutuliza migogoro kati ya ndugu Wakristo (1 Wakorintho 6:2).

### *Maswali kutoka kwa Wakorintho (1 Wakorintho 7:1-16:4)*

Paulo sasa anahutubia mfululizo wa maswali ambayo Wakorintho waliuliza katika barua waliyomtumia Paulo (1 Wakorintho 7:1). Kila mada inatangulizwa na kifungu, "Basi kwa habari ya…". Paulo ananukuu swali lao kisha anajibu hoja iliyoibuliwa.

*Useja na Ndoa (1 Wakorintho 7:1-24)*

Baadhi walifundisha kuwa "…ni heri mwanamume asimguse mwanamke" (1 Wakorintho 7:1). Paulo anajibu kuwa ndoa ni muktadha sahihi wa kujiweka wazi kimapenzi. Katika kipengele hiki, anaelezea pia tatizo la talaka, suala ambalo mahususi kabisa lilikuwa gumu kwa waamini wapya waliokuwa wameoa ama kuolewa na wasioamini.

*Wasioolewa na wajane (1 Wakorintho 7:25-40)*

Kwa sababu ya dhiki iliyopo, Paulo aliamini kuwa ilikuwa njema zaidi kwa wale ambao hawajaolewa kubaki katika hali ya kutoolewa. Hata hivyo, aliweka wazi kuwa hii ilikuwa ni mtazamo wake binafsi, na sio amri kutoka kwa Bwana. Wakati huo, waamini walikuwa

[46] "Kumtolea Shetani mtu huyo…" (1 Wakorintho 5:5) pia humaanisha kumtoa kutoka katika kanisa. Nje ya kanisa, yuko katika dunia, ulimwengu wa shetani.

wakiteswa na serikali ya Roma. Paulo angekuwa akiwaza pia kuhusu jinsi gani mateso yangeongezeka kabla ya kurudi kwa Bwana (1 Wakorintho 7:29).

*Chakula kilichotolewa sadaka kwa sanamu (1 Wakorintho 8:1-11:1)*

►Katika muktadha wa huduma yako, ni mazoea yapi ya kitamaduni ambayo yanaweza kulinganishwa na suala la Wakorintho la chakula lilichotolewa sadaka kwa sanamu?

Mjadala mrefu wa Paulo ni jibu kwa swali gumu la chakula kilichotolewa sadaka kwa sanamu. Wakorintho walikita mjadala wao juu ya ufahamu wao kuwa sanamu sio mungu wa kweli. Paulo anajibu hili kuwa badala ya kukita maamuzi yetu moja kwa moja kwenye ufahamu (ambao huleta kujiinua), tunatakiwa kutenda kwa upendo (ambao hujenga) (1 Wakorintho 8:1).

Paulo anatofautisha kati ya kula katika meza za mahekalu ya kipagani na kufanya manunuzi katika masoko ya umma, Kama mwamini mwenye ufahamu huu anakula katika ukumbi wa karamu katika hekalu, itamjaribu mwamini dhaifu (yule ambaye hana ufahamu huu) kula chakula kilichotolewa sadaka kwa sanamu. Kama mfano wa roho ambayo Wakorintho wanapaswa kuonyesha, Paulo anawakumbusha kuwa alitoa haki yake ya kutegemea msaada wa kifedha kama mchungaji wao ili kutoa injili katika mji wao (1 Wakorintho 9:12, 14-15). Katika namna ile ile, wanatakiwa kuwa tayari kuacha shughuli yeyote inayoweza kusababisha mtu mwingine kutenda dhambi (1 Wakorintho 8:9).

Zaidi, kula katika hekalu la kipagani ilikuwa ni ushirika katika vitendo vya sanamu (1 Wakorintho 10:20).[47] Paulo anahitimisha, "…Hamwezi kushirikiana katika meza ya Bwana na katika meza ya mashetani" (1 Wakorintho 10:21).

Wakati waamini hawatakiwi kula katika hekalu ya kipagani kwa muktadha wa kidini, Paulo anachukulia kitofauti suala la kufanya manunuzi katika soko la umma ambalo huuza nyama tofauti tofauti zilizotolewa sadaka kwa sanamu hapo awali. Kwa sababu hakuna uhusiano wa moja kwa moja na ibada za sanamu, Paulo anasema waamini hawapaswi kuuliza maswali lakini wanapaswa kununua kile kilichopo. Jambo pekee kwa uhuru huu huibuka pale anapokuwepo mtu anayeweza kuchukizwa. Ndugu dhaifu anaweza hata kuhusisha manunuzi ya nyama hii na ibada ya sanamu. Kwa hali hii, Paulo anawakumbusha Wakorintho majukumu ya mkristo kutotaka mema yake tuu bali mema ya nduguye (1 Wakorintho 10:24).

Kanuni kuu ni upendo. Upendo kwa Mungu hunizuia mimi kufanya karamu za sanamu zinazotolewa katika hekalu la kipagani. Upendo kwa ndugu yangu dhaifu hunizuia mimi, kama mwamini imara, kula nyama inayoweza kuharibu imani yake.

[47] 1 Wakorintho 10:1-22 hutumia hadithi ya uaminifu wa wana wa Israeli kama onyo dhidi ya kushiriki ibada za sanamu.

*Desturi za Ibada na Karama za Kiroho (1 Wakorintho 11:2-14:40)*

Paulo baadae anaelezea masuala ya mamlaka, uangalizi wa chakula cha Bwana, na matumizi ya karama za kiroho. Vitendo vya ibada isiyo sahihi vilivyopatikana katika kanisa la Wakoritho ilikuwa ni matokeo ya kiburi na matengano. Wakorintho walitumia karama za kiroho kupandisha hadhi zao wenyewe, badala ya kuhudumiana wao kwa wao kwa hamasa ya upendo.

*Ufufuo wa Yesu na wa Wafu (1 Wakorintho 15)*

Katika kujibu maswali kuhusu mustakabali wa waamini waliokufa, Paulo anaanza kwa kuthibitisha ukweli wa kihistoria wa ufufuo wa Kristo. Kisha anajadili kuwa ufufuo wa Yesu ni "…limbuko lao waliolala" (1 Wakorintho 15:20). Kwa sababu Kristo aliishinda mauti, waamini wanayo ahadi ya ufufuo.

*Kusanyiko la Matakatifu wa Yerusalemu (1 Wakorintho 16:1-4)*

Katika safari yake ya tatu ya kimisheni, Paulo alikusanya sadaka kutoka kwa makanisa ya wamataifa ili kuunga mkono waamini walioko Yerusalemu waliokuwa wakipitia mateso. Sadaka hii ilikuwa ya muhimu kwa Paulo kama maelezo ya kivitendo kuhusu fundisho la umoja katika kanisa. Kupitia sadaka hii, waongofu wa mataifa walionesha kuwa ushirika wao katika kanisa ulihusisha jukumu la kushika mkono ndugu zao wa kike na wa kiume (Wayahudi) katika Kristo.

***Kuagana (1 Wakorintho 16:5-24)***

Paulo anahitimisha barua yake kwa maelezo ya mipango yake ya baadae ya kutembelea Korintho, salamu kwa watu wote, na kwaheri.

## 2 Wakorintho

### Usuli wa 2 Wakorintho

***Muundo***

2 Wakorintho iliandikwa mwaka mmoja baada ya 1 Wakorintho. Ilitokea kwamba ziara ya Timotheo haikuleta suluhu kwa matatizo katika Korintho. Kisha Paulo mwenyewe akalitembelea kanisa. Ilikuwa ni ziara ya maumivu, ambayo kwayo kanisa lilikatalia mamlaka yake (2 Wakorintho 2:1). Paulo alirejea Efeso, ambapo hapo aliandika barua nyingine (sasa imepotea) na akaituma kupitia Tito (2 Wakorintho 2:3-9).

Kutoka Efeso, Paulo alisafiri kwenda Makedonia, ambapo alisubiri habari kutoka Korintho. Tito aliripoti kuwa Wakorintho wengi walitubia uasi wao (2 Wakorintho 7:5-16). Hata hivyo, kundi dogo la watu liliendelea kukataa mamlaka ya Paulo, sehemu ya mwisho ya 2 Wakorintho inaelezea kundi hili na kuandaa njia kwa ajili ya ziara ya tatu ya Paulo.

### *Kusudi*

Kusudi la 2 Wakorintho ni:

- Kuwasifu Wakorintho kwa kutubu kwao, kama ilivyo ripotiwa na Tito (2 Wakorintho 1-7).
- Kukamilisha makusanyo ya sadaka ya Yerusalemu (2 Wakorintho 8-9).
- Kuelezea uasi ulioendelezwa na baadhi ya waumini (2 Wakorintho 10-13).

## Ratiba ya huduma ya Paulo kwa Wakorintho

Chati ifuatayo inaonesha ratiba ya 1 na 2 Wakorintho. Wakati baadhi ya tarehe hazina hakika, hii ndio ratiba yenye uwezekano mkubwa wa uhusika wa Paulo kwa kanisa la Korintho.

| **Paulo na kanisa katika Korintho** | |
|---|---|
| 50 B.K. | Kanisa lilipandwa wakati wa safari ya pili ya kimishenari ya Paulo. |
| | Paulo aliandika barua, ambayo hatuna (1 Wakorintho 5:9). |
| 55 B.K. | Katika Efeso, Paulo aliandika 1 Wakorintho, na Timotheo akapeleka. |
| | Paulo alifanya safari ya "kwa huzuni" kwenda Korintho, wakati ambapo mamlaka yake yalikataliwa (2 Wakorintho 2:1). |
| | Katika Efeso, Paulo aliandika barua ngumu, ambayo hatuna. Alimtuma Tito kuipeleka, na ilisababisha toba (2 Wakorintho 7:8-16). |
| 56 B.K. | Katika Makedonia, Paulo aliandika 2 Wakorintho, na Tito akapeleka. |
| 57 B.K. | Paulo alitembelea Korintho kwa mara ya mwisho (2 Wakorintho 12:14). |

## 2 Wakorintho (inaendelea)

### Mada kuu za 2 Wakorintho

Muundo wa 2 Wakorintho unaonesha makusudi mbalimbali. Unatoa mwitikio wa Paulo kwa masuala tofauti tofauti. Mada zinazopatikana katika waraka zinajumuisha:

- Utetezi wa Paulo juu ya Utume wake.
- Utetezi wa Paulo wa uadilifu wake.
- Mipango ya Paulo kwa ajili ya safari ya tatu.

### *Utetezi wa Paulo juu ya Utume Wake*

Kwa aibu ya wazi iliyoonekana, Paulo anatetea utume wake katika kifungu kipana cha maneno. Maadui zake walitumia mateso na udhaifu wa Paulo kama ushahidi dhidi ya

mamlaka yake kama mtume. Maadui hawa walijivunia walijitukuza katika mafanikio na nguvu; Paulo alijivunia udhaifu wake, ili kwamba nguvu ya Kristo iweze kukaa juu yake (2 Wakorintho 12:9). Mamlaka yake yanatoka kwa Mungu, ambaye amechagua kutenda kazi kupitia udhaifu wa Paulo kama njia ya kufunua utukufu wa Mungu.

### *Utetezi wa Paulo kwa Uadilifu wake*

Paulo alikusudia kutembelea Korintho mapema lakini alichelewesha ziara yake ili kuruhusu vidonda kutoka katika ziara ya mwanzo kupona. Kwa sababu hii, alisafiri kwenda Makedonia badala ya kwenda moja kwa moja Korintho. Mabadiliko haya ya mpango yalikuwa eneo la Paulo kushambuliwa na adui zake; walimlaumu kwa kutoaminika. Paulo alielezea kwamba alibadilisha mpango wake ili kuhudumia mahitaji yao kwa ufanisi zaidi (2 Wakorintho 1:15-2:4, 12-17).

### *Mipango ya Paulo kwa ajili ya safari ya tatu*

Kuna wale ambao waliendelea kukataa mamlaka ya Paulo na kusema kwamba ni dhaifu. Paulo anaandika kwamba atarudi tena Korintho na kuwaomba watubu kabla ya ujio wake. Mwanzoni mwa barua, anamhakikishia msamaha mkosaji aliyetubu (2 Wakorintho 2:5-11). Mwishoni mwa barua yake, anaomba tena kuhusiana na urejesho. Lengo la Paulo ni upatanisho, na si kisasi.

## Wagalatia

### Maneno Munhimu

Tunapojiandaa kujifunza kitabu cha Wagalatia, kuna maneno na maana ambazo tunahitaji kuelewa:

- ***Judaizers***. Waalimu wa uongo katika kanisa la kwanza ambao walifundisha kwamba tunahesabiwa haki kwa imani katika Kristo pamoja na utii kwa sheria za Kiyahudi. Walikiri kuwa Wakristo, lakini walisisitiza kwamba Waamini wa Mataifa wanapaswa kufuata Sheria ya Kiyahudi ili kuwa sawa mbele za Mungu.
- ***Legalism***. Imani kwamba kutimiza matakwa ya sheria ya Musa, au baadhi ya mfumo fulani wa sheria, unamfanya mtu kuwa sawa mbele za Mungu.
- ***Legalist***. Mtu ambaye anajaribu kupata wokovu kwa kutii Sheria za Mungu.
- ***Antinomianism***. Mafundisho potofu kwamba waamini wako huru kufuata tamaa zao za mwili kwa sababu wamehesabiwa haki kwa imani, si kwa kutii sheria.

## Usuli wa Wagalatia

### *Tarehe*

Paulo na Barnaba walihubiri eneo la Kusini la Galatia wakati wa safari yao ya kimisheni ya kwanza, kuanzia 47 B.K. Ni kama Paulo aliandika Wagalatia kati ya 48 B.K kama mwitiko wa shida zilizoibuka kati ya hizi zilibadilika baada ya kuondoka kwake.

Moja ya hoja zinazokubalika zaidi kuhusiana na tarehe hii ni ukweli kwamba Paulo haja taja Baraza la Yerusalemu katika hii barua. Kwa kuwa barua inalenga suala la Mataifa na Sheria (Suala lililoamriwa kwenye Baraza la Yerusalemu mnamo 49 B.K), inaonekana kwamba Paulo angekuwa ametaja baraza hili endapo alikuwa akiandika baada ya kutokea. Tarehe ya 48 B.K. inafanya Wagalatia kuwa waraka wa kwanza wa nyaraka za Paulo.

### *Kusudi*

Baada ya Paulo na Barnaba kuondoka Galatia, Judaizers walianza kuwashawishi waamini wapya hapa. Walimu hawa hawakukataa kwa ujumla kazi ya ukombozi ya Yesu, lakini walihubiri kuwa Mataifa walioamini wanapaswa kutahiriwa na kushika au kufuata sheria za Kiyahudi. Walifundisha kwamba tunahesabiwa haki kwa imani katika Kristo Pamoja na utii kwa sheria.

Kusudi la Paulo la kuandika Wagalatia ni kuwaita kutoka injili ya uongo ya Judaizers na kurudi kwenye injili ya kweli ya wokovu kupitia imani kwa Kristo pekee.

## Mada Kuu za Wagalatia

Wagalatia ni waraka wa Paulo wenye maneno magumu sana. Anawakemea Wagalatia kwa ajili ua ujinga wao wa kugeukia injili ya namna nyingine na kuwaita wao warudi kwenye injili ya kweli ya Kristo.

### *Injili ya Kweli*

Tofauti na barua zake za baade, ambapo Paulo mara nyingi anajitambulisha mwenyewe kama Mtume na kama mtumwa wa Yesu Kristo. Katika Wagalatia anajitambulisha mwenyewe kwa maneno yenye mamlaka tu: "Paulo, mtume, (si mtume wa wanadamu, wala kutumwa na mwanadamu, bali na Yesu Kristo, na Mungu Baba aliyemfufua kutoka kwa wafu)" (Wagalatia 1:1). Hii ni lugha ya mamlaka ya kiutume.

Ujumbe wa Paulo ulikuwa ukipingwa na Judaizers katika Galatia. Walikuwa wakisema, "Paulo hakuwa thenashara wa Yesu. Kimsingi, alilitesa kanisa! Kwa nini msikilize ujumbe wake? Yeye sio mtume wa kweli." Paulo anajibu, "Sikuchaguliwa na mtu au kupitia juhudi za mtu. Mimi ni mtume aliyeitwa na Yesu mwenyewe na Mungu Baba, ambaye alimfufua kutoka wafu."

Paulo anawataka waamini wa Galatia kujua kuwa injili aliyoihubiri kwao ni injili ya kweli ya Yesu Kristo. Moja ya mahubiri ya Paulo katika mji wa Galatia yamenakiriwa katika Matendo ya Mitume 13:16-41.

► Soma mahubiri ya Paulo katika Matendo ya Matendo ya Mitume 13:16-41. mada gani zimejumuishwa katika mahubiri?

Kuwa makini na yaliyomo katika ufupisho wa injili:

- Mungu alitenda kupitia historia ya Israeli ili kumuinua mwokozi (Matendo ya Mitume 13:17-23).
- Yesu ni mwokozi, alitangazwa na Yohana Mbatizaji (Matendo ya Mitume 13:24-25).
- Yesu alikataliwa na watu wa Yerusalemu pamoja (Matendo ya Mitume 13:27).
- Walimsulubisha Yesu, lakini Mungu alimfufua kutoka wafu (Matendo ya Mitume 13:28-30).
- Yesu alionekana kwa mashahidi wengi baada ya kufufuka (Matendo ya Mitume 13:31).
- Tunahesabiwa haki kwa imani, na sio kwa sheria ya Musa (Matendo ya Mitume 13:38-39). (Huu ulikuwa ujumbe wa muhimu kwa Mataifa walioamini.).

Hii ni injili ya kweli, ujumbe wa kuhesabiwa haki kwa imani pekee. Kwa muda ambao Paulo anaandika Wagalatia, waamini hawa wapya walikuwa wamegeukia injili tofauti, injili ambayo sio hata injili (Wagalatia 1:6-7). Utuwa wa kuhesabiwa haki kwa matendo ya Sheria ni mbali sana na habari njema ya kuhesabiwa haki kwa imani iliyohubiriwa na Paulo.

| Mafundisho Kuhusu Kuhesabiwa Haki | |
|---|---|
| **Injili ya Kweli** | Tunahesabiwa haki kwa imani. |
| **Injili ya Uongo ya Judaizers** | Tunahesabiwa haki kwa imani jumlisha kutii sheria. |
| **Injili Potofu Leo** | Tunahesabiwa haki jumlisha __________. |

### *Kuhesabiwa haki kwa Neema, na sio Matendo*

Paulo alifundisha kwamba tunahesabiwa haki kwa neema, na sio kwa matendo. Katika hoja zake dhidi ya legalism, alionesha mambo manne:

1. **Uzoefu wake***.* Paulo analenga katika injili iliyofunuliwa kwake akiwa njiani kwenda Dameski. Paulo alikuwa adui wa injili, akilitesa kanisa. Alisema "Nami naliendelea katika dini ya Kiyahudi kuliko wengi walio hirimu zangu katika kabila yangu, nikajitahidi sana katika kuyashika mapokeo ya baba zangu" (Wagalatia 1:14). Kama wokovu ulikuja kwa utii kwa sheria, Paulo hakuhitaji injili, alikuwa mwaminifu kufuata na kutii sheria, lakini Mungu alimfundisha Paulo kwamba, "…hali tukijua ya kuwa mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, bali kwa imani ya Kristo Yesu…" (Wagalatia 2:16).

2. **Uzoefu wa Wagalatia**. Wakati ambapo Wagalatia walisikia injili, walipokea Soho kwa imani. Hawakuwa wameokolewa kwa matendo (Wagalatia 3:2). Vile vile haiwezekani kwa wao kuutimiliza wokovu wao kwa utii kwa sheria (Wagalatia 3:3).

3. **Uzoefu wa Ibrahimu***.* "…Ibrahimu alivyomwamini Mungu akahesabiwa haki" (Wagalatia 3:6). Sasa, wale wote wanaoamini ni watoto wa Ibrahimu (Wagalatia 3:7). Kama vile Ibrahimu alihesabiwa haki kwa imani, vivyo hivyo waamini wanahesabiwa haki, si kwa matendo.

4. **Sheria yenyewe**. Paulo anaonesha kuwa wote wanaotegemea matendo ya sheria wanasimama chini ya "laana ya Mungu, lakini mwenye haki ataishi kwa imani", lakini "Mwenye haki ataishi kwa imani" (Wagalatia 3:11). Paulo anawatia changamoto waongofu wa Galatia: "Katika ungwana huo Kristo alituandika huru; kwa hiyo simameni, wala msinaswe tena chini ya kongwa la utumwa" (Wagalatia 5:1).

***Kutimiliza Sheria***

► Je, uhuru wetu kutoka matendo ya sheria unaturuhusu sisi kufuata tamaa za dhambi?

Paulo alitambua kwamba ujumbe wa kuhesabiwa haki kwa imani pekee unaweza kutumiwa vibaya." Msomaji wa barua ya Paulo aliweza amua, "Hizi ni habari za kushangaza! Ninahesabiwa haki kwa neema kupitia imani. Sheria haijalishi. Naweza kufanya chochote ninachotaka kufanya! Naweza kuishi kwa kadri ya tamaa yangu ya mwili."

Kote katika Warumi na Wagalatia, Paulo anayajibu mafundisho haya potofu. Katika Warumi, anawakumbusha wasomaji wake kwamba wameifia dhambi na kwamba, kwa sababu ya hili, hawawezi kuendelea kuishi tena katika hiyo (Warumi 6:2). Katika Wagalatia, Paulo anawaagiza wasomaji wake: "…lakini uhuru wenu usiwe sababu ya kuufuata mwili, bali tumikianeni kwa upendo. Maana torati yote imetimilika katika neno moja, nalo ni hili, Umpende jirani yako kama nafsi yako" (Wagalatia 5:13-14).

Uhuru kutoka kwa Sheria sio ruhusa ya kutenda dhambi. Badala yake, tukiwa tumeokolewa kwa neema, roho mtakatifu anatusaidia kumtii Mungu na kutimiza sheria ya upendo.

Paulo hajawahi kufundisha kwamba Sheria ya Mungu haina kazi. Kiukweli, sheria ni ya thamani kwa waamini; kupitia hiyo tunajua jinsi ya kuishi katikactabia inayompendeza Mungu. Lakini tutatii sheria ya upendo, sio utumwa. Upendo unatimiza sheria.

## Kuangalia kwa ukaribu Legalism na Utii

Kama mtu akimtii Mungu kwa uangalifu, hiyo ina maanisha yeye ni legalist? Hapana! Mungu anatarajia watoto wake kutii. Legalist ni mtu ambaye anayejaribu kupata wokovu kwa kutii sheria za Mungu. Legalism ni suala la moyo.

Kwa nje, legalist na mtu wa imani wanaweza kuonekana sawa. Lakini legalist anamtii Mungu ili kwamba apate upendeleo wa Mungu, lakini mtu wa imani anamtii Mungu kwa sababu

anampenda Mungu na anataka kumpendeza. Hamasisho la mtu utii – sio utii wake wenyewe – ndio kitu ambacho huonesha kama yeye ni legalist.

| Mitazamo Mitatu ya Matendo | | |
|---|---|---|
| **Legalism** | **Antinomianism** | **Upendo wa Mungu** |
| "Nimeokolewa kwa matendo. Ninatii sheria ya Mungu ili kwamba niokolewe." | "Nimeokolewa kwa neema. Matendo hayajarishi. Ninapaswa kutii sheria ya Mungu." | "Nimeokolewa kwa neema. Kwa sababu ya upendo wangu kwa Yesu ambaye aliniokoa kwa neema yake, ninamtii Mungu kwa nguvu ya Roho." |

## Wagalatia (Mwendelezo)

### Mada kuu za Wagalatia (mwendelezo)

#### *Maisha katika Roho*

Paulo alilinganisha matendo ya mwili na tunda la Roho (Wagalatia 5:19-23). Kama tunapanda katika mwili, tutavuna uharibifu (Wagalatia 6:8). Kama tunapanda kwa Roho, tutavuna uzima wa milele (Wagalatia 6:8).

Paulo anafundisha kuwa kama tukitembea kwa Roho (kama tunaishi katika utii Kwake) hatutatimiza tamaa za mwili (Wagalatia 5:16). Badala yake, tunda la roho litaonekana katika maisha yetu, na tutatimiliza sheria ya upendo.

Wagalatia 6:1-10 inatuonesha kuwa kuishi kwa sheria ya upendo kuna matokeo muhimu ya kivitendo kwa mwamini:

- Tunawarejesha wale walio dondoka katika majaribu.
- Tunabebeana mizigo.
- Tunafikiri sawasawa kuhusiana na sisi wenyewe.
- Tunafanya mema kwa watu wote, hasa waamini wenzetu.

Hii ni uhuru wa kweli wa Kikristo.

## Wakorintho na Wagalatia katika Kanisa Leo

Tunapokutana na matatizo katika kanisa, wakati mwingine tunajaribiwa kufikiri, "Haikuwa mbaya hivi wakati wa nyuma!" Hata hivyo Wakorintho na Wagalatia vinatukumbusha kuwa matatizo ya leo siyo mapya. Nyaraka hizi zinaongeza moja kwa moja kwa kanisa la karne ya 21.

1 Wakorintho inatukumbusha kuhusu umoja wa kanisa. Ingawa tunatofautiana katika maeneo mengi, mwili wa Kristo ni mwili mmoja. Ukweli huu unapaswa kutuongoza katika

kushughulikia tofauti katika kanisa; unapaswa kutuongoza katika kushughulikia migogoro kati ya waamini, na unapaswa kutuongoza katika kutumia vipawa vyetu kujenga mwili wa Kristo.

Nyaraka hizi pia hutukumbusha kuwa tumeitwa katika huduma ya upatanisho. Katika Wakorintho, Paulo anaonesha kuwa msamaha unapaswa kutolewa bure wakati ambapo kuna mgawanyiko katika kanisa. Vivyo hivyo, katika Wagalatia, Paulo anaonesha kuwa tunapaswa kutafuta kuwarejesha wale waliopotea.

Wagalatia inatukumbusha mafundisho makuu ya kuhesabiwa haki kwa neema kupitia imani. Paulo anaonya dhidi ya bidii yoyote katika kufundisha "Tunahesabiwa haki kwa imani jumlisha chochote kingine." Hakuna (sio sheria ya Musa, wala matendo wala chochote kingine) inaweza kuongezwa kwa imani katika kazi ya Kristo kama msingi wa kuhesabiwa haki kwetu mbele ya Mungu.

Wagalatia inatukumbusha pia kuhusu matokeo ya maisha ya sheria ya upendo. Sheria ya upendo inabadili maisha yetu kama waamini.

## Hitimisho

Mwanzoni mwa 1738, William Holland alishuhudia uhakika wa imani baada ya kusikia kwa Charles Wesley akisoma kutoka maelezo ya *Commentary on Galatians ya* Martin Luther*.* Charles Wesley aliandika shajara yake, "Nilitumia masaa baadhi jioni hii kwa faragha pamoja na Martin Luther, ambaye alikuwa baraka sana kwangu... nilifanya kazi kwa bidii, nilisubiri, na kusali ili kuhisi nani aliyenipenda na kujitoa kwa ajli yangu."

Siku chache tu baadaye, katika Jumapili ya Pentekoste, Charles mwenyewe alishuhudia kuwa na uhakika. Siku nne baadaye, akisikiliza William Holland akisoma kutoka "Preface to Romans," cha Martine Luther, John Wesley alifikia uhakika wa Imani.

Ujumbe wa kuhesabiwa haki kwa imani ulimbadilisha Luther, Wesleys, na mamilioni ya waamini wengine. Ujumbe huu ni wa muhimu leo kama ilivyokuwa katika karne ya 17.[48]

[48] J. I. Packer, *"Introduction," in Galatians: by Martin Luther,* (Wheaton, IL: Crossway Classic Commentaries, 1998), xii.

## Somo la 6 Mazoezi

(1) Chagua Mojawapo kati ya mazoezi yafuatayo:

- Kama kiongozi cha kujifunzia 1 Wakorintho, andaa muhtasari wa ukurasa mmoja ukionesha kila suala ambalo Paulo analishughulikia katika waraka huu. Muhtasari wako unatakiwa kujumuisha mambo matatu kwa kila suala:
    - Rejea za vifungu vya maandiko.
    - Swali au tatizo.
    - Ufupisho mfupi wa jibu la Paulo.
- Andika insha ya ukurasa mmoja juu ya changamoto za wakati huu juu ya fundisho la kuhesabiwa haki kwa imani pekee. Wakati hatupambani na Judaizers na majaribio yao kwa kutaka tohara, ni vitu gani vingine ambavyo huwa vinaongezwa kama msingi wa kuhesabiwa haki?

(2) Mwanzoni mwa somo linalofuata, utafanya jaribio kulingana na somo hili. Soma maswali ya jaribio kwa umakini katika maandalizi.

## Somo la 6 Jaribio

(1) Kwa nini Korintho ni mji muhimu sana kwa mkakati wa Paulo wa injili?

(2) Ni nani alifanya kazi pamoja Paulo katika kupanda kanisa Korintho?

(3) Ni matatizo gani matatu makubwa katika kanisa yaliyo muhamasisha Paulo kuandika 1 Wakorintho?

(4) Ni kifungu gani cha maneno kinatoa utangulizi kwa swali ambalo Paulo anajibu katika 1 Wakorintho?

(5) Orodhesha mada kuu tatu zinazo shughulikiwa na Paulo katika 2 Wakorintho.

(6) Nini ni kusudi la Paulo la kuandika Wagalatia?

(7) Judaizers walifundisha nini kuhusiana na namna tunavyohesabiwa haki?

(8) Legalist ni nani?

(9) Ni mambo gani manne ambayo Paulo anayaonesha katika hoja zake dhidi ya legalism?

(10) Kulingana na Paulo, sheria ni ya thamni kiasi gani kwa waamini?

(11) Andika 1 Wakorintho 1:20-21 na Wagalatia 5:22-23 kutoka katika kumbukumbu.

# Somo la 7
# Waefeso, Wafilipi, Wakolosai, na Filemoni
# Nyaraka Kutoka Gerezani

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kufahamu tarehe zinazowezekana na mazingira ya kihistoria ya Nyaraka za Kifungoni.

(2) Kueleza mada kuu na kusudi la nyaraka Nyaraka za Kifungoni.

(3) Kuelewa maana ya kibiblia ya Uchaguzi.

(4) Kuthamini umuhimu wa mafundisho ya biblia katika fundisho la kanisa na fundisho la Kristo.

(5) Kufupisha kanuni za vitendo kwa maisha ya mkristo zilizotolewa katika Nyaraka za Kifungoni.

(6) Kuhusianisha ujumbe wa vitabu hivi na mahitaji ya dunia ya leo.

## Maandalizi kwa Ajili ya Somo Hili

► Soma Waefeso, Wafilipi, Wakolosai, na Filemoni.

► Kariri Waefeso 4:11-16 na Wakolosai 3:1-4.

## Utangulizi

Mapema katika miaka ya 60 B.K., Paulo alikuwa akishikiliwa chini ya kizuizi cha nyumbani kule Rumi kwa miaka miwili. Ingawa alikuwa mfungwa, aliishi katika nyumba iliyopangishwa na aliruhusiwa kupokea wageni (Matendo ya Mitume 28:30-31). Wakati wa kifungo chake, Paulo aliandika nyaraka nne (pia ziliitwa nyaraka za kifungoni). Barua tatu kati ya hizi ziliyaelekea makanisa; ya nne ilimuelekea mtu aliyegeuzwa chini ya huduma ya Paulo.

Barua hizi ni baadhi ya barua za furaha sana za Paulo. Zinaonyesha ushindi wake dhidi ya nyakati ngumu katika maisha, na zinatutia moyo kuendelea kutunza roho ya furaha wakati wa mateso yetu binafsi.

Barua hizi pia ziko kwa vitendo sana. Zinaelezea mambo kama mahusiano ya kifamilia na vita vya kiroho (Waefeso), utu na umoja (Wafilipi), imuhimu thabiti wa Kristo (Wakolosai),na msamaha na urejesho (Filemoni).

## Waefeso

### Usuli wa Waefeso

#### *Mazingira ya Kihistoria*

Kanisa la Efeso lilipandwa wakati wa safari ya tatu ya kimishenari ya Paulo. Mwandishi mahiri Apolo alihubiri Efeso; Prisila na Akila walifanya kazi pale; na Paulo alitumia miaka mitatu pale akihubiri na kufundisha. Mji ukawa kitovu cha uinjilisti na kufikia majimbo yaliyozunguka; kutoka Efeso, wote waliokaa Asia walisikia neno la Bwana Yesu (Matendo ya Mitume 18:24-19:10).

Efeso ilikuwa ni nyumba ya hekalu maarufu kwa mungu Diana (pia aliitwa Artemi). Vitendo vya kishirikina vilikuwa vya kawaida, na uchumi wa mji ulikuwa ukishikiliwa kwa upana na mauzo ya vitu vilivyohusiana na hekalu. Huduma ya Paulo ilivuruga maslahi haya yote. vitabu vya sanaa ya uchawi vyenye thamani kama vile dola milioni 6' vilichomwa na waamini wapya (Matendo ya Mitume 19:19).[49] Matokeo yake, Demetrio na mafundi stadi wengine waliojipatia maisha kupitia kuuza vitu vilivyomuheshimu Diana walianzisha mgomo kupinga huduma ya Paulo. Vita vya kiroho ni dhana muhimu katika Waefeso.

Kigezo kimoja cha ziada lazima kitajwe kuhusu Waefeso. Si kawaida kwa barua za Paulo kutohusisha salamu binafsi kwa watu katika kanisa. Hata barua kwa Rumi, ambapo Paulo hakuwa ametembelea bado, ilihusisha salamu kwa waumini wa kanisa waliojulikana na Paulo. Katika barua kwa Efeso, kanisa ambalo Paulo alihubiri miaka mitatu, mmoja angetaraji mlolongo mkubwa wa majina. Badala yake, Waefeso haijabeba salamu yoyote binafsi. Sababu inayodhaniwa hasa ni kwamba Waefeso, kama Wakolosai, ilikusudiwa kusambazwa katika ya makanisa mengi katika Asia ndogo. Tikiko alichaguliwa kuwasilisha Waefeso na Wakolosai na kuleta salamu kwa makanisa haya (Waefeso 6:21, Wakolosai 4:7).

### Yaliyomo katika Waefeso

Muhtasari wa Waefeso unaonesha sehemu kubwa mbili:[50]

1. **Mafundisho**: Nini Mungu amefanya kwa jili ya kanisa (Waefeso 1-3).
2. **Matumizi**: Nini Mungu anafanya ndani ya kanisa (Waefeso 4-6)

Katika sehemu ya kwanza, Paulo anaelezea fundisho la uchaguzi na kanisa. Katika sehemu ya pili, Paulo anahimiza wasomaji wake kuishi katika namna inayopasa nafasi zao kama kanisa lililochaguliwa la Bwana.

---

[49] *English Standard Version Study Bible*

[50] Imechukuliwa kutoka Walter A. Elwell and Robert W. Yarbrough, *Encountering the New Testament*. (Ada: Baker Academic, 2005).

***Fundisho: Kile Mungu alichofanya kwa kanisa (Waefeso 1-3)***

*Wokovu wa waamini (Waefeso 1:3-2:10)*

Baada ya salamu fupi, Paulo anaanza na maombi ambapo anataja baraka tulizopokea katika Kristo. Waefeso 1:3-14 ni kielelezo kizuri cha ibada ambapo Paulo anakumbusha wasomaji wake faida za kiroho tunazopokea kupitia nafasi zetu katika Kristo..

► Soma Waefeso 1:3-14. Ni baraka gani za kiroho tunazipokea katika Kristo?

Wokovu wetu unahusisha nafsi zote tatu katika Utatu Mtakatifu:

1. **Baba: Uchaguzi** (Waefeso 1:3-6). Baba ametuchagua katika Kristo kabla ya misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu na tusio na mawaa mbele za baba yetu katika upendo. Mpango wa wokovu ulikuwa ni muundo wa Baba.

2. **Mwana: Ukombozi** (Waefeso 1:7-12). Kwa sababu ya kifo cha upatanisho cha Yesu, tuna ukombozi kupitia damu yake, msamaha wa dhambi, kwa kadri ya utajiri wa neema ya Mungu. Kumkomboa mtu humaanisha kumfidia kutoka katika uteka. Mfano mkubwa katika Agano la Kale ni ukombozi wa Israeli toka katika utumwa kule Misri. Katika agano jipya, wote wanaomwamini Yesu wamekombolewa kutoka katika utumwa wa shetani.

3. **Roho: Uhifadhi** (Waefeso 1:13-14). Kupitia Roho, tumewekwa chapa ya umiliki wa Mungu. Katika muonekano mzuri, Paulo anasema kuwa Roho ni malipo ya awali juu ya urithi wetu katika ufalme wa milele wa Mungu. Kwa sababu ya Roho, sisi ni milki iliyonunuliwa wa Mungu na tuna ahadi ya mbingu.

Fundisho la ukombozi linaendelea katika Waefeso 2, ambapo Paulo anatukumbusha kuwa sisi tulikuwa "…wafu kwa sababu ya makosa na dhambi" (Waefeso 2:1). Wokovu wetu si kwa kustahili kwetu wenyewe.

> … Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema (Waefeso 2:4-5).
>
> Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu (Waefeso 2:8-9).

Mchakato mzima ni zawadi ya Mungu. Hatuwezi kujisifu kwa chochote.

### Kuangalia kwa Makini Uchaguzi

Paulo anaandika kwamba sisi **tumechaguliwa tangu asili** kwa ajili ya kuasiliwa/kufanywa wana kupitia Yesu Kristo (Waefeso 1:5). Tulichaguliwa katika Yeye kabla ya misingi ya ulimwengu (Waefeso 1:4).

Baadhi ya watu hutumia neno **uchaguzi** kumaanisha kuwa, kabla ya misingi ya ulimwengu, Mungu alichagua kila mtu ambaye angeokolewa. Wanasema kuwa wale waliochaguliwa wamekusudiwa wokovu. Kimsingi, hii humaanisha kuwa watu wengine wote wamekusudiwa kukataliwa na hawawezi kuokolewa. Hitimisho hili huonekana kupingana na ujumbe wa Biblia: Mungu anapenda watu wote.

Wengine hutumia uchaguzi kumaanisha kuwa hakuna zaidi ya maarifa ya awali ya Mungu kwa wale watakao chagua kuokoka. Huhoji kuwa kukusudiwa ni maarifa ya awali ya Mungu ya uchaguzi binafsi. Katika mtazamo huu, wokovu umejikita katika uchaguzi binafsi. Hata hivyo, uelewa huu huonekana kukinzana na msisitizo wa Biblia juu ya Ukuu wa Mungu.

Kanuni hizi mbili (ukuu wa Mungu na upendo wa Mungu) zimeamuliwa katika vifungu viwili vya msingi juu ya Kuchaguliwa tangu asili: Warumi 9-11 and Waefeso 1. Warumi 9-11 inaonyesha haki ya Mungu katika kuamua njia ya wokovu. Mungu ni mkuu, hakuna nayeweza kuokolewa isipokuwa kupitia imani katika Kristo Yesu, njia ambayo Mungu ameitangaza milele kama njia pekee ya wokovu.

Katika Waefeso 1, Paulo anaonyesha kuwa **wokovu ni kwa watu binafsi kwa sababu ya nafasi zetu katika Kristo.** Kabla ya misingi ya dunia, Kristo alichaguliwa kama yule ambaye kupitia yeye wokovu huja. **Wote wanaoamini wamechaguliwa katika yeye.** Kwa sababu ya upendo mkuu wa Mungu, njia ya wokovu iko wazi kwa wote waaminio.

Uwioano huu pia unaonekana katika Agano la Kale. Israeli ilikuwa taifa teule, watu waliochaguliwa na Mungu. Hata hivyo, si kila aliyezaliwa na Israeli alikuwa mali ya Israeli. (Warumi 9:6). Uchaguzi wa Mungu wa Israeli kama taifa teule haukumaanisha kuwa kila muisraeli aliokolewa. Kupitia kutokutii, baadhi (kama Akani, Yoshua 7) walipoteza ahadi Wengine ambao hawakuzaliwa Israeli (kama Rahabu, Yoshua 2 na Yoshua 6) waliamini ahadi za Mungu na kurithi ahadi zilizokuwa za Israeli. Wokovu ulitaka kuwa watu waamini na kushiriki ahadi za Mungu.

Katika namna ile ile, Kristo alichaguliwa kabla ya misingi ya ulimwengu kama mtu pekee ambaye kupitia yeye wokovu unatolewa. Tunapokuwa katika Kristo kupitia imani, tunapokea baraka za wokovu ambazo ni zake. Tumechaguliwa katika Kristo.

Uchaguzi ni uamuzi wa Mungu mkuu kwa imani katika Kristo kuwa njia pekee ya wokovu. Matendo ya Mitume 4:12 inasema, "Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo." Wazo hili hili linaonekana pia katika 1 Petro 1:18-20. Tumekombolewa , si kwa vitu viharibikavyo, bali kwa damu ya thamani ya Kristo. Petro anasema Kristo alijulikana hapo awali kabla ya misingi ya ulimwengu. Kwa hiyo, uchaguzi ni kwa Kristo mwenyewe na kupitia Kristo pekee.

## Waefeso (Mwendelezo)

### Yaliyomo katika kitabu cha Waefeso (Mwendelezo)

***Fundisho: Kile Mungu alichofanya kwa kanisa (Waefeso 1-3) (Mwendelezo)***

*Umoja wa kanisa (Waefeso 2:11-3:21)*

► Ni nini siri ya Injili ambayo Paulo anairejelea katika Waefeso 3:3-9?

Katika Waefeso 1, Paulo anafurahi katika wokovu wa waamini. Katika Waefeso 2-3, anafurahi katika uumbaji wa Mungu, kanisa. Dhamira muhimu ya Waefeso ni umoja wa kanisa: mwili mmoja ulioundwa na Wayahudi na mataifa pia. Mataifa, ambao hapo awali walikuwa wageni kwenye maagano ya ahadi, sasa wameletwa karibu kwa damu ya Kristo. (Waefeso 2:12-13). Kutokea mwanzo, mpango wa Mungu ulikuwa kuwahusisha mataifa katika familia yake. Kwa ndugu Wayahudi wa Paulo, hiki kilikuwa kipengele cha kushangaza cha Injili: Kanisa limeundwa na Wahayudi na mataifa pia katika Kristo*.* Hio ndio siri ya injili ambayo Paulo anarejelea.

Katika Biblia, siri si kitu ambacho hakiwezi kujulikana: bali, siri ni kitu ambacho hapo awali hakikujulikana lakini sasa kimefunuliwa. Katika Waefeso 3, Paulo anaielezea siri: "…Mataifa ni warithi pamoja nasi wa urithi mmoja, na wa mwili mmoja, na washiriki pamoja nasi wa ahadi yake iliyo katika Kristo Yesu kwa njia ya Injili" (Waefeso 3:6). Kama ishara ya nguvu za neema ya Mungu, Paulo amechaguliwa "ya kuwahubiri Mataifa utajiri wake Kristo usiopimika" (Waefeso 3:8)—Paulo, ambaye hujichukulia mwenyewe "mdogo kuliko yeye aliye mdogo wa watakatifu wote" na ambaye hapo zamani alimuudhi Kristo na kanisa lake. Paulo anahitimisha sehemu ya fundisho kwa ombi kwamba waamini wa Efeso, ambao tayari ni watakatifu na waaminifu katika Kristo Yesu, wajazwe kwa utimilifu wote wa Mungu.

***Matumizi: Kile Mungu anachofanya katika kanisa. (Waefeso 4-6)***

Katika nusu ya pili ya barua yake, Paulo anatoa changamoto kwa waamini : "…mwenende kama inavyoustahili wito wenu mlioitiwa" (Waefeso 4:1). Maisha yanayostahili mwito wetu:

- Huleta umoja katika kanisa (Waefeso 4:1-16).
- Hupelekea mwenendo wa kimaadili (Waefeso 4:17-5:21).
- Huathiri uhusiano wa kifamilia na kazi (Waefeso 5:21-6:9).
- Unauishi tu katika nguvu za uweza wa Bwana (Waefeso 6:10-18).

Fundisho la kikristo haliwezi kutenganishwa na maisha ya mkristo. Fundisho la kanisa lazima lionekane katika maisha ya kanisa ambapo kila sehemu inafanya kazi ipasavyo, kanisa ambalo linajijenga lenyewe katika upendo (Waefeso 4:16). fundisho la wokovu kwa neema linaonekana katika tabia ya "utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli" (Waefeso 4:24).

Paulo anamalizia barua yake kwa kulitia moyo kanisa kuwa linaweza kutimiliza utume wake na kuzishinda nguvu za giza. Anahitimisha kwa kuomba maombi kwa ajili ya muendelezo wake wa kuitangaza injili na kwa baraka.

## Wafilipi

### Usuli wa Wafilipi

#### *Mazingira ya kihistoria*

Kanisa la Filipi lilipandwa wakati wa safari ya pili ya umisheni wa Paulo. (Matendo ya Mitume 16:9-40). Lilikuwa ni kanisa la kwanza kuanzishwa barani Ulaya. Paulo na Sila walisafiri kwenda Filipi baada ya Paulo kuwa na maono ya mtu toka Makedonia akiomba msaada. Ingawa Filipi ilikuwa ni mji mkuu wa sehemu ya Makedonia, haikuwa na idadi kubwa ya Wayahudi. Kikundi cha wanawake kilikutana kando ya mto kwa ajili ya maombi kwa sababu hakukuwa na sinagogi (Matendo ya Mitume 16:13).[51]

Mmoja kati ya waamini wa kwanza katika Filipi alikuwa Lidia, mwanamke mwenye utajiri. Baada ya ubatizo wake, nyumba ya Lidia ilikuwa mahala pa kukutanikia waamini. Katika miji yenye Wayahudi wengi, upinzani wa Injili mara nyingi ulitokea kwa viongozi wa kidini wa Kiyahudi; lakini katika Filipi, upinzani uliinuka baada ya Paulo na Sila waliharibu kipato cha watu waliokuwa wakimdhibiti binti mfungwa aliyepagawa na roho chafu. Paulo na Sila walikamatwa, kupigwa, na kuwekwa gerezani. Usiku ule, tetemeko lilifungua malango ya gereza, na wafungwa walifunguliwa minyororo yao. Hakuna mfungwa alitoroka, na Paulo na Sila wakapata fursa ya kuhubiri injili kwa walinzi wa gereza.

Katika Matendo ya Mitume, Luka inahusiha kwa kina kuwa Filipi ilikuwa ni koloni la Rumi (Matendo ya Mitume 16:12). Usemi huu rahisi ulibeba maana kubwa kwa wasomaji wa awali wa Matendo ya Mitume. Filipi lilifanywa koloni la Rumi mwaka wa 42 B.K na jemadari mkuu wa Rumi Antony. Askari wengi walistaafia katika mji huu, na raia wake walipokea msamaha wa kodi nyingi za kirumi. Hadhi ya Filipi kama koloni ilikuwa ni sababu ya kiburi kwa raia wake. Wakati Paulo anawaandikia Waamini katika Filipi, kwa makusudi alitumia maneno mawili ya kigiriki akimaanisha uraia:

> Kwa maana sisi, **wenyeji** wetu (*politeuma*) kutoka huko tena tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo (Wafilipi 3:20).
>
> Lakini **mwenendo** wenu (*politeuomai*) na uwe kama inavyoipasa Injili ya Kristo… (Wafilipi 1:27).

Kwa kutumia lugha hi, Paulo anawaita Wafilipi kuishi kama raia wa mbinguni.

[51] Mji wowote ambao ndani yake wanaume 10 wa Kiyahudi walikaa walikuwa na Sinagogi.

### *Kusudi*

Wafilipi ni moja kati ya barua chanya, inayoonesha matatizo machache ambayo anayaelezea katika barua zake kwa Korintho na Galatia. Kuna malengo mawili kwa barua hizi:

1. **Kusudi Binafsi:** Kuleta habari za ufungwa wa Paulo na kuonyesha shukurani kwa msaada wa kifedha wa kanisa kwa huduma yake (Wafilipi 4:14-18). Paulo anafurahia uaminifu wao na anawatia moyo kuishi maisha ya furaha.

2. **Lengo la Kimaelekezo:** Kuelezea hatari mbili zinazowakabili kanisa la Filipi:
   - Hatari ya nje : Mafundisho ya uongo ya Judaizers.[52]
   - Hatari ya ndani: mgawanyiko kati ya waamini katika kanisa.

### Yaliyomo katika Wafilipi

### *Furaha licha ya mazingira (Wafilipi 1)*

Ingawa Paulo yuko kifungoni, ana ujasiri kuwa Mungu anafanyia kazi makusudi yake. (Wafilipi 1:12). Kwa sababu ya kukamatwa kwa Paulo, anapata fursa ya kuhubiri injili kwa walinzi wa kasri (jumba la mfalme). (Wafilipi 1:13). Paulo hajui kama kufungwa kwake kutamalizika kwa kufunguliwa au mauti (Wafilipi 1:19-20). Lakini bila kujali matokeo, anafurahi kwa sababu kuishi ni Kristo na kufa ni faida (Wafilipi 1:21).

Mazingira mengine ambayo yangetishia furaha ya Paulo ni wivu wa waamini wenza (Wafilipi 1:15). kikundi katika Rumi kinamhubiri Kristo kwa ushindani, kuongezea mateso ya Paulo (Wafilipi 1:17). Hata hivyo, mbali na nia zao, Paulo anafurahi kwa sababu injili inahubiriwa. (Wafilipi 1:18). Paulo ana ujasiri kuwa mema yatatokea kwenye injili inayohubiriwa, bila kujali nia zisio sahihi za watu hawa. Hali binafsi ya Paulo si ya muhimu sana kuliko ufalme wa Mungu.

### *Unyenyekevu kama Ufunguo wa Umoja (Wafilipi 2)*

Baadae katika barua, Paulo ataelezea mgawanyiko kati ya wanawake wawili katika kanisa la Filipi (Wafilipi 4:2-3). Ni wafuasi waaminifu wa Kristo ambao wamefanya kazi ngumu na Paulo kwa ajili ya injili. Bahati mbaya, ugomvi binafsi baina ya dada hawa wawili katika Kristo unatishia umoja wa kanisa. Kabla ya kuongelea mgawanyiko huu, Paulo anaelekezea mfano wa Kristo kama kielelezo cha umoja wa Kanisa.

Ugomvi mwingi ni matokeo ya tamaa zetu kulinda haki zetu. Katika Wafilipi 2:5-11, Paulo anaelekezea mfano wa Kristo, ambaye alikatilia mbali vipaumbele vyake kama Mungu ili kuokoa wanadamu. Yesu hakujiambatanisha na upendeleo wa Mungu lakini alikuwa mtii mpaka mauti, hata mauti ya msalaba. Alikumbana na kila fedheha, Alisulubiwa hata kifo

[52] Kwa taarifa zaidi kuhusu Judaizers, ona sehemu juu ya Wagalatia katika somo la 6.

cha aibu, ili kuleta wokovu. Matokeo yake, Mungu akamtukuza Yesu katika nafasi yake sahihi ya mamlaka ya ulimwengu.

Kila mfuasi wa Yesu lazima awe na nia hii ya unyenyekevu, kuangalia mahitaji ya waamini wenza. "Kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo ya wengine" (Wafilipi 2:4).

**Inamaanisha nini kwamba Yesu "Alijinyenyekesha"?**

Wafilipi 2:5-11 mara kwa mara huitwa "Hymn of Christ" ("Wimbo wa Kristo") kwa sabau inafupisha maisha ya Yesu , kifo, ufufuo, na kupaa kwake.

Watu wengi wamehojiana kuhusu maana ya Wafilipi 2:8 ambapo Paulo anaongea kuhusu Yesu kujinyenyekesha. Yesu hakukatilia mbali uungu wake. Alikatilia mbali heshima yake kama mfalme wa ulimwengu. Alijinyenyekesha kwa kuchukua uanadamu; hakukatilia mbali asili yake ya uungu.

### *Onyo dhidi ya Maadui wa Injili (Wafilipi 3)*

Ingawa Wafilipi kwa upana ni chanya, Paulo anaandika tahadhari kuu dhidi ya kundi la waletao matatizo ambao hutishia kanisa. Hawa ni Judaizers wanaoonekana mapema katika barua kwa Galatia. Wanasisitiza kuwa waamini lazima watahiriwe na sheria ya Kiyahudi. Paulo huwarejelea kama "mbwa," "watendao mabaya," na "wajikatao" (Wafilipi 3:2).

Katika Wafilipi 3:4-6, Paulo anawajibu Judaizers' akisisitiza katika kuzingatia matambiko ya sheria kwa kujielekezea maisha yake mwenyewe kama mfano. Kama kuzingatia sheria kulileta wokovu, Paulo angekuwa na ujasiri katika mwili. Alitahiriwa kwa mujibu wa sheria; alikuwa wa kabila lililopendelewa la Benyamini, muebrania wa Waebrania; alikuwa farisayo ambaye alitii sheria kwa umakini; alikuwa na bidii kwa imani ya kiyahudi, hata kiasi cha kuwatesa wafuasi wa Kristo; kuhusu sheria, Paulo hakuwa na hakulaumiwa. Hata hivyo, vitu vyote hivi huhesabika kama takataka kwa sababu ya thamani ya kumjua Kristo inayozidi yote (Wafilipi 3:8). Paulo aliokolewa, Wafilipi waliokolewa, na tumeokolewa, si kwa kuzingatia sheria, bali kwa ufahamu wa Kristo Yesu, Bwana wetu (Wafilipi 3:8-9).

### *Mahusia Yanayohitimisha (Wafilipi 4)*

Katika Wafilipi 4:2, Paulo anamhimiza Euodia na Sintike kuonyesha umoja ambao alifundisha katika Wafilipi 2. Kama wanawake hawa wana nia ya Kristo, watatatua ugomvi wao. Anahimiza kanisa kufurahi katika Bwana katika hali zote na kutunza amani ya Mungu katika mioyo yao na akili zao (Wafilipi 4:4-9). Anahitimisha kwa shukurani kwa mkono wa shirika toka katika kanisa kwa huduma yake (Wafilipi 4:10-19).

## Wakolosai

### Usuli wa Wakolosai

#### *Muundo wa kihistoria*

Wakolosai iliandikwa wakati wa ufungwa wa Paulo katika Rumi. Timotheo anaitwa pia mwandishi. Wakolosai 1:1), pengine akihudumu kama karani wa Paulo.

Hakuna ushahidi kuwa Paulo alitembelea kanisa katika Kolosai. Muunganiko unaodhaniwa kati ya Paulo na kanisa ni Epafra (Wakolosai 1:7, Wakolosai 4:12). Epafra, mzaliwa wa asili wa Kolosai, aweza kuwa aliokoka wakati wa huduma ya Paulo katika Efeso, umbali wa kama kilomita 160.[53] Epafra alirejea kupanda kanisa katika Kolosai, vile vile katika miji ya karibu ya Laodikia na Hierapoli. Paulo aliandika nyaraka kwa yote mawili Laodikia na Kolosai, akiwaelekeza waamini katika kila mji kusoma barua zote (Wakolosai 4:16).

#### *Malengo*

Wakati wa kifungo cha Paulo, Epafra aliripoti uzushi ambao ulitishia kanisa katika Kolosai. Paulo aliandika Wakolosai kuelezea fundisho hili hatari. Kwa kuongezea, Paulo aliandika kuwatia moyo waumini Wakolosai kuendelea mbele na ukomavu katika Kristo. Kitabu hujuisha maonyo dhidi ya fundisho la uongo na msisitizo wa kuuendea ukuaji wa kiroho.

### Yaliyomo katika Wakolosai

Wakolosai inashiriki dhana nyingi na Waefeso: umoja wa kanisa, uhalisia wa vita vya kiroho, na umuhimu wa kuishi katika namna inayostahili mwito wetu kama wafuasi wa Kristo. Mfanano huu haushangazi kwa sababu Paulo anaandika barua hizi wakati unaofanana na barua zinaelezea mahitaji yale yale.

Wakati maelezo ya uzushi uliofundishwa katika Kolosai waweza kutofautiana na mafundisho ya uongo ambayo yanatishia kanisa la leo, ujumbe wa Paulo unabaki kuwa wa muhimu:

- Kristo ndiye mkuu juu ya uumbaji wote
- Kristo ndiye kichwa cha kanisa.
- Tunatakiwa kuishi katika namna inayostahili mwito wetu kama watoto wa Mungu.

#### *Ukuu wa Kristo (Wakolosai 1)*

Mada kuu ya Wakolosai ni ukuu wa Kristo aliyefufuka. Katika sentensi nzuri kutoka Wakolosai 1:15-23, Paulo anaonyesha ukuu wa Kristo juu ya vitu vyote vilivyoumbwa, mamlaka yake juu ya kanisa, na kazi yake ya ukombozi. Kristo ni muumbaji (vitu vyote viliumbwa kupitia yeye) , na vitu vyote humilikiwa na yeye (vitu vyote viliumbwa kwa ajili yake). Kristo ni kichwa cha mwili, cha kanisa. Kupitia Kristo na damu ya msalaba wake. Sisi ambao hapo awali tulikuwa tumetengwa na tuliofungwa akilini, tukifanya matendo maovu

[53] Maili 100

sasa tumepatanishwa na Mungu. Kristo ni chanzo cha uumbaji, kichwa cha kanisa na Bwana wa ukombozi.

### *Fundisho Potofu la Kolosai (Wakolosai 2)*

Baada ya hii sentensi chanya juu ya asili ya Kristo, Paulo anasogea kwenye onyo hasi dhidi ya fundisho la uongo ambalo hutishia kanisa katika Kolosai. Asili thabiti ya uzushi/fundisho potofu la Kolosai si wazi. Hata hivyo, mwitikio wa Paulo hufunua baadhi ya tabia za uzushi huu. Uzushi wa Kolosai ulijumuisha mchanganyiko wa mawazo ya uongo kutoka katika ushawishi wa aina tatu:

- **Uyudaizimu wa Kiothodoksi**: Wayahudi wa kiothodoksi waliwataka waamini wa Kolosai kutazama sherehe za kiyahudi, sheria za vyakula na tohara (Wakolosai 2:16, Wakolosai 3:11).
- **Jewish mysticism**: Fumbo la kiyahudi liliwataka waumini wa kolosai kufunga ili kuungana na ibada zilizotukuka za malaika kwa Mungu (Wakolosai 2:18).[54]
- **Upagani**: Wapagani waliwatia moyo waumini wa kolosai kufanya matambiko kwa ajili ya ulinzi dhidi ya roho chafu, Paulo hakatai nguvu za roho chafu lakini anaweka sawa kuwa jibu halipatikani katika matambiko ya kipagani, lakini katika ushindi kwamba Kristo alishashinda nguvu za giza (Wakolosai 2:15).

► Uzushi wa Kolosai unahusiana vipi na sisi leo?

*Syncretism* hurejelea mchanganyiko wa dini zaidi ya moja. Katika Kolosai, syncretism ilichanganya vipengele vya uyahudi, Jewish Mysticism, upagani na ukristo. Leo, makanisa katika tamaduni za kipagani mara chache hujaribiwa kuchanganya fundisho la kikristo na vitendo vya tamaduni zinazozunguka (kwa mfano: ibada za mizimmu, sherehe za siku takatifu za kipagani, na ushiriki wa matambiko kuondoa mzimu na roho chafu). katika karne ya 1 na 21, jibu kwa mafundisho yote haya ni lile lile: Yesu ni Bwana. Amezishinda nguvu za giza, na tunao ushindi kupitia Kristo pekee. Hakuna matambiko au desturi nyingine zenye nafasi katika desturi za Kikristo.

### *Ukuaji katika ukomavu wa Kikristo (Wakolosai 3-4)*

Kama katika Waefeso, Paulo hutoka katika fundisho kwenda katika vitendo. Tangu Kristo aketi katika mkono wa kuume wa Mungu, sisi tuliofufuliwa katika Kristo lazima tuweke akili zetu katika vitu vya mbinguni. Badala ya kuzingatia mafundisho ya uongo. Lazima tukumbuke kuwa tulikufa katika mambo hayo na sasa tunaishi na Kristo katika Mungu. (Wakolosai 3:1-3).

---

[54] Katika mstari huu, "kuabudu malaika" pengine hakukumaanisha kwamba walikuwa wanaabudu malaika (ambapo ingekuwa kinyume na mafundisho yote ya Kiyahudi). Badala yake, kifungu hiki cha maneno pengine kilirejelea dhana za kisiri za Kiyahudi ambazo kupitia matendo ya ascetic (taratibu za kidini za kujikana), kama vile kufunga kwa muda mrefu, wanaoabudu wanaungana na malaika katika kiti cha enzi cha Mungu mbinguni. Waalimu wa uongo katika Kolosai walikuwa wanawaalika waamini kufuata taratibu hizi.

Maisha yaliyofichwa katika Kristo yanafananaje? Paulo anaelezea maisha yake mapya kwa vitendo, maisha haya hubeba mambo mawili ya msingi:

1. **Tunatakiwa kuvua utu wa kale na matendo yake (Wakolosai 3:5-9)**. Lazima tuue yale yaliyo ya dunia: uasherati, tamaa mbaya, hasira, mazungumzo machafu, kukosa uaminifu na zaidi. Vitendo hivi hustahili ghadhabu ya Bwana.

2. **Tunatakiwa kuvaa utu mpya ambao ni sura ya Kristo (Wakolosai 3:12-17)**. Tabia za utu mpya ni huruma, wema, utu, upole, uvumilivu, msamaha, na zaidi ya yote, upendo. Tunapokuwa na tabia hizi, amani ya Mungu itatawala mioyoni mwetu, na neno la Kristo litadumu ndani yetu. Maidha haya mapya hubadili mahusiano ya familia na kazi (Wakolosai 3:18-4:1) na kufanya injili iwe yenye kuvutia kwa wasioamini (Wakolosai 4:5-6).

## Filemoni

### Usuli wa Filemoni

#### *Mazingira ya Kihistoria*

Barua fupi ya Paulo inaelekezwa kwa Filemoni, mwamini tajiri kutoka Kolosai. inaonekana kuwa Filemoni aliokoka wakati wa huduma ya Paulo katika Efeso. Nyumba yake ikawa mahala pa kukutania kwa kanisa la Kolosai.

Kama ilivyokuwa kawaida katika karne ya kwanza, Filemoni alikuwa akimiliki watumwa. Onesimo, mtumwa wa Filemoni, alikimbilia Rumi. Rumi ulikuwa ni mji uliosongamana sana katika ngome, mahala salama kwa wakimbizi kujificha. (Wakimbizi siku hizi husafiri kwenda New York City, Mexico City, Lagos, au miji mingine mikuu na kupotolea huko.)

Hata hivyo, Onesimo asingeweza kujifichwa kwa Mungu. Katika mji huu mkubwa,Mungu alimleta Paulo na mtumwa mkimbizi pamoja. Onesimo aligeuzwa na kuanza kumsaidia Paulo.

Wakati fulani, muamini huyu mpya alilazimishwa kuikabili historia yake ya nyuma. Inawezekana kuwa aliiba fedha toka kwa bwana wake kabla ya kukimbia (Filemoni 1:18). Onesimo alikabiliana na uwezekano wa kuadhibiwa; mtumwa mtoro hakuwa na chapa katika paji la uso kama mkimbizi au mfungwa au hata kuuawa. Akilijua hili, Paulo aliandika barua kumuimea msamaha Onesimo kumchukua tena wakati ataporudi kumkabili Filemoni.

#### *Kusudi*

Lengo la Paulo katika kuandika barua hii ni kukata shauri la patano. Onesimo amepatanishwa na Mungu; Paulo sasa anamuomba Filemoni apatanishwe na mtumwa wake aliyetoroka.

## Yaliyomo katika Filemoni

> "Sisi sote ni *Onesimi* wa Bwana. Tusio na faida na tukawa wa faida. Ni picha ya kudumu ya Kristo akishughulika na wanadamu. Sisi sote ni watumwa tunaokimbilia dhambi."
>
> - Martin Luther.

Paulo anaanza kwa kumshukuru Filemoni kwa ukarimu wake kwa waamini wenzie, Upendo wa Filemoni kwa kaka na dada zake katika imani utakuwa msingi wa rufaa ya Paulo kwa niaba ya Onesimo, ambaye sasa ni mmoja wao.

Paulo anaomba si kwa mamlaka yake ya kitume (kama katika Wagalatia), lakini katika misingi ya upendo. Ni kama yuko nusu ya barua yake kabla hajasema sababu ya kuandika kwake: "Nakusihi kwa ajili ya mtoto wangu...yaani, Onesimo…" (Filemoni 1:10). Filemoni ni mwana wa Paulo katika imani; sasa Paulo ana mwana mwingine, mtumwa wa Filemoni.

Jina Onesimo humaanisha "yenye manufaa" ama "ya faida"; lilikuwa ni jina lililozoeleka kwa watumwa. Paulo anaandika, "ambaye zamani alikuwa hakufai, bali sasa akufaa sana, wewe na mimi pia" (Filemoni 1:11). Onesimo sasa ataishi kulingana na jina lake. Kupitia nguvu ya Kristo, amekuwa wa manufaa.

Paulo anadokeza kuwa Filemoni angeweza kumfungua Onesimo, lakini hashurutishi (Filemoni 1:13). Anamuomba Filemoni ampokee Onesimo katika roho ile ile ambayo Filemoni angempokea Paulo (Filemoni 1:17).

Paulo anahitimisha kwa kumuomba Filemoni aombee kuachiliwa kwa Paulo. Anaandika kuwa anatumai kumtembelea Filemoni baada ya kuachiliwa toka gerezani. Je unadhani hii ni ukumbusho kuwa Paulo hivi punde ataona jinsi Filemoni anavyomchukulia Onesimo?

Watu wengi wamelalamika kwa sababu Paulo hakuhukumu utumwa. Hata hivyo, Paulo anaamuru mabwana watengeneze mazingira ambayo utumwa hautadumu.[55] Haiwezekani kumshikilia katika utumwa mtu ambaye unamuona kama ndugu au dada katika Kristo kweli kweli.

## Hitimisho la kihistoria

Andiko halisemi kilichotokea baada ya Onesimo kurudi kwa Filemoni. Hata hivyo, historia inatoa dokezo mbili zinazo pendekeza kuwa Filemoni alimwachia Onesimo:

- Andiko la kale katika Laodikia (iliyokuwa karibu na Kolosai) mfungwa ameliekeza kwa Bwana wake aliyemwachia. Jina la Bwana huyu ni Marcus Sestius Philemon (Marcus Sestius Filemoni).
- Miaka michache baada ya barua hii. Mtu alieitwa Onesimo alikwa Askofu wa kanisa la Efeso.

[55] Wagalatia 3:28, Waefeso 6:9, Wakolosai 4:1, Filemoni 1:16

Yawezekana kuwa Filemoni alimwachia Onesimo arudi kwa Paulo, ambaye hapo alimfundisha Onesimo kama Mchungaji. Kama ndivyo, huduma ya Paulo katika Efeso yaweza kuwa imeendelea kupitia mafundisho ya Onesimo, mtumwa wa awali wa Filemoni, ambaye hapo mwanzo aliokoka chini ya mafundisho ya Paulo kule Efeso. Makusudi ya Mungu ni zaidi ya yale tuyaonayo.

## Nyaraka za Kifungozi katika kanisa Leo

Nyaraka za Kifungozni zinatufundisha sisi kwamba:

1. **Fundisho lazima zitendewe kazi katika maisha ya kila siku**. Katika nyaraka hizi, Paulo anawapa changamoto wasomaji wake kuishi katika namna inayoustahili mwito wao kama waaminio. Haitoshi tu kukiri mfundisho sahihi; lazima tuiishi imani yetu katika maisha ya kila siku.

2. **Vita vya kiroho ni halisi, lakini Kristo amekwisha shinda ushindi wa mwisho.** "Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho" (Waefeso 6:12).

   Tunapigana kwa ujasiri kwa sababu Kristo amekwisha kushinda vita. Umakini wetu wa kwanza lazima uwe kwake, si kwa adui anayepigana vita aliyoishindwa.

3. **Lazima tuiishi Injili ya upatanisho katika dunia halisi.** Paulo hakuridhishwa na ujumbe ambao haufanyi kazi katika maisha halisi. Alisisitiza kuwa injili ile ile iliyompatanisha Mungu na mwenye dhambi ingeweza pia kumpatanisha Filemoni na mtumwa. Katika ulimwengu uliojaa ugomvi na mahusiano yaliyovunjika. Lazima tonyeshe nguvu ya injili katika kuleta upatanisho.

## Hitimisho

Waamini katika Dola ya Rumi walijifunza nini maana ya kuiishi injili katika dunia iliyoanguka. Paulo aliandika kuwa waamini lazima waishi kama watoto wa Mungu bila lawana yoyote katikati ya kizazi kilichoharibirika na kutikiswa. Tufanyapo hivyo, tunang'aa kama nuru katika ulimwengu (Wafilipi 2:15). Paulo alijua kuwa nuru ya kanisa hung'aa kwa mwanga zaidi kadri dunia inavyozidi kuwa giza.

Katika siku za giza za himaya ya Rumi, baadhi ya wafuasi wa Kristo walijulikana kwa jina la"Gamblers for Christ" ("Wacheza kamari wa Kristo") kwa sababu walihatarisha maisha yao ili kuwaokoa wengine.. Paulo anatumia kifu hii akimzungumzia Prisila na Akila in Warumi 16:3-4, "Nisalimieni Priska na Akila, watenda kazi pamoja nami katika Kristo Yesu; waliokuwa tayari hata kukatwa kichwa kwa ajili ya maisha yangu; ambao ninawashukuru, wala si mimi tu, ila na makanisa ya Mataifa yote pia; nisalimieni na kanisa lililomo katika nyumba yao."

Katika karne ya 1 , waamini wa kirumi walijihatarisha dhidi ya gadhabu ya jamii ili kuokoa watoto wachanga waliokuwa hawatakiwi ambao walikuwa wametupwa katika majalala ya

mji. Katika karne ya 3, askofu wa Carthage aliita kusanyiko lake pamoja wakati wa mapigo, akiwataka wawajali walio katika hali ya kufa na kuwazika waliokwisha kufa, wakihatarisha maisha yao kuokoa mji.

Kanisa la awali lilijua kuwa kuvua utu wa kale na kuvaa utu mpya humaanisha zaidi ya kuhudhuria makusanyiko ya ibada. Humaanisha kuishi maisha mapya yanayomilikiwa na Mungu na kusudi lake. Inaweza hata kumaanisha kuwa tayari kuyatoa maisha yetu ili kung'aa kama nuru katika ulimwengu.

## Somo la 7 Mazoezi

(1) Andaa ujumbe au somo la Biblia kwa msingi wa kitabu/mada zilizounganishwa katika orodha hapa chini. Unaweza kuwasilisha hii ama katika maandishi (kurasa 5-6) au wasilisha rekodi ukiwa unahubiri au kufundisha.

Chagua mojawapo ya chaguo zifuatazo:

- Waefeso – *Familia*
- Waefeso – *Kanisa*
- Wafilipi – *Furaha katika maisha ya Kikristo*
- Wakolosai – *Maisha yetu mapya ndani ya Kristo*

(2) Mwanzoni mwa somo linalofuata, utafanya jaribio kulingana na somo hili. Soma maswali ya jaribio kwa umakini katika maandalizi.

## Somo la 7 Jaribio

(1) Lini na kutoka mji gani ambapo Nyaraka za Kifungoni ziliandikwa?

(2) Kwa nini hakuna salamu binafsi zilizojumuishwa katika Waefeso?

(3) Taja sehemu kubwa mbili za Waefeso.

(4) Kulingana na Waefeso 1, nini ni wajibu wa Baba katika wokovu wetu? Wa Mwana? Na wa Roho Mtakatifu?

(5) Fafanua *uchaguzi*.

(6) Kulingana na Waefeso 3, siri ya Injili ni nini?

(7) Orodhesha hatari mbili zilizokuwa zinawakabili kanisa la Filipi?

(8) Katika Wafilipi 2, inamaanisha nini kwamba Yesu Kristo "alijinyenyekesha"?

(9) Uzushi wa Kolosai ulijumuisha mchanganyiko wa mawazo ya uongo kutoka katika ushawishi gani wa aina tatu?

(10) S*yncretism* inarejelea nini?

(11) Taja mambo matatu ambayo Nyaraka za Kifungoni zinalifundisha kanisa la leo.

(12) Andika Waefeso 4:11-16 na Wakolosai 3:1-4 kutoka katika kumbukumbu.

# Somo la 8
# Wathesalonike
# Kurudi kwa Kristo

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kufahamu tarehe inayokadiriwa na mazingira ya kihistoria ya 1 na 2 Wathesalonike.

(2) Kueleza mada za msingi na makusudi ya 1 na 2 Wathesalonike.

(3) Kutiwa moyo kuendelea kuwa mwaminifu wakati wa upinzani kutoka kwa wasioamini.

(4) Kuonyesha uelewa wa kina wa fundisho la kurudi kwa Kristo.

(5) Kuishi leo kwa ufahamu wa kina na makini kuhusu kurudi wa Kristo.

(6) Kuhusianisha ujumbe wa vitabu hivi na mahitaji ya ulimwengu wa leo.

## Maandalizi kwa Ajili ya Somo Hili

► Soma 1 na 2 Wathesalonike.

► Kariri 1 Wathesalonike 5:23-24.

## Utangulizi

Kanisa la Thesalonike lilianzishwa katika kipindi cha mateso. Waumini hawa walijua maana ya kuteseka kwa ajili ya jina la Kristo. Waligeuzwa walipoamini ukweli wa mhubiri ya Paulo: "Yesu huyu ninayewapasha ninyi habari zake ndiye Kristo" (Matendo ya Mitume 17:3). Walikuwa jasiri, tayari kuteswa kwa ajili ya imani yao.

Kwa sababu ya upinzani, Paulo alikaa kwa muda mfupi tu huko Thesalonike. Kwa sababu ya hali hiyo, Paulo hakuweza kuwafundisha kikamilifu mafundisho ya kikristo. Baada ya Paulo kuondoka Thesalonike, maswali mengi yalizuka kuhusu kurudi kwa Kristo. Walipo kabiliwa na mateso, waumini hawa wachanga walikuwa na maswali kuhusu tumaini lao la baadae.

Paulo anaandika barua hizi mbili ili kuwatia moyo wendelee kuwa waaminifu. Anawahakikishia kwamba Yesu atarudi na kwamba wanapaswa kuishi leo kwa kuzingatia ahadi hiyo.

## Usuli wa 1 na 2 Wathesalonike

Kanisa la Thesalonike lilianzishwa wakati wa safari ya pili ya umishonari ya Paulo. Baada ya kuondoka Filipi, Paulo alisafiri kupitia Amfipoli na Apolonia hadi Thesalonike (Matendo ya Mitume 17:1), umbali wa takribani kilomita 160 kutoka[56] Filipi.

Paulo alifundisha katika sinagogi huko Thesalonike kwa sabato tatu (Matendo ya Mitume 17:2). Baadhi ya Wayahudi na Wagiriki wengi waliokuwa waumini waligeuzwa (Matendo ya Mitume 17:4).[57] Kwa kujibu hilo, kikundi cha Wayahudi wasioamini walianzisha ghasia, wakishambulia nyumba ya Yosani, ambako Paulo na Sila walikuwa wakikaa (Matendo ya Mitume 17:5-9).

Kwa sababu ya hatari hiyo, Paulo na Sila waliondoka mjini usiku na kusafiri kwenda Beroya, umbali wa takribani kilometa 80[58] kutoka Thesalonike (Matendo ya Mitume 17:10). Wayahudi wa Thesalonike waliposikia kwamba Paulo alikuwa Beroya, walimfuata na kuleta machafuko huko pia (Matendo ya Mitume 17:13). Inaonekana upinzani huo ulimlenga Paulo, kwa sababu aliweza kuwaacha Sila na Timotheo Beroya wakati alipokuwa akiendelea kwenda Athene (Matendo ya Mitume 17:14).

Kutoka Athene, Paulo alisafiri kuelekea Magharibu hadi Korintho, ambako alihudumu kwa miezi 18. Sila na Timotheo waliungana na Paulo huko Korintho. Baadaye Timotheo alitembelea Thesalonike kisha akarudi kwa Paulo, akimletea habari za kanisa changa.

Paulo aliandika 1 Wathesalonike akijibu taarifa kutoka kwa Sila na Timotheo. Inawezekana alimpeleka Timotheo kupeleka barua hiyo huko Thesalonike. Miezi michache baadaye, akijibu habari zaidi, aliandika waraka wa 2 Wathesalonike. Barua hizi mbili ziliandikwa kutoka Korintho katika mwaka 50-51 B.K. Hizi zimo miongoni mwa barua zake za mwanzo kabisa, zikitanguliwa tu na Wagalatia.

[56] Maili 100

[57] Katika mstari huu, kifungu cha maneno "Wayunani waliomcha Mungu" Kinarejelea watu wa mataifa walipokuja katika Sinaogi kumwabudu Yahweh, ingawa hawakuwa wameongoka kikamilifu katika dini ya Kiyahudi.

[58] Maili 50

| Paulo na kanisa la Thesalonike | |
|---|---|
| A.D. 50 | **Paulo, Sila, naTimotheo walihubiri Thesalonike (Matendo ya Mitume 17:1-4).** |
| | Baada ya majuma machache, walitoroka kwenda Beroya (Matendo ya Mitume 17:5-10). |
| | Paulo aliwaacha Sila na Timotheo huko Beroya wakati aliposafiri kuelekea Athene (Matendo ya Mitume 17:14-15) na kwenda hadi Korintho (Matendo ya Mitume 18:1). |
| | Sila naTimotheo waliungana na Paulo huko Korintho (Matendo ya Mitume 18:5). |
| | **Paulo alimtuma Timotheo kutembelea Thesalonike (1 Wathesalonike 3:1).** |
| | **Timotheo alileta habari kutoka Thesalonike (1 Wathesalonike 3:6).** |
| A.D. 50-51 | **Paulo aliandika 1 Wathesalonike kujibu ripoti ya Timitheo** |
| | **Paulo aliandika 2 Wathesalonike kujibu maswali zaidi (2 Wathesalonike 2:1, 5).** |

## 1 Wathesalonike

### Kusudi la 1 Wathesalonike

Wakati Timotheo alipowasili Korintho, taarifa yake kuhusu kanisa la Thesalonike ilikuwa ya kutia moyo; waumini hawa wachanga walikuwa wakidumisha uaminifu wao kwa Injili. Paulo aliwaandikia akiwatia moyo katika imani yao na kujibu maswali waliyokuwa nayo kuhusu kurudi wa Kristo. Baadhi ya washirika wa kanisa walikuwa wamefariki, na wengine waliogopa kwamba wale waliokufa walikuwa wamekosa ahadi ya kurudi kwa Kristo. Wale waliokuwa wakivumilia mateso, ilikuwa jambo la kuvunja moyo kufikiri kwamba uaminifu wao unaweza kuwa bure. Paulo akaandika ili awatie moyo Wathesalonike waendelee kuwa waaminifu katikati ya upinzani na kuwahakikishia kwamba Kristo atarudi kwa wale waliokufa katika imani na kwa wale ambao wataendelea kuwa hai wakati wa kuja kwake.

### Mada kuu za 1 Wathesalonike

► Je wazo la kuja kwa pili linaleta hofu au tumaini? Mafundusho ya kuja mara ya pili yanaathirije maisha yako ya kila siku?

Ikiwa imeandikwa muda mfupi baada ya huduma ya Paulo kwa Thesalonike, barua hii ni ya kipekee sana. Ingawa Paulo hawataji watu binafsi, anaeleza kwa kina huduma yake huko

Thesalonike. Anawaandikia waumini walioko chini ya huduma yake; barua yake inaonyesha huruma yake ya kina kwa watoto wake katika imani.

### *Kutia Moyo katika Kupambana na Upinzani*

Alipokuwa akihubiri Thesalonike, Paulo alilionya kanisa kutarajia mateso (1 Wathesalonike 3:3-4). Sasa, Paulo anawaandikia waraka kuwatia moyo katika mateso hayo kwa:

- **Kuwahakikishia kwamba Anawaombea** (1 Wathesalonike 1:2, 1 Wathesalonike 3:9-13). Anataka wajue kwamba hajawasahau. Anaendelea kuwaombea wanapokabili upinzani.
- **Kuwakumbusha kielelezo chake mwenyewe cha uaminifu katika mateso** (1 Wathesalonike 2:1-2). Paulo anaonyesha matunda ya utayari wake mwenyewe wa kuvumilia mateso: kuokoka kwa Wathesalonike. Huduma yake huko Thesalonike ilimghalimu kibinafsi: mateso kutoka kwa adui zake na ulazima wa kufanya kazi za mikono ili kujitegemea (Matendo ya Mitume 17; 1 Wathesalonike 2:2, 9, 16). Hata hivyo thawabu zilistahili gharama hiyo. Waongofu hawa wapya ni utukufu na furaha yake (1 Wathesalonike 2:20). Hili linapaswa kuwahimiza Wathesalonike, wakijua kwamba mateso yao pia yataleta thawabu ya Mungu.
- **Kumshukuru Mungu kwa ajili ya uaminifu wao** (1 Wathesalonike 1:6-10, 1 Wathesalonike 3:6-10). Paulo anatiwa moyo na taarifa alizopokea na kwa upande wake, anawatia moyo na Wathesalonike. Uongofu wao na uaminifu wao katikati ya mateso vimekuwa ushuhuda kwa waumini wote wa Makedonia na Akaya (1 Wathesalonike 1:7).

### *Kurudi kwa Yesu Kristo*

Paulo alilazimika kuondoka Thesalonike kabla hajamaliza mafundisho yake. Kwa sababu ya hiyo, Waongofu wapya hawakuwa wamefundishwa kikamilifu kuhusu kifo cha waumini. Paulo anaandika ili kutoa mafundusho zaidi kuhusu kurudi kwa Kristo na siku za mwisho (1 Wathesalonike 4:13-5:11).

Ahadi ya kurudi kwa Kristo ni faraja kwa Wathesalonike, lakini sasa wanakabiliwa na tatizo linalowachanganya. Baadhi ya washirika wao wamekufa kabla ya kuuona utimilifu wa ahadi hii. Paulo anawahakikishia kwamba hata wale waliokufa wataona kurudi kwa Bwana (1 Wathesalonike 4:13-16).

Badala ya kuomboleza bila tumaini, wafuasi wa Kristo wanapaswa kukumbuka kwamba Bwana atashuka kutoka mbinguni na sauti ya mwaliko, na walio kufa katika Kristo watafufuka kwanza. Kisha wale walio hai na waliobaki watanyakuliwa pamoja nao, na pamoja tutakuwa na Bwana milele (1 Wathesalonike 4:16-17).

Wathesalonike walitaka maelezo kuhusu wakati wa kurudi kwa Kristo. Paulo anawaambia kwamba hawahitaji yeye awaandikie habari hiyo. Anawakumbusha yale ambayo tayari wanayajua: Kristo atarudi wakati usiotarajiwa (1 Wathesalonike 5:1-2).

Wakati siku ya Bwana itakapokuja kama mwizi usiku, uharibifu utawapata watoto wa giza. Lakini kwa watoto wa nuru siku wa Bwana itakua siku ya wokovu kupitia Bwana wetu Yesu Kristo (1 Wathesalonike 5:2-5, 9). Kwa waumini, kurudi kwa Yesu ni ujumbe wa kutia moyo, si wa kuogopesha. Wathesalonike wanapaswa kukabiliana na wakati ujao kwa ujasiri kwa sababu ya imani yao katika Kristo.

### *Kuishi Leo katika Utayari wa Kurudi kwa Kristo*

Mafundisho ya Paulo daima yanaelekezwa kwenye matumizi ya vitendo. Haya yanaongoza mafundsho ya Paulo juu ya eskataolojia. (*Eschatolojia* inarejelea fundisho au somo la siku za mwisho.) Paulo hana nia ya kubashiri bure kuhusu tarehe ya kurudi kwa Kristo. Hili linaongoza mafundisho yake kuhusu eskatolojia.

Baada ya kuwaonyesha kwamba Kristo atarudi kwa walio hai na wafu, Paulo anazungumzia umuhimu wa kuishi leo katika utayari wa kurudi kwa Kristo (1 Wathesalonike 4:1-12 na 1 Wathesalonike 5:1-24). Paulo anawahitaji wasomaji wake waishi kama watoto wa nuruni, na si kama watoto wa gizani. Waraka unatoa maelekezo maalumu kutuandaa sisi leo kwa ajili ya kurudi kwa Kristo kesho:

- Kuendelea kutembea kwa uangalifu katika njia inayompendeza Mungu (1 Wathesalonike 4:1-2).
- Kuishi maisha yenye usafi (1 Wathesalonike 4:3-8).
- Kuendelea kuongezeka katika upendano wa ndugu (1 Wathesalonike 4:9-10).
- Kuchukua tahadhari ya mambo yako binafsi (1 Wathesalonike 4:11).
- Kufanya kazi kwa kujitegemea mwenyewe, ili kuepuka aibu katika macho ya wasio amini (1 Wathesalonike 4:11-12).
- Uwe na kiasi na macho (1 Wathesalonike 5:6-8).
- Kutiana moyo na kuelimishana kuhusu kurudi kwa Bwana (1 Wathesalonike 5:9-11).
- Waheshimu wale walio na majukumu ya uongozi katika kanisa (1 Wathesalonike 5:12-13).
- Dumisha amani kati ya waumini (1 Wathesalonike 5:13).
- Sahihisha wale ambao hawaishi ipasavyo: wale walio wavivu, waliokata tamaa na dhaifu (1 Wathesalonike 5:14).
- Tenda mema, kwa waumini wengine na kwa watu wa ulimwengu unaowazunguka (1 Wathesalonike 5:15).
- Ishi maisha ya furaha (1 Wathesalonike 5:16).
- Ishi maisha ya kudumu katika maombi (1 Wathesalonike 5:17).

- Ishi maisha ya shukrani (1 Wathesalonike 5:18).
- Usizime kazi za Roho Mtakatifu (1 Wathesalonike 5:19).
- Usikatae neno linalonenwa kwa jina la Bwana. Badala yake, jaribuni mafundisho yote na mshike sana yaliyo mema (1 Wathesalonike 5:20-21).
- Jiepushe na aina zote za uovu (1 Wathesalonike 5:22).

Paulo anafanya zaidi ya kutoa maagizo; anawaombea waongofu hawa, ambao anahisi kuwa na uhusuano nao wa karibu. Maombi mawili katika 1 Wathesalonike lengo lake ni kwamba, waishi kwa uangalifu wakizingatia kuja kwa Kristo. katika 1 Wathesalonike 3:11-13, Paulo naomba kwamba waumini hawa wakue katika upendo na utakatifu kama maandalizi ya kuja kwa Yesu.

Kisha katika 1 Wathesalonike 5:23, Paulo anaomba kwamba Mungu aliyewapatanisha waumini hawa na yeye mwenyewe awatakase kabisa-roho, nafsi na mwili-na awahifadhi bila lawama wakiwa tayari kwa kuja kwa Bwana Yesu Kristo. Katika neno la mwisho la kutia moyo, Paulo anawahakikishia wasomaji wake kwamba utakaso huu ni kazi ya Mungu (1 Wathesalonike 5:24). Mungu, anayewaita waumini katika utakatifu, ndiye anayefanya kazi hiyo na kutuweka watakatifu.

## 2 Wathesalonike

### Kusudi la 2 Wathesalonike

Muda mfupi baada ya kutuma 1 Wathesalonike, Paulo alipata maswali zaidi kuhusu kuja kwa pili. Katika 2 Wathesalonike, Paulo anajibu maswli haya na kwa mara nyingine anawatia moyo Wathesalonike kuendelea kuwa waaminifu katika kujindaa na kurudi kwa Kristo. 2 Wathesalonike inatoa mafafanuzi zaidi ya mafundisho ya Paulo katika 1 Wathesalonike. Paulo anazungumzia kuchanganyikiwa kuhusiana na kurudi kwa Bwana na tabia zisizofaa miongoni mwa waumini.

| 1 Wathesalonike | 2 Wathesalonike |
|---|---|
| Kristo atarudi. | Kristo hajarudi bado. |

### Mada kuu za 2 Wathesalonike

#### *Kuelewa siku ya Bwana (2 Wathesalonike 1-2)*

Katika 1 Wathesalonike, Paulo alifundisha kwamba hatupaswi kukata tamaa kuhusu kifo cha waumini; Kristo atarudi kwa walio hai na walio kufa. Baada ya salamu fupi na kutoa shukrani kwa Mungu kwa ajili ya imani na upendo wao unaokua, 2 Wathesalonike inatoa mafunndisho zaidi kuhusu kurudi kwa Kristo. Paulo anaandika kwamba kuja kwa pili kutaleta wakati wa hukumu na uharibifu wa milele (2 Wathesalonike 1:9). Hata hivyo,

waamini hawapaswi kuogopa; siku ya hukumu pia itakuwa ni siku ambayo Kristo atatukuzwa katika watakatifu wake (2 Wathesalonike 1:10).

Katika 1 Wathesalonike, Paulo anajibu wazo potofu kwa waumini walio kufa kwamba wamekosa kurudi kwa Bwana. Katika 2 Wathesalonike, anajibu wazo potofu kwamba Bwana tayari amekwisha kurudi. Katika 1 Wathesalonike, Paulo anafundisha kwamba Kristo atarudi; katika 2 Wathesalonike, Paulo anafundusha kwamba Kristo bado hajarudi.

Mtu fulani aliripoti kwa uongo kwamba siku ya bwana ilikuwa tayari imewadia. Paulo hakujua chanzo cha mafundisho haya. Huenda kulikuwa na mtu aliyedai kuwa ana karama ya unabii ("kwa roho"), au neno lililohubiriwa, au barua ya kughushiwa, inayodaiwa kuandikwa na Paulo (2 Wathesalonike 2:2). Bila kujali chanzo chake, Paulo anawahakikishia wasomaji wake kwamba ile siku bado haijawadia. Matukio mawili lazima yatokee kabla siku ya Bwana kufika: uasi na ufunuo wa mtu mharibifu (2 Wathesalonike 2:3-4). Matukio haya bado hayajatokea. Paulo anawahakikishia kwamba kurudi kwa Kristo badi ni tukio la wakati ujao, na anawaonesha kwa mshangao kwamba wamesahau mafundisho yake ya kwanza kwenye somo hili (2 Wathesalonike 2:5).

### *Ishi kwa utayari kwa ajili ya siku ya Bwana (2 Wathesalonike 3)*

Kama ilivyo katika 1 Wathesalonike, wasiwasi wa kwanza wa Paulo katika 2 Wathesalonike ni namna waumini wanavyoishi leo katika nuru ya ujio wa Kristo hapo badae. Katika 1 Wathesalonike, Paulo alifundisha, "kwa sababu Kristo anakuja, muishi hivi……." katika 2 Wathesalonike, Paulo anafundisha , "kwa sababu Kristo bado hajarudi, endeleeni kuishi namna hii…."

Kwa kadiri Wathesalonike wanavyo subiria kurudi kwa Kristo, wanapaswa:

- Kusimama imara katika mafundisho waliyo fundishwa (2 Wathesalonike 2:15).
- Kuepuka uvivu (2 Wathesalonike 3:6-12).
- Kuepuka kujishughulisha na mambo ya wengine (2 Wathesalonike 3:11-12).[59]
- Kuendelea kutenda mema (2 Wathesalonike 3:13).
- Kuwashauri walio wakaidi wasio tii maelekezo ya Paulo (2 Wathesalonike 3:14-15).

[59] 2 Wathesalonike 3:6-12 ilishughulikia matatizo mawili waliyokuwa nayo. Wale wote ambao walikuwa hawafanyi kazi badala yake walikuwa wakijishughulish na mambo wa waumini wenzao. Paulo akawaambia wafanye kazi zao na kuacha kushughulika na mambo ya wengine. Kama wangetii maelekezo ya kwanza, wasingekuwa na muda wa kuingilia mambo ya wengine.

## 1 na 2 Wathesalonike katika Kanisa Leo

Kuna mvuto mkuwa sana leo katika somo la mambo ya siku za mwisho na kurudi kwa Yesu. Manabii waalimu walijaribu kuhubiri wakati wa kurudi kwa Bwana. Vitabu vinavyojulikana kama "Biblia za siri" vina jaribu kufunua siri ya kweli katika maandiko. Waandishi wa kikristo walichapisha Riwaya maarufu zilizo zingatia kwenye kile wanachofikiri kitatokea baada ya kurudi kwa Yesu.

1 na 2 Wathesalonike inaonyesha utofauti mkubwa wa msisitizo. Barua hizi zinaonyesha kwamba tunapaswa kuendelea kuishi kwa uaminifu hadi kurudi kwa Kristo, kuliko kufunua taarifa zilizofichika kuhusu kurudi kwake. Paulo hakupoteza muda kujadili wakati wa kurudi kwa Kristo. Badala yake, ujumbe wake ulikuwa huu: Kristo atarudi; hakikisha kwamba unaishi katika njia ambayo unataka kuonekama atakaporudi. Huu unapaswa kuwa ni ujumbe tunao usisitiza tunapo hubiri kuhusu kurudi kwa Kristo.

> "John Wesley alikuwa akiuliza je! Angefanya nini kama angefahamu Bwana wake atakuja siku inayofuata. Alisema, usiku ningekwenda kitandni na kulala. Na asubuhi ningeliamka na kuendelea na kazi yangu, kwasababu ningetaka anikute nikifanya kile alicho nipa nikifanye.'".
>
> - Imenakiliwa na
> G. Campbell Morgan.

## Hitimisho

Mwaka 1998, imani potofu katika Taiwan ilitabiri kwamba Yesu angerudi tarehe 31 mwezi wa tatu. Baadhi ya wakristo waliuza nyumba zao na kuacha kazi zao. Walikutana pamoja mlimani kwa ajili ya kungojea kurudi kwa Kristo. Magazeti yalichapishwa huko Taiwan yakiripoti kuhusu kundi hili na mafundisho yao. Wakati Yesu hakurudi kwenye huo muda walio utarajia, makanisa yalidhihakiwa na marafiki zao wasioamini.

Hii haikuwa mara ya kwanza kwa huo utabiri wa uongo kuhusu kurudi kwa Yesu kuleta aibu kanisani. Marekani, kitabu kilitabiri Yesu anarudi katika mwaka wa 1988 waliuza takribani nakala milion 5 za vitabu. Baadhi ya redio za dini na vituo vya televisheni zilitoa maelekezo muhimu ya kujiandaa kwa unyakuo.

Hivi karibuni, Harold Camping alitabiri unyakuo mwaka 2011. Utabiri huo ulionekana kuwa ni wa uongo. Tena, wasioamini wakawacheka Wakristo kwa kumini utabiri huo.

Watu bado wanarudia kutoa utabiri kuhusu unyakuo, na hizo tabiri zote zimeonekana kuwa ni za uongo. Yesu mwenyewe alionya kuhusu kujaribu kuamua siku ya kurudi kwake (Mathayo 24:36). Badala ya kujaribu kufanya utabiri, tunapaswa kufanya kazi ya Bwana wetu. Kama waumini wa Thesalonike, tunapaswa kujitoa wenyewe kuishi katika njia ambayo itatufanya sisi kujiandaa kwa kurudi kwa Yesu wakati wowote.

## Somo la 8 Mazoezi

(1) Chagua moja katika ya mazoezi yafuatayo:

- Baada ya kusoma 1 na 2 Wathesalonike, andika insha ya ukurasa mmoja juu ya "Kuishi Leo katika Utayari kwa ajili ya Ujuo/kurudi kwa Kristo." Hii inatakiwa kuwa insha ya kivitendo ambayo inaonesha namna ambavyo kurudi kwa Kristo kunaathiri maisha yetu leo.
- Andaa ujumbe au somo la Biblia juu ya kurudi kwa mara ya pili kwa msingi wa 1 na 2 Wathesalonike. Unaweza kuwasilisha hii ama katika maandishi (kurasa 5-6) au wasilisha rekodi ukiwa unahubiri au kufundisha.

(2) Mwanzoni mwa somo linalofuata, utafanya jaribio kulingana na somo hili. Soma maswali ya jaribio kwa umakini katika maandalizi.

## Somo la 8 Jaribio

(1) Kwa nini waumini Wathesalonike walijua maana ya kuteseka kwa ajili ya jina la Kristo?

(2) Orodhesha namna tatu ambazo Paulo analitia moyo kanisa la Thesalonike katika wakati wa mateso.

(3) Ni nini ambacho Wathesalonike walikuwa tayari wanafahamu kuhusiana na kurudi kwa Kristo?

(4) Nani anawafanya na kuwatunza waamini kuwa watakatifu?

(5) Kama ujumbe wa msingi wa 1 Wathesalonike ni "Kristo atarudi," nini ni ujumbe wa msingi wa 2 Wathesalonike?

(6) Tunapohubiri juu ya kurudi kwa Bwana, ni ujumbe gani ambao tunapaswa kusisitiza?

(7) Andika 1 Wathesalonike 5:23-24 kutoka katika kumbukumbu

# Somo 9
# Timotheo na Tito
# Nyaraka kwa Wachungaji

## Malengo ya Somo

Mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kufahamu tarehe sahihi na mazingira ya kihistoria ya Nyaraka za Kichungaji.

(2) Kuorodhesha mada kuu na kusudi la Nyaraka za Kichungaji.

(3) Kuibua sifa za kibiblia kwa viongozi wa Kanisa.

(4) Kupata heshima ya ndani kwa majukumu ya kichungaji kwenye maeneo kama vile mafundisho ya kimaelekezo, taasisi ya kanisa, na uongozi wa Roho Mtakatifu.

(5) Kupewa changamoto kuishi maisha ya uaminifu kwa wito wa Mungu.

(6) kufupisha kanuni za kiutendaji kwa huduma ya Kikristo kutoka kwenye nyaraka za kichungaji.

(7) Kuhusianisha ujumbe wa vitabu hivi katika uhitaji wa ulimwengu wa leo.

## Maandalizi kwa ajili ya Somo hili

► Orodhesha baadhi ya mambo ya kuzingatia kwa Mchungaji Kijana. Kisha, tafuta lipi kati ya mambo haya yameshughulikiwa kwenye 1 Timotheo na Tito. Soma 1 na 2 Timotheo na Tito.

► Kariri 2 Timotheo 4:7-8 na Tito 2:11-14.

## Utangulizi

Tito na 1 na 2 Timotheo zinajulikana kama Nyaraka za Kichungaji, au Barua za Kichungaji. 1 Timotheo na Tito kuna uwezekano ziliandikwa kati ya 64 B.K. na 65 B.K. 2 Timotheo ni barua ya mwisho ya Paulo, iliandikwa muda mfupi kabla ya kifo chake mnamo mwaka 66 au 67 B.K.

Barua hizi ziliandikwa kwa vijana ambao Paulo aliwafundisha. Kwa sasa walikuwa ni wachungaji ambao walikuwa wakiongoza makanisa. Paulo anaandika kushughulikia matatizo ambayo yaliibuka katika maakanisa yao.

Kinyume cha nyaraka kwa makanisa, hizi ni nyaraka binafsi. Ni barua kutoka kutoka kwa mwalimu mwenye kuheshimiwa kwa wanafunzi ambao wanakumbana na changamoto

kwenye uteuzi wao wa kwanza. Kwa sababu ya historia hii, vitabu hivi ni chanzo cha thamani sana kwa wachungaji wapya wanaotafuta ushauri wa kibibria kwenye kuliongoza kanisa.

## 1 Timotheo

### Usuli wa 1 Timotheo

#### *Mpangilio wa kihistoria*

Wakati Paulo aliposafiri kwenda Makedonia kufuatia kufunguliwa kwake kutoka gerezani, aliondoka akamwacha Timotheo kuchunga kanisa Efeso (1 Timotheo 1:3). Paulo alipanda kanisa hili dogo takribani miaka mitano hadi nane ya hapo mwanzoni.

#### *Kusudi*

Paulo ananandika barua hii:

1. Kumpa Timotheo maelekezo kuhusu walimu wa uongo,mambo ya sera za kanisa, na uteuzi wa maafisa wa kanisa.
2. Kumtia moyo Timotheo katika nafasi yake kama Mchungaji.

### Mada kuu za 1 Timotheo

#### *Walimu wa uongo ndani ya Kanisa*

Lengo la kwanza ndani ya barua hii ni kumsaidia Timotheo kushughulika na walimu wa uongo ambao wanalisumbua Kanisa huko Efeso. Kuliko kushughulikia mafundisho yake kwa kina, Paulo anaonya dhidi ya madhara ya fundisho. Fundisho potofu limetokana na maswali ya hoja na mahaojiano (1 Timotheo 1:4, 6). Walimu hawa wanataka kuonekana kama walimu, lakini hawafahamu vitu wanavyovifundisha (1 Timotheo 1:7). Badala ya malumbano yasiyo na maana na uvumi, Mungu analitaka kanisa lake kujengana kila mmoja katika upendo unaotoka katika Moyo safi, ufahamu mzuri, na imani ya kweli (1 Timotheo 1:5).

Ina onekana kwamba sehemu ya ujumbe wa hawa walimu wa uongo unahusiana na matumizi yasiyo sahihi ya sheria. Paulo anathibitisha thamani ya sheria pale ambapo inatumika kwa usahihi na anaorodhesha baadhi ya dhambi ambazo ni matokeo ya kutokutii kanuni zilizofundishwa katika sheria. (1 Timotheo 1:8-10). Wakati Wagalatia inaonyesha kwamba wafuasi wa Kristo wana hesabiwa haki kwa neema, na sio kwa sheria; 1 Timotheo inaonyesha kwamba sheria inafanya jukumu la umuhimu sana katika kuonya dhidi ya kufanya yale yasiyo mpendeza Mungu.

Paulo anaitikia kazi ya walimu wa uongo kwa:

- **Kumtia moyo Timotheo**. Paulo anampa ushuhuda wake binafsi kama mtu ambaye alikuwa adui wa Kristo lakini ambaye alipokea rehema (1 Timotheo 1:12-17).

Ushuhuda wa Paulo unampa Timotheo ujasili katika nguvu ya Kristo kubadilisha maisha.

- **Kusisitiza fundisho la kweli.** Paulo anajibu fundisho la uongo kwa fundisho la kweli. Katika 1 Timotheo 4, Paulo anaagiza fundisho sahihi kama dawa kwa sumu ya fundisho la uongo.

- **Tahadhari dhidi ya dhamira isiyo sahihi***.* Baadae kwenye barua, Paulo anatazama kwenye dhamira ya walimu wa uongo. Kwenye 1 Timotheo 6:3-5, Paulo anaonya kwamba mafundisho yao yanatokana na Kiburi na fikra zilizoharibika na uchoyo. Jibu kwa jambo hili ni kuridhika na kile tulichonacho (1 Timotheo 6:6-8). Kupenda pesa kumesababisha baadhi ya watu kutangatanga kutoka kwenye imani (1 Timotheo 6:9-10). Badala yake, wakristo wa kweli lazima "…ukafuate haki, utauwa, imani, upendo, saburi, upole" (1 Timotheo 6:11).

### *Maelekezo kwa Kanisa*

► Zipi ni sifa za viongozi katika kusanyiko lako? Tengeneza orodha kisha linganisha orodha yako kwa 1 Timotheo 3:1-13 and Tito 1:5-9.

Mengi ya 1 Timotheo yana husisha ushauri wa Paulo kwa Timotheo. Paulo anatoa mwongozo kwa kijana Timotheo juu ya maswala kama vile:

1. **Maombi ya ushirika na ibada ya umma** (1 Timotheo 2). Maswala ya kuabudu na tabia kwenye ibada za umma vilikuwa ni muhimu kwa mchungaji kijana kama Timotheo.

2. **Sifa kwa viongozi wa Kanisa** (1 Timotheo 3). Kulikuwa na ofisi mbili kwa kanisa la kwanza. Maaskofu (waangalizi) walifundisha na kuhubiri. Walikuwa wanawajibika na kulitunza kundi na kuongoza waamini dhidi ya madhara ya kiroho. (Matendo ya Mitume 20:28-31). Mashemasi walikuwa wanahusika zaidi na maeneo ya huduma za kimwili. (Neno la kigiriki kwa Shemasi, *diakonos*, likiwa na maana ya " Mtumishi.") Sifa za Paulo kwa ofisi zote mbili zililenga zaidi kwenye tabia kuliko kwenye jukumu maalumu. Jambo la msingi ambalo Paulo alizingatia ni kwamba viongozi wa kanisa wawe na tabia ambayo zitawawezesha wao kuliongoza Kanisa la Mungu.

3. **Uhitaji wa makundi maalumu ndani ya Kanisa** (1 Timotheo 5:1-6:2). Jambo lingine kwa mchungaji kijana ni jinsi gani ya kushughulikia mahitaji ya makundi tofauti tofauti ndani ya Kanisa. Paulo anatoa maelekezo juu ya kuwasaidia wajane, wazee wa kanisa, na hata wafungwa.

### Hitimisho la 1 Timotheo

Paulo anahitimisha waraka wake kwa Timotheo na maagizo ya kubaki kuwa mwaminifu katika kuvipiga vita vizuri vya Imani na kumkumbusha kuto kuyumbishwa na mbwembwe zisizo na heshima na maarifa ya uongo (1 Timotheo 6:12-21). Timotheo amekabidhiwa

injili, na hiyo kwake inapaswa kuwa kitu cha msingi kuzingatia—na kitu cha msingi cha kuzingatia kwa kila Mchungaji ambaye anafuatia nyayo za Timotheo.

## Tito

### Usuli wa Tito

#### *Mpangilio wa kihistoria*

Tito alikuwa muumini mmataifa, yawezekana aliokoka chini ya huduma ya Paulo (Tito 1:4), ambaye alimsaidia Paulo katika huduma. Alikuwa pamoja na Paulo angalau mara moja wakati wa kutembelea Yerusalemu (Wagalatia 2:1-3) na alimwakilisha Paulo ndani ya Korintho kipindi cha mahangaiko ya Paulo na lile kanisa sumbufu (2 Wakorintho 7:13-14, 2 Wakorintho 8:16-17). Wakati wa waraka huu, Tito alikuwa akitumika kwenye kisiwa cha milima ya Krete. Alimfuatana na safari ya Paulo kutembelea Krete, Tito aliachwa kusimamia makanisa ndani ya miji yenye idadi kubwa ya watu pembezoni mwa Pwani.

Mwishoni mwa Barua, Paulo anamuomba Tito kuungana naye katika mji wa Nikopoli (Tito 3:12). Kuanzia 2 Timotheo 4:10, inaonekana kwamba Tito baadaye alitumwa kutoka Nikopoli kwenda mkoa jirani wa Dalmatia. Kwa kipindi hiki, Paulo alikuwa amekamatwa na kupelekwa Rumi, ambapo angeteseka kwa kufa kwa ajili ya imani.

#### *Kusudi*

kama 1 Timotheo, Tito iliandikwa kuongoza mchungaji kijana katika kujenga kanisa la mahali. Paulo anaelezea walimu wa uongo, sifa za uongozi wa kanisa, na tabia za kikristo. Ujumbe mkuu wa waraka ni umuhimu wa mtindo wa maisha ya mkristo kama kielelezo kionekanacho cha Imani iokoayo.

### Mada kuu za Tito

#### *Hatari ya walimu wa uongo*

Mafundisho ya uongo yalikuwa ni hatari za mara kwa mara ndani ya kanisa la kwanza. Paulo anaitikia katika njia tatu:

1. Aliitaji uongozi bora ndani ya Kanisa. (Tito 1:5-9).
2. Alielezea kwamba mtindo wa maisha wa walimu wa uongo unathibitisha makosa ya ujumbe wao. (Tito 1:10-16, Tito 3:9-11).
3. Alitoa picha ya kuishi kwa haki (Tito 2:1-3:9).

Kama ilivyo siku zote, njia ya Paulo ni kusisitiza Ukweli, sio tu kushambulia makosa.

***Umuhimu wa Kazi Nzuri***

Walimu wa uongo walijulikana kwa mtindo wao mwovu wa maisha ambao unazalishwa na mafundisho yao. Wale waliowafuata walimu wa uongo kule Krete walikuwa wenye kuchukiza, kutokutii, wasiofaa kwa kazi yoyote nzuri (Tito 1:16). Hata hivyo, fundisho la kweli linapaswa kujulikana kwa mtindo wa maisha linaouchochea. Baada ya kuonya dhidi ya walimu wa uongo, Paulo anauelekeza waraka katika picha ya maisha ya kweli ya Kikristo. Paulo anasisistiza kwamba fundisho la kweli litaongoza kwenye tabia sahihi.

> **Tito 2:11.**
>
> "'*Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa.'*
>
> Ni huru kama vile jua linavyo angaza kwa kila mtu, hivyo Jua la kiroho limetutokea kwetu sote.Katika kesi zote mbili,wale tu ambao kwa utayari wamefumba macho yao hunyimwa faida ya Neema."
>
> - Imetolewa toka Adam Clarke *Ufafanuzi juu ya Agano Jipya.*

Paulo anampa changamoto Tito kufundisha tabia ambayo ni thabiti na fundisho la kweli (Tito 2:1). Kama washirika wa kanisa la krete wanaishi ipasavyo, maisha yao yataendana na fundisho lilofundishwa na Paulo na Tito. Paulo anatoa maelekezo maalumu kwa wanaume wazee, wanawake wazee, vijana wa kike, vijana wa kiume, na watumishi. Paulo anamkumbusha Tito kwamba kiongozi lazima aonyeshe mfano wa mambo yote mawili kazi nzuri na fundisho sahihi.

Mtindo makini wa maisha ni ushuhuda wenye thamani wa kweli ya Injili. Paulo anatoa motisha ya kazi nzuri:

1. Kwamba asiwepo mtu wa kulikufuru Neno la Bwana kwa sababu ya tabia mbaya ya mwamini (Tito 2:5).
2. Kwamba tabia ya mwamini inaleta heshima kwa fundisho la Mungu (Tito 2:10).

Mtindo wetu wa maisha unapaswa kudhihirisha mfano wa Yesu. "ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki yake mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema" (Tito 2:14). Wasioamini wanavutiwa kwenye Injili kupitia maisha ya watu wa Mungu.

Mafundisho ya Paulo katika kitabu cha Tito ni muunganiko wa umuhimu kwa mafundisho yake kwenye Wagalatia. Kwenye Wagalatia, Paulo anaonya dhidi ya wale wanaoamini kwamba kazi nzuri itawapatia kuhesabiwa haki. Kwenye Tito, Paulo anaonya dhidi ya wale ambao wanafundisha kwamba kuhesabiwa haki hakuzalishi kazi nzuri.

Kwa hakika tunapohesabiwa haki kwa neema kupitia imani, tutaishi maisha yaliyobadilishwa. Paulo anaweka wazi kwenye Tito, kama ilivyo kwenye Wagalatia, kwamba tunaokolewa sio kwa matendo na kazi zetu za haki, bali ni kwa rehema za Mungu. (Tito 3:5). Japo hatuokolewi kwa kazi zetu njema, wokovu umebadilisha kila mtazamo wa maisha yetu. Kabla ya kuhesabiwa haki "…tulikuwa hatuna akili, tulikuwa waasi, tumedanganywa, huku tukitumikia tamaa na anasa za namna nyingi, tukiishi katika uovu na husuda,

tukichukiza na kuchukiana” (Tito 3:3). Sasa kwa kuwa tumefanywa wapya, lazima tuwe waangalifu katika kujitoa wenyewe kwa kazi nzuri (Tito 3:8).

Paulo anahitimisha waraka na maelekezo binafsi. Anamtuma Artema au Tikiko kuwa mbadala wa Tito uko Krete. Wakati mbadala huu utakapowasili, Tito anatakiwa kumleta Zena na Apolo na kuungana na Paulo uko Nikopoli.

## 2 Timotheo

### Historia kwa 2 Timotheo

#### *Kusudi*

2 Timotheo, waraka wa mwisho wa Paulo, uliandikwa mnamo 65-67 B.K. kipindi ambapo akingojea hukumu ya kifo chake. Baadhi ya jamaa walimtenga, na wengine walikuwa mbali kwenye shughuli, hivyo yupo mwenyewe. Anaandika Timotheo, anaomba msaada wake. Paulo anasikia baridi, hivyo anamwomba Timotheo kumletea nguo. Anaitaji msaidizi, hivyo anamwomba Timotheo kumleta Yohana Marko. Anataka kuendelea na kazi yake mpaka mwisho, hivyo anaagiza vitabu vyake na ngozi (2 Timotheo 4:9-13).

| Vifungo viwili vya Paulo | |
|---|---|
| **Kifungo cha kwanza** | **Kifungo cha Pili** |
| Alishtakiwa na wayahudi | Alikamatwa na Rumi |
| Paulo ana uhuru wa kukaribisha wageni | Paulo ni mpweke |
| Katika nyumba ya kupangisha | Ndani ya chumba cha baridi cha gereza. |
| Kinaishia na kufunguliwa kwa Paulo. | Kinaishia na utekelezaji wa Paulo. |

### Ujumbe wa 2 Timotheo

#### *Uaminifu*

Mwishoni mwa maisha yake, Paulo alitazama nyuma kwenye maisha yake ambayo amekuwaa akiyaishi katika uaminifu na utii kwa wito wa Mungu. Alitazama mbele pia kwa wale kama akina, Timotheo, ambao wataiendeleza huduma huko mbeleni. Uaminifu ni jambo la muhimu sana kwa Paulo kwa wakati huu katika maisha yake. Anampa changamoto Timotheo kuendelea kwa uaminifu kwenye huduma.

Kama mfano wa kutokuwa na uaminifu, Paulo anataja baadhi kwenye jimbo la Asia ambao walimtenga, hususani Figelo na Hermogene (2 Timotheo 1:15). Paulo anateseka na kusalitiwa na watenda kazi wenzake ambao wameacha huduma au kujitoa kutoka kwenye fundisho la kweli. Baadae, anamtaja Dema, mtenda kazi mwingine wa mwanzoni ambaye amemwacha (2 Timotheo 4:10). Uaminifu kwa Mungu haimanishi kwamba maisha hayatakuwa na kukatishwa tamaa. Lakini zaidi ya mateso ya kimwili ya mashua/meli

kuvunjika wakiwa baharini na kufungwa, na zaidi ya msongo wa kimawazo wa jinsi ya kushughulika na matatizo ya makanisa kama vile Galatia na Korintho, Paulo ameteseka kutokana na maumivu ya kihisia ya kutengwa na kuachwa katika kipindi hiki kigumu.

Kwa shukrani, Paulo anaweza kushangilia katika mifano ya uaminifu. Anakumbuka Onesiforo, mfano wa huduma ya uaminifu sehemu zote mbili ndani ya Efeso na ndani ya Rumi (2 Timotheo 1:16-18). Pia anawataja watenda kazi wenzake kama vile Kreske, Tito, na Tikiko , ambao wanatumika kwa uaminifu (2 Timotheo 4:10-12). Katika uongozi mzuri na wa ajabu wa Neema ya Mungu, Paulo anaomba kwamba Marko amsaidie Timotheo huko Rumi. Miaka kumi na tano mwanzoni, Marko alijiondoa kutoka kwenye timu ya umisheni iliyofanya kazi kwenye safari ya kwanza ya kimishenari ya Paulo. Kutokana na hili, yeye alikuwa ni sababu ya kutengana kati ya Paulo na Barnaba (Matendo ya Mitume 15:36-39). Marko ambaye alikuwa si wakuaminika kwenye siku za nyuma, lakini sasa amethibitisha kuwa mwaminifu. Paulo anaelekeza, "Umtwae Marko, umlete pamoja nawe, maana anifaa kwa utumishi" (2 Timotheo 4:11).

Hizi ni zaidi ya kumbukumbu binafsi za nyuma; Paulo anataka kuchochea uaminifu ndani ya Timotheo. Kupitia maneno ya mifano, Paulo anaonyesha inamaana gani kuwa mwaminifu:

- Askari ni mwaminifu kwa yule ambaye amemteua (2 Timotheo 2:3-4).
- Mwanariadha anashindana kwa kuzingatia sheria (2 Timotheo 2:5).
- Mkulima hufanya kazi kwa kutegemea ujira wa mavuno (2 Timotheo 2:6).

### *Walimu wa uongo*

Tishio la fundisho la uongo linaendelea kuwa jambo la kuzingatia kwa Paulo. Anampa changamoto Timotheo kubaki kuwa mwaminifu na kukataa kuyumbishwa na mambo ya kijinga na kipumbavu (2 Timotheo 2:23). Huku kuyumbishwa kunatoka kwa watu waovu na wadanganyifu ambao wanadanganya na kudanganyika. (2 Timotheo 3:13). Paulo anamwambia Timotheo, "Bali wewe ukae katika mambo yale uliyofundishwa na kuhakikishwa…" (2 Timotheo 3:14). Timotheo ufanye yafuatayo:

- Hubiri neno.
- Kalipia, kemea, na himiza.
- Kuwa na akili timamu.
- Vumilia mateso.
- Fanya kazi ya muhubiri wa Injli.

Kwa kifupi, anapaswa kutimiza huduma yake (2 Timotheo 4:2, 5). Hapa, kama ilivyo kwenye 1 Timotheo na Tito, jibu kwa mafundisho ya uongo ni uaminifu kwa Kweli.

### *Kuaga*

2 Timotheo ni neno la kuaga la Paulo mwishoni mwa maisha yake hapa duniani na huduma yake. Paulo anautazama wakati ujao kwa ujasiri; anatazamia thawabu ya uaminifu.

Miaka ya kabla, Paulo alishuhudia, "Lakini siyahesabu maisha yangu kuwa kitu cha thamani kwangu kama kuumaliza mwendo wangu na huduma ile niliyopokea kwa Bwana Yesu, kuishuhudia Habari Njema ya neema ya Mungu" (Matendo ya Mitume 20:24). Sasa, kukabili kifo, anashuhudia:

> Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, Imani nimeilinda; baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana, mhukumu mwenye haki, atanipa siku ile; wala si mimi tu, bali na watu wote pia waliopenda kufunuliwa kwake (2 Timotheo 4:7-8).

## Nyaraka za kichungaji Katika Kanisa Leo

Nyaraka za kichungaji zinatufundisha sisi:

1. **Umuhimu wa fundisho la kweli**. Jibu sahihi kwa fundisho la uongo ni Ukweli. Katika barua hizi, Paulo anatoa angalizo kwa fundisho la kweli zaidi kuliko kwa fundisho la uongo. Hivyo hivyo, jibu letu sahihi kwa mafundisho ya uongo leo ni Injili, ambayo mara moja kwa zote ilitolewa kwa watakatifu (Yuda 1:3).

2. **Sifa kwa viongozi wa Kanisa**. Katika nyakati ambazo maadili yameharibika na mafundisho ya uzushi yameharibu baadhi ya viongozi wa kanisa, Nyaraka za Kichungaji ni za thamani kwa kufundishia vigezo vya Mungu kwa viongozi wa Kanisa. Hakuna kanisa lnaloweza kuacha kuzingata viwango hivi. Makanisa yenye hekima yatachagua ambao wamejidhatiti kwenye sifa ambazo Paulo amezibainisha kwenye 1 Timotheo na Tito.

3. **Umuhimu wa kazi nzuri kama kielelzo cha Injili**. Tito hususani inasisitiza ujumbe huu. Wakati ambapo wale wanaodai kumfuata Yesu wanaongea na kutenda katika njia ambazo ni tofauti na zake, ushuhuda wa kanisa unaharibika. Waamini lazima waifanye Injili ivutie wale wasioamini kupitia maisha ya kimungu. Fundisho sahihi ni lazima lizalishe na tabia sahihi.

4. **Wito wetu wa uaminifu kwa maisha yote**. Wanafunzi, kadri unavyoendelea katika huduma, unakutana na changamoto ya kimaisha. Kama Paulo, unaweza kutengwa na watenda kazi wenzako. Kama Timotheo na Tito, unaweza kukutana na walimu wa uongo. Na kama waamini wa nyakati zote, utakutana na majaribu na kupingwa. Maneno ya mwisho ya Paulo yanakukumbusha: Tuzo ya thamani ni ya gharama. Usikate tamaa; Taji inakusubiria.

## Hitimisho

William Borden alizaliwa kwenye familia ya Kitajili mwaka 1887. Borden alijiunga na Chuo Kikuu cha Yale kujiandaa na mambo ya biashara, lakini Mungu alimwita kuwa mmishionari kwa waislamu wa Kaskazini mwa China. Akiwa njiani kwenda China, huku akijifunza kiarabu nchini Misri, Borden akapata ugonjwa wa homa ya uti wa mgongo na akafariki akiwa na umri wa miaka 25. Hakuiona china.

Baada ya kifo chake, wazazi wake walipewa Biblia ya William. Ndani ya Biblia, walikuta ujumbe kutoka siku ambayo alisema ndiyo kwa wito wa Mungu kumtaka aende China. Borden aliandika maneno, "Hakuna kujibakiza." Alijitoa yeye mwenyewe kikamilifu (pasipo kujibakiza) kwa wito wa Mungu. Wakati familia yake ilipopinga wito wake na kumlazimisha William kujiunga na biashara ya familia, aliandika, "Hakuna kurudi nyuma." Borden alijithatiti kuendelea kupiga mbio pasipo kurudi nyuma. Siku chache tu kabla ya kifo chake, Borden aliongeza ujumbe mwingine: "Hakuna majuto." Borden angeweza kuitazama mbele yake kwa ujasiri kwamba ameishi katika kutii wito wa Mungu.

William Borden aliulewa ushuhuda wa mwisho wa Paulo. Kwa kila mtu anayejitoa pasipo kujibakiza na kumfuata Mungu pasipo kurudi nyuma, kuna taji ya haki. Siku ile, tutasema na Paulo na William Borden, "Sina majuto." Hili ni lengo linalostahili kwa kila Mwamini.

**Somo la 9 Mazoezi**

(1) Fanya mazoezi yote yanayofuata:

- Andaa orodha ya sifa kwa ajili ya viongozi wa kanisa katika mazingira yako. Unatakiwa kutumia viwango vya Biblia vya 1 Timotheo na Tito katika mazingira ya utamaduni ambao unatumika.

- Baada ya kusoma 2 Timotheo, andika barua ya kuagana ya ukurasa mmoja. Kana ungekuwa unakabiliwa na kifo, ni ushuhuda gani ungeuacha nyuma? Zoezi hili linaweza kukusaidia kufanyia tathmini maisha yako ya sasa na kutengeneza huduma yako ya mbele kwa kadiri unavyokuwa na ufahamu wa urithi ambao utauacha kwa wale ambao wanakufuata.

(2) Mwanzoni mwa somo linalofuata, utafanya jaribio kulingana na somo hili. Soma maswali ya jaribio kwa umakini katika maandalizi.

**Somo la 9 Jaribio**

(1) Nyaraka za Kichungaji zinaaminika ziliandikwa katika kipindi gani cha tahehe?

(2) Ni nini yalikuwa makusudi mawili ya Paulo ili kuandika 1 Timotheo?

(3) Ni kwa jinsi gani ushuhuda wa Paulo unamtia moyo Timotheo wakati anapopambana na waalimu wa uongo?

(4) Ni nini maashofu wanafanya? Wajibu wao ulikuwa ni nini?

(5) Mashemasi walikuwa wana wajibika na nini? Neno la Kiyunani *diakonos* lina maana gani?

(6) Tito alikuwa nani?

(7) Ni kwa kusudi gani kwamba waraka kwaTito uliandikwa?

(8) Ni misukumo gani miwili kwa ajili ya kazi njema ambayo Paulo anampatia Tito?

(9) Kwa nini ni muhimu kwamba Paulo anataka Marko kuja kwake (2 Timotheo 4:11)?

(10) Ni mambo gani manne ambayo Nyaraka za Kichungaji zinamfundisha mwamini leo?

(11) Andika 2 Timotheo 4:7-8 na Tito 2:11-14 kutoka katika kumbukumbu.

# Somo la 10
# Waebrania na Yakobo
# Nyaraka za Watu Wote, Sehemu ya 1

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kufahamu tarehe zinazokadiriwa na mazingira ya kihistoria ya Waebrania na Yakobo.

(2) Kuorodhesha mada kuu na kusudi la Waebrania na Yakobo.

(3) kutambua upendeleo na majukumu yetu chini ya Agano Jipya.

(4) Kutii maonyo ya Kibiblia dhidi ya uasi.

(5) Kuelewa uhusiano kati ya imani na kazi katika maisha ya Mkristo.

(6) Kutekeleza kanuni kwa vitendo kwa Mkristo kuishi kutokana na Waebrania na Yakobo.

(7) Kuhusianisha ujumbe wa vitabu hivi na mahitaji ya ulimwengu wa leo.

## Maandalizi kwa ajili ya somo hili

► Soma Waebrania na Yakobo.

► Kariri Waebrania 4:14-16 na Yakobo 2:17-18.

## Utangulizi

Vitabu nane vya Agano Jipya vinaitwa Nyaraka za Watu Wote:[60] waraka kwa Waebrania na nyaraka zilizoandikwa na Yakobo, Petro, Yohana, na Yuda. Zinaitwa Nyaraka za Watu Wote kwa sababu hazina hadhira maalum au ziliandikwa kwa watua ambao tunawafahamu kidogo.

Nyaraka hizi zinatofautiana kutoka waraka mrefu kwa Waebrania kwenda waraka mfupi kutoka kwa Mtume Yohana kwa Gayo. Nyaraka za Watu Wote zinashughulika changamoto mbalimbali, lakini maisha ya Mkristo kwa vitendo ni msisitizo unaojirudia kwenye vitabu vyote. Vitabu hivi vinatufundisha jinsi ya kuishi kama wafuasi wa Kristo katika ulimwengu wa wasio Wakristo. Waamini wa karne ya kwanza walipata changamoto zinazofanana na changamoto tunazopata sasa: mafundisho ya potofu, majaribu, upinzani kutoka kwa wasioamini. Kila tatizo kati ya haya limepewa majibu katika nyaraka hizi. ingawa nyaraka nyingi ni ndogo kwa ukubwa, zote ni za muhimu kwa waamini ambao wanapata changamoto katika imani zao.

---

[60] Katika muktadha huu, *catholic* ni neno lingine kwa ajili ya "jumla"; halirejeleai kanisa la Roman Katholoki. Haya ni matumizi sawasawa na yale yaliyopo katika tamko la Imani ya Mitume: "Ninaamini katika… kanisa takatifu lililo moja, ushirika wa watakatifu…."

## Waebrania

### Historia ya Waebrania

#### *Mwandishi*

Kitabu cha Waebrania hakioneshi mwandishi wake. Mara nyingi Paulo anadhaniwa kuwa ni mwandishi.

Hoja zinazounga mkono uandishi wa Paulo:

1. Waebrania inamsisitiza utu na kazi ya Kristo.
2. Mwandishi anahusiana na Timotheo (Waebrania 13:23).
3. Maombi ya baraka katika sura ya mwisho ni sawa na ya maombi mengine ya baraka ya Paulo (Waebrania 13:18-25).

Hoja dhidi ya uandishi wa Paulo zinajumuisha tofauti mbalimbali katika mtindo kati ya Waebrania na nyaraka zinazojulikana kutoka kwake:

1. Waebrania haitumii kamwe neno "Kristo Yesu." Neno hili limetumika zaidi ya mara 50 katika nyaraka za Paulo.

2. Mwandishi anasema kuwa aliisikia injili kutoka kwa mitume (Waebrania 2:3). Katika Wagalatia 1:12, 15-19 na Wagalatia 2:6, Paulo anasisitiza kuwa alisikia injili moja kwa moja kutoka katika ufunuo wa Yesu Kristo na kwamba hakupata ujumbe wake wowote kutoka kwa mitume wengine.

3. Waebrania haianzi wala kuisha na salamu binafsi zinazopatikana mara nyingi katika barua za Paulo.

Katika historia yote ya kanisa, idadi ya waandishi wengine imependekezwa. Waandishi wengi waliopendekezwa ni washirika wa Paulo, kama vile Barnaba, Luka, au Apolo. Hii inaweza kutoa sababu za kufanana na mtindo wa Paulo. Kimsingi, mwandishi hajulikani.

#### *Kusudi*

Kitabu cha Waebrania kinajumuisha vipengele vya (salamu binafsi mwishoni) na sifa za mahubiri (ufafanuzi wa maandiko ya Agano la Kale). Mwandishi anarejelea waraka wake kama "neno...lenye maonyo" (Waebrania 13:22), kwa kutumia neno lilelile la Kiyunani lililotumika katika Matendo ya Mitume 13:15 kufafanua mahubiri. Waebrania ni mahubiri kutoka kwenye waraka.

Wapokeaji wa kwanza wa waraka huu ni wafuasi wa Kristo wa Kiyahudi ambao wanajaribiwa kugeuka kutoka kwenye imani katika Kristo kurudi katika matendo yao ya kale. Historia yao ya Kiyahudi inaonekana katika uelewa wao kwenye sadaka na desturi za Agano la Kale.

Waamini hawa wamestahimili mateso kwa uaminifu lakini wako kwenye hatari ya kuchoka na kuzimia (Waebrania 10:32-34, Waebrania 12:3). Mwandishi wa Waebrania anaandika

kuwaonya dhidi ya uasi na anawatia moyo waendelee kuwa waaminifu. Anaeleza kuwa Yesu ni ukamilisho ya Agano la Kale. Kwa hiyo, kama wakimkana Yesu na kurudi kwenye imani zao za kale, wanaikana pia imani yao ya kale. Endapo badala yake wataendelea katika imani, watautunza urithi wa Agano la kale na mashujaa wake.

### *Tarehe*

Waraka kwa Waebrania huenda uliandikwa kabla ya mwaka 70 B.K. Waraka unazungumzia mfumo wa utoaji wa sadaka wa Kiyahudi kama ukweli uliopo.[61] Hii inamaanisha kwamba waraka uliandikwa kabla ya kuharibiwa kwa Hekalu na Warumi katika mwaka 70 B.K.

### Agano la Kale katika Waebrania

►Ni nini uhusiano kati ya Agano la Kale na Agano Jipya?

Kabla ya kuangalia yaliyomo katika Waebrania, ni muhimu kujibu dhana potofu kuhusu kitabu. Wasomaji wengi wametafsiri Waebrania kama shambulio la Agano la kale. Kwa sababu Waebrania inafundisha kwamba Agano Jipya ni agano bora, baadhi wandhani kuwa Agano la kale halikutimiza lengo lake.

Hata hivyo, Waebrania inaonesha heshima kubwa kwa Agano la Kale.

- Mashujaa katika Waebrania 11 ni watu kutoka katika Agano la Kale.
- Masomo yanayofundishwa katika Waebrania yana msingi wa maandiko kutoka kwenye Agano la Kale.[62] Kwa mfano, Waebrania 1 ina mistari 14. Kati ya hiyo, mistari 9 ni nukuu za moja kwa moja kutoka kwenye Agano la Kale.[63]

Waebrania haifundishi kuwa Mungu alilazimika kubadili mpango wake kutokana na kushindwa kwa Agano la Kale. Badala yake, wokovu kwa njia ya imani katika Kristo ulipangwa kabla ya misingi ya ulimwengu (1 Petro 1:20). Hata kwenye Agano la Kale, wokovu ulitolewa kwa neema ya Mungu kwa njia ya imani, siyo kwa desturi za nje. Hii inaonekana katika Waebrania 11, ambayo inasema kwamba kila shujaa aliyetajwa wa Agano la Kale alimpendeza Mungu "Kwa imani."

Kuna mwendelezo wa wazi kati ya Agano la Kale na Agano Jipya. Kristo ndiye ukamilisho wa ahadi na sheria za Agano la Kale. Tatizo katika Agano la Kale lilikuwa ni kushindwa kwa Israeli, siyo kushindwa kwa ahadi za Mungu. Israeli ilishindwa kulielewa kwa undani agano (Waebrania 8:8-12). Israeli iligeuza mfumo wa utoaji uliokuwa na msingi wa imani kuwa desturi zisizo na imani. Manabii wote wa Agano la Kale na Yesu waliihukumu Israeli kwa kuharibu kusudi la Mungu.

---

[61] Waebrania 8:3-5, Waebrania 9:7-8, Waebrania 10:1-3

[62] Utanufaika kutokana ma kusoma Waebrania katika kujifunza Biblia ambapo inaonesha mistari ya Agano la Kale ambayo imenukuliwa katikaWaebrania.

[63] Vifungu vya Agano la Kale vilivyonukuliwa katika Waebrania 1 vinajumuisha: Zaburi 2; 2 Samweli 7:14; Kumbukumbu la Torati 32:43; Zaburi 104:4; Zaburi 45:6, 7; Isaya 61:1, 3; Zaburi 102:25-27; na Zaburi110:1.

Tangu misingi ya ulimwengu, Agano la Kale lilionesha ujio wa Kristo . Agano la Kale kamwe halikukusudiwa kujikamilisha lenyewe; lilionesha ukamilisho wa baadaye. Agano la Kale linakamilishwa maisha na kazi ya Yesu Kristo. Agano jipya ni bora zaidi kwa sababu linakamilisha ahadi ya Agano la Kale lisilo kamilifu.

**Mada Kuu na Yaliyomo katika Waebrania**

Kitabu cha Waebrania kinaonesha mada mbili sambamba. Mada moja (Namna bora zaidi) inatofautisha fursa ya maisha katika Kristo na fursa ndogo inayopatikana chini ya Agano la Kale.

Mada ya pili (Jihadhari) inaonekana katika mfululizo wa maonyo matano kwa wale wanaojaribiwa kuiacha imani na kurudi katika maisha yao ya kale, katika kila sehemu ya maonyo Waebrania inatoa maonyo na kisha inatoa faraja kwa msomaji.

***Namna bora zaidi***

Katika mfululizo wa kulinganisha, Waebrania inaonesha kwamba:

- Kristo yuko juu kuliko manabii wa Agano la Kale (Waebrania 1:1-3).
- Kristo yuko juu kuliko malaika kwa sababu Yeye ni mwana wa Mungu (Waebrania 1:4-14).
- Kristo yuko juu kuliko malaika kwa sababu yeye ni mwana wa Adamu, ambaye ulimwengu ulifanywa kuwa chini yake (Waebrania 2:5-9).
- Kristo ni mkuu kuliko Musa, mtumishi mwaminifu wa Mungu na kiongozi wa Israeli (Waebrania 3:1-6).
- Kristo ni mkuu kuliko Haruni na ukuhani mkuu (Waebrania 4:14-7:28).
- Kristo ametoa agano bora (Waebrania 8:1-13).
- Kristo ametoa sadaka bora (Waebrania 9).

Waebrania inaonesha pia mfuatano wa tofauti kati ya ahadi **nzuri** za agano la kale na uakamilisho **bora** ambao ni wetu kupitia Kristo. Kwa wafuasi wa Yesu wa Kiyahudi kurudi kwenye Agano la Kale ungekuwa ni upumbavu! Wamekionja kipawa cha mbinguni na wameshiriki katika Roho Mtakatifu. Kurudi kwenye hali zao za kale ingekuwa kumsulubisha tena Mwana wa Mungu (Waebrania 6:4-6)!

***Jihadhari***

►Uasi ni nini? Je, inawezekana kwa mtu aliyebadilishwa kweli kuiacha imani?

Pamoja na ushuhuda wa njia iliyo bora zaidi uliotolewa na Kristo, Waebrania inatoa maonyo kwa wale ambao wanajaribiwa kuiacha imani. Kadiri neema inavyoongezeka ndivyo wajibu unavyoongezeka. Kwa kuzingatia wajibu huu, Waebrania anatoa maonyo makali matano

kwa waamini ambao wameonja mambo mema ya Agano Jipya na wanajaribiwa kurudi kwenye mambo ya kale.

Kila onyo linaambatana na kuhimizwa kubaki mwaminifu. Wakati Waebrania inafundisha kuwa uasi unawezekana, mpango wa Mungu kwa kila mwamini ni maisha ya uaminifu. Waebrania inaonesha kuwa maisha ya ushindi yanapatikana kwa kila mfuasi wa Kristo.

*Onyo la 1 – Waebrania 2:1-18*[64]

- **Onyo:** Hatupaswi kuuacha ujumbe tuliousikia (Waebrania 2:1).
- **Sababu ya onyo ni dhahiri:** Kama watu wa Mungu katika nyakati za Agano la Kale walipokea adhabu ya haki kwa kutokutii kwao, tutaponaje kama tukiukataa ujumbe ambao tumeupokea kupitia Kristo na mitume? (Waebrania 2:2-3).
- **Himizo:** Yesu mwenyewe alipata majaribu, na sasa anatusaidia tunapojaribiwa (Waebrania 2:18).

*Onyo la 2 – Waebrania 3:12-4:16*

- **Onyo :** Hatupaswi kuiacha imani na mioyo yetu kufanywa migumu kwa udanganyifu wa dhambi (Waebrania 3:12-13).
- **Sababu ya onyo ni dhahiri:** Inawezekana kujitenga na Mungu aliye hai. Tunashiriki katika Kristo kama tukishikamana na mwanzo wa uthabiti wetu kwa nguvu mpaka mwisho (Waebrania 3:12-14).
- **Himizo:** Yesu ni kuhani wetu mkuu. Anatoa rehema na neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji (Waebrania 4:14-16).

*Onyo la 3 – Waebrania 5:11-6:12*

- **Onyo:** Hatupaswi kumwacha Kristo baada ya kuonja uzuri wa neno (Waebrania 5:11-6:6).
- **Sababu ya onyo ni dhahiri:** Watu binafsi ambao wanafanya uasi (wanageuka kwa hiari kutoka kwenye imani ya Kikristo) wanajitoa wenyewe kutoka kwenye wokovu. Hii ni kwa sababu wanaendelea kumsulubisha Mwana wa Mungu na kumdhihaki (Waebrania 6:4-6).
- **Himizo:** Tuna mfano wa watu wa kuigwa ambao wametunza na kurithi ahadi (Waebrania 6:9-12).

[64] Maonyo haya yametolewa kutoka Walter Elwell and Robert Yarbrough, *Encountering the New Testament*, (Ada: Baker Academic, 2005).

*Onyo la 4 – Waebrania 10:26-39*

- **Warning Onyo:** Hatupaswi kuendelea kutenda dhambi kwa makusudi baada ya kupokea maarifa ya ukweli (Waebrania 10:26-27).
- **Sababu ya onyo ni dhahiri**: Iwapo wale walioipuuza sheria ya Musa walihukumiwa kwa ukali, tunastahili adhabu gani kali zaidi iwapo tumemkanyaga Mwana wa Mungu? "Ni jambo la kutisha kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai" (Waebrania 10:28-31).
- **Himizo**: Wapokeaji wa Waebrania tayari waneshakuwa waaminifu wakati wa mateso. Hivyo, tuna ujasiri katika nguvu za Mungu kumshikilia mwamini imara (Waebrania 10:32-39). Waebrania 11 inatoa orodha ya wanaume na wanawake ambao walibaki kuwa waaminifu kwa Mungu.

*Onyo la 5 – Waebrania 12:25-29*

- **Onyo:** Tusimkatae Yeye ananenaye (Waebrania 12:25).
- **Sababu ya onyo ni dhahiri:** Iwapo Mungu aliwaadhibu ambao walimkataa chini ya Agano la Kale, atawaadhibu kwa namna gani wale wanakataa neema ya Agano Jipya. "…Mungu wetu ni moto ulao" (Waebrania 12:25-29).
- **Himizo:** Mungu ametupa ufalme ambao hauwezi kutetemeshwa. Kwa sababu ya utoaji wake, tunaweza kumfanyia ibada ya kumpendeza kwa unyenyekevu na kicho (Waebrania 12:28-29).

## Kuangalia kwa ukaribu Uasi

### Uasi ni nini?

Uasi unafafanuliwa kama "kukataa kwa makusudi na kuiacha imani ambayo mtu ameikiri."[65] Tafsiri hii inasisitiza vipengele vitatu vya uasi:

1. **Ni kwa makusudi**. Mashaka kuhusu mafundisho, kutokuwa na uhakika juu ya wokovu, au hata kuanguka kwenye dhambi hakumaanishi uasi. Uasi ni kukataa kwa makusudi imani ya Kikristo.
2. **Kukataa na kuasi katika imani***.* Ni zaidi ya dhambi; ni kuukataa ukweli wa imani ya Kikristo. Kwa Waebrania, uasi ungekuwa kukataa kazi ya upatanisho ya Yesu na kurejea kwa mila za kabla ya Ukristo. Judaizers (wafuasi wa dini ya kiyahudi) **waliongeza** vigezo kwenye kazi ya upatanisho ya Kristo**;** waasi **walikataa** kabisa kazi ya upatanisho ya Kristo.

[65] L.G. Whitlock, "Apostasy" in *Evangelical Dictionary of Theology*, Edited by Walter Elwell. (Ada: Baker Books, 1984).

3. **Ni kuikataa imani ambayo mtu ameikiri**. Uasi ni tofauti na kutokuamini kwa mtu ambaye hajawahi kumjua Kristo. Ni kuikataa imani kwa mtu ambaye ameonja neno zuri la Mungu na nguvu za zamani zijazo (Waebrania 6:5).

### Ni nini tofauti kati ya Uasi na Kurudi nyuma?

Uasi katika Waebrania ni wa kudumu zaidi na kukataa kwa hiari imani kuliko kurudi nyuma. Petro alimkataa Yesu lakini baadaye aliitubia dhambi yake. Ujasiri wa Petro ulipotea; hakuitakaa imani ya Ukristo. Kurudi kwake nyuma yalikuwa ni matokeo ya hofu, siyo kumkataa Kristo.

Aliyerudi nyuma ameanguka katika dhambi lakini bado anaukubali ukweli wa imani ya Kikristo. Kinyume chake, aliyeasi anaukataa ukweli wa imani ya Kikristo.

Baadhi ya maonyo katika Waebrania yanahusiana na kurudi nyuma na kutojali. Hata hivyo, kukataa kabisa imani ya Kikristo linaonekana kuwa wazo lilioko nyuma yake Waebrania 6:4-6. Wakati muasi anapokataa kifo kinachookoa cha Yesu, anaikataa njia ya urejesho. Mtu aliyerudi nyuma, na kutubu, hata hivyo, anaweza kurejeshwa kupitia kifo cha upatanisho cha Yesu.

### Je inawezakana Mwamini wa Kweli kufanya Uasi?

Baadhi ya wainjilisti wanadai kuwa haiwezekani kwa Mkristo wa kweli kufanya uasi. Hata hivyo, maonyo ya Waebrania yanaleta maana iwapo tu mwandishi anakabiliana na hatari halisi. Waebrania 6:4-6 inaonesha waziwazi kwamba uasi kamili na wa kudumu unawezekana.

## Waebrania (Muendelezo)

### Waebrania katika kanisa leo

Nyaraka za watu wote zinajadili matishio kwa kanisa, mara nyingi onyo dhidi ya mafundisho potofu ambayo yanaharibu mafundisho ya Kikristo. Kitabu cha Waebrania kinaonya dhidi ya hatari halisi ya uasi—kuacha kabisa imani ya Kikristo. Hatari hii ni halisi leo kama ilivyokuwa katika karne ya kwanza.

Ndio, Waebrania inafundisha kuwa inawezekana kuacha imani. Lakini kilicho muhimu sana, Waebrania inafundisha uwezekano wa kubaki mwaminifu. Tuna faida ya kuombewa na Kristo kwa niaba yetu. Kwa kushikilia sana ungamo la tumaini letu, kwa kuhimizana katika upendo na kazi nzuri, na kwa kuhimizana katika kukusanyika pamoja kwa ajili ya ibada, tunaweza kubaki waaminifu (Waebrania 10:23-25). Waebrania 11 ni kilele cha kitabu, pamoja na ushuhuda wake wa wale ambao walikuwa waaminifu na ambao sasa wanatoa wingu la mashahidi kwa wote wanaokimbia kwa uvumilivu mbio zilizowekwa mbele yetu (Waebrania 12:1).

## Yakobo

### Historia yaYakobo

#### *Mwandishi na Tarehe*

Mwandishi wa waraka huu alikuwa Yakobo, mtumishi wa Mungu na wa Yesu Kristo (Yakobo 1:1). Yakobo, ndugu wa kufikia wa Yesu (Mathayo 13:55), hakuwa akimwamini Yesu kipindi cha maisha yake (Yohana 7:3-5). Alimwamini Yesu kama Masihi baada ya ufufuo (1 Wakorintho 15:7). Yakobo alikufa kama shahidi wa imani mwaka 62 B.K.

Huenda waraka huu uliandikwa mwanzoni hadi katikati ya miaka ya 40. Kwa kuwa Yakobo alikuwa kiongozi katika Baraza la Yerusalemu, ambalo lilijadili masuala ya imani na kazi, ni kama Yakobo angelitaja Baraza kama waraka ungeandikwa baada ya mwaka 49 B.K (Matendo ya Mitume 15).

#### *Wapokeaji na Kusudi*

Yakobo anayaandikia makabila kumi na mbili "waliotawanyika" (Yakobo 1:1). *Diaspora*, neno la Kigiriki lililo nyuma ya usemi huo, kimsingi linarejelea kutawanyika kwa Wayahudi kufuatia kuanguka kwa Yerusalemu mwaka 586 K.K. Sasa, Yakobo anawarejelea waamini wa Kiyahudi walioteswa ambao wanaishi nje ya Uyahudi. Marejeleo ya mara kwa mara ya Yakobo kwenye Agano la Kale yanaonesha pia anawaandikia waamini wa Kiyahudi. Ni dhahiri kwamba wanapitia aina mbalimbali za majaribu. Yakobo anawakumbusha waamini kuwa imani yao lazima ionekane katika matendo yao (namna wanavyoishi). Waamini lazima waweke imani yao katika matendo.

### Yakobo na Agano la Kale

Kama nabii Amosi, Yakobo anaonesha kuwa ukiri wetu wa imani lazima uathiri maisha yetu ya kila siku. Wote Amosi na Yakobo wanasisitiza kuwa dini ya kweli iitaonekana katika namna tunavyowatendea wengine. Katika mistari 108, Yakobo anatoa zaidi ya amri 50. Huu ni waraka wa vitendo.

► Soma Yakobo 5:1-5 pamoja na Amosi 4:1-2 Amosi 5:21-24. Ujumbe huu unalinganishwaje?

Kama Mithali, Yakobo anatumia misemo mifupi ambayo inafupisha kweli muhimu. Mada nyingi katika Yakobo zinafanana katika kitabu cha Mithali: kuuchunga ulimi, utajiri, hasira, na hekima.

Kama sheria ya Agano la Kale*,* Yakobo inaonesha namna ambavyo mtakatifu anaakisi tabia ya Mungu Mtakatifu. Kanuni ya utakatifu katika Mambo ya Walawi 19 inaonesha namna ambavyo watakatifu wataishi katika utii kwa Mungu Mtakatifu. Vilevile, Yakobo anaonesha namna ambavyo waamini wa Agano Jipya wanapaswa kuishi kwa kumtii Mungu. Wote wanaonesha kuwa imani tunayoikiri lazima ionekane katika maisha tunayoyaishi.

| Kanuni ya Utakatifu na Yakobo | |
|---|---|
| **Mambo ya Walawi** | **Yakobo** |
| **Mambo ya Walawi 19:13** "…ijara yake aliyeajiriwa isikae kwako usiku kucha hata asubuhi." | **Yakobo 5:4** "Angalieni, ujira wa wakulima waliovuna mashamba yenu, ninyi mliouzuia kwa hila, unapiga kelele, na vilio vyao waliovuna vimeingia masikioni mwa Bwana wa majeshi." |
| **Mambo ya Walawi 19:15** "…usimpendelee mtu maskini, wala kumstahi mwenye nguvu…" | **Yakobo 2:9** "Bali mkiwapendelea watu, mwafanya dhambi na kuhukumiwa na sheria kuwa wakosaji." |
| **Mambo ya Walawi 19:18** "Usifanye kisasi, wala kuwa na kinyongo juu ya wana wa watu wako…" | **Yakobo 5:9** "Ndugu, msinung'unikiane…" |
| **Mambo ya Walawi 19:18** "…bali umpende jirani yako kama nafsi yako…" | **Yakobo 2:8** "Mpende jirani yako kama nafsi yako." |

### Mada Kuu katika Yakobo

#### *Imani na Matendo*

Martin Luther alimwita Yakobo "waraka wa majani" kwa sababu ya msisitizo kuhusu matendo. Aliamini kuwa waraka ulipingana na mafundisho juu ya kuhesabiwa haki kwa njia ya imani peke yake. Kwa mtazamo wa juu juu, inaonekana kuwa na mgogoro katikati Yakobo 2:24 ("…mwanadamu huhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo yake; si kwa imani peke yake") na Warumi 3:28 ("Basi, twaona ya kuwa mwanadamu huhesabiwa haki kwa imani pasipo matendo ya sheria").Hata hivyo, sentensi hizi zinaelekezwa katika walengwa wawili tofauti, inayopitia majaribu tofauti. Tunapoelewa muktadha wa kila mstari, mgongano dhahiri kati ya mistari unatatuliwa.

Paulo anawaeleza watu ambao wanajaribu kupata wokovu kupitia matendo (utii wa sheria). Paulo anasema **tunahesabiwa haki**—**tunafanywa wenye haki mbele za Mungu**—kwa neema ya Mungu, ambayo inapokelewa kwa imani (Warumi 3:24, 28).

Yakobo anawaeleza watu ambao wanaiangalia imani kama si kitu zaidi ya imani ya kufikirika (Yakobo 2:14-26). Yakobo anasisitiza kuwa imani ya kweli ni inayobadilisha maisha. Yakobo anasema **tunahesabiwa haki—inaoneshwa kuwa waamini**— kwa matendo yetu. Ujumbe wa Yakobo hauchanganyani na ujumbe wa Paulo. Yakobo hafundishi namna tunavyookolewa; anafundisha namna ambavyo maisha yetu yataonesha kuwa tumeokolewa.

### *Imani katika Matendo*

> "Tatizo la matatizo ni kuuweka Ukristo katika matendo."
>
> - Maneno haya huhusishwa na John Wesley

Imani inaonekana katika matendo. Yakobo anaonesha namna ambavyo imani itaathiri tabia ya mwamini katika maeneo mbalimbali ya maisha. Yakobo anawafundisha waamini kuhusu:

- Uthabiti kwenye majaribu na mateso (Yakobo 1:2-18).
- Kusikia na kutenda Neno (Yakobo 1:19-27).
- Kutokuwa na upendeleo (Yakobo 2:1-13).
- Kuuchunga ulimi (Yakobo 3:1-13).
- Kutokuwa rafiki na ulimwengu (Yakobo 3:14-4:4).
- Kutokujivuna (Yakobo 4:5-11).
- Majaribu katika mali (Udhalimu) (Yakobo 4:13-5:6).
- Uvumilivu katika mateso (Yakobo 5:7-11).
- Majaribu kwa wenye mafanikio (Yakobo 5:19-20).

Katika maonyo yake, Yakobo anaonesha kuwa imani ya kweli itabadilisha namna tunavyoishi. Imani ni zaidi ya kukubaliana na ukweli; imani hutubadilisha katika ukamilifu wetu.

### Yakobo katika Kanisa la leo

Ingawa waraka wa Yakobo ulielekezwa kwa Wayahudi Wakristo walioteswa katika karne ya kwanza, msisitizo wake katika Ukristo wa matendo unazungumza kwa undani sana kwa ulimwengu wa sasa. Mafundisho ya kivitendo kuhusu kuuchunga ulimi, mali, hasira, na uhusiano ndani ya kanisa ni endelevu. Yakobo ni kitabu kinachotumika katika kila kizazi.

*Antinomianism* ni mafundisho potofu ambayo waamini wako huru kufuata tamaa za mwili kwa sababu zinahalalishwa kwa imani, na siyo kwa utii kwa sheria. Fundisho linapendekeza kuwa waamini ambao wamehesabiwa haki kwa neema wako huru mbali na vizuizi vyote . Katika kila kizazi, kanisa linajaribiwa na mvutano wa upinzani wa sheria za dini. Yakobo anasimama kama ukumbusho wenye nguvu kuwa maisha ya mwamini yatatambulika tofauti na maisha ya asiyeamini. Kupitia matendo yetu, ulimwengu huona mabadiliko yanayotokana na imani ya wokovu ndani ya Kristo.

## Hitimisho

Wote Waebrania na waraka wa Yakobo zinamrejelea Ibrahimu kama mfano wa imani katika matendo. Waebrania 11 inamtaja Ibrahimu kama mmojawapo wa mashujaa wa imani; Yakobo 2 inaonesha kuwa ni kupitia matendo yake kwamba tunaiona imani ya Ibrahimu.

Imani ya Ibrahamu inaonekana kwenye utii wake kwa wito wa Mungu:

> Kwa imani Ibrahimu alipoitwa aliitika, atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa urithi; akatoka asijue aendako (Waebrania 11:8).

Imani ni zaidi ya kusema “Naziamini ahadi za Mungu.” Imani husema nitakwenda pale utakaponiongoza.”

Imani ya Ibrahimu inaonekana tena katika utii wake kwa amri ya Mungu ya kumtoa Isaka kama sadaka (Waebrania 11:17-19, Mwanzo 22). Tena, imani ilikuwa zaidi ya kusema “Ninamwamini Mungu.” Imani ilisema “Nitaitii amri yako, hata kama sielewi.” Hii ni imani ya kweli.

Yakobo aliwaonya wasomaji kutokudai imani ikiwa maisha yao hayakubadilishwa na imani hii. Yakobo alimtaja Ibrahimu kama mfano wa kile kinachotokea kama matokeo ya imani ya kweli. Imani ya Ibrahimu ilionekana katika utii wake wa amri ya Mungu ya kumtoa Isaka kwenye madhabahu. Yakobo anahitimisha, “Waona kwamba imani ilitenda kazi pamoja na matendo yake, na ya kwamba imani ile ilikamilishwa kwa njia ya matendo yale” (Yakobo 2:22).

Mfano wa Ibrahimu unaonesha uhusiano sahihi kati ya imani na matendo. Iwapo tunaamini kiukweli (imani), imani yetu itabadilisha namna tunavyoishi (matendo). Iwapo tunakiri kuwa na imani, lakini hakuna badiliko katika namna tunavyoishi, imani imekufa. Kujaribu kubadili namna tunavyoishi mbali na imani ya kweli hakuna maana kabisa. Warumi, Wagalatia, Waebrania, na Yakobo wote wanakubaliana: Imani ya kweli italeta matokeo ya maisha yaliyobadilishwa.

## Soma la 10 Mazoezi

(1) Andaa ujumbe au somo la Biblia juu ya mojawapo ya mada zifuatazo. Unaweza kuwasilisha hii ama katika maandishi (kurasa 5-6) au wasilisha rekodi ukiwa unahubiri au kufundisha.

- "Mifano ya Imani." Tumia mifano ya Imani kutoka Waebrania 11 na pia kutoka katika Historia ya Kanisa*.* Tazama mifano kutoka katika nchi yako au mazingira ya kiutamaduni ambayo yanahamasisha uaminifu katika kutaniko.
- "Uasi." Kama Waebrania, mahubiri yanatakiwa kujumuisha vyote viwili maonyo dhidi ya uasi na kutia moyo ili kubakia waamifu.
- Suala moja kwa ajili ya maisha ya Kikristo (kwa mfano: ulimi, mgogogoro, utajiri, au maombi). Mahubiri haya au somo la Biblia litakuwa na msingi katika kitabu cha Yakobo.

(2) Mwanzoni mwa somo linalofuata, utafanya jaribio kulingana na somo hili. Soma maswali ya jaribio kwa umakini katika maandalizi.

## Somo la 10 Jaribio

(1) Kwa nini waraka kwa Waebrania na nyaraka zilizoandikwa na Yakobo, Petro, Yohana, na Yuda zinaitwa "Nyaraka za Watu Wote"?

(2) Taja hoja mbili zinazokubaliana na Paulo kuwa mwandishi wa Waebrania.

(3) Taja hoja mbili kinyume na uandishi wa Paulo wa Waebrania.

(4) Orodhesha njia mbili ambazo kitabu cha Waebrania inaonesha heshima kubwa kwa Agano la Kale.

(5) Ni kwa nini Agano Jipya ni bora kuliko Agano la Kale?

(6) Ni nini tofauti kati ya aliyerudi nyuma na muasi?

(7) Ni lini Yakobo, kaka (kaka wa mama mmoja) wa kufikia wa Yesu, alikuja kumwamini Yesu kama Masihi?

(8) Yakobo alikuwa anawarejelea akina nani alipotumia neno la kiyunani *diaspora*?

(9) Katika aya 1-2, elezea ni kwa nani Paulo na Yakobo walikuwa wanaandika na ni nini kila mmoja alikuwa anamaanisha kwa kutumia neno "Kuhesabiwa Haki" katika Warumi 3:28 na Yakobo 2:24.

(10) Fafanua *antinomianism*.

(11) Andika Waebrania 4:14-16 na Yakobo 2:17-18 kutoka katika kumbukumbu.

# Somo la 11
# Petro, Yohana, na Yuda
# Nyaraka za Watu Wote, Sehemu ya 2

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kufahamu Tarehe na mazingira ya kihistoria ya Nyaraka za watu wote.

(2) Fupisha mada kuu na makusudi ya Nyaraka za watu wote.

(3) Kuelewa fundisho la kibiblia la uthibitisho/uhakika.

(4) Kuwa makini na hatari ya mafundisho ya uongo.

(5) Kuhusianisha ujumbe wa vitabu hivi na mahitaji ya ulimwengu wa leo.

## Maandalizi kwa Ajili ya Somo hili

► Soma 1 na 2 Petro, 1–3 Yohana, na Yuda.

► Kariri 1 Petro 1:6-7, 1 Yohana 1:6-7, na Yuda 1:24-25.

## Utangulizi

Katika kila kizazi, kanisa limepitia changamoto. Hadi kufikia nusu ya mwisho ya karne ya kwanza, mateso kutoka nje na waalimu wa uongo kutokea ndani ilikuwa ni hatari kubwa kwa kanisa. Hatari hizi zimeendelea katika wakati wote wa historia ya kanisa. Nyaraka za Petro, Yohana, na Yuda zinaonya kuhusiana na hatari hizi. Muhimu zaidi, zinatutia moyo sisi kuendelea kuwa waaminifu tunapopitia hatari hizi. Nyaraka hizi fupi zimebeba ujumbe mkubwa: Mungu aliyetuita sisi ana uwezo wa kutupa ushindi juu ya kila kitu ambacho kinaweza kututenga sisi na Yeye.

## Nyaraka za Petro

### Usuli wa Nyaraka za Petro

#### *Mwandishi*

Simoni Petro alikuwa mmojawapo wa viongozi waliojulikana sana katika kanisa la kwanza. Baada ya kutambulishwa kwa Yesu na ndugu yake Andrea, Petro alikuwa mwanafunzi mmojawapo kati ya wanafunzi watatu wa karibu sana wa Yesu. Jina lake kwa kwanza ni Simoni ("Amesikio"), lakini Yesu akabadilisha jina lake kuwa Petro ("mwamba").

Uongeaji wake na ujasiri wake ulimsababishia matatizo yaliyojirudia rudia wakati wa huduma ya Yesu ya duniani, hasa wakati Petro alipomkana Yesu wakati wa kesi yake. Baada ya ufufuo, Petro alirejeshwa. Watu elfu tatu waliokoka chini ya huduma yake siku ya

Pentekoste. Alisafiri kama mmishenari na kisha akasulubiwa huko Rumi wakati wa mateso ya Nero.[66] kulingana na utamaduni wa kanisa, Petro aliomba kwamba asulubiwe juu chini[67] kwa sababu aliona hakustahili kufa kifo sawa sawa na mwokozi ambaye alimkana.

► Ni kwa namna gani kushindwa kwa Petro wakati wa huduma ya Yesu ya duniani kulimsaidia wakati anawaandikia waamini, akiwatia moyo kubakia waaminifu katika nyakati ngumu? Alijifunza nini kutokana na uzoefu wake ambao ulikuwa na mchango mkubwa katika mfundisho yake katika nyaraka zake?

### *Wapokeaji na Sehemu ya Kuandikwa*

Petro aliandika kutokea Rumi. Mwishoni mwa waraka wake, anaandika, "Mwenzenu mteule hapa Babeli awasalimu…" (1 Petro 5:13). Katika Biblia, *Babeli* mara nyingi iliwakilisha nguvu ambazo ziliwapinga watu wa Mungu. Petro anatumia *Babeli* kurejelea Rumi kama adui wa watu wa Mungu. Sambamba na Babeli kimafumbo, Petro anaelekeza waraka wake wa kwanza kwa waliotawanyika katika Asia Ndogo (1 Petro 1:1). Kama ambavyo Waisraeli walivyotawanyika wakati wa uhamisho, ndivyo ambavyo kanisa lilikuwa wakati wa mateso. Tofauti na Israeli, waamini waliteseka kwa ajili ya Imani yao badala ya kutotii kwao; walikuwa wakishiriki katika mateso ya Kristo (1 Petro 4:12-13).

Wapokeaji wa nyaraka hizi kimsingi ni Wamataifa. Hawa walikuwa waamini ambao hawakuishi tena katika tamaa ambazo walikuwa nazo wakati wa ujinga wao wa kwanza (1 Petro 1:14). 2 Petro haitambulishi wapokeaji, lakini ni waraka wa pili kwa kundi lile lile la wasomaji (2 Petro 3:1).

### *Tarehe*

Inawezekana kwamba Petro aliandika nyaraka hizi muda mfupi kabla ya kifo chache mnamo kati kati ya miaka ya 60 K.K. Mara nyingi nyaraka zinawekwa katia ya mwaka 62 na 67 K.K.

### *Kusudi*

1 na 2 Petro ainawatia moyo waamini wanaoteswa kubakia waaminifu. Kama vite tu Kristo alivyoteseka na akainuliwa, wafuasi wa Kristo wanateseka katika ulimwengu huu na kufurahia utukufuwa milele. Wanapaswa kuwa waaminifu kukabili vyote viwili yaani mateso (1 Petro) na mafundisho ya uongo (2 Petro). Petro anawahakikishia wasomaji wake kwamba Mungu atawapa tuzo wale wanaovumilia.

## Mada Kuu za 1 Petro

### *Tumaini la mkristo*

Kama waliochaguliwa kulingana na maarifa ya kabla ya Mungu Baba, waamini wameahidiwa urithi ambao hauharibiki, usio na uchafu, na usio nyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yao (1 Petro 1:2, 4). Kupitia mateso katika ulimwengu huu, tunalindwa na nguvu za Mungu kwa

[66] Eusebius, *Church History*, 2:25.5-8
[67] Eusebius, *Church History*, 3.1.2.

njia ya imani kwa ajili wa wokovu ambao umeandaliwa kufunuliwa wakati wa mwisho (1 Petro 1:5). Pasipo kujali majaribio ya imani yetu, tuna tumaini la utukufu wa milele. Tumaini hili linaleta furaha kwa waamini ambayo haielezeki kikamilifu (1 Petro 1:8).

### *Wito wa Utakatifu*

Tumaini la utukufu wa milele linatuhamasisha sisi kuitikia wito wa Mungu wa Utakatifu. Akinukuu Mambo ya Walawi 19:2, Petro anawatia changamoto wasomaji wake kuwa watakatifu kama Mungu alivyo mtakatifu (1 Petro 1:16). Hii itaonekana katika upendo wetu kwa ndugu zetu (1 Petro 1:22), kiu yetu ya kweli ya kiroho (1 Petro 2:2), na mwenendo wetu safi (1 Petro 2:11).

Katika waraka kwa waamini wanaoteseka, inaweza kuwa ya kushangaza sana kwamba Petro anawasisitiza kutii mamlaka. Kwa kujua kwamba mateso yanaweza kuwajaribu wafuasi wa Kristo kuzikataa mamlaka zote duniani, Petro anaandika kwamba watu watakatifu wanapaswa kujiweka chini ya taasisi zote za wanadamu kwa ajili ya Bwana (1 Petro 2:13). Utii huu ni kwa ajili ya Kristo, ambaye alijitoa mwenyewe kwa viongozi wa kidunia. Waamini wanapaswa kutii mamlaka ya kisiasa na waajiri wao, na pia mamlaka sahihi ya familia (1 Petro 2:13-3:7). Endapo tunateseka, tunapaswa kuteseka kama Wakristo, na si kama watenda mabaya (1 Petro 3:17, 1 Petro 4:12-19).

### *Kuteseka Juu ya Njia ya Kuelekea Utukufu*

Manabii wa Agano la Kale walitabiri kwamba Kristo atateseka kabla ya kupokea utukufu (1 Petro 1:11). Kristo aliteseka kwa ajili yetu katika mwili (1 Petro 4:1), na sisi pia tunapaswa kutegemea mateso. Kama mabavyo Kristo aliinuliwa katika utukufu, sisi pia tutapokea utukufu ambao watoto wa Mungu wameahidiwa. Petro mwenyewe alishuhudia mateso ya Kristo na alipokea ahadi ya utukufu ambao utafunuliwa (1 Petro 5:1). Ahadi hiyo inamtia moyo kila mwamini anayeteseka.

> "…kutuua, kututesa, kutuhukumu , kututupa chini; kutotenda haki kwenu ni ushahidi kwamba hatuna hatia. Kwa hiyo, Mungu anaruhusu kwamba sisi tuteswe….kwa kadiri tunavyotupwa chini na ninyi, ndivyo idadi yetu inavyoongezeka; damu ya Wakristo ni mbegu ya kanisa.".
>
> - Tertullian mwaka 197 K.K.

## Mada Kuu za 2 Petro

### *Kukua katika Uchaji wa Mungu*

Katika waraka huu wa pili, Petro anawatia changamoto wafuasi wa Kristo kuendelea katika uchaji wa Mungu. Anasema kwamba kupitia ahadi ya Mungu ya thamani na iliyo kuu, waamini wanachukuwa asili ya uungu.

> Naam, na kwa sababu iyo hiyo mkijitahidi sana kwa upande wenu, katika imani yenu tieni na wema, na katika wema wenu maarifa, na katika maarifa yenu kiasi, na katika kiasi chenu saburi, na katika saburi yenu utauwa, na katika utauwa wenu upendano wa ndugu, na katika upendano wa ndugu, upendo (2 Petro 1:4-7).

### *Onyo Dhidi ya Mafundisho Potofu*

Mateso (jambo kuu katika 1 Petro) yanatoka nje ya kanisa; mafundisho potofu (jambo kuu katika 2 Petro) mara nyingi yanaibuka kutoka ndani ya kanisa. Petro anayafunua mafundisho ya manabii wa uongo ambao wamevamia na wanashiriki ndani ya kanisa. Hatari ya mafundisho inaweza kuonekana katika tabia zao zisizo za kimungu, zimefupishwa katika 2 Petro 2:10-19. Maelezo yanamaliza na mithali, "Mbwa ameyarudia matapiko yake mwenyewe, na nguruwe aliyeoshwa amerudi kugaa-gaa matopeni" (2 Petro 2:22).

### *Uaminifu katika Mwanga wa Ujio wa Bwana*

Wapingaji walijaribu kuwavunja moyo wafuasi wa Kristo kwa maswali juu ya ujo wa Bwana. Walisisitiza kwamba mambo yote yameendelea kama yalivyokuwa tangu mwanzo wa uumbaji (2 Petro 3:4). Petro awajibu kwamba kuchelewa kwa Kristo ni matokeo ya uvumilivu wa rehema za Mungu. Mungu hataki kwamba tupotee, lakini tuje katika toba (2 Petro 3:9). Kuchelewa kwake kunawapa fursa ya kutubu. Hata hivyo, kuchelewa kwake kusitupekee sisi kutilia shaka kuhusiana na kweli ya kurudi kwa Kristo. "siku ya Bwana itakuja kama mwivi…" (2 Petro 3:10). Kwa sababu ya uhakika wa kurudi kwake, tunapaswa tuishi kama watu watakatifu; lazima tutafute kuwa na amani na Yeye, bila mawaa wala lawama; na, tunapaswa kuelendelea kukua katika neema na ufahamu wa Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo (2 Petro 3:11, 14, 18).

| Ulinganifu wa 1 na 2 Petro* | |
|---|---|
| **1 Petro** | **2 Petro** |
| Hatari ya Nje: Mateso | Hatari za Ndani: Mafundisho ya Uongo |
| Kuteswa ka ajili ya Kristo | Utukufu wa Mungu |
| Faraja na Kutia moyo | Maonyo |
| Tuna tumaini katika majaribu. | Tuna ufahamu katika nyakati za uongo. |
| * Imechukuliwa kutoka Merrill F. Unger, *Unger's Bible Handbook* (Chicago, IL: Moody Press, 1966) | |

## Nyaraka za Yohana

### Usuli wa Nyaraka za Yohana

### *Mwandishi na Tarehe*

Mababa wa kwanza wa kanisa kama vile Irenaeus na Klementi wa Iskanderia wanamrejea mtume Yohana kama mwandishi wa vitabu hivi. Kama Petro, Yohana alikuwa mvuvi na akawa mmojawapo wa wanafunzi watatu wa Yesu waliokuwa karibu sana Naye. Alikuwepo wakati wa mashitaka ya Yesu na alikuwa pamoja na Mariamu wakati wa kusulubishwa. Pamoja na Petro, Yohana alikuwa shuhuda wa kwanza wa kaburi wazi. Katika Injili yake,

Yohana anajirejelea kama “yule mwanafunzi mwingine” na mwanafunzi “ambaye Yesu alimpenda” (Yohana 20:2).

Kulingana na Eusebius, Yohana na wafuasi wengine wa Kristo walikimbia kutoka Yerusalemu muda mfupi kabla ya mji kuharibiwa na Rumi mwaka 70 K.K. waamini walikimbIlia mji wa Pella kule Perea (mwashariki mwa mto Yordani). Yohana baadae alihudumu huko Efeso. Nyaraka tatu kutoka kwa Yohana pengine ziliandikwa huko Efeso wakati wa sehemu ya mwisho ya karne ya kwanza.

### *Wapokeaji*

1 Yohana haitaji mpokeaji mahususi. Yohana anawarejelea wasomaji wake kama “Watoto wangu wadogo” (1 Yohana 2:1), “Wapenzi” (1 Yohana 3:2), na “Ndugu” (1 Yohana 3:13). Maneno haya yanapendekeza kwamba alikuwa anawaelekezea waamini wenzake ambao alikuwa na mahusiano ya karibu.

2 Yohana inaelekezwa kwa “…mama mteule na watoto wake niwapendao katika kweli…” (2 Yohana 1:1). Kuna uwezekano wa tafsiri mbili za kifungu hiki cha maneno. “mama mteule” inaweza kurejelea:

- Mwanamke ambaye aliruhusu kanisa kukutana nyumbani kwake.
- Kanisa la mahali pamoja ambalo lilifahamika na Yohana. “Watoto wake” inaweza kurejelea washirika katika kanisa hilo.

3 Yohana inaelekezwa kwa Gayo, mwamini aliyeokoka katika huduma ya Yohana (3 Yohana 1:1).

### Mada kuu za 1 Yohana

Waraka wa kwanza kati ya tatu ndio mrefu zaidi. Badala ya salamu ya kawaida, Yohana anaanza na maelezo yanayounga mkono mamlaka ya waraka wake. Haandiki kuhusiana na tetesi au habari zilizo tengenezwa, bali kuhusiana na mambo ambayo yeye mwenyewe ameyashuhudia: “Lile lililokuwako tangu mwanzo, tulilolisikia, tulililoliona kwa macho yetu, tulilolitazama, na mikono yetu ikalipapasa…” (1 Yohana 1:1). 1 Yohana inafanana na Injili ya Yohana katika msisitizo wake juu ya kweli zenye msingi za maisha ya Kristo.

### *Masharti ya Ushirika na Mungu*

Yohana anataja kusudi lakela kuandika mwanzoni mwa waraka wake: “Na haya twayaandika, ili furaha yetu itimizwe” (1 Yohana 1:4). Furaha hii ni kupitia ushirika na Baba na Mwana wake Yesu Kristo (1 Yohana 1:3). Aliandika kuhusiana na ushirika na Mungu, Yohana anatumia neno *Kujua* (1 Yohana 2:3, 13-14, 1 Yohana 4:7-8). Kumjua Mungu ni zaidi ya ufahamu wa kiakili; ni uzoefu katika mahusiano. Yohana anataja masharti ya kutunza ushirika na Mungu:

- Lazima tutembee nuruni (1 Yohana 1:6-7).
- Tusitembee katika dhambi (1 Yohana 2:1-2).

### *Dhambi na Ushirika na Mungu*

Mafundisho ya Yohana kuhusiana na dhambi yanahusisha kweli mbili muhimu:

- **Mungu hutoa nguvu kwa ajili ya maisha ya ushindi**. "Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi…" (1 Yohana 2:1). Endapo tutatuza ushirika na Mungu, hatutakuwa na ushirika na dhambi (1 Yohana 1:6–2:5, 1 Yohana 3:6-9). Kama watoto wa Mungu, hatutaendela kutenda dhambi ya makusudi. Hatuwezi kutembea katika dhambi na kutembea na Mungu kwa wakati mmoja.

- **Mungu hutoa neema kwa wale walioanguka**. "…Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki" (1 Yohana 2:1). Ingawaje Mungu anataka maisha ya ushindi kila wakati, anaahidi neema kwa wale ambao watatubu baada ya kuanguka (1 Yohana 1:9, 1 Yohana 2:1-2).

### *Upendo na Ushirika na Mungu*

Ushindi endelevu dhidi ya dhambi hauna msingi katika adabu binafsi au kudhibiti; bali una msingi katika upendo kwa Mungu (1 Yohana 2:5). Kanuni inayodhibiti maisha ya Kikristo ni Upendo kwa Mungu.[68] Ni kupitia **upendo kwa Mungu** kwamba tutatunza maagizo yake. Endapo tunampenda Mungu, hatutaupenda ulimwengu wala mambo yaliyomo ndani yake (1 Yohana 2:15).

Mtu asiyempenda ndugu yake huyo si wa Mungu. Kama tunampenda Mungu, tutawapenda watoto wa Mungu (1 Yohana 3:10-11, 1 Yohana 4:20-21). Ushahidi kwamba tulipita mautini na kuingia uzimani ni **upendo wetu kwa ndugu Wakristo**. Upendo huu ni zaidi ya maneno; unaonekana katika matendo yetu (1 Yohana 3:14-18).

### *Uhakika/Uthibitisho wa Watoto wa Mungu*

Yohana aliandika ili kwamba wasomaji wake wafahamu ili kwamba wawe na uzima wa milele na ili kwamba waweze kumwamini Yesu (1 Yohana 5:13). Uhakika endelevu unahitaji utii. Tunafahamu kwamba sisi ni watoto wa Mungu wakati maisha yetu yana sifa tatu:

1. **Kutii Kweli (1 Yohana 1:6-7)**. Nyanja hii ya uthibitishi iko sambamba na maneno ya Yesu yaliyonukuliwa katika Yohana 8:31: "Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli." Uthibitisho wetu kama wanafunzi wa Yesu una msingi katika umakini mkubwa na kutii neno lake.

2. **Uhuru toka dhambi ya makusudi (1 Yohana 3:8-10)**. Kwa sababu hatuwezi kuwa na ushirika na Mungu endapo tunaendelea katika uasi wa makusudi dhidi ya Mungu, hatuna uthibitisho/uhakika endapo tutaendelea katika uasi wa namna hiyo.

3. **Kuwapenda waamini wengine (1 Yohana 3:14-19)**. Yesu aliwaambia wanafunzi wake, "Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu,

---

[68] Ili kupata zaidi, ona A. Philip Brown, II. *Loving God: The Primary Principle of the Christian Life*. (Cincinnati: Revivalist Press, 2005).

mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi" (Yohana 13:35). Yohana amerudia msisitizo huu katika nyaraka zake: "Sisi tunajua ya kuwa tumepita toka mautini kuingia uzimani, kwa maana twawapenda ndugu…" (1 Yohana 3:14).

### Yaliyomo katika 2 Yohana

Ujumbe wa 2 Yohana uko sambamba na ule wa 1 Yohana. Ushirika na Mungu unahusisha maisha katika upendo wa Mungu na kutembea katika kweli ya Mungu. Upendo ulioamriwa katika 2 Yohana sio amri mpya; ilifundishwa tangu mwanzo (2 Yohana 1:5-6).

Upendo ulioamriwa katika 2 Yohana ni upendo unaotambua ambao unashikilia kweli. Utambuzi ni muhimu kwa sababu kuna wadanganyaji wengi ambao hawamkiri Kristo. Yohana anamuonya mama mteule kushikilia kweli ya ujio wa Yesu katika mwili (2 Yohana 1:7-8). Ushirika pamoja na Mungu unahitaji kwamba tukatae mafundisho yeyote potofu (2 Yohana 1:10-11).

### Kusudi la 3 Yohana

Kusudi la msingi la 3 Yohana ni kufundisha kuhusiana na ukarimu wa Kikristo. Ukarimu wa Kikristo ni zaidi ya urafiki ambao unawaonesha watu wengine; unaonesha umoja wa kanisa. 2 Yohana anaonya dhidi ya kukaribisha wale wanaofundisha mafundisho potofu. 3 Yohana anaonya dhidi ya kukataa wale wanaofundisha mafundisho ya kweli.

Gayo aliwakaribisha wainjilisti wanaotembea kwa ukarimu wa Kikristo na kuwatendea wao kama watumishi wenza katika Kweli (3 Yohana 1:5-8). Kinyume chake, Diotrefe anakataa kuwapokea ndugu hawa. Diotrefe anatafuta nafasi kwa ajili yake mwenyewe, anakataa mamlaka ya kitume ya Yohana, na anawafukuza wafuasi wa Kristo ambao walimtia changamoto (3 Yohana 1:9-10).

3 Yohana analinganisha tabia ya Diotrefe dhidi ya ile ya upendo wa Kikristo inayooneshwa na Demetrio (3 Yohana 1:12). Waraka huu mfupi unaonesha matumizi ya kivitendo ya upendo wa Kikristo ambao unaamriwa katika 1 Yohana na umoja wa kanisa katika kufuatilia kweli ambayo inaamriwa katika 2 Yohana.

## Yuda

### Usuli wa Yuda

#### *Mwandishi na Tarehe*

Yuda alikuwa kaka (kaka wa mama mmoja) wa kufikia wa Yesu. Kama kaka yake Yakobo, Yuda hakumwamini Yesu hadi alipofufuka.[69] Katika barua yake, Yuda anajitambulisha kama mtumishi wa Yesu Kristo na ndugu wa Yakobo (Yuda 1:1).

[69] Mathayo 13:55, Yohana 7:3-5, 1 Wakorintho 15:7

Ushahidi pekee kuhusiana na tarehe ya kuandikwa kwa waraka wa Yuda ni mfanano wake na 2 Petro. Ukweli kwamba nyaraka zinashughulikia jambo moja inaonesha kwamba Yuda inaweza kuwa iliandikwa wakati ule ule na 2 Petro, mwanzoni mwa miaka ya 60.

### *Wapokeaji*

Yuda imeelekezwa kwa wale walioitwa, waliopendwa katika Mungu Baba na kuhifadhiwa kwa ajili ya Yesu Kristo (Yuda 1:1). Rejea kwa mada ya Kiyahudi inaonesha kwamba waraka huu ulielekezwa kwa Waamini wa Kiyahudi.

### Kusudi na Yaliyomo katika Yuda

Yuda anaonesha kwamba alitumaini kuandika waraka wa mafundisho juu ya wokovu wetu (Yuda 1:3). Hata hivyo, kwa sababu ya waalimu wa uongo waliolivamia kanisa na kushiriki ndani yake, Roho Mtakatifu alimvuvia Yuda kuwaonya waamini wenzake dhidi ya mafundisho ya uongo.

Ujumbe wa Yuda unajumuisha:

- Onyo dhidi ya waalimu wa uongo na ujumbe wao
- Maelelezo ya hukumu ambayo itawajia waalimu hawa wa uongo
- Wito wa kuvumilia.
- Hitimisho la shangwe ya sifa "Yeye awezaye kuwalinda ninyi msijikwae, na kuwasimamisha mbele ya utukufu wake bila mawaa katika furaha kuu" (Yuda 1:24).

## Nyaraka za watu wote Katika Kanisa Leo

Nyaraka za watu wote, kimahususi kabisa 1 Petro, inatutia moyo sisi kubakia waaminifu katika mateso. Petro anawatia changamoto wasomaji wake kujinyenyekesha leo ili kwamba, kwa wakati sahihi, Mungu awainue (1 Petro 5:6). Mateso ni ya kawaida kwa maisha ya Mkristo, lakini mateso hupelekea utukufu. Ahadi hii iliwatia moyo waamini wa karne ya kwanza na inapaswa itutie moyo sisi katika karne ya 21.

Kila kimojawapo cha vitabu hivi kinahamasisha kuishi kikristo kivitendo. Wakati wito wa Petro ni kunyenyekea kwa mamlaka, ujumbe wa 1 Yohana ni upendo kwa ndugu zetu katika Bwana, mahusia ya 2 Yonaha kushikilia kweli, wito wa 3 Yohana ni ukarimu wa Kikristo, au onyo la Yuda dhidi ya waalimu wa uongo, Nyaraka za watu wote zinafundisha kanisa kweli ambayo ni zaidi ya ufahamu wa kiakili. Tunaitwa kuziishi kweli za kibiblia katika maisha yetu ya kila siku.

## Hitimisho

Katika karne ya kwanza, wafuasi wengi wa Yesu (wakiwemo mitume wengi) walikufa kwa ajili ya Imani yao. Katika karne ya pili, Polycarp aliuawa kwa ajili ya kukataa kuchoma uvumba kwa empara. Katika karne ya nne, Catherine wa Iskanderia alikatwa kichwa baada ya kumushuhudia Empara.

Katika karne ya 14, mwili wa John Wycliffe ulichomwa moto kwa sababu alitafsiri Biblia kwenda Kiingereza. Katika karne ya 15, John Huss alichomwa moto akiwa hai kwa sababu aliyakaa mafundisho ya Uromani Katoliki. Katika karne ya 16, waamini 26 walisulubiwa huko Nagasaki, Japan, wakati wa mateso wakati ambapo waamini waliabudu kwa siri.

Katika karne ya 20, maelfu ya wafuasi wa Kristo walikufa kama wafia Imani hiko China, umoja wa Kisovieti, na katika nchi zinazotawaliwa kwa mfumo wa kiimla. Katika karne ya 21, waamini katika nchi zenye waamini wengi wa dini nyingine kila siku wanapitia matishio ya kuteswa na vifo.

Katika kila kizazi, wafuasi wa Yesu wamekufa kwa ajili ya imani yao. Lakini kwa kanisa, hakuna sababu ya kuvunjika moyo. Petro anawakumbusha waamini wanaoteswa: "Na Mungu wa neema yote, aliyewaita kuingia katika utukufu wake wa milele katika Kristo, mkiisha kuteswa kwa muda kidogo, yeye mwenyewe atawatengeneza, na kuwathibitisha, na kuwatia nguvu" (1 Petro 5:10). Kanisa limeshinda! Hii ni ahadi ya Nyaraka za Watu Wote.

## Somo la 11 Mazoezi

(1) Andaa ujumbe au somo la Biblia juu ya mojawapo ya mada zifuatazo. Unaweza kuwasilisha hii ama katika maandishi (kurasa 5-6) au wasilisha rekodi ukiwa unahubiri au kufundisha.

- "Mateso katika Maisha ya Kikristo." Tumia kanuni zilizofundishwa katika 1 Petro na uzielezee kwa mifano kutoka historia ya kawaida, hasa hasa kutoka katika historia ya kanisa katika nchi yako.
- "Ushirika na Mungu." Jumuisha vigezo vya ushirika na Mungu vinavyopatikana katika 1 Yohana.

(2) Mwanzoni mwa somo linalofuata, utafanya jaribio kulingana na somo hili. Soma maswali ya jaribio kwa umakini katika maandalizi.

## Somo la 11 Jaribio

(1) Ni kwa namna gani Petro anatumia neno *Babeli* katika 1 Petro 5:13?

(2) Ni nini ilikuwa hatari ya nje iliyolikumba kanisa katika 1 Petro?

(3) Ni nini ilikuwa hatari ya ndani iliyolikumba kanisa katika 2 Petro?

(4) 2 Yohana inaelekezwa kwa "mama mteule…" Hii inaweza kurejelea mambo gani mawili?

(5) Ni kweli gani mbili ambazo ni muhimu katika 1 Yohana zinafundisha kuhusu dhambi?

(6) Kulingana na 1 Yohana, sifa gani tatu ambazo zinatakiwa kuwa katika maisha ya watoto wa Mungu?

(7) Nini ni kusudi la msingi la 3 Yohana?

(8) Yuda alihusianaje na Yesu?

(9) Andika 1 Petro 1:6-7, 1 Yohana 1:6-7, na Yuda 1:24-25 kutoka katika kumbukumbu.

# Somo la 12
# Ufunuo
# Yesu ni Bwana

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kumfahamu mwandishi, tarehe, na mazingira ya kihistoria ya Ufunuo.

(2) Kutambua mada kuu muhimu katika Ufunuo.

(3) Kulinganisha nadharia muhimu za kutafsiri Ufunuo.

(4) Kuhusisha ujumbe wa Ufunuo kwa mahitaji ya ulimwengu wa leo.

## Maandalizi kwa ajili ya Somo hili

► Soma Ufunuo. Kabla haujaanza, chagua mojawapo wa mazoezi ya kuandika yaliorodheshwa mwishoni mwa somo hili.

► Kariri Ufunuo 3:20-21.

## Utangulizi

Waamini wa karne ya kwanza walipambana na kweli mbili ambazo zilikuwa zinashindana. Kwa upande mmoja, walifahamu kwamba Yesu Kristo ni Bwana (Wafilipi 2:11). Mfuasi wa Kristo alijikita chini ya mamlaka na Ubwana wa Yesu Kristo. Kwa upande mwingine, Rumi ilihitaji kila mmoja chini ya mamlaka ya dola kumrejelea Kaisari kama *dominus et deus noster* (kifungu cha maneno cha kilatini kinacho maanisha "bwana wetu na mungu wetu").

Rumi ilivumilia dini nyingi, endapo tu empara alitambuliwa kama mamlaka ya juu zaidi. Wanahistoria wengi wanasema kwamba Rumi hawakuwatesa wafuasi wa Kristo kwa sababu ya imani yao. Kila mmoja aliruhusiwa kumwabudu Yesu endapo tu angeapa uaminifu wa empara. Hata hivyo, mwamini wa kweli hawezi kamwe kumtambua empara kama mamlaka ya mwisho.

Kulingana maelezo ya shahidi wa kuona wa mauaji ya Polycarp, hakimu alitoa ofa ya kumfungulia mtakatifu mzee endapo tu angemtambua Kaisari kama mungu. Alimwambia Polycarp, "Kuna madhara gani katika kusema, ' Kaisari ni bwana,' na kufukiza uvumba?"[70] Polycarp alifahamu kwamba kwa mfuasi wa Kristo, kuna Bwana mmoja tu. Uaminifu wa juu sana hautolewi kwa mwanadamu yeyote.

[70] "The Letter of the Smyrnaeans on the Martyrdom of S. Polycarp," katika *The Apostolic Fathers*, imetafsiriwa na J.B. Lightfoot (London: Macmillan and Co., 1912), 205. Kinapatikana mtandaoni katika https://archive.org/details/a590752000clemuoft/page/n221

Huu ndio ulikuwa mzizi wa mgogoro kati ya Rumi na kanisa la kwanza. Kutokana na mgogoro huu, kitabu cha Ufunuo wa Yohana kilisema kwa waamini wa kwanza, "Yesu ni Bwana." Hata katika ulimwengu ambao hautambui mamlaka yake, Yesu ni Bwana. Ufunuo wa Yohana unatoa picha ya kielelezo ya maneno ya Paulo:

> Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina; ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi; na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba (Wafilipi 2:9-11).

Yesu ni Bwana.

## Usuli wa Ufunuo wa Yohana

### Mwandishi, Tarehe, na Mahali

Mwandishi wa Ufunuo wa Yohana anajitambulisha mwenyewe kama "…Yohana, ndugu yenu na mwenye kushiriki pamoja nanyi katika mateso…" (Ufunuo 1:9). Tamaduni za kanisa la kwanza zinamtambulisha Yohana, mwanafunzi aliyependwa, kama mwandishi wa Injili ya Yohana, nyaraka tatu, na Ufunuo wa Yohana.

Tarehe ya waraka huu ni swali gumu. Kuna uwezekano wa tarehe mbili, zote zikiwa ndani ya maisha ya Yohana na kipindi cha mateso katika kanisa la kwanza. Tarehe moja inayowezekana ni wakati wa utawala wa Nero (54-68 B.K), wakati wa mateso makali. Tarehe inayopewa kipaumbele zaidi ni wakati wa mateso chini ya Empara Domitian (81-96 B.K). Katika karne ya pili, Irenaeus aliweka tarehe ya kitabu cha Ufunuo katika miaka ya baade ya utawala wa Domitian.[71] Wengi wa wainjilisti wanakubali hii kama tarehe inayowezekana ya kuandikwa kwa Ufunuo.

Ufunuo iliandikwa kutoka Patmo, kisiwa kidogo ndani ya Bahari ya Aegea, ambapo Yohana alikuwa huko uhamishoni kama kifungo kwa ajili ya imani yake. Ingawa empara aliidhinisha kuhamishwa kwa Yohana, Yohana anaweka wazi kwamba Yesu ni Bwana. Yuko Patmo kwa ajili ya Neno la Mungu na kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu Kristo (Ufunuo 1:9). Hata huko Patmo, Mungu anatawala.

### Kusudi

Ufunuo inajibu swali, "Nani ni Bwana?" jibu linatolewa katika utangulizi: "…Yesu Kristo, shahidi aliye mwaminifu, mzaliwa wa kwanza wa waliokufa, na mkuu wa wafalme wa dunia" (Ufunuo 1:5). Kwa waamini ambao walikuwa wanapata mateso, Yohana anaandika: Yesu Kristo ni mtawala juu ya watawala wote juu ya dunia. Bila kujali mazingira ya nje, Mungu anatawala.

Ukweli kwamba Yesu ni Bwana unawasilishwa katika njia tatu:

---

[71] Irenaeus, *Against Heresies* 5.30.3.

1. Ujumbe kwa makanisa saba (Ufunuo 2-3). Yesu ni Bwana juu ya kanisa lake.
2. Katika maono ya Mungu juu ya kiti cha enzi na Kristo kama Mwanakondoo aliyeshinda (Ufunuo 4-5). Yesu ni Bwana mbinguni.
3. Katika kutazama historia kutoka mtazamo wa mbinguni (Ufunuo 6-22). Yesu ni Bwana juu ya falme za ulimwengu.

## Kusoma Ufunuo wa Yohana

### Fasihi ya Apokaliptiki

Kama kitabu cha apokaliptiki, Ufunuo ni cha tofauti na vitabu vingine vya Agano Jipya. Danieli ni kitabu cha Agano la Kale ambacho ni mfano wa Agano la Kale wa Fasihi ya apokaliptiki. Maandishi ya apokaliptiki yanatumia alama na maono kufunua ukweli. Maandishi ya apokaliptiki yanafunua kusudi la Mungu katika historia ya mwanadamu.

#### *Alama*

Fasihi ya apokaliptiki hutumia alama za kushangaza ili kuwasiliana. Ufunuo imejaa majoka, wanyama wa kutisha, majanga ya kiasili kama vile tetemeko la adhi na mvua za mawe. Ugumu mmoja katika kusoma fasihi ya apokaliptiki ni kwamba alama hubadilisha maana zake mara kwa mara kila wakati katika mazingira tofauti ya kiutamaduni. Kwa mfano, joka hutumika huko Magharibi kama alama ya uovu na hatari; katika tamaduni nyingi za Mashariki, joka ni alama ya nguvu na mafanikio. Tofauti na namna alama zinavyo tafsiriwa zinaweza kufanya Ufunuo kuwa mgumu kwa msomaji.

Ufunguo mkuu kwa ajili ya kutafsiri alama katika Ufunuo ni kutambua kwamba alama nyingi zinatoka Agano la Kale, na hasa Kutoka, Zaburi, Danieli, Ezekieli, Isaya, na Zekaria. Zaidi nusu ya mistari katika Ufunuo inajumuisha baadhi ya viashiria katika dhana au taswira ya Agano la Kale. Msomaji makini wa Ufunuo ataangalia kwanza katika Agano la Kale wakati anajifunza alama.

#### *Maono*

Fasihi ya apokaliptiki huonesha uhalisia wa kihistoria au kinabii kupitia maono. Ufunuo unajumuisha zaidi ya maono 60. Maono haya mara nyingi, yanaingiliana, ambayo hufanya kuwa ngumu kutengeneza mpangilio wa mfuatano halisi wa matukio ili kupanua taarifa au kuleta mbadala wa mtazamo katika matukio.

#### *Mada kuu*

Pengine cha muhimu zaidi ni kwa msomaji kukumbuka wakati anapojifunza Fasihi ya apokaliptiki kuweka umakini katika dhana kuu pasipo kubebwa na kushangazwa na taarifa. Katika Ufunuo, mada kuu ni ubwana wa Yesu, ukuu wa Mungu, na ushindi mkuu wa kanisa. Mada hizi zinaunganisha habari katika kitabu chote.

**Nadharia za Kutafsiri**

Kwa sababu Ufunuo kina mtindo usio wa kawaida wa fasihi ya Kibiblia, kimesababisha njia nyingi za kutafsiri. Kuna njia nne za kutafsiri kitabu hiki. Ndani ya kila moja ya hizi, kuna misisitizo tofauti inayotofautiana. Vyanzo vilivyoorodheshwa kwa ajili ya somo hili kutakupa vitabu zaidi kwa ajili ya kujifunza zaidi.

**Preterist View (Mtazamo wa Preterist): Ufunuo kilitokea wakati wa Dola ya Rumi.** Preterists wanaamini kwamba Ufunuo ni kuhusu matukio yaliyotokea mwishoni mwa karne ya kwanza. Katika mtazamo huu, matukio katika Ufunuo yalitokea wakati wa maisha ya Yohana au mapema baadae. Mtazamo huu unaona Ufunuo kama picha ya mgogoro kati ya kanisa na dola ya Rumi. Mgogoro huu ulimalizwa na ushindi wa Ufalme wa Kristo wakati kanisa lilipokuwa linasambaa ulimwenguni. Kulingana na mtazamao huu, nabii katika Ufunuo zilitimilika katika karne ya kwanza.

**Historicist View (Mtazamo wa Kihistoria): Ufunuo ni mtazamo wa kialama wa historia ya Kanisa,** kutoka wakati wa kanisa la kwanza hadi kurudi kwa Kristo na kuanzishwa kwa mbingu mpya na nchi mpya. Katika mtazamo huu, Ufunuo 1-3 inazungumzia makanisa katika siku za Yohana. Ufunuo 4-19 inatupa mfuatano wa picha ya kanisa katika kipindi chote cha historia. Ufunuo 20-22 inaonesha ujio wa baadae wa Kristo. Kulingana na mtazamo huu, unabii wa Ufunuo 20-22 tu, ndio unaosubiri utimilifu wa baadae.

**Idealist View (mtazamo wa Idealist): Ufunuo ni alama kamili ya vita kati ya wema ana uovu.** Idealists hukubaliana na historicists kwamba Ufunuo unatupa picha ya mgogoro kati ya wema (Kristo na Kanisa) na uovu (shetani na wafuasi wake). Hata hivyo, idealists wanadai kwamba hii lugha ya picha isiyokuwa na mtiririko wowote wa kihistoria. Katika mtazamo huu, Ufunuo 4-19 haihusishi kupindi chohcote mahususi katika historia. Ni alama ya mgogoro unaoendelea kati ya Kristo na Uovu, mgogoro ambao utamalizwa na ujio wa Kristo kuanzisha mbingu mpya na nchi mpya zinaelezewa katika Ufunuo 20-22. Kulingana na mtazamo huu, Ufunuo hakitabiri matukio mahususi ya wakati ujao, ispokuwa tukio la kuja kwa Kristo.

**Futurist View (Mtazamo wa Futurist): Ufunuo 4-22 unaelezea matukio ya mbele yanayokuja.** Kama historicists, futurists husoma Ufunuo kama picha ya matukio mahususi ambayo yatatokea katika kipindi mahususi. Tafsiri hii huona Ufunuo 1-3 kama inaelezea kanisa la wakati wa Yohana. Wakitofautiana na historicists, futurists huona sehemu kubwa ya Ufunuo 4-22 ikielezea mambo yajayo. Futurists wengi hushikilia msimamo kati ya tafsiri nne zifuatazo za yajayo yanayooneshwa katika Ufunuo.

Angalizo: Neno *millennium* humaanisha “kipindi cha miaka elfu moja.” Katika majadiliano ya Ufunuo, neno hili hurejelea kipindi ambacho Yesu atatawala juu ya ulimwengu, kama inavyotajwa katika Ufunuo 20:4. Utofauti mkubwa wa mitazamo juu ya Ufunuo huusisha utofauti katika tafsiri juu ya millennium.

***Classical premillennialism*** (kutoka karne ya pili au mapema zaidi) walitegemea mateso ya kanisa hadi kipindi cha mwisho wa nyakati. Mateso yatafika kilele chake wakati wa dhiki kuu kabla ya kurudi kwa Kristo. Kristo atakapokuja, kutakuwa na ufufuo wa mwili wa waamini, ukifuatiwa na millennium wakati Kristo atakapotawala juu ya ulimwengu. Millennium itafuatiwa na hukumu ya waovu kiti kikubwa cheupe (Ufunuo 20:11-15). Kisha Mungu ataanzisha mbingu mpya na nchi mpya, makao ya milele ya wale ambao majina yao yameandikwa katika kitabu cha Uzima cha Mwana Kondoo.

***Dispensational premillennialism*** ni mtazamo wa kisasa unaotofautiana na mafundisho ya classical premillennial. Katika mtazamo huu, kanisa litaondolewa duniani katika unyakuo kabla ya kipindi cha miaka saba ya dhiki kuu. Hali mbaya na ngumu katika Ufunuo 4-19 inaonekana kama dhiki ya Israeli duniani kwa kipindi cha miaka saba wakati kanisa liko mbinguni pamoja na Yesu. Kisha Kristo atarudi na kutawla juu ya ulimwengu kwa miaka elfu moja. Kama inavyofundishwa na classical premillennialism, dispensational premillennialists wanaamini kwamba kipindi hiki kitafuatiwa na hukumu na kuumbwa kwa mbingu mpya na nchi mpya.

***Postmillennialism*** (ilikuwa maarufu katika karne ya 18 na 19) inafundisha kwamba injili itasambaa ulimwenguni kote na kubadilisha jamii hadi kuwa wakati wa haki na amani. Katika mtazamo huu, Kristo hatatawala kimwili juu ya ulimwengu kwa miaka elfu moja. Kristo atarudi baada ya millennium, kumshinda Shetani milele, na kuanzisha mbingu mpya na nchi mpya.

***Amillennialism*** (tarehe ni takribani mwishoni mwa karne ya pili) wanakubaliana na postmillennialism kwamba Krsito hatatawala kimwili juu ya ulimwengu kwa miaka elfu moja. Amillennialists wanaona millennium kama kipindi chote cha kanisa. Wanasema ahadi ya millennium inatimizwa kwa namna ya kiroho kupitia huduma ya kanisa. Ufunuo huonesha vyote viwili baraka na mahangaiko ya kanisa katika lugha ya picha. Kipindi hiki kitamalizwa na ujio wa Kristo, ukifuataiwa na hukumu na kuanzishwa kwa mbingu mpya na nchi mpya kwa ajili ya waamini.

Tusichanganye tafsiri yetu ya Ufunuo na mamlaka ya maandiko yenyewe. Watu wawili wanaoamini mamlaka ya maandiko wanaweza kuwa na tafsiri tofauti za kitabu hiki. Kuwa makini usimkatae mwamini mwenzio ambaye anaweza kufikia hitimisho tofauti. Hizi ni tofauti katika tafsiri za Biblia, na si utofauti kuhusiana na mamlaka ya kibiblia.

> "Katika mambo ya msingi, umoja.
> Katika mambo yasiyo ya msingi, uhuru.
> Katika mambo yote, upendo."
>
> - Rupertus Meldenius, 1627

## Mada kuu za Ufunuo

### *Yesu ni Bwana*

Fasihi ya kiapokaliptiki hufunua kile ambacho kimefichwa. Ufunuo humfunua Yesu katika utukufu wake wote. Wakati wa huduma yake hapa duniani, utukufu wake haukuonekana

katika ukamilifu wake. Paulo aliahidi kwamba siku inakuja ambapo kila goti litapigwa, la vitu vya mbinguni. Na vitu vya duniani, na vitu vya chini ya nchi (Wafilipi 2:10). Ufunuo hufunua picha ya utukufu wa siku hiyo.

Alama nyingi katika Ufunuo zimechukuliwa kutoka Agano la Kale. Hata hivyo, alama hizi zinafundisha theolojia ya kipekee ya kikristo. Kitabu kimeunganishwa na theolojia ya Kikristo ambayo inashikamanisha kila nyanja ya kazi za Mungu katika historia ya mwandamu. Kutoka katika maono ya Yohana ya Mwana wa Adamu na picha yake ya mwanakondoo aliyeshinda, mada kuu ya Ufunuo ni ubwana wa Yesu Kristo (Ufunuo 1:9-20, Ufunuo 5:6-14). Yesu ni Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana (Ufunuo 19:16).

### *Mungu Aanatawala*

Kwa kanisa linalo teseka, ujumbe wa Ukuu wa Mungu ulikuwa ni ujumbe wa matumaini. Yohana anamtambulisha Mungu kama yeye aliyeko, na aliyekuwako na atakayekuja (Ufunuo 1:4). Maono ya Mungu akiwa kwenye kiti cha enzi katika Ufunuo 4-5 ni sawa na Isaya 6. Yohana, kama Isaya, anamuona Mungu kama Mtakatifu, mwenye utisho, na mwenyezi. Kwa kanisa linalipingwa na Rumi, ilikuwa inatia moyo kusoma katika Ufunuo kwamba kuna siku inakuja wakati ambapo kila kiumbe kilichoko mbinguni na juu ya nchi na chini ya nchi ya juu ya bahari, na vitu vyote vilivyomo ndani yake vitaungana kwa pamoja kumsifu Mungu na Mwana Konodoo (Ufunuo 5:13).

### *Ushindi wa Watu wa Mungu*

Ufunuo hufunua makusudi ya Mungu katika historia ya mwanadamu. Pamoja na kwamba kuna alama nyingi ambazo msomaji wa kipindi hiki anahangaika kuzielewa, ujumbe wa jumla wa Ufunuo uko wazi: watu wa Mungu wanahakikishiwa ushindi kwa sababu Yesu ni Bwana. Ufunuo mara kwa mara unahamisha mtazamo kutoka duniani kwenda mbinguni, ukitukumbusha sisi kwamba tunaona upande mmoja wa historia.[72] Pasipo kuonekana, Mungu analitenda kusudi lake ulimwenguni. Kama watu wa Mungu, tunahakikishiwa ushindi mkuu. Ujumbe kwa kanisa la Laodikia unahitimisha na kututia moyo: "Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi…" (Ufunuo 3:21).

## Ufunuo katika Kanisa Leo

Kuna hatari mbili za kuepuka wakati wa kusoma Ufunuo. Baadhi ya wasomaji huona Ufunuo unachanganya sana kiasi kwamba wanaepuka kabisa kusoma. Kwa sababu hawana uhakika wa tafsiri sahihi, hawakisomi kabisa.

Hatari iliyo kinyume na hiyo ni kwamba baadhi ya wasomaji wana uhakika na tafsiri zao kiasi kwamba wanakataa mtu yeyote mwenye tafsiri tofauti na tafsiri yao. Wanaweka umakini katika taarifa ndogo na kupoteza mwanga wa mada kuu ya jumla ya kitabu. Ni bahati mbaya kwamba ujumbe mkubwa wa Ufunuo umekuwa wakati mwingine unapotea

[72] Kwa mfano: Ufunuo 6:1-7:8 vipo juu ya ulimwengu; Ufunuo 7:9-8:6 vipo mbinguni. Ufunuo 8:7-11:14 vipo juu ya ulimwengu; Ufunuo 11:15-19 vipo mbinguni.

katika mabishano kuhusiana na taarifa za tafsiri. Ujumbe wa Ufunuo ni muhimu kwa kanisa leo.

Katika wakati ambapo watakatifu wanauawa kila mwaka, ujumbe ni kwamba Yesu ni Bwana unawatia moyo wale ambao wanateseka na kuvumilia. Pasipo kujali njia/namna ya mtu ya tafsiri, Ufunuo unalitia moyo kanisa kwa ahadi ya ushindi mkuu.

Ufunuo unatukumbusha sisi namna ambavyo waamini wanapaswa kuishi leo katika mwanga wa nyakati za mwisho. Kujifunza kuhusiana na siku za mwisho (*eskatolojia*) kimsingi si katika kutabiri mambo yajayo; madai ya msingi ya eskatolojia ni kuishi wakati huu katika mwanga wa kusudi kuu la Mungu. Kama waamini, Ufunuo unatutia moyo sisi kuamini kusudi la Mungu. Kama watumishi, tunahubiri Ufunuo ili kutia moyo makusanyiko yetu kubakia waaminifu. Kuliko kusoma Ufunuo kama kitabu chenye ujumbe kuhusiana na yajayo, tusome Ufunuo kama Neno la Mungu kwa ajili ya watu wa Mungu leo.

## Hitimisho

John na Betty Stam walikuwa wamishenari huko China wakati vikosi vya wakomunisti vilipovamia mji wao mwaka 1934. Wanandoa hawa wachanga walikamatwa, walishikiliwa kwa ajili ya fidia, na walitembezwa chini ya ulinzi hadi kwenye mji wa Miaosheo. Mpita njia aliuliza, "Mnakwenda wapi?" John Stam alijibu, "Hatujui wao wanakwenda wapi, lakini sisi tunakwenda mbinguni."

Siku iliyofuata, John na Betty Stam walichinjwa na wachinjaji wa kikomunisti. Barua ya mwisho iliandikwa na John kwa msimamizi wake wa umisheni na ikiwa imetoroshwa katika nguo za mtoto wao mchanga wa kike. Barua ilihitimishwa na maneno haya: "...kwetu sisi, Mungu atukuzwe, ikiwa ni kwa maisha au kifo." John na Betty Stam walijua kwanza ukweli wa Ufunuo: Yesu ni Bwana na atashinda ushidni wa mwisho. Ikiwa ni kupitia maisha/uhai au kifo, Mungu anatawala, na njia zake ndio njia nzuri zaidi.

## Somo la 12 Mazoezi

(1) Chagua moja katika ya mazoezi yafuatayo:

- Andaa ujumbe au somo la Biblia ambalo utafanyia kazi ujumbe wa mojawapo ya makanisa saba kulingana na mahitaji ya kanisa lako mwenyewe (Ufunuo 2-3). Unaweza kuwasilisha hii ama katika maandishi (kurasa 5-6) au wasilisha rekodi ukiwa unahubiri au kufundisha.
- (Hii inaweza kukamilishwa wakati wa maandalizi ya Somo la 12.) wakati unasoma Ufunuo wa Yohana, chukua notisi za sura ambazo zinatoa mtazamo wa kile kinachotokea ulimwenguni na sura zipi zinatoa picha ya kile kinachotokea mbinguni. Andika insha fupi ukifupisha kile ambacho Ufunuo wa Yohana unatuonesha sisi kuhusiana na mtazamo wa mbinguni kuhusiana na matukio ya duniani. Ni kwa namna gani mtazamo kutoka mbinguni unatofautiana na mtazamo wetu wenye ukomo juu ya ulimwengu?

(2) Mwanzoni mwa somo linalofuata, utafanya jaribio kulingana na somo hili. Soma maswali ya jaribio kwa umakini katika maandalizi.

## Somo la 12 Jaribio

(1) Dola ya Rumi ilihitaji watu kumrejelea Kaisari kama *dominus et deus noster*. Kifungu hiki cha maneno cha kilatini kinamaanisha nini?

(2) Ufunuo pengine kiliandikwa wakati wa miaka ya baadae ambapo mtawala gani alitawala? Ni miaka gani alitawala?

(3) Kisiwa cha Patmo kipo sehemu gani?

(4) Orodhesha jia tatu ambazo Yohana aliwasilisha ukweli kwamba Yesu ni Bwana.

(5) Taja sifa mbili za fasihi ya kiapokaliptiki.

(6) Kwa sentensi moja kwa kila moja, fafanua mitazamo minne ya Ufunuo.

(7) Orodhesha mitazamo minne ya yajayo miongoni mwa futurists.

(8) Orodhesha mada kuu muhimu katika Ufunuo.

(9) Andika Ufunuo 3:20-21 kutoka katika kumbukumbu

# Vyanzo Vinavyopendekezwa

Ili kujifunza zaidi kuhusiana na mada zilizojadiliwa katika kitabu hiki, tafadhali ona vyanzo vifuatavyo.

## Ulimwengu wa Agano Jipya

### Vitabu

Beitzel, Barry. *The Moody Atlas of the Bible*. Chicago: Moody Press, 2009.

Elwell, Walter A. and Robert W. Yarbrough. *Encountering the New Testament*. Ada: Baker Academic, 2013.

Ferguson, Everett. *Backgrounds of Early Christianity*. Grand Rapids: Eerdmans, 2003.

Jensen, Irving. *Jensen's Survey of the New Testament*. Chicago: Moody Press, 1981.

McDowell, Josh. *The New Evidence That Demands a Verdict*. Nashville: Thomas Nelson, 1999.

Tenney, Merrill C. *New Testament Survey*. Grand Rapids: Eerdmans, 1994.

### Vyanzo vya Mtandaoni

Maps of the Bible. Katika https://biblemapper.com/blog/chronolist/.

McDowell, Josh. Bible: Fact, Fiction, or Fallacy. Mfululizo wa video za Mtandaoni Katika https://www.josh.org/resources/apologetics/videos/.

Smith, Dr. Randall. "They Thought You Knew." Katika https://www.youtube.com/watch?v=phUhvp812Mo.

"Why Bible Background Matters." Katika https://www.youtube.com/watch?v=-wiIK8A2EFk.

Wight, Fred H. *Manners and Customs of the Bible*. Chicago: Moody Press, 1953. Katika https://archive.org/details/B-001-014-057/

The Works of Josephus. Katika http://www.ccel.org/j/josephus/works/JOSEPHUS.HTM.

## Uhakika na kuaminiwa kwa Agano Jipya

### Vitabu

Bruce, F.F. *The New Testament Documents: Are They Reliable?* InterVarsity, 1988.

McDowell, Josh. *The New Evidence That Demands a Verdict.* Thomas Nelson, 1999.

**Vyanzo vya Mtandaoni**

McDowell, Josh. Bible: Fact, Fiction, or Fallacy. Mfululizo wa video za Mtandaoni. https://www.josh.org/resources/apologetics/videos/.

Orr-Ewing, Amy. Reliability of the Manuscripts. Video ya Mtandaoni kutoka RZIM HQ. http://www.youtube.com/watch?v=dLI7W4bnVpA.

**Injili Zinazoona Pamoja**

**Vitabu**

Bock, Darrell L. *Baker Exegetical Commentary on the New Testament: Luke*. Ada: Baker, 1996.

Garland, David E. *The NIV Application Commentary: Mark*. Grand Rapids: Zondervan, 1996.

France, R.T. *New International Commentary on the New Testament: Matthew*. Grand Rapids: Eerdmans, 2007.

**Vyanzo vya Mtandaoni**

"The Gospel of Mark." Katika https://www.youtube.com/watch?v=8J2LP9_f3SY.

"Matthew and the Great Commission." Katika https://www.youtube.com/watch?v=6PiltJ0DDhI.

Robertson, A.T. *A Harmony of the Gospels*. New York City: Harper, 1922. Kinapatikana mtandaoni Katika http://www.gutenberg.org/files/36264/36264-h/36264-h.htm.

Smith, Dr. Randall. "Introduction to the Gospels." Katika https://www.youtube.com/watch?v=LZ4udDfiQBc.

Wesley, John. *Wesley's Explanatory Notes on the New Testament*. Katika https://studylight.org/commentaries/eng/wen.html.

**Injili ya Yohana**

**Vitabu**

Bruce, F.F. *The Gospel of John*. Grand Rapids: Eerdmans, 1994.

Morris, Leon. *New International Commentary on the New Testament: John*. Grand Rapids: Eerdmans, 1995.

**Vyanzo vya Mtandaoni**

Robertson, A.T. *A Harmony of the Gospels*. New York City: Harper, 1932. Kinapatikana mtandaoni Katika http://www.gutenberg.org/files/36264/36264-h/36264-h.htm.

Wesley, John. *Wesley's Explanatory Notes on the New Testament*. Katika https://studylight.org/commentaries/eng/wen.html.

## Matendo ya Mitume

### Vitabu

Bence, Philip A. *Acts: A Commentary in the Wesleyan Tradition*. Fishers: Wesleyan Publishing House, 1998.

Marshall, I. Howard. *Tyndale New Testament Commentaries: Acts*. Grand Rapids: Eerdmans, 1980.

McCain, Danny. *Notes on Acts of the Apostles*. Nigeria: Africa Christian Textbooks, 2001.

Rasmussen, Carl. *Zondervan Atlas of the Bible*. Grand Rapids: Zondervan, 2010.

Stott, John R.W. *The Message of Acts*. Downers Grove: Intervarsity Press, 1990.

### Vyanzo vya Mtandaoni

Wesley, John. *Wesley's Explanatory Notes on the New Testament*. Katika https://studylight.org/commentaries/eng/wen.html.

## Warumi

### Vitabu

Bray, Gerald, ed. *Ancient Christian Commentary on Scripture: Romans*. Downers Grove: Intervarsity Press, 1998.

Clarke, Adam. *Commentary on the New Testament*. Nashville: Abingdon Press, n.d.

Greathouse, William M and George Lyons. *New Beacon Bible Commentary: Romans* (2 volumes). Kansas City: Beacon Hill Press, 2008.

### Vyanzo vya Mtandaoni

"Does Romans 7 Teach that Christians will Continue Sinning?" Katika https://www.youtube.com/watch?v=aBXYp7cMblM.

"Does Romans 9-11 Teach Calvinist Predestination?" Katika https://www.youtube.com/watch?v=nCLtbVnOqq4.

"Romans." Katika https://www.youtube.com/watch?v=OpBPE-dEVhQ.

Wesley, John. *Wesley's Explanatory Notes on the New Testament*. Katika https://studylight.org/commentaries/eng/wen.html.

## Wakorintho na Wagalatia

### Vitabu


Clarke, Adam. *Commentary on the New Testament*. Nashville: Abingdon Press, n.d.

Gill, David. "1 Corinthians" in *Zondervan Illustrated Bible Backgrounds Commentary*. Grand Rapids: Zondervan, 2002.

Morris, Leon. *Galatians: Paul's Charter of Christian Freedom*. Downers Grove: Intervarsity Press, 2003.

Stott, John. *The Message of Galatians*. Downers Grove: Intervarsity Press, 1984.

Wilson, Earle L. *Galatians, Philippians, Colossians: A Commentary for Bible Students*. Fishers: Wesleyan Publishing House, 2007.


### Vyanzo vya Mtandaoni


"Paul's Leadership Challenges at Corinth." Katika https://www.youtube.com/watch?v=Gu_ELh_UXPg.

Wesley, John. *Wesley's Explanatory Notes on the New Testament*. Katika https://studylight.org/commentaries/eng/wen.html.


## Nyaraka za Kifungozi

### Vitabu


Beet, Joseph Agar. *A Commentary on St. Paul's Epistles to the Ephesians, Philippians, Colossians, and to Philemon*. Salem: Schmul Publishing, 1982.

Earle, Ralph, ed. *Beacon Bible Commentary, Vol. IX: Galatians through Philemon*. Kansas City: Beacon Hill Press, 1965.

Holmes, Mark A. *Ephesians: A Bible Commentary in the Wesleyan Tradition*. Fishers: Wesleyan Publishing House, 1997.

Stott, John R.W. *The Message of Ephesians*. Downers Grove: InterVarsity Press, 1979.

Wilson, Earle L. *Galatians, Philippians, Colossians: A Commentary for Bible Students*. Fishers: Wesleyan Publishing House, 2007.


### Vyanzo vya Mtandaoni


"Church and Mission in Ephesians." Katika https://www.youtube.com/watch?v=4Fzjwcu_tUI.

Wesley, John. *Wesley's Explanatory Notes on the New Testament*. Katika https://studylight.org/commentaries/eng/wen.html.

## Wathesalonike

### Vitabu

Airhart, Arnold E. *Beacon Bible Commentary: I and II Thessalonians*. Kansas City: Beacon Hill Press, 1965.

Clarke, Adam. *Commentary on the New Testament*. Nashville: Abingdon Press, n.d.

Klopfenstein, W.O. *Wesleyan Bible Commentary: I and II Thessalonians*. Grand Rapids: Eerdmans, 1965.

Morris, Leon. *Tyndale New Testament Commentaries: 1 and 2 Thessalonians*. Grand Rapids: Eerdmans, 2007.

### Vyanzo vya Mtandaoni

Wesley, John. *Wesley's Explanatory Notes on the New Testament*. Katika https://studylight.org/commentaries/eng/wen.html.

## Nyaraka za Kichungaji

### Vitabu

Gould, J. Glenn. *Beacon Bible Commentary: I and II Timothy, Titus*. Kansas City: Beacon Hill Press, 1965.

Nicholson, Roy S. *Wesleyan Bible Commentary: The Pastoral Epistles*. Grand Rapids: Eerdmans, 1965.

Oden, Thomas C. *Ministry through Word and Sacrament*. Crossroad, 1989.

Stott, John R.W. *The Message of 2 Timothy*. Downers Grove: Intervarsity Press, 1973.

### Vyanzo vya Mtandaoni

Wesley, John. *Wesley's Explanatory Notes on the New Testament*. Katika https://studylight.org/commentaries/eng/wen.html.

## Waebrania na Yakobo

### Vitabu

Cockerill, Gareth L. *Hebrews: A Bible Commentary in the Wesleyan Tradition*. Fishers: Wesleyan Publishing House, 1999.

Osborne, Grant. *James: Cornerstone Biblical Commentary*. Carol Stream: Tyndale House Publishers, 2011.

Turner, George Allen. *The New and Living Way.* Minneapolis: Bethany Fellowship, 1975.

Walters, John. *Hebrews: Asbury Bible Commentary*. Grand Rapids: Zondervan Publishing House, 1992.

Earle, Ralph ed. *Beacon Bible Commentary, Vol. X: Hebrews through Revelation*. Kansas City: Beacon Hill Press, 1965.

**Vyanzo vya Mtandaoni**.

Cockerill, Gareth. "Hebrews and Contemporary Preaching." Katika https://www.youtube.com/watch?v=7IDOorJbZYY.

Wesley, John. *Wesley's Explanatory Notes on the New Testament*. Katika https://studylight.org/commentaries/eng/wen.html.

## Nyaraka za Watu Wote

**Vitabu**

Bray, Gerald. *Ancient Christian Commentary on Scripture: James-Jude*. Downers Grove: Intervarsity Press, 2000.

Brown, A. Philip, II. *Loving God: The Primary Principle of the Christian Life*. Cincinnati: Revivalist Press, 2005.

Maier, Paul L., trans. *Eusebius: The Church History.* Grand Rapids: Kregel Publishing, 2007. (An easy to read translation of this ancient source.).

Marshall, I. Howard. *1 Peter*. Downers Grove: Intervarsity Press, 1991.

Marshall, I. Howard. *The Epistles of John (New International Commentary on the New Testament)*. Grand Rapids: Eerdmans, 1978.

Wiersbe, Warren. *Be Alert: 2 Peter, 2 & 3 John, Jude*. Colorado Springs: David C. Cook, 2010.

**Vyanzo vya Mtandaoni**

"John Wesley and Christian Orthodoxy." Katika https://www.youtube.com/watch?v=WJ93nzeFS8U.

Wesley, John. *Wesley's Explanatory Notes on the New Testament*. Katika https://studylight.org/commentaries/eng/wen.html.

## Ufunuo wa Yohana

**Vitabu**.

Gentry, Kenneth L., Sam Hamstra, C. Marvin Pate, and Robert L. Thomas. *Four Views on the Book of Revelation*. Edited by Stanley Gundry and C. Marvin Pate. Grand Rapids: Zondervan, 1998.

Blaising, Craig A., Kenneth L. Gentry Jr., and Robert B. Strimple. *Three Views on the Millennium and Beyond*. Edited by Stanley N. Gundry and Darrell L. Bock. Zondervan, 1999.

Blaising, Craig, Alan Hultberg, and Douglas Moo. *Three Views on the Rapture: Pretribulation, Prewrath, or Posttribulation*. Edited by Stanley N. Gundry and Alan Hultberg. Grand Rapids: Zondervan, 2010.

Osborne, Grant. *Revelation*. Ada: Baker, 2002.

Rotz, Carol. *New Beacon Bible Commentary: Revelation*. Kansas City: Beacon Hill Press, 2012.

**Vyanzo vya Mtandaoni**

"Revelation and Apocalypticism." Katika https://www.youtube.com/watch?v=D3CP4gE8Jt8.

Wesley, John. *Wesley's Explanatory Notes on the New Testament*. Katika https://studylight.org/commentaries/eng/wen.html

# Fomu kwa ajili ya Kumbukumbu ya Kazi za Kufanya

Jina la Mwanafunzi ______________________________________.

Katika jedwali hapa chini, andika tarehe ya kumaliza pembezoni mwa kila zoezi. Mitihani yote huhesabika kwamba "imekamilika" wakati mwanafunzi anapokuwa amepata matokeo ya alama 70% au zaidi. Kazi zote ulizopewa kufanya ni lazima zikamilishwe kwa ukamilifu ili uweze kupatiwa cheti cha kuhitimu kutoka Shepherds Global Classroom.

| Somo | Jaribio | Zoezi la 1 | Zoezi la 2 |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |
| 4 | | | |
| 5 | | | |
| 6 | | | |
| 7 | | | |
| 8 | | | |
| 9 | | | |
| 10 | | | |
| 11 | | | |
| 12 | | | |

Maombi kwa ajili ya kupewa Cheti cha Kufuzu kozi kutoka Shepherds Global Classroom yanaweza kukamilishwa kupitia ukurasa wetu wa wavuti www.shepherdsglobal.org. Vyeti vitatumwa kwa mfumo wa kidigitali kutoka kwa Rais wa SGC kwenda kwa wakufunzi na wawezeshaji ambao watakamilisha maombi hayo kwa niaba ya mwanafunzi (au wanafunzi).